**17 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

_________

## MAJADILIANO YA BUNGE

__________

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 17 Mei, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tano, Kikao cha Ishirini na Nane.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. TAMIMA HAJI ABBASS K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang.

Na. 362

### Sekondari za Simbay, Sumaye na Mary Nagu Kuwa na Kidato cha Tano na Sita

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi Shule za Sekondari za Simbay, Sumaye na Mary Nagu zilizopo Hanang kuwa za Kidato cha Tano na Sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa mazingira bora ya ufundishaji kwa wanafunzi wote wenye sifa za ufaulu wa kujiunga na kidato cha tano na sita, hasa katika kipindi hiki cha utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo. Kipaumbele cha Serikali ni ujenzi wa Shule mpya za Kitaifa na upanuzi wa shule, kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Aidha, Serikali kupitia Mradi wa *SEQUIP* inaendelea na ujenzi wa shule mpya 26 za Mikoa, kwa ajili ya wasichana na shule saba za kanda, kwa ajili ya wavulana.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Halmashauri zimeelekezwa kutenga bajeti pamoja na kushirikiana na wananchi kufanya upanuzi wa miundombinu inayohitajika kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita yakiwemo Mabweni, Mabwalo na Madarasa na kisha kuomba kibali cha kupandisha hadhi shule kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Eneo la Damaygwa, Kata ya Gendabi, wanafunzi wanatembea kilomita zaidi ya 14 kwenda Shule ya Sekondari Sumaye. Hali iko hivyo hivyo pia, eneo Gasaboy, Kata ya Darwar. Je, Serikali iko tayari kujenga shule za sekondari kwenye kata hizo mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Tarafa nzima ya Simbay haina shule ya kidato cha tano na sita. Je, Serikali ina kauli gani kuhakikisha kwamba, eneo hilo pia, linapata shule ya kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Hanang iliweza kujengewa shule mbili za kata katika Kata ya Indesak na Kata ya Ishponga kwa jumla ya shilingi bilioni 1.05. Kwa hiyo, namhakishia kwamba, Serikali inatambua sana umuhimu wa kuhakikisha kila kata inaweza kupata shule hizi za sekondari na katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kata ya Darwar, aliyoizungumzia Mheshimiwa Mbunge, imetengewa jumla ya shilingi milioni 584.2 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba, kwa kadiri ya fedha zinavyopatikana Serikali inakuja kujenga shule katika jimbo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili. Amezungumza kuhusiana na Tarafa ya Simbay ambayo bado haina shule ya kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumfahamisha kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 90.6, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, matundu ya vyoo na pia, imetenga shilingi milioni 80 katika fedha za ndani za halmashauri kwa ajili ya kuendeleza miundombinu muhimu ambayo itawezesha shule hii kupandishwa hadhi kuwa ya kidato cha tano na sita. Kwa hiyo, namhakikishia Serikali ipo kazini, inatambua umuhimu wa shule hizi na itaendelea kuzijenga kwa kadiri ya fedha zinavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus, swali fupi la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa, Shule za Sekondari Ngunichile na Kiegei zina miundombinu ya kutosha. Je, Serikali iko tayari kupandisha hadhi ya shule hizi, ili tupate kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa sana, hii ya kuhakikisha miundombinu yote muhimu inayohitajika katika shule zake hizo inajengwa. Natumia nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri yake aweze kupeleka maombi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa ajili ya hatua ya kuzipandisha hadhi shule hizo alizozitaja, ili ziweze kuwa shule za kidato cha tano na sita.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi.

Na. 363

**Serikali Kuongeza Shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza shule za sekondari za kidato cha tano na sita kwa kuzingatia umoja na kulinda utaifa wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kujenga na kupanua Shule za Sekondari za kidato cha tano na sita za Kitaifa, ili kukidhi uwepo wa ongezeko la wanafunzi wa kidato cha tano na sita nchini kufuatia mafanikio ya utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Ada iliyoanza kutekelezwa Mwaka 2016. Idadi ya shule za kidato cha tano na sita imeongezeka kutoka shule 318 Mwaka 2016 hadi shule 615 Mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 48.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Serikali kupitia Mradi wa *SEQUIP* imepanga kujenga Shule za Bweni za

Wavulana za Kitaifa saba zenye kuchukua wanafunzi 1,080 kwa kila shule. Aidha, Serikali inaendelea na mpango wa ukamilishaji wa ujenzi wa shule 26 za sayansi za bweni za wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na jitihada zake za kuongeza ujenzi na upanuzi wa Shule za Kitaifa za bweni za kidato cha tano na sita katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanapewa fursa ya kusoma katika utekelezaji wa mipango ya Serikali ya kutoa fursa ya elimu kwa wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Mimi nimesoma Shule ya Sekondari *Songea Boys* Mkoa wa Ruvuma na hii ilikuwa ni kunifanya mimi nifahamu kwamba, kuna wangoni, kuna wamakonde, nakadhalika na kwamba, na wao ni Watanzania. Pia, ilinifanya nifahamu kwamba, sisi ni Taifa moja. Je, Serikali inalizingatiaje suala hili, ili kuendelea kujenga umoja wa Taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Sera ya elimu na mitaala mipya ambayo Serikali imeitayarisha inataka kuanzia chekechea mpaka kidato cha nne watoto wasome kwenye kijiji au kata ile ile aliyozaliwa. Je, Serikali imeweka mkakati gani kuhakikisha kwamba, angalau sasa kidato cha tano na sita watoto hawa wanatoka nje ya mazingira yao, ili kuhakikisha kwamba, Taifa letu linakuwa moja na kwamba, mshikamano na umoja wa Taifa letu unazingatiwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, yote mawili kwa pamoja. Naomba kumhakikishia kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa utaifa na inaanza kufanya hivyo kuanzia katika utoaji wa elimu. Ndio maana shule za kidato na sita ni shule za kitaifa na ndio maana

kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kuhakikisha kwamba, shule za kidato cha tano na sita zinapata miundombinu yote muhimu ikiwemo mabweni, ili kuweza kupokea wanafunzi wale wanaofaulu waweze kuingia katika shule hizi za kitaifa ambazo ni za kidato cha tano na sita. Vilevile kuna miradi mbalimbali ambayo inahakikisha kwamba, miundombinu ya kidato cha tano na sita inaimarika na wanafunzi wengi wanaomaliza kidato cha nne wanaweza kuingia katika shule hizi za kitaifa za kidato cha tano na sita. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala lake la kuwaza dhamira njema ya utaifa linazingatiwa katika utekelezaji wa kusimamia elimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Shule ya Ikuti katika Wilaya ya Rungwe ina miundombinu yote ambayo inafaa kuwepo kidato cha tano na sita. Je, ni lini Serikali itaiongezea hadhi shule hiyo iwe shule ya juu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili shule ya sekondari ipandishwe hadhi kuwa shule ya kidato cha tano na sita ni ikishakuwa tayari na miundombinu inayohitajika, kinachofanyika ni kupeleka maombi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kuipandisha shule hiyo. Kwa hiyo, kama Shule hii ya Ikuti aliyoitaja ina miundombinu yote inayohitajika, basi ni wajibu wa mkurugenzi kuweza kupeleka maombi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa ajili ya kuomba ipandishwe hadhi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, aulize swali lake.

Na. 364

**Ujenzi wa Barabara ya Mchombe Hadi Ijia – Mlimba**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mchombe hadi Ijia, Mlimba, yenye Kilometa 2.7 kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Ujenzi wa barabara za lami katika Kata ya Mchombe, Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, ambazo zitachochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Wananchi wa Halmashauri hiyo. Katika Mwaka 2023/2024, Serikali inatarajia kujenga Barabara ya Mchombe – Lukorongo – Ijia kwa kiwango cha lami kwa urefu wa mita 350 kwa gharama ya shilingi milioni 200. Aidha, usanifu umekamilika, mkandarasi amepatikana na anatarajia kuanza kazi pindi mvua za masika zitakapoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TARURA* itaendelea kuhudumia miundombinu ya Barabara ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, ikiwemo ujenzi wa Barabara ya Mchombe – Ijia kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kutokana na mvua hizi za el-nino zilizonyesha zimechangia uharibifu wa miundombinu, kwa maana ya Barabara za Tarafa ya Mgeta, Mlimba na kata zake zote.

Nini mpango wa Serikali kurejesha mawasiliano ya barabara hizi kukatika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, urejeshaji wa barabara hizi zilizokatika unaenda sambamba na ujenzi wa madaraja. Nini mpango wa Serikali kujenga madaraja yafuatayo, Daraja la Mbasa, Daraja la Mvuji, Daraja la Isago na Daraja la Chiwachiwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli mvua hizi tulizokuwanazo kwa wakati huu zimeleta uharibifu mkubwa sana wa miundombinu nchi nzima. Kwa muktadha huu hata kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge wamepata madhara makubwa sana ambayo pia, yamesababisha kukatika kwa mawasiliano. Kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha kwamba, yale maeneo ambayo mawasiliano yamekatika, mawasiliano yanarudishwa. Kwa hiyo, nakuhakikishia, tayari nimeshapata orodha ya maeneo na barabara zote ambazo mawasiliano yamekatika na tutayafanyia kazi kwa udharura unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili. Ni kweli kuna umuhimu mkubwa sana wa ujenzi wa madaraja, na hasa haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Namhakikishia kwamba, Serikali imeshafanya usanifu wa kina na fedha zikipatikana tutahakikisha kwamba, madaraja haya yanajengwa, ili yaweze kuwa ni madaraja ya kudumu tofauti na ilivyo sasa hivi. Kwa hiyo, nakuhakikishia, suala hili tunalipa kipaumbele sana, tunafahamu ni kiasi gani jimbo lako limeathirika na mvua hizi. Nikupe *comfort* tu kwamba, tutakuja kufanyia kazi kama Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, akiwa Makamu wa Rais,

aliahidi kutengeneza barabara ya lami kutoka Hospitali Teule ya Mgana mpaka Kaja. Tunamshukuru alishatuletea fedha shilingi bilioni 500 tukatengeneza sehemu ya barabara hiyo kilometa 1.2, lakini bado kilometa 3.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itatupatia fedha, ili barabara hiyo iweze kukamilika na ahadi ya Mheshimiwa Rais iweze kukamilika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Viongozi Wakuu wa nchi, na hasa ahadi za Mheshimiwa Rais, ni kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa mipango ya Serikali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama vile ambavyo tayari Serikali imeanza awamu ya kwanza kwa kuleta fedha, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii, nakuhakikishia kwamba, itahakikisha inaleta fedha, ili kukamilisha ahadi hii ya Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo. Kwa niaba, linaulizwa na Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 365

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kirua**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza:-

Je, lini Kituo cha Afya Kata ya Kirua, Vunjo Kusini, kitajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mahitaji na imeendelea kujenga vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2023/2024 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 3.9, kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na upanuzi wa vituo vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali itatenga shilingi milioni 250 kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kirua, Vunjo, na Serikali itaendelea kutenga bajeti ya kuendeleza ujenzi wa kituo hicho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa kiwango kilichotajwa cha fedha bado hakitoshi na kwa kuwa wananchi waliingia gharama kubwa sana kununua ekari hizo tano kwa ajili ya kituo hicho? Je, Serikali ipo tayari sasa kuongeza kiwango hicho kwenye hii bajeti ya 2024/2025? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ninaomba nimwulize Waziri, yupo tayari kufuatana na Mheshimiwa Mbunge, kwenda kutembelea kituo hicho ili aone umuhimu wake na jinsi gani wananchi wanakisubiri kwa hamu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Vunjo lakini pia Mheshimiwa Mama, Shally Raymond pamoja na Wananchi wa Kata ya Kirua Vunjo Kusini, kwa kununua eneo lenye ukubwa wa ekari tano kwa ajili ya kujenga kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kwamba Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeshapeleka zaidi ya shilingi bilioni 3,900,000,000 katika Halmashauri ya Moshi na tayari Mwaka wa Fedha 2025/2026, tumeshaweka mpango wa kupeleka shilingi milioni 250. Niwahakikishie kwamba huu ni mwanzo baada ya 250 kuanza kazi, tutapeleka fedha nyingine kuhakikisha kwamba 500 inatimia na majengo hayo yanakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo, kwenda kukagua miradi ya maendeleo, lakini pia kuona ujenzi wa kituo hiki mara kitakapokuwa kimeanza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, nimekuona.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Halmashauri ya Mji Njombe imeshajenga vituo vinne kwa fedha za halmashauri yenyewe, lakini tuliomba tuongezewe kituo kimoja na Serikali imeshatujengea kimoja. Tuliomba tuongezewe kituo cha pale Njombe Mjini kituo kikogwe ambacho kimechakaa sana. Nini mpango wa Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwanyika, kwa namna ambavyo anawatumikia Wananchi wa Jimbo la Njombe Mjini. Niwapongeze sana Menejimenti ya Halmashauri ya Njombe Mjini kwa kuonesha mfano wa kujenga vituo vya afya vinne kwa mapato ya ndani ya Halmashauri. Nitumie nafasi hii kuwa-*encourage* wakurugenzi wengine wajifunze kutumia fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tulishachukua taarifa zote na mahitaji ya upanuzi na ukarabati wa Kituo cha Afya cha pale Njombe Mjini. Ni suala la muda Mheshimiwa Mbunge tutahakikisha kwamba fedha zinapelekwa na ukarabati huo unafanyika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana Manaibu Waziri, wote wawili kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, sasa aulize swali lake. Kwa niaba Mheshimiwa Hawa.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Cecil David Mwambe…

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Cecil David Mwambe naomba sasa swali lake namba 366 lipate majibu ya Serikali.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nililisimamia hilo swali mbona.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa, kama una swali atauliza Mheshimiwa Mariam. Mheshimiwa Mariam, swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe. Kama una swali huwezi kuuliza swali la mtu mwingine.

Na. 366

**Wanaojitolea Kupewa Kipaumbele Katika Ajira**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha wanaojitolea wanapewa kipaumbele cha kupata ajira pindi nafasi za ajira zinapotolewa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshmiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008, Toleo la Pili ikisomwa pamoja na Kanuni ya *D.6* (1) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2009 Toleo la Tatu, nafasi za ajira katika Utumishi wa Umma zinatakiwa kujazwa kwa ushindani na kwa kuzingatia sifa stahiki kwa mujibu wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya kada hiyo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo Bunge lako liliielekeza Serikali itoe mwongozo mahususi kwa wanaojitolea ili kuwawezesha kupata kipaumbele punde ajira za kudumu zinapotolewa Serikalini. Ukamilishaji wa mwongozo huo upo katika hatua za mwisho za mashauriano ndani ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwongozo huo wa Serikali bado haujatoka na upo kwenye mchakato na kwa kuwa zipo baadhi ya shule na vituo vya afya ambavyo havina watumishi, hali hiyo imesababisha halmashauri wachukue angalau vijana waje wasaidie katika shule hizo kufundisha masomo mbalimbali. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuangalia kwa jicho la kipekee vijana hawa ambao wanajitolea bure bila malipo kufanya kazi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wapo vijana sasa hivi wapo katika sehemu mbalimbali wanafanya kazi za kujitolea pamoja na wengine kazi za mkataba, lakini vijana hawa wanaofanya

kazi za mkataba hawapewi bima ya afya na wala hawapewi nyongeza yoyote ile ya kiutumishi isipokuwa ni kifuta jasho pale *Boss* anapoamua. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa vijana hawa ambao wanajitolea katika maeneo ya mashirika mbalimbali ili kuwasaidia angalau wapate hata nauli? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pili kulihakikishia Bunge lako kwamba Serikali inatambua upungufu katika baadhi ya maeneo hasa katika maeneo ya shule hususani kwenye kada hii ya walimu ambao tunawahitaji sana kwa ajili ya kuwaelekeza watoto wetu. Yapo maelekezo mahususi ambayo yamepelekwa kwenye halmashauri zetu ambayo yanazinataka halmashauri kupitia mapato yake ya ndani kuendelea kutenga pesa kwa ajili ya hawa walimu ambao wanajitolea. Pia, siyo hao walimu wanaojitolea tunawapa pia wale madaktari wanaojitolea katika zahanati zetu. Kwa hiyo, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, lakini pia kurudia tena maelekezo ya Serikali. Serikali inasisitiza halmashauri zetu ziendelee kupanga mapato ya ndani ili kuwezesha huduma hizi muhimu ikiwemo ya walimu kufundisha shuleni na kada nyinginezo ziendelee kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Mbunge alitaka kujua je, Serikali inaendelea vipi kuwaangalia wale wanaojitolea? Ninataka Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia miongozo mbalimbali pamoja na kwamba sasa bado tunaendelea kutengeneza mwongozo huo wa ajira za kujitolea, lakini maelezo na nia ya Serikali ya kuwasaidia wanaojitolea bado ipo wazi. Mimi ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya hivyo kadiri ambavyo uwezo wa kipesa ndani, lakini pia wa kibajeti utakavyoweza kupatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kwa majibu hayo. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland Mbunge wa Mvomero, aulize swali lake.

Na. 367

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Kata za Msongozi na Mangae - Mvomero**

**MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mradi wa maji uliopo katika Kata za Msongozi na Mangae – Mvomero?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Jimbo la Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia wataalamu wa ndani inaendelea na utekelezaji wa Miradi ya Maji ya Msongozi na Mangae iliyopo Wilaya ya Mvomero Mkoani Morogoro. Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa matanki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita 250,000, ujenzi wa vyumba viwili vya mitambo *(Power house)*, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 32.78 pamoja na ujenzi wa vituo 38 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji unaendelea na miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2024 na kunufaisha wananchi wapatao 7,720 waishio kwenye vijiji vya Msongozi na Mangae.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas Van Zeeland.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kata ya Mzumbe ni miongoni mwa kata ambazo bado zina changamoto kubwa sana ya maji hasa katika Kijiji cha Sangasanga, Vikenge, Changarawe na Tangeni. Je, lini Serikali itaanza kujenga mradi wa maji katika kata hii ili kupunguza tatizo hili la maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kata ya Dakawa Kitongoji cha Sokoine, wananchi wamekuwa wakiteseka kwa muda mrefu sana kupata maji. Mwaka juzi tulipata mradi wa maji ambao tulitegemea ungekamilika mwaka jana mpaka sasa mradi huo haujakamilika. Je, ni lini sasa mradi huu utakamilika ili Wananchi wa Kitongoji cha Sokoine, waweze kunufaika na maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Jonas, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Jonas anaendelea kufanya kazi nzuri sana katika Jimbo lake la Mvomero na hakika anaendelea kutupa ushirikiano mkubwa sana sisi Serikali katika kubainisha vyanzo vya maji ili tuhakikishe kwamba kazi yetu ya ufikishaji wa maji inaendelea kuwa nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, usanifu wa Mradi wa Vijiji vya Sangasanga, Tangeni pamoja na Changarawe unaendelea kufanyika na utakamilika muda si mrefu. Vilevile, Serikali kupitia bajeti ambayo tumepitisha wiki iliyopita tayari tumetenga fedha kwa ajili ya kwenda kuhakikisha kwamba, mradi huo unaanza. Tunatarajia mradi huo utaanza kati ya Mwezi Julai na Agosti. Kwa hiyo, tukuombe tu Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kuhakikisha kwamba mradi huu unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha pili, kuhusu Dakawa katika Kitongoji cha Sokoine, mradi ule tayari umeshafikia 90% na kinachofuatia sasa hivi ni ile kazi ya maunganisho ya umeme pamoja na pampu. Tunaamini kwamba muda si mrefu kazi hiyo itakamilika na wananchi katika eneo hilo wataanza kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali fupi la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kati ya majimbo yanayotumia fedha kidogo kwenye miradi ni Jimbo la Makete, kutokana na maji mengi ni ya mserereko. Kata ya Lupila mmetupatia Mradi ya maji Vijiji Sita mwaka 2022. Hadi sasa miradi hii imesimama na gharama zake ni shilingi milioni 150, shilingi milioni 200 na shilingi milioni 300. Wana-Makete wanauliza ni lini mtatoa fedha miradi hii ikamilike ili wananchi wapate maji kwa uhakika kama ahadi ya Serikali ilivyo kwa wananchi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tuna mradi ambao wa Vijiji Sita katika Jimbo la Makete. Mradi huu hakika unaenda kusaidia sana Wananchi wa Makete kulingana na kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Mbunge wao katika eneo hilo na kwa kweli anaendelea kutupa ushirikiano kama Serikali, lakini tunatambua kwamba Serikali pia inaendelea kutafuta fedha na sasa tumeshapata fedha kwa ajili ya vijiji viwili ambavyo ni Malanduku pamoja na Kijiyombo. Vile vingine ambavyo vitakuwa vimebaki Serikali itaendelea kutafuta fedha na ikishapata basi tutaenda kutekeleza miradi hiyo ili iweze kukamilika na wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendela na swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa.

Na. 368

**Ujenzi wa Visima vya Maji Kikombo Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa visima wiwili vya maji vilivyoanza kujengwa mwaka 2021 Kikombo – Mpwapwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha uchimbaji wa visima viwili katika Eneo la Kikombo Wilayani Mpwapwa ambapo kwa pamoja vina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 1.6 kwa siku. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali itajenga miundombinu ya usambazaji maji kupitia visima hivyo itakayonufaisha wananchi wapatao 5,000 wa Kata ya Mpwapwa Mjini. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na nyumba ya mitambo *(power house),* ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 11.5 na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 200,000, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Natany Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja ya nyongeza.

Kwa kuwa swali hili nimeuliza mara ya pili leo, majibu yamekuwa ni yale yale bila utekelezaji. Wananchi wa Mpwapwa wangetaka kujua, nini *commitment* ya Serikali juu ya kutekeleza mradi huu ili adha wanayoipata ya maji iweze kuondoka? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia mradi huu kwa karibu sana. Sisi kama Wizara tumeamua sasa kuhakikisha kwamba huu mradi unaenda kutekelezwa. *Commitment* ya Serikali katika mradi huu ni kwamba tayari katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 tumetenga kiasi cha shilingi milioni 862 ambapo tunaenda sasa kuanza rasmi mradi huu. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji ikishakamilika wananchi wa Jimbo lake la Mpwapwa Mjini wataendelea kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, aulize swali lake.

Na. 369

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Mwibara**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi - Mwibara?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda imeshatoa eneo lenye ukubwa wa meta za mraba 20,230 katika Eneo la Kibara kwa ajili ya kujenga kituo cha Polisi Daraja B na nyaraka zimewasilishwa Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Mara kwa ajili ya kupata hati.

Fedha kwa ajili ya ujenzi zinatarajiwa kutengwa kwenye Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza, ninaipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake mzuri wa kujenga Kituo hicho kikubwa cha Polisi Kibara. Ninalo swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Jimboni Mwezi wa Pili mwaka huu aliagiza kituo kidogo kingine cha Polisi kijengwe Bulamba karibu na shule ya sekondari ya wasichana inayojengwa. Je, agizo hili litatekelezwa lini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Kajege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Viongozi Wakuu wa Taifa ni maelekezo kwetu. Kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge jambo hilo tutalichukua na tutaweka kwenye mpango wetu ili kujenga Kituo cha Polisi katika Eneo la Bulamba kama alivyouliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. Kwa niaba Mheshimiwa Ng'wasi Kamani.

Na. 370

**Wahamiaji Haramu Waliomaliza Vifungo na Wapo Gerezani**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y. MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, ipi kauli ya Serikali kuhusu wahamiaji haramu waliomaliza vifungo vyao na bado wako magerezani?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kuwaondoa nchini wahamiaji haramu waliomaliza vifungo vyao magerezani. Katika kipindi cha mwaka 2022 hadi Aprili, 2024 jumla ya wahamiaji haramu 7,120 waliomaliza vifungo walioondolewa nchini. Hata hivyo, wahamiaji haramu 224 bado wapo magerezani na wote ni Raia wa Ethiopia wakisubiri taratibu za kuondoshwa kwao zikamilike ikiwemo kupata hati za kusafiria kutoka nchini kwao, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali kwa majibu mazuri ambayo yanaonesha kwamba, tayari wanachukua hatua kuhakikisha kwamba idadi hii kubwa ya wahamiaji haramu waliopo katika magereza yetu wanarudishwa kwenye nchi zao. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, je, Serikali haioni haja ya kupitia upya sera, sheria, taratibu na kanuni zetu ili kubadilisha namna ya kusimamia wahamiaji haramu pale wanapokamatwa ili tofauti na ilivyo sasa kwamba wakikamatwa wanafungwa magerezani na kuingizia Serikali gharama kubwa wawe wanarudishwa kwenye nchi zao papo kwa papo kwa wakati huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakiksha kwamba inashughulikia tatizo hili la uhamiaji haramu kwa haraka kwa kulinda mipaka yetu kwa uhakika kupunguza idadi hii kubwa ya wahamiaji haramu wanaoingia kwenye nchi yetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inabadilishwa pale ambapo unafanya tathmini na kuona kuna mapungufu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 sasa inafanyiwa mapitio. Kwa hiyo, ushauri huu pia tutauzingatia katika kuhakikisha jambo hilo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, mkakati uliopo wa Serikali kuzuia wahamiaji haramu ni pamoja na misako ya mara kwa mara, doria na pia kutoa elimu kwa umma kuhakikisha kwamba tunatambua majirani zetu. Upo msemo wetu unaosema; "Mjue Jirani yako." Kwa hiyo kwa kuzingatia hayo yote na kwa kushirikiana na wananchi pia tutatokomeza uhamiaji haramu hapa nchini, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana kwamba Serikali haitambui tatizo kubwa lililopo kwa wananchi wanaotoka Mikoani ama nje ya nchi wanalolipata wanapoleta wagonjwa wao katika hospitali ya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wamekuwa wakilala kwenye vibanda vya chipsi, wamekuwa wakilala kwenye majengo ya pembeni mwa hospitali ya Muhimbili wakisubiri pakuche ili waweze kwenda kuangalia wagonjwa wao. Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kufanya dharura ili angalau hawa watu wanaoleta wagonjwa wao waweze kupata sehemu ya kujisitiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wa watu hawa wanaoteseka ni wanawake ambao wanakuwa na watoto wameleta familia zao pale hospitalini, anapoamka asubuhi hana uhakika wa mtoto atakula nini, hana uhakika wa yeye mwenyewe atajisitiri wapi ili aweze kwenda kumwangalia mgonjwa wake.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka, Mheshimiwa majibu.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni sasa....

**MWENYEKITI:** Swali moja tu Mheshimiwa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si maswali mawili?

**MWENYEKITI:** Haya uliza swali la pili.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kuna umuhimu wa kutosubiri na badala yake kuweza kuweka majengo angalau kwa kuanzia ili hawa watu waweze kupata maeneo ya kujihifadhi?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwambie Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kwamba kwanza Serikali inatambua na ninataka kukuambia tu kuwa kampasi ya Muhimbili wagonjwa tu wanaoingia kwa siku moja ni 12,000. Maana yake kila mgonjwa anasindikizwa labda na watu wawili, jumla ni watu 24,000. Kipaumbele na dharura ya Serikali ni magonjwa haya, kuna watu wengi wanakuja hawawezi kulipa, kuna watu wengi wanakuja na magonjwa mbalimbali, leo tukizungumzia tu kwenye eneo la mama na mtoto kwa mwaka ni bilioni 124.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake tunaelekeza nguvu hivi, ndiyo maana tunasema kwa mfano kwenye *masterplan* ya sasa inaenda kujengwa maeneo ya namna hiyo lakini wakati huo huo tutashirikiana na sekta binafsi. Kwa sababu nikuambie Mheshimiwa Mbunge, kuna mambo ambayo ni lazima tuyafikirie kwa kina kwa sababu la sivyo tutaumiza zaidi yale ya dharura hasa ambayo sisi tunatakiwa ku-*concentrate* kwa mgonjwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi sasa, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 371

**Hitaji la Taa za kuongoza Magari na Taa za Barabarani – Mji wa Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka taa za kuongoza magari na taa za barabarani katika Mji wa Tarime kwa kwani Mji huo unapitisha magari mengi ya abiria na biashara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Mara iliweka jumla ya taa 133 katika Mji wa Tarime kuanzia eneo la Buhemba hadi Tarime *Hill* eneo la Magere. Aidha, ujenzi wa barabara ya kuanzia Tarime Mjini hadi Mogabiri yenye urefu wa kilometa 9.3 utajumuisha pia uwekaji wa taa za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika ujenzi wa barabara ya Tarime - Mugumu unaoendelea, tumepanga kuweka taa za kuongoza magari Tarime Mjini katika eneo la Jembe na Nyundo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mji wa Tarime ni Mji ambao unakua kwa kasi sana, na kwa kuwa umekuwa na magari mengi ya watalii ambayo yanatoka nchi jirani ya Kenya kwenda Mbunga ya Serengeti, pia mabasi ambayo yanaenda nchi jirani ya Kenya na magari makubwa ambayo yanafuata bidhaa mbalimbali za mazao na kuleta bidhaa za ujenzi, na kwa kuwa,

*roundabout* ya Jembe na Nyundo ni hatarishi imekuwa ikisababisha ajali nyingi sana.

Ni kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa kujenga hiyo *roundabout* iwe ya kisasa na kuweka taa sasa hivi, kuliko kusubiri ujenzi wa barabara ya Mugumu - Tarime? *(Makofi)*

Swali la pili, umeeleza hapa kwamba umeweka taa Buhemba, Tarime *Hill* na kwenda kule Zaka Filling, lakini kwa Mji wa Tarime ambao unapitisha watalii kama nilivyosema awali ni kwa nini Serikali msiweke taa kuanzia kona ya Gilikola mpaka Buhemba na pia kuanzia Gilikola kwenda Musoma *Road* kwenda mpaka Zaka Filling? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, suala la kwanza la maeneo ambayo ameyataja nadhani katika jibu letu la msingi tumesema kwamba tunakwenda kujenga na mradi huo unaendelea. Kwa hiyo, katika huo mradi taa ni sehemu yake katika hilo eneo la Nyundo na eneo la Jembe katika huo mradi, tumeshaweka kwenye huo mpango ambao tayari unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu urefu wa hizo taa kwamba tuongeze hayo maeneo ndiyo maana tumesema tutaongeza taa katika Mji wa Tarime katika huo mradi. Sasa hivi sehemu zote ambazo tunajenga barabara kwa sasa tunahakikisha kwamba tunaweka taa, lakini kama kuna suala la ziada hilo tutalipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuagiza tu Meneja wa maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge aende akayaangalie na alete mapendekezo kama hizo taa ni muhimu basi Serikali itaweka ili kuokoa maisha ya wananchi wa Tarime na Watanzania wote ambao wanapita hapa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali hayo, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula aulize swali lake.

Na. 372

**Ahadi ya Kuweka *Block Fam* ya Korosho – Kalangasi – Igalula**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuweka *block farm* ya korosho pamoja na kupeleka trekta Kalangasi – Igalula?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui inaendelea na jitihada za kutafuta eneo linalofaa kwa ajili ya kuanzisha *block farm* ya shamba la korosho katika Jimbo la Igagula. Kupatikana kwa eneo hilo kutawezesha utekelezaji wa ahadi iliyotolewa na Serikali ya kuanzisha shamba hilo ikiwa ni pamoja na kupima afya ya udongo na kupeleka trekta katika Kijiji cha Kalangalasi kama nyenzo ya kazi zitakazofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Ofisi ya Mheshimiwa Mbunge isaidie jitihada zinazoendelea za kutafuta eneo ambalo litatumika kuanzisha *block farm* ya zao la korosho katika Jimbo la Igagula.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant Daud Protas.

**MHE. VENENT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ofisi ya Mbunge haina eneo lakini Halmashauri ina eneo, Halmashauri ilikwishaandika kwenye Wizara kwamba Kalangalasi wametambua wajenge *block farm*. Je, ni lini Waziri pamoja na wataalam wake wapo tayari tuambatane nikamuoneshe hilo shamba ili alete huo mradi?

Swali langu la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Bashe ambaye alikuwa Naibu Waziri na sasa ni Waziri alifika Kalangalasi akaahidi trekta, sasa wakati ninyi mnajivuta vuta huko ni lini hilo trekta litakwenda kule ili itakapofika ule mradi msianze tena na kigezo kingine cha kutafuta trekta?*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amesimama namuona pale, Mheshimiwa Bashe majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nimshukuru kwanza Naibu Waziri kwa majibu aliyoyatoa na ninamshukuru Mheshimiwa Venant.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka tu niwe mkweli, ninamwomba Mbunge, Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Uyui na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora wakamalize mgogoro ulioko Kalangalasi. Kwa sababu kama Serikali tulikuwa tayari kutekeleza mradi, mradi ulizuiliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa hoja mbalimbali na Waziri wa Mazingira alishapelekwa pale mradi ukafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara ya Kilimo tuko tayari kuutekeleza Mradi wa Kalangalasi jana, Mkoa wa Tabora wakamalize mvutano ulioko kati ya wananchi wa Kalangalasi ambao wanautaka mradi wakati Ofisi ya Mkuu wa Mkoa haitaki mradi utekelezwe. Wakimaliza hilo tatizo sisi tutatekeleza hata kesho na mimi nipo tayari kwenda siku wakiwa tayari Mbunge akisema tu wamemaliza hilo tatizo mimi nitaenda pale na trekta lipo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Naibu wake wote wawili kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mohamed Said Issa Mbunge wa Konde aulize swali lake.

Na. 373

**Kuondoa usumbufu wa Kikodi wasafiri wa Zanzibar na Tanzania Bara**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawaondolea usumbufu wa kikodi wananchi wanaobeba vitu vya matumizi binafsi wanaposafiri kati ya Zanzibar na Tanzania Bara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Sillo kwa niaba ya Waziri wa Fedha, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaosimamiwa na *TRA* kwa wasafiri kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ni kwamba, wasafiri wanaobeba vitu kwa matumizi binafsi hawalipishwi kodi ya vitu hivyo, isipokuwa changamoto hujitokeza pale wafanyabiashara wengine wasiokuwa waaminifu kutumia nafasi hiyo kubeba vitu vya biashara na kutokutaka vitozwe kodi. Wafanyabiashara hao wanavipitisha bandarini wakiwa wamevigawanya kwa abiria au kutumia wabeba mizigo wa bandarini ili kuvitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya bidhaa hizo kupita maeneo ya bandari mfanyabiashara husika anakabidhiwa vitu vyake bila kuvilipia kodi. Kutokana na utaalam na weledi wa Maafisa Forodha, mazingira kama haya ya wafanyabiashara hao hugundulika, mchezo huo ukigundulika wafanyabiashara hutelekeza mizigo hiyo bandarini na kuanza kutoa lawama kwa *TRA* kwamba wanashikilia bidhaa za wasafiri kitu ambacho hakina ukweli wowote.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge zungumzeni taratibu, Mheshimiwa Waziri anajibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuleta maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, je, ni mizigo yenye thamani kiasi gani inaruhusiwa kama matumizi binafsi ya nyumbani?

Swali la pili, kwa wale ambao wanaharibu nia thabiti ya utaratibu huu. Je, Serikali itachukua hatua gani ili iwe funzo kwa wengine wakiwemo Maafisa wa Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kama jibu la swali la kwanza unalo utajibu, kama huna utajibu kwa maandishi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mohamed kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la kwanza kubwa ni kutumia tu busara na hekima kwa sababu mtu anaweza akawa na *TV* moja au ana chakula cha watoto au ana vyombo vyake vichache vya ndani nadhani ni kutumia tu busara kwa watumishi wa *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, ili kukomesha tabia hii kwa Watumishi wa Umma taratibu zipo za kinidhamu na za kisheria, lakini kwa wafanyabiashara pia mizigo hiyo hutozwa kodi na hutaifishwa pale ambapo wameweka mizigo iliyozidi matumizi ya kawaida. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Daniel Sillo kwa majibu hayo ya maswali ya Wizara ya Fedha. Tunamalizia Wizara ya mwisho, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, aulize swali lake.

Na. 375

**Mgogoro wa Ardhi kati ya Hifadhi na Wananchi - Kondoa**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kushughulikia mgogoro wa ardhi kati ya Hifadhi na wananchi wa Mtaa wa Mangoroma?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro kati ya wananchi wa Kata ya Serya - Mtaa wa Mongorona na Pori la Akiba Swagaswaga ni miongoni mwa migogoro 975 iliyokuwa inafanyiwa kazi na Kamati ya Mawaziri nane (8) wa kisekta. Mgogoro huo unahusisha wananchi wa Mtaa wa Mongoroma kuingia ndani ya mipaka ya Pori la Akiba Swagaswaga kwa shughuli za kilimo, ufugaji na makazi. Aidha, kaya zilizoingia ndani ya eneo la Pori ni 86 kwa vitongoji vitatu vya Magangati, Surugu na Matembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutafuta suluhu ya mgogoro tajwa, wananchi wamemegewa eneo lenye ukubwa wa hekta 3,597.76 kutoka katika Pori la Akiba Swagaswaga. Hadi sasa zoezi la usimikaji vigingi limekamilika, ambapo jumla ya vigingi 250 vimesimikwa kuzunguka pori hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua hizo, mgogoro huu tayari upo kwenye mpangokazi wa utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri ambapo hatua inayofuata ni kufanya marejeo ya tangazo la Serikali kulingana na mipaka iliyorejewa, kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na uongozi wa Mkoa na Wilaya kutoa tamko la kuwaondoa wananchi ndani ya eneo la Hifadhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Juma Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nioneshe masikitiko yangu makubwa sana juu ya majibu haya ya Serikali kupitia Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaonesha masikitiko hayo kwa sababu kwanza niseme majibu haya ni ya uwongo, naomba niseme ni ya uwongo kwa sababu swali langu *specific* linasema Mtaa wa Mongoroma. Hakuna hekta hata moja aliyopewa mwananchi kwenye eneo hili na haya majibu ya Wizara ya Maliasili ndiyo yalipelekea mimi kumuomba Mheshimiwa Rais kwenye mkutano wa hadhara atume Wizara ya Ardhi kwenda kuwasikiliza hawa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kumweleza Naibu Waziri ambaye alikuwepo kipindi kile Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, akatoa maelekezo Waziri wa Ardhi afike Mongoroma kwenda kuwasikiliza hawa wananchi, niliyakataa majibu haya na tayari *DC* wangu Dkt. Mkanachi alikwishakupeleka tangazo kwa wananchi waondoke tukazuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijiwe swali langu na Wizara ya Ardhi kwamba ni lini watakwenda kwa kufuata maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuwasikiliza wananchi wa Mongoroma?

**MWENYEKITI:** Wizara ya Maliasili au Wizara ya Ardhi?

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Wizara ya Ardhi inijibu maelekezo alipewa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Rais, ni lini atakwenda kumaliza huu mgogoro kwa sababu haya majibu ndiyo niliyakataa na nikamweleza Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais akatoa maelekezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kama una majibu, kama hauna Waziri wa Ardhi atajibu hilo swali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, mgogoro huu umeshughulikiwa na timu ya Mawaziri wa Kisekta. Kwa hiyo fursa bado iko wazi, kama

anaona hajaridhishwa Serikali itaendelea kuwasiliana nae, Wizara ya Ardhi imesikia, tutakaa nae ili tuweze kupata suluhu kwa jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo. Waheshimiwa Wabunge tumemaliza kipindi chetu cha maswali na sasa ni wakati wa matangazo mbalimbali na hapa nina matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kwanza, tunao wageni waliokaa Jukwaa la Mheshimiwa Spika, kuna mgeni wa Mheshimiwa Spika, Ndugu Judith Masunda Kileo, kutoka London nchini Uingereza aliyesoma naye Zanaki Sekondari ameambatana na ndugu yake Lenity Exaud Muro, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Spika wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima Mbunge ambae pia ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum tuna Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe – Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Amon A. Mpanju - Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae Ndugu Sophia Simba - Mwenyekiti wa Bodi ya Magavana wa Ustawi wa Jamii, karibuni sana. Mheshimiwa Sophia Simba bado Wabunge wanakupenda sana, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae ACP. Faithat Suleiman - Mratibu wa Dawati la Jinsia Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae Dkt. Joyce Nyoni - Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, karibu sana. *(Makofi)*

Tunae Dkt. Salma Mahmoud - Mkuu wa Skuli ya Afya Chuo Kikuu cha Serikali Zanzibar, karibu sana, *(Makofi)*

Tunae Dkt. Bakari George - Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Dkt. Naike Moshi, Mkurugenzi *Women in Management Africa (Wima)*, karibu sana. *(Makofi)*

Kuna Ndugu Laurent Makko, Mratibu wa Shirika la Ujamaa *Community Resource Team (UCRT)*, karibu sana. *(Makofi)*

Kuna Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mbunge na Waziri Mstaafu. Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Wakili Methusela Gwajima, Mume wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Zeyana Mohamed Ali, Mtoto wa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi. *(Makofi)*

Pia tunaye Ndugu Rehema Kambaga, Mke wa Katibu Mkuu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye Jukwaa hilo la Mheshimiwa Spika, pia tuna wageni 15 wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge, ambao ni wawekezaji kutoka Marekani na Israel ambao ni Ndugu Kum Ja Lee – USA, Ndugu Omer Shalev - Israel, Ndugu Mouli Somayajula – USA, Ndugu Oren Flax – Israel, Ndugu Jeremy Ezra – Israel, Ndugu Elia Mirevski – USA, Ndugu Farshid Hakim Yar – USA, Ndugu Teresa A. G. Christ- USA, Ndugu J. P. Gomez – USA, Ndugu Jachinda Kihwelo – USA, Ndugu Ernest Omalla - Tanzania, Ndugu Sospeter Galus Omollo – Tanzania, Ndugu John Masanja – Tanzania, Ndugu Issa Kipemba – Tanzania na Meja Jenerali Mstaafu Philip Churn – USA. Karibuni sana wageni katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula, mdogo wake kutoka Nyamagana Jijini Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Mgeni wa Mheshimiwa Cecilia Paresso, Ndugu yake kutoka Babati Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Riziki Lulida, wenye mahitaji maalumu na mkalimani wao, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni watoto wake na binamu yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro, Viongozi wa CCM, ABAMWE na Waheshimiwa Madiwani kutoka Ngara Mkoa wa Kagera. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma ambao ni viongozi wa Jumuiya ya UVCCM Kata kutoka Hanang Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, ambao ni wanakwaya wa Kwaya ya Moravian Vwawa Kati kutoka Mkoa wa Songwe. Karibuni wanakwaya wetu. *(Makofi)*

Kuna wageni 42 wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambao ni Mkurugenzi, Waheshimiwa Madiwani na Wakuu wa Idara kutoka Missenyi Mkoa wa Kagera. Karibuni sana wageni wetu kutoka huko Kagera. *(Makofi)*

Tuna wageni 99 wa Mheshimiwa Venant Daud, watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui Mkoa wa Tabora. Karibuni sana wageni wetu kutoka huko Tabora. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tuna Wanafunzi 70 na Walimu watano kutoka Shule ya Awali na Msingi *Royal Feat* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka *Royal Feat*. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 55 wa Chuo cha Mipango na Maendeleo ya Vijijini kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Ahsanteni sana wageni wetu wote, tunawakaribisha katika Bunge letu.

Katibu, tuendelee.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, namkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ili aje kutuletea Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Mheshimiwa Waziri, karibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba hotuba yangu iingizwe kwenye Hansard za Bunge kwa kumbukumbu kama ilivyowasilishwa kwenye kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa mwaka 2023/2024 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo ili kuwasilisha hotuba yangu. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kutuongoza vyema kwa mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali kwa kipindi hiki cha miaka mitatu ya uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Natambua kuwa Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa ya kuona hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini inaimarika na utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii unafanyika kwa kasi kubwa na ufanisi. Ninamuahidi kwamba nitaendelea kutimiza majukumu yangu kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafika kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, kuhimiza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi pamoja na kuzingatia haki za wazee, wanawake, wanaume na watoto katika jamii. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo anayoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi ya Jamii. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 15 Aprili, 2024 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu. Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inaahidi kuendelea kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na weledi katika kuendelea kuongoza vikao vyetu vya Bunge. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uchapakazi wake uliotukuka. Mwenyezi Mungu awajalie utashi, weledi na ufanisi mkubwa katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, Mbunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mbunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Nawatakia majukumu mema katika kuliongoza Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Mbunge...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tupunguze sauti, Mheshimiwa Waziri aweze kuwasilisha vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, Mbunge, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa

ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mbunge, Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Utekelezaji wa Jukwaa la Kizazi chenye Usawa kwa jitihada zake katika kufikia kizazi chenye usawa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao unaiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Wizara itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha mafanikio katika nyanja za maendeleo na ustawi wa jamii yanafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge na Makamu wake, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia wenye lengo la kuboresha huduma za ustawi na maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pole kwa Serikali na Chama cha Mapinduzi kufuatia kifo cha Ndugu, Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ndugu Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninatoa pole kwako, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali na Mheshimiwa

Ahmed Yahaya Abdul-wakil, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa pole kwa wakazi wa Wilaya ya Hanang pamoja na wananchi wa Mkoa wa Manyara kwa ujumla kufuatia maporomoko ya matope yaliyotokea Desemba 3, 2023 kutokana na mvua kubwa na kusababisha vifo, majeruhi, upotevu wa mali na makazi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/2024, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele mbalimbali vyenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii na vipaumbele hivyo nimevitaja kwenye Aya ya 16 ya Kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 8.5 kutoka kwenye vyanzo kadhaa ambavyo nimeviainisha kwenye Aya ya 17 ya Kitabu changu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili 2024, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 3.1, sawa na asilimia 37.4 ya makadirio ya mapato kama mchanganuo ulivyo katika Jedwali Namba moja, ukurasa wa tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya mapato kunatokana na sababu mbalimbali zikiwemo; wanafunzi kutoripoti wote kama ilivyokadiriwa, kutokukamilika kwa malipo ya Ada ya Malazi kwa wanafunzi vyuoni, kuchelewa kuanza kwa utaratibu wa usajili na utambuzi wa wafanyabiashara ndogondogo

ambao umeanza mwezi Machi, 2024. Pia, ufutaji wa usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 14, kutokana na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia shughuli za mashirika hayo. Wizara inafanya jitihada kuhakikisha makusanyo yote yaliyobaki tunayakusanya katika kipindi hiki kilichobakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha shilingi 74,223,193,000. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 43.6, ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 26.5 ni fedha za matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi bilioni 17.08, ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 30.5 kilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo shilingi bilioni 26.8 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3.7 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia Aprili, 2024, Wizara imepokea jumla ya shilingi 30,114,668,978.89 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 68.9. Kati ya Fedha zilizopokelewa, shilingi 15,640,771,358.89 ni matumizi mengineyo na shilingi bilioni 14.47 ni mishahara. Aidha, kufikia Aprili, Wizara imepokea fedha za maendeleo shilingi 4,949,880,000, sawa na asilimia 16.2. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,883,800,000 ni fedha za ndani na shilingi 66,080,000 ni fedha za nje. Maelezo kwa kina yapo kwenye Jedwali namba mbili, ukurasa wa 11. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ulilenga kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo, utambuzi na uratibu wa makundi maalum, kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, kuboresha huduma za ustawi wa jamii, kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi, kuratibu utekelezaji wenye ufanisi wa mashirika yasiyo ya kiserikali na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya jamii. Dhana ya maendeleo ya jamii ni kuwashirikisha wananchi kujiletea maendeleo

yao wenyewe kwa kutumia rasilimali zilizopo na kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele vyao, ambapo maafisa maendeleo ya jamii hushirikiana nao kwa kuwapatia utaalamu wa namna ya kufanikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, imeendelea kutekeleza Kampeni endelevu ya Ujenzi wa Nyumba Bora zenye gharama nafuu katika maeneo yenye makazi duni inayotumia mifumo ya asili ya kusaidiana miongoni mwa jamii. Kupitia kampeni hiyo, idadi ya nyumba bora imeongezeka kutoka nyumba 5,732 kwa 2022/2023 hadi nyumba 11,883 kufikia Aprili, 2024, sawa na ongezeko la nyumba 6,151. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine iliyotekelezwa kupitia kampeni hii ni jumla ya miradi 29,641 kama ilivyoelezwa kwenye Aya wa 26 ya ukurasa wa 13 mpaka wa 14 wa Kitabu changu na kama ilivyotajwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI wakati akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri, uwepo wa maafisa maendeleo ya jamii wa kutosha, utaongeza kasi na ari ya wananchi kushiriki na kumiliki shughuli za maendeleo ikiwemo kubuni miradi mbalimbali. Shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa kuongeza ajira 762 za maafisa maendeleo ya jamii kwa mwaka 2023/2024 hivyo, kuwezesha kufikia idadi ya maafisa 3,675, sawa na asilimia 69.4 kati ya 5,296 wanaohitajika. Jambo hili litachochea zaidi uwajibikaji ngazi ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi ambao ulianza 2022/2023 na unaolenga kuchochea hamasa na utayari wa wananchi kushiriki kwenye maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mpango huu, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imefanya mafunzo kwa wataalamu 1,146 ikijumuisha watalaamu kutoka Sekretarieti za Mikoa

na Mamlaka za Serikali za Mitaa na washiriki wengine. Kufikia Aprili, 2024 jumla ya viongozi na wataalamu 1,979 wameweza kupatiwa mafunzo kuhusu mpango huo. Maelezo zaidi turejee Aya ya 24, ukurasa wa 28. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia ina jukumu la kuzalisha wataalamu wanaotekeleza afua za maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii ili kuweza kuongeza idadi ya wataalamu hawa katika Sekta hii. Wizara imefanya mapitio ya mitaala inayotumika kutoa mafunzo ya taaluma kwa ngazi ya Astashahada hadi Stashahada. Mitaala hiyo imeandaliwa ikilenga kuwapa wahitimu maarifa na ujuzi unaoakisi mahitaji ya soko la ajira, mahitaji ya Sekta na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Kufikia Aprili, 2024, mitaala hii iliyoboreshwa na inatumika katika jumla ya vyuo 67 vinavyotoa mafunzo ya programu za maendeleo ya jamii, vikiwemo vyuo vya watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais, kwa kutupatia fedha za kuboresha miundombinu ya vyuo, hali iliyotuwezesha kuongeza idadi ya udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 5,255 mwaka 2022/2023, hadi 5,499 kwa mwaka 2023/2024. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 4.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia vyuo vyake inatekeleza programu ya uanagenzi kwa wanafunzi waliohitimu mafunzo katika vyuo vyetu. Wahitimu hawa huunganishwa na kampuni, mashirika na taasisi mbalimbali kwa lengo la kuwapa ujuzi na stadi mbali mbali zitakazowawezesha kukabiliana na changamoto za soko la ajira. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya wanafunzi 2,200 walijiunga na *program* hiyo, ambapo kati yao wanafunzi 1,104 sawa asilimia 50.2 walifanikiwa kuhitimu. Maelezo kwa kuna kuhusu *program* hizi yapo aya ya 33 hadi 36 ya kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutambua na kuratibu wa shughuli za kiuchumi za makundi maalum; habari hii ipo ukurasa wa 21 mpaka wa 27 wa kitabu change; Wizara imeendelea kutambua, kuratibu na kusimamia mipango mbalimbali ya kuwezesha na kuendeleza makundi maalum katika mambo mbalimbali zikiwemo

shughuli za kiuchumi. Makundi yanayolengwa ni wafanyabiashara ndogo ndogo halali wote, mfano wakiwemo machinga, mama/baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji, wasusi, wanaofanya biashara za kushona nguo na wengine mbali mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi haya yanakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kutofikia fursa za kiuchumi kama kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha, kupata maeneo wezeshi ya kufanyia biashara zao pamoja na kuwepo kwa ofisi zao rasmi za kuwawezesha kukutana kujadili mambo yao. Katika kuwaondolea changamoto hizo Serikali imekamilisha mpango wa kutoa mikopo kwa kundi ambapo tarehe 06 Mei, 2024 Wizara imeingia mkataba wa makubaliano na Benki ya *NMB.* Kupitia makubaliano haya katika mwaka 2023/2024 Serikali itaipatia Benki ya *NMB* kiasi cha shilingi bilioni 18.5 kwa ajili ya kutoa mikopo yenye riba nafuu ya 7%.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI inafuatilia maendeleo ya ujenzi wa ofisi za wafanyabiashara ndogo ndogo katika ngazi ya mikoa yote. hadi sasa mikoa tisa imekamilisha ujenzi wa ofisi hizo na mikoa 17 ujenzi upo katika hatua mbali mbali. Turejee jedwali namba tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki na maendeleo ya mtoto, habari hii ipo ukurasa wa 27 hadi 41 wa kitabu changu. Wizara inalo jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya mtoto pamoja na upatikanaji wa haki za msingi kwa mtoto. Haki za mtoto ni pamoja na haki ya kuishi, kulindwa dhidi ya vitendo vya ukatili, kuendelezwa kupitia vipaji na elimu, kushiriki katika masuala yanayomhusu kulingana na umri wake na kutobaguliwa kwa namna yoyote ile. Mtoto anahitaji malezi bora yenye kuzingatia haki na mahitaji yake ya msingi hasa katika kipindi cha umri wa miaka 0 – 8 wakati ubongo wake unakua kwa kasi ya asilimia 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, baadhi ya watoto wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na malezi duni na vitendo vya ukatili kutoka kwa ndugu wa karibu, familia na jamii inayowazunguka. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za

kisekta imeendelea kuboresha mifumo ya Kisheria ili kuimarisha ulinzi na usalama wa mtoto kwa kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Mtoto Sura ya 13, Sheria ya Ushahidi Sura ya 6 na Sheria ya Makosa ya Mtandao Sura ya 443.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu Sheria ya Ushahidi Sura ya 6 imefanyiwa marekebisho katika Kifungu cha 127(2) ili kuhakikisha maslahi ya mtoto yanalindwa, hasa pale anapotoa ushahidi wake mahakamani. Katika kuwalinda watoto dhidi ya ukatili mitandaoni, Wizara ilizindua Kampeni ya Kitaifa ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto Mtandaoni tarehe 10 Februari mwaka huu Jijini Dodoma. Kwa kina maelezo yapo ukurasa wa 29 aya ya 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na suala zima la mmomonyoko wa maadili, Serikali imeunda Kamati maalum inayojumuisha Wizara yangu pamoja na Wizara nyingine za kisekta, na taasisi za Serikali zilizo chini ya wizara hizi. Lengo la kamati hii ni kubaini vyanzo vya mmomomyoko wa maadili kwa ujumla ukiwemo ule wa watoto, kutambua ukubwa wa tatizo na kuandaa mpango kazi wa kutekeleza ili kuzuia na kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto za malezi na makuzi duni ya watoto wenye umri kati ya miaka 0 – 8 Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia programu mbalimbali zikiwemo Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ya mwaka 2021/2022 inakwenda mpaka 2025/2026 inayojulikana kama *MMMAM***.** Aidha, programu hii pia inamlenga kijana balehe kwa kumpatia elimu ya uelewa wa masuala ya makuzi na kujikinga na athari mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia Aprili, 2024 Serikali kwa kushirikiana na Wadau imejenga uelewa kuhusu programu hiyo kwa Maafisa 3,123 wa Serikali na wadau wengine katika mikoa yote 26 na halmashauri zake zote 184. Kupitia mikutano ya utambulisho wa programu hii, washiriki waliweza kuainisha vipaumbele vya *MMMAM* kwa ajili ya kuingizwa kwenye mipango na bajeti ya mikoa na halmashauri kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na viongozi wa dini imeandaa kitabu cha malezi ya watoto kwa muktadha wa dini ya kiislam na kikristo kinachoitwa "Wazazi wangu, kesho yangu''. Maudhui ya Kitabu hicho yanalenga kuimarisha malezi bora kwa watoto na familia kwa muktadha wa dini za kiislamu na kikristo. Wizara ina jukumu la kusimamia ukuaji chanya wa watoto kupitia malezi ya familia pamoja na vituo vya kulelea watoto wadogo na wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha hili, Wizara imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo na watoto wachanga ambavyo vinatoa huduma ya uchangamshi wa awali unaowasaidia watoto kukua kimwili, kiakili, kiafya, kihisia na kimaadili na hatimae kuwaandaa kujiunga na elimu ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivi ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha ulinzi wa watoto na usalama wao wakati wazazi na walezi wao wakijihusisha na shughuli za kiuchumi badala ya kuwepo mitaani. Vituo hivi vina jukumu pia la kusimamia afya na lishe bora kwa watoto, pamoja na kuimarisha malezi yenye mwitikio na nafasi ya kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia Aprili, 2024 jumla ya vituo 3,862 vya kulelea watoto wadogo mchana vyenye jumla ya watoto 397,935 vimesajiliwa, na vituo vya kijamii 206 vyenye jumla ya watoto 11,675. Hatua hii imefanya kuwa na ongezeko la vituo 829 sawa na asilimia 21.5 na ongezeko la watoto 225,003 sawa na asilimia 55. Habari zaidi ipo aya ya 62 hadi 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika kuratibu utekelezaji wa programu hii Tanzania ilipewa heshima ya kuandaa Mkutano wa Kimataifa wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki. Mkutano huu ulifanyika kuanzia tarehe 11 hadi 14 Machi, 2024 Jijini Dar Es Salaam. Habari zaidi zipo aya ya 64 mpaka 66.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na mila na desturi zenye madhara kwa watoto na jamii, Wizara imeendelea kuratibu

utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa mwaka 2020/2021 mpaka 2024/2025. Takwimu za hali ya afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria Tanzania za mwaka 2022/2023 zinaonesha kupungua kwa vitendo vya ukeketaji nchini kutoka asilimia asilimia 10 kwa mwaka 2015/2016 hadi asilimia 8% kwa mwaka 2022/2023. Mikoa mitatu yenye kiwango cha juu zaidi cha ukeketaji ni Arusha asilimia 43, Manyara asilimia 43 na Mara asilimia 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania inaendelea kufanya vizuri katika udhibiti wa ukeketaji, Oktoba, 2023 Serikali ilipata heshima ya kuwa mwenyeji wa mkutano mwingine wa Kimataifa wa Kutokomeza Ukeketaji kwa nchi za wanachama wa Umoja wa Afrika. Taarifa zaidi ipo aya ya 72 hadi 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za ustawi wa jamii ukurasa wa 41 hadi 58 imeelezwa. Wizara ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kutoa huduma za Ustawi wa Jamii zikiwemo haki, matunzo na ulinzi kwa wazee, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, watoto walio katika mkinzano na sheria, huduma kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia na waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2024, jumla ya watoto 708,957 wanaoishi katika mazingira hatarishi wametambuliwa katika halmashauri zote nchini na kupatiwa huduma kuendana na mahitaji yao ikiwemo watoto 275,058 kusaidiwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau kupata vyeti vya kuzaliwa. Huduma zingine za ustawi kama huduma za mahabusu za watoto, huduma za mahakama za watoto, malezi ya kambo na kuasili na huduma za makao ya watoto utekelezaji wake kwa kina upo kwenye aya ya 80 mpaka 84 kwenye kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepanua wigo wa utambuzi wa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani kwa kuyafikia maeneo mengi zaidi ambayo ni masoko, vituo vya mabasi,

minada na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya shughuli za kiuchumi. Utambuzi huu, umewezesha kupata jumla ya watoto 8,372 kutoka katika halmashauri za mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali bado imeendelea kuwapatia watoto hawa huduma zikiwemo kuunganishwa na familia zao, mathalani 2,457. Pia kuwawezesha kujitegemea katika jamii 873 na 5,042 wanaendelea kupatiwa huduma kwenye makao ya Kulelea watoto nchini kote. Serikali kupitia wizara hii itaratibu wadau kuongeza kasi ya kuwaondoa watoto waishio na kufanya kazi mitaani sambamba na mkakati wa kuzia wasiingie kuishi na kufanya kazi mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia ni moja ya majukumu ya Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. kufikia Aprili, 2024 mashauri yaliyoshughulikiwa yalikuwa 31,380 ikilinganishwa mashauri 28,773 yaliyoshughulikiwa mwaka 2022/2023, ikiwa ni ongezeko la mashauri 2,607 sawa na asilimia asilimia 8.3. Natoa wito kwa viongozi wa dini zote kuendelea kutoa mafunzo kwa wanandoa wanaofunga ndoa na kwa vijana kupitia mikusanyiko ya vijana katika madhehebu yao ili kuwaandaa kubeba majukumu ya ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha huduma za msingi zinatolewa kwa wazee na watu wasiojiweza, Wizara imeendelea kutoa huduma za chakula, malazi, mavazi, matibabu na msaada wa kisaikolojia na kijamii katika makazi 13 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali, pamoja na wazee wanaoishi katika jamii. kufikia Aprili, 2024 wazee wasiojiweza 240 wakike 95 na wakiume 145 walihudumiwa katika makazi ya wazee. Habari zaidi zipo aya ya 99 ukurasa wa 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejipanga kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi kwa kuleta mapendekezo ya kutunga sheria ya usimamizi wa watoa huduma za ustawi wa jamii katika nyanja zote za sekta ya umma na binafsi kwa lengo la kuwatambua, kuwasajili na kudhibiti ubora wa huduma wanazozitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika kutekeleza maagizo ya Kamati ya Mheshimiwa Rais ya kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Maboresho ya Haki Jinai, Wizara kwa kushirikiana na wizara za kisekta na taasisi nyingine ipo katika hatua ya kukamilisha uanzishwaji kisheria kwa idara ya ustawi wa jamii kama idara inayojitegemea ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mabadiliko ya sera ya wazee. Ambapo miongoni mwa maboresho yatakayozingatiwa ni pamoja na umuhimu wa jamii kujiandaa kabla ya uzee, huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia kwa wazee, miundombinu na mazingira wezeshi kwa wazee na uwezeshwaji wa wazee kwenye mabadiliko ya teknolojia kama *TEHAMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu bado inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa maafisa ustawi wa jamii 17,485 ambayo ni sawa na asilimia 94.6. Jedwali namba tano ukurasa wa 56 liechanganua zaidi takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa kibali cha kuajiri maafisa 350 watakaosambazwa kulingana na mahitaji na mchakato wa ajira umeshaanza. Nichukue fursa hii kumshuruku Mheshimiwa Rais kwa kutoa kibali cha ajira hizo. Vile vile napenda kumshukuru Waziri wa Ofisi ya Rais Utumishi Mheshimiwa George Simbachawene kwa ufuatiliaji wake hadi kufanikisha suala hili. Nakiri kuwa bado uhitaji ni mkubwa hivyo Serikali itaendelea kuongeza wataalamu hawa kadri uwezo wa ajira unavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wanawake, habari hizi zipo ukurasa wa 58 mpaka 80. katika eneo la maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wanawake, Wizara ina jukumu la kuhakikisha kuwa kuna usawa wa kijinsia katika jamii yetu, na kwamba wanawake wanawezeshwa kiuchumi ili kuweza kuchangia katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya familia na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kufanikisha hili Wizara inatekeleza Programu ya Kitaifa ya Kizazi Chenye Usawa ya Mwaka 2021/2022 – 2025/26 ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kinara wa utekelezaji wa eneo la haki na usawa wa kiuchumi. Moja ya mkakati wa kumkomboa wanamke ambao unazingatiwa katika programu ni kuhakikisha anapata muda wa kushiriki katika shughuli za kiuchumi ili kuchangia maendeleo ya familia na nchi kwa ujumla. Katika kufanikisha hili, Wizara imeweka mkazo katika utekelezaji wa afua ambazo zinalenga kumpa muda zaidi mwanamke zikiwemo, matumizi ya nishati safi, uanzishaji wa vituo vya kulelea watoto wachanga na wadogo na upatikanaji wa maji safi na salama. Maelezo kuhusu utekelezaji wa pogramu hizi kwenye kila sekta yameandikwa kwenye aya ya 112 mpaka 151.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuonesha dhamira ya Serikali katika kukuza usawa wa kijinsia, Wizara imeratibu wadau wa kisekta na kukamilisha hatua za kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 iliyozinduliwa tarehe 8 Machi mwaka huu. Sera hiyo imezingatia masuala mbali mbali kama mabadiliko ya tabianchi, ushirikishwaji wa wanaume katika jitihada za kuleta usawa wa kijinsia, matumizi ya teknolojia katika uzalishaji na mawasiliano, na ukatili wa kijinsia na ukatili wa mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ni fursa kwa wanawake kuweza kukutana na kujadili masuala mbalimbali wanayokabiliana nayo katika shughuli zao. majukwaa haya yameongeza kazi zenye staha kwa wanawake katika sekta rasmi na sekta isiyo rasmi. Vilevile kwa kufanikisha utambuzi na usajili wa vikundi vipatavyo 43,574 vya wanawake baada ya kukidhi vigezo vya kupata mikopo ya asilimia 10 inayoyotokana na mapato ya ndani ya halmashauri. Vikundi vilivyotambuliwa vina jumla ya wanachama 13,778,700 vinavyojishughulisha na ujasiliamali wa bidhaa na huduma mbali mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya majukwaa 3,391 yameanzishwa. inakamilisha maandalizi ya

mwongozo wa uundaji na uratibu wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ili kuyafanya yawe na ufanisi zaidi. Habari hii ipo aya ya 126.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ambao una lengo la kuwawezesha wanawake kwa kuwapatia mikopo ya fedha ili kujikwamua kiuchumi. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya shilingi milioni 77.5 zimerejeshwa kutokana na mikopo iliyotolewa kwa wanawake ikiwa ni jumla ya shilingi 664 zilizokopeshwa kwa wajasiriamali 104 kutoka kwenye vikundi 11 na wakopaji mmoja mmoja 14. Aidha Wizara kuanzia Julai, 2024 itarejesha mikopo hii kwa utaratibu utakaotangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa wanawake wote kuzingatia masharti ya mikopo kwa kufanya marejesho kwa mujibu wa mikataba. Aidha, ninatoa wito kwa halmashauri zote zinazodaiwa fedha zinazotokana na mfuko huu kurejesha mikopo yao kwa makubaliano yaliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta pamoja na wadau wengine ina jukumu la kuelimisha jamii kuachana na vitendo vya ukatili wa kijinsia. Juhudi zote katika eneo hili, mathalani kampeni, madawati ya jinsia kwenye vyuo na kwenye maeneo ya umma pamoja na ujumuishaji wa jinsia katika utumishi wa umma vimeelezwa kwa kina kwenye aya ya 134 hadi 140.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali, ukurasa wa 81 hadi 88. usajili, uratibu na ufuatiliaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali unalenga kuweka mazingira wezeshi kwa mashirika hayo kuendelea kutoa michango yao katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla kupitia miradi mbali mbali. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imesajili jumla ya mashirika 1,028 na kufanya jumla ya mashirika yote yaliyosajiliwa kufikia 10,538. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya mashirika 1,124 yamefuatiliwa. Aidha, mashirika 775 yalibainika kuwa na mapungufu, yakiwemo kutowasilisha kwa wakati ripoti za mwaka

kuhusu kazi zao na kutokulipa ada za usajili za mwaka. Wizara kupitia Ofisi ya Msajili, ilitoa onyo kwao na kuwataka kuzingatia matakwa ya Kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaratibu shughuli mbalimbali zikiwemo za mikataba ya ufadhili kwa mashirika yasiyo ya kiserikali. Wizara imetoa vibali vya mikataba 316 yenye thamani ya shilingi bilioni 377 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kisekta. Kila mwaka Wizara inaandaa taarifa ya mchango wa mashirika hayo katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2022 jumla ya Mashirika 1,257 yaliyowasilisha taarifa zao yalipokea kiasi shilingi trilioni 2.2 kutoka vyanzo mbali mbali vya fedha. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 1.9 zilitumika katika utekelezaji wa miradi kwenye afua za mazingira, afya, uwezeshaji jamii, ulinzi wa jamii, kilimo, elimu, utawala bora, maji, haki za binadamu na jinsia; na kiasi cha shilingi bilioni 289.9 zilitumika katika kulipa posho na mishahara, kodi za ujuzi, kodi za mishahara, michango katika hifadhi ya jamii na mfuko wa fidia wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kazi na huduma za mashirika haya zimeweza kutoa ajira kwa jumla kwa watu 9,974 ambapo, kati yao Watanzania ni 9,818 na Wageni 156. Manufaa Mengine ni kuchangia katika pato la Taifa kwa kulipa Kodi na michango mbalimbali kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie machache kuhusu uratibu wa Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto; Wizara imeendelea na jukumu la kuratibu utekelezaji wa Mpango wa kupunguza na kuondoa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto maarufu kama MTAKUWWA-I Mwaka 2017/2018 – 2021/2022). Mpango huu, ulilenga kuimarisha uchumi wa kaya pamoja na kuimarisha huduma za msaada wa waathirika wa vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tathmini iliyofanyika Oktoba 2022 imeonesha kupungua kwa ukatili wa kimwili kwa wanawake kutoka asilimia 40 mwaka 2015 hadi asilimia 27 mwaka 2022, na ukatili wa kingono umepungua kutoka asilimia 17 mwaka 2015 hadi asilimia 12 mwaka 2022. Aidha, vitendo vya ukeketaji vimepungua kutoka asilimia 10 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 8 mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendeleza juhudi dhidi ya ukatili wa wanawake na watoto, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Kisekta, imeandaa Mpango Kazi wa Taifa Awamu ya Pili wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA-II) kwa kipindi cha Mwaka 2024/2025 – 2028/2029) ambao tumeuzindua juzi tarehe 15 Mei, 2024. Maboresho ya mpango huu yameelezwa aya ya 173 hadi 175.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machache kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Arusha na Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Kijitonyama Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hizi zina jukumu kubwa la kutoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii kwa ngazi za Cheti, Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Aidha, majukumu mengine ya Taasisi hizi ni pamoja na kufanya utafiti na kutoa huduma za ushauri elekezi katika nyanja zinazo shabihiana na taaluma wanazotoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2023/2024, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeongeza idadi ya udahili wa wanafunzi kutoka 2,918 mwaka 2022/2023 hadi kufikia wanafunzi 3,019 katika mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la 3.5%, na Habari hii iko kwenye Jedwali Na. 7 ukurasa wa 93. Taasisi inaendelea kuboresha mafunzo na kutoa wahitimu wenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, udahili wa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2023/2024, umeongezeka

kufikia 3,039 ikilinganishwa na wanafunzi 2,966 mwaka 2022/2023 na hili ni ongezeko la wanafunzi sawa na 2.5%. Taarifa kwa kina nayo iko Jedwali Na. 8 Ukurasa wa 94. Kwa ujumla maelezo ya kina kuhusu programu za Taasisi hizi mbili yanaendelea kupatikana Ukurasa wa 94 hadi 102.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maendele, nimeeleza ukurasa wa 102 hadi 104 kwamba, kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Wizara imepokea fedha za ndani za maendeleo kiasi cha bilioni 4.88, kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambazo shilingi bilioni 2 zilienda eneo hili, utekelezaji wa shughuli za programu ya kizazi chenye usawa shilingi bilioni 2.48 zilienda eneo hili na Mradi wa Huduma za Ustawi wa Jamii shilingi milioni 400. Maelezo ya kina kuhusu mgawanyo wa fedha hizi kwenye utekelezaji yapo aya ya 194 nadi 198.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepokea fedha za nje kiasi cha shilingi milioni 66 kwa ajili ya kufanya kampeni ya ulinzi na usalama wa mtoto mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niseme kuhusu Vipaumbele vya Wizara na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2024/2025; katika Mwaka wa Fedha ujao 2024/2025, Wizara kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake itatekeleza vipaumbele sita (6) ili kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo:-

(i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa Ngazi ya Msingi;

(ii) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia na kutokomeza vitendo vya ukatili, uwezeshaji wanawake kiuchumi, upatikanaji wa haki, ulinzi na malezi chanya ya watoto;

(iii) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za msingi za ustawi wa jamii;

(iv) Kutambua, kuratibu na kuendeleza Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo;

(v) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na

(vi) Kuimarisha ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara kwa mwaka 2024/2025 imekadiria kutumia kiasi cha shilingi 67,905,259,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 47,487,079,000 ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo shilingi 21,650,426,000 ni Fedha za Mishahara na shillingi 25,836,653,000 ni fedha za uendeshaji wa ofisi. Aidha, shilingi. 20,418,180,000 ni fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo shillingi 18,025,673,000 ni fedha za ndani na shillingi 2,392.507,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2024/2025 ni pamoja na: -

(a) Eneo la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi kiasi cha shilingi bilioni 3.2 zimetengwa;

(b) Katika eneo la kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kiasi cha shilingi bilioni 3.15 kimetengwa;

(c) Katika eneo la kutambua na kuratibu shughuli za kiuchumi za Makundi Maalum hususan wafanyabiashara ndogondogo, kiasi cha shilingi bilioni 10.5 kimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kuongeza mitaji na kuboresha shughuli zao za kiuchumi;

(d) Kwenye eneo la huduma za ustawi wa jamii na watoto kwa ujumla wake shilingi bilioni 1.2 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za marekebisho ya tabia kwa

watoto waliokinzana na sheria; kufuatilia utoaji wa huduma katika Makao ya Watoto, Vituo vya Kulelea Watoto wadogo Mchana na Watoto Wachanga; Kukarabati Shule ya Maadilisho ya Upanga na Mtwara; na Kuendeleza ujenzi wa Mahabusu ya Watoto Mwanza;

(e) Katika eneo la ustawi wa Wazee wasiojiweza, shilingi bilioni 1.06 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma katika Makazi ya Wazee 13;

(f) Kwenye eneo la Taasisi na Vyuo, kiasi cha shilingi bilioni 2 kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, na Vyuo vitatu (3) vya Maendeleo ya Jamii vya Uyole, Rungemba na Buhare;

(g) Kuhusu eneo la Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na shughuli zake zote tumetenga shilingi bilioni 2.5;

(h) Katika eneo la maendeleo ya jamii tumetenga kiasi cha shilingi milioni 826.1 kwa ajili ya kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Kuamsha Ari ya Jamii kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi kwa mwaka 2022/2023 - 2025/2026 *(Bottom Up)* katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara; na

(i) Katika eneo la ufuatiliaji na tathmini, shilingi milioni 150 zimetengwa kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Taasisi, Vyuo na Vituo vya Ustawi wa Jamii vilivyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani. Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta mbalimbali. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi rafiki zikiwemo; Marekani, Japan, Ufalme wa Uingereza,

Ufalme wa Sweden, Jamhuri ya Watu wa China, Ufalme wa Norway, Falme za Nchi za Kiarabu, Italia, Ujerumani, Ubelgiji, Ufaransa, Canada, Ufalme wa Denmark, Ireland, Jamhuri ya Uswisi, Bangladesh na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo *UNICEF, UNFPA, UN-Women, WHO, UNDP, ILO, IOM, WFP, FAO, UNESCO* na UNHCR. Vilevile, ninashukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC),* Umoja wa Afrika *(AU),* Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* na Jumuiya za Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*. Pia ninayashukuru Mashirika ya Kimataifa ambayo ni: -Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mfuko wa *Abbott Fund*, *Global Fund na Hilton Condrad Foundation*. Aidha, nazishukuru Taasisi za Kifedha za hapa nchini zinazoshirikiana na Wizara ambazo ni pamoja na Benki ya *CRDB*, *NMB,* Benki ya Biashara Tanzania, Stanbic, Azania, *NBC, Equity*, Benki ya Watu wa Zanzibar, *Akiba Commercial Bank* na Benki ya Mkombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayashukuru Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi na Mashirika ya Dini. Mashirika hayo ni pamoja na; *World Vision, PACT Tanzania, The Aga Khan Foundation, Foundation for Civil Society, HelpAge International, Compassion International, Responsible Organization Tanzania, Both Ends Believing, Safe Society Platform Tanzania, Children in Crossfire, Care International Tanzania, Railway Children Tanzania, WiLDAF, ICS, TAWLA, TAYOA, LSF, SOS Children's Village Tanzania, BRAC Maendeleo Tanzania, Plan International - Tanzania,* Kivulini, Uongozi wa Mgodi wa Geita, *FSDT, WFT, TANLAP, Save the Children, Equality for Growth (EfG), Landesa, CAMFED, CSEMA;* tunao *REPPSI, Amani Girls Home, Pelum Tanzania, LHRC,* Haki Elimu*, TWCC, TECDEN, EGPAF, FAGDI na* MEWATA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani zangu kwa Jumuiya za makundi mbalimbali, tuna jumuiya nyingi tunafurahi Wizara ya Maendeleo ya Jamii; Baraza la Wazee Tanzania, Chama cha Wazee Wanaume Tanzania, Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki

Tanzania, Machifu na Viongozi wa Kimila Tanzania, Umoja wa Wanawake Tanzania, Chama Cha Wanawake Wajane Tanzania, Jukwaa la ULINGO, Jumuiya ya Wazazi CCM, Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TAWIA, Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania na Umoja wa Mama na Baba Lishe Tanzania. Pia, naomba nizishukuru Klabu za Mpira wa Miguu Tanzania hususan Yanga, Simba, Azam na vikundi na kampeni za Kijamii kama SMAUJATA, SAWATA na *Malezi Bora Network* pamoja na vyombo vyote vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe shukrani zangu kwa viongozi na taasisi zetu za dini zikiwemo Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania *(CPCT),* Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania *(TEC),* Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania *(CCT)* na Kanisa la Waadventista Wasabato *(SDA)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe, Katibu Mkuu wa Wizara yangu ninayoiongoza kwa ushirikiano wake na kazi nzuri anayoifanya na Bw. Amon A. Mpanju, Naibu Katibu Mkuu kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Makamishna, Wasajili, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wataalam wote wa Wizara kwa utendaji wao mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba kuwashukuru Bodi na Menejimenti za Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, nawashukuru Wakuu wa Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wenu mzuri. Natoa shukrani kwa sekta zote na wananchi wote kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kupitia OR – TAMISEMI shukrani ziende kwa Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri zote na Wataalam wote chini ya Ofisi zao na Wadau wote wa sekta mbalimbali wanao hudumia katika maeneo yao pamoja na wananchi mmoja mmoja na mitandao yote ya habari za kijamii ambao wamekuwa wakifuatilia na kutoa

ushirikiano mkubwa kwenye utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu hasa kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia na kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuishukuru sana familia yangu, hususan mume wangu mpendwa Wakili Msomi Methusela Gwajima ambaye ninapopambana siku zote amesimama imara katika usawa wa kijinsia kunipa ushirikiano. Nakushukuru sana na Mungu akubariki mume wangu mpendwa, lakini na watoto wetu pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu kwa uvumilivu wao wa kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niombe fedha; Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2024/2025. Katika mwaka 2024/2025, Wizara imekadiria kukusanya kiasi cha shilingi 7,040,129,000 kutoka katika vyanzo mbalimbali, vyanzo hivyo ni pamoja na; Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii; Ada ya malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Usajili na Ada za mwaka za Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida; kwa mwaka 2024/2025, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha shilingi 47,487,079,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 25,836,653,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 21,650,426,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Miradi ya Maendeleo; kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia shilingi 20,418,180,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 18,025,673,000.00 ni Fedha za Ndani na shilingi. 2,392,507,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2024/2025, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) inaomba jumla ya shilingi 67,905,259,000.00 ili kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum www.jamii.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM, MHE. DKT. DOROTHY O. GWAJIMA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25. - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

***1. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka 2023/24 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/25. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2024/25.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo ili kuwasilisha hotuba yangu. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kutuongoza vyema kwa mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali kwa kipindi hiki cha miaka mitatu ya uongozi wake. Kipekee niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Natambua kuwa Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa ya kuona hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini inaimarika na utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii unafanyika kwa kasi kubwa na ufanisi. Ninamuahidi kwamba nitaendelea kutimiza majukumu

yangu kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu.

***3. Mheshimiwa Spika,*** pia, napenda kumpongeza na kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, kuhimiza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi pamoja na kuzingatia haki za wazee, wanawake, wanaume na watoto katika jamii. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo anayoyatoa.

***4. Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi ya Jamii. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 15 Aprili, 2024 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2024/25.

***5. Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya kipekee naomba nimpongeze **Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko (Mb)**, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kuaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu. Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inaahidi kuendelea kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake.

***6. Mheshimiwa Spika****,* ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na weledi wa kuendelea kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb),** Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uchapakazi wake uliotukuka. Mwenyezi Mungu awajalie utashi, weledi na ufanisi mkubwa katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***7. Mheshimiwa Spika****,* vilevile, nawapongeza **Mheshimiwa Dkt**. **Joseph Mhagama (Mb)**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na **Mheshimiwa Deo Mwanyika (Mb)**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Nawatakia majukumu mema katika kuliongoza Bunge.

***8. Mheshimiwa Spika,*** kipekee namshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mb),** Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

***9. Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii, kumshukuru **Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb),** Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Utekelezaji wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa kwa jitihada zake katika kufikia kizazi chenye usawa nchini. Chini ya uenyekiti wake, Kamati imeweza kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa (Tanzania Generation Equality Programme - TGEP, 2021- 2026) inayoainisha afua muhimu zitakazo tekelezwa na Wizara za Kisekta na kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeachwa nyuma katika maendeleo na ujenzi wa Taifa letu.

***10. Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao unaiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Wizara itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha mafanikio katika Nyanja za Maendeleo na Ustawi wa Jamii yanafikiwa.

***11. Mheshimiwa Spika***, kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya **Mwenyekiti Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq (Mb)** na **Makamu wake, Mheshimiwa Riziki Said Lulida (Mb)** kwa ushauri na

maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia wenye lengo la kuboresha huduma za ustawi na maendeleo ya jamii.

***12. Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa pole kwa Serikali na Chama cha Mapinduzi kufuatia kifo cha Ndugu, **Ally Hassan Mwinyi** aliyekuwa Rais wa awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ndugu **Edward Ngoyai Lowassa** Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nitoa pole kwako, Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu **Mheshimiwa Francis Leonard Mtega** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali na **Mheshimiwa Ahmed Yahaya Abdul-wakil** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani Zanzibar.

***13. Mheshimiwa Spika***, napenda pia kutoa pole kwa wakazi wa Wilaya ya Hanang' pamoja na wananchi wa Mkoa wa Manyara kwa ujumla kufuatia maporomoko ya matope yaliyotokea Desemba 3, 2023 kutokana na mvua kubwa na kusababisha vifo, majeruhi, upotevu wa mali na makazi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

***14. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/24, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/25.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24

***15. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Mpango Mkakati pamoja na Makubaliano ya Kimataifa na Kitaifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii nchini. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee

(2003), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008) na Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023). Vilevile, katika kuandaa mpango na bajeti, Wizara imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020, Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals, 2030); na Agenda ya Afrika Tuitakayo (2063). Aidha, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ahadi za Nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum – GEF, 2021 – 2026).

***16. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele mbalimbali vyenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii katika maeneo yafuatayo: -

i) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi (Generation Equality Forum - GEF);
ii) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA);
iii) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi wa mwaka 2022/23 - 2025/26 (Bottom Up);
iv) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo;
v) Kutambua na kuratibu Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo ili kuboresha mazingira ya biashara zao;
vi) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii;
vii) Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum ikiwemo huduma za msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;
viii) Kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa haki za watoto na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee;

ix) Kuimarisha mifumo ya malezi, ulinzi na maendeleo ya watoto na familia; na
x) Kuimarisha utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili mchango na ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya taifa uweze kutambulika na kuwa na tija kwa Jamii.

**Mapato na Matumizi ya Fedha za Wizara (Fungu 53)**

***17. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 8,500,000,000.00** kutoka kwenye ada za wanafunzi, uuzaji wa Mitaala ya kufundishia fani za Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii pamoja na malipo ya hosteli katika vyuo nane (8). Vyanzo vingine ni mapato ya ada ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ada za mwaka na faini kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 pamoja na marekebisho yake na mapato mengineyo (Fedha za mwaka uliopita zinazorejeshwa). Hadi kufikia mwezi Aprili 2024, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,184,370,155.50** sawa na asilimia **37.46** ya makadirio ya mapato kama inavyoonesha katika ***Jedwali Na. 1.***

**Jedwali Na. 1:** Ukusanyaji Mapato ya Ndani kwa Kipindi cha Julai, 2023 – Aprili, 2024

| Chanzo cha Mapato | Mapato Yaliyoidhinishwa | Makusanyo Halisi | Ufanisi (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| Ada ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 6,204,497,000 | 2,355,091,240.50 | 37.96 |
| Uuzaji mtaala wa maendeleo ya jamii | 40,000,000 | 51,500,000 | 128.75 |
| Ada ya Malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 600,000,000 | 167,231,239 | 27.87 |
| Ada ya usajili wa wafanyabiashara ndogondogo | 1,000,000,000 | 64,284,000 | 6.43 |

| Chanzo cha Mapato | Mapato Yaliyoidhinishwa | Makusanyo Halisi | Ufanisi (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| Usajili na Ada za mwaka za NGOs | 638,500,000 | 534,013,676 | 83.64 |
| Uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Ustawi | 15,000,000 | 10,500,000 | 70.00 |
| Mapato Mengineyo | 2,003,000 | 1,750,000 | 87.37 |
| **Jumla** | **8,500,000,000** | **3,184,370,155.50** | **37.46** |

***18. Mheshimiwa Spika,*** kutofikiwa kwa lengo la Makusanyo ya Mapato kunatokana na sababu zifuatazo; wanafunzi kutoripoti wote kama ilivyokadiriwa; Kumekuwa na upungufu wa wanafunzi 1,691 ambao hawajaripoti kutoka katika makadirio ya 7,190; Kutokukamilika kwa malipo ya Ada ya Malazi kwa wanafunzi vyuoni, Kuchelewa kuanza kwa utaratibu wa usajili na utambuzi wa wafanyabiashara ndogondogo ambao ulianza mwezi Machi, 2024 na hadi sasa tumeweza kukusanya kiasi cha shilingi 64,284,000 kati ya Shillingi Billioni moja. Aidha, ufutaji wa usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 14 kutokana na ukiukwaji wa Sheria na Kanuni na Miongozo inayosimamia shughuli za Mashirika hayo, imechangia kupunguza mapato.

***19. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inafanya jitihada kuhakikisha makusanyo yote yaliyobaki yanakusanywa katika kipindi kilichobakia ili kuweza kuongeza makadirio ya makusanyo yaliyokadiriwa kwa mwaka 2023/2024.

***20. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha **Shilingi 74,223,193,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 43,664,963,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 26,577,510,000.00** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 17,087,453,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, kiasi cha **Shilingi 30,558,230,000.00** kilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 26,800,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,758,230,000.00** ni fedha za nje.

***21. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2024, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 30,114,668,978.89** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 68.97. Kati ya Fedha zilizopokelewa, **Shilingi 15,640,771,358.89** ni Matumizi Mengineyo na Shilingi **Shilingi 14,473,897,620.00** ni Mishahara. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2024, Wizara imepokea Fedha za Maendeleo **Shilingi 4,949,880,000.00** sawa na asilimia 16.20. **Shilingi 4,883,800,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 66,080,000.00** ni Fedha za Nje, kama inavyoonesha katika ***Jedwali Na. 2.***

**Jedwali 2:** Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Zilizopokelewa Julai 2023 hadi Aprili 2024.

| Eneo | Fedha zilizoidhinishwa | Fedha zilizotolewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **Fedha za Matumizi ya Kawaida** | | | |
| Mishahara | 17,087,453,000 | 14,473,897,620 | 84.70 |
| Matumizi Mengineyo | 26,577,510,000 | 15,640,771,359 | 58.85 |
| **Jumla Ndogo (a)** | **43,664,963,000** | **30,114,668,979** | **68.97** |
| **Fedha za Miradi ya Maendeleo** | | | |
| Fedha za Ndani | 26,800,000,000 | 4,883,800,000 | 18.22 |
| Fedha za Nje | 3,758,230,000 | 66,080,000 | 1.76 |
| **Jumla Ndogo (b)** | **30,558,230,000** | **4,949,880,000** | **16.20** |
| **JUMLA KUU** | **74,223,193,000** | **35,064,548,979** | **47.24** |

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA (FUNGU 53)

***22. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ulilenga kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo, utambuzi na uratibu wa Makundi maalumu, kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, kuboresha huduma za ustawi wa jamii, kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, kuratibu utekelezaji wenye ufanisi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi

wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Uratibu wa utekelezaji wa majukumu haya ulifanywa na Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali.

**ENEO LA 1: MAENDELEO YA JAMII**

***23. Mheshimiwa Spika***, dhana ya maendeleo ya jamii ni kuwashirikisha wananchi kujiletea maendeleo yao wenyewe kwa kutumia rasilimali zilizopo na kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele vyao, ambapo maafisa maendeleo ya jamii hushirikiana nao kwa kuwapatia utaalamu wa namna ya kufanikisha shughuli za maendeleo yao. Kupitia dhana hii, Wizara imeendelea kutekeleza **programu ya Amsha Ari ya Jamii na Mpango wa Taifa wa kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi** ulioanza **2022/23** kwa ushirikiana wa jamii na Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kutoka katika Halmashauri zote nchini. Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wameendelea kutoa mchango wao katika kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Jamii kwa kupitia Programu ya Kuamsha Ari ya Jamii ambayo inalenga kukuza moyo wa uzalendo, kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo ikiwemo kampeni ya kitaifa ya ujenzi wa Makazi Bora.

***24. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, imeendelea kutekeleza Kampeni endelevu ya Ujenzi wa Nyumba Bora zenye gharama nafuu katika maeneo yenye makazi duni inayotumia mifumo ya asili ya kusaidiana miongoni mwa jamii. Mafanikio ya zoezi hili yanategemea ari ya wananchi, uongozi bora na juhudi za Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii. Kupitia kampeni hiyo, idadi ya nyumba bora imeongezeka kutoka 5,732 kwa 2022/23 hadi 11,883 kufikia Aprili, 2024, sawa na ongezeko la nyumba 6,151. ***Nitumie fursa hii kuzishukuru Wizara za kisekta ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR-TAMISEMI kwa ushirikiano kwenye kampeni hii.***

***25. Mheshimiwa Spika***, miradi mingine iliyotekelezwa kupitia kampeni hii ya Amsha Ari katika Mikoa yote ni pamoja na iliyo kwenye sekta mbalimbali mfano Afya na Elimu ambapo ni jumla ya

miradi **29,641** mathalani inayohusu ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya 6,761 (Zahanati 5,887 na Vituo vya afya 874), ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na madarasa ya awali 17,986 na madarasa ya shule za sekondari 4,894 kama **ilivyotajwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa (Mb),** Waziri wa OR TAMISEMI wakati akiwasilisha Bungeni makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/25. Ni dhahiri, uwepo wa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa kutosha utaongeza kasi na ari ya wananchi kushiriki na kumiliki shughuli za maendeleo ikiwemo kubuni miradi mbalimbali. Shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa kuongeza ajira 762 za Maafisa Maendeleo ya Jamii mwaka 2023/24 hivyo, kuwezesha kufikia idadi ya maafisa 3,675 (69.4%) kati ya 5,296 wanaohitajika jambo litakalochochea zaidi uwajibikaji ngazi ya msingi.

***26. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi ambao ulianza 2022/23 na unaolenga kuchochea hamasa na utayari wa wananchi kushiriki kwenye maendeleo. Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inatekeleza mpango huu kwa lengo la kuwezesha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo ngazi ya jamii na Taifa kwa kutumia rasilimali walizonazo katika kuibua changamoto, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

***27. Mheshimiwa Spika,*** kupitia mpango huu Wizara kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI imefanya mafunzo kwa wataalam **1,146** ikijumuisha watalaam kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na washiriki wengine, ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya viongozi na wataalam **1,979** wameweza kupatiwa mafunzo kuhusu mpango huo. Mafunzo hayo yalilenga kuchochea na kufanya mageuzi ya kifikra, mtazamo na utendaji wa wataalam ngazi ya Kata ili kuwezesha jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo katika maeneo yao na kujiletea maendeleo yao wenyewe. Miongoni wa wataalam waliopatiwa mafunzo ni Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Kilimo, Maafisa Mifugo na Maafisa Afya.

Mpango huo umeendelea kutekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Wizara za Kisekta zikiwemo Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Elimu na Afya kwa kusudi la kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa jamii katika ngazi za msingi.

***28. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Chama cha Wataalam wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Community Development Professional Association of Tanzania - CODEPATA) ilifanya kongamano la wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (Arusha International Conference Center - AICC) tarehe 20 – 22 Novemba, 2023. Kongamano lililenga kufanya tathimini ya mchango wa maendeleo ya jamii katika kuchochea na kukuza ari ya jamii kujiletea maendeleo endelevu pamoja na kubadilishana uzoefu na mbinu mpya zinazotumika katika kukabiliana na changamoto za jamii na kuwafanya wananchi kuwa kitovu cha maendeleo; kupokea na kujadili mifano mizuri ya kuwezesha wananchi na kujenga uwezo wa washiriki kupitia mada mbalimbali zinazohusiana na maendeleo ya jamii. Aidha, Kaulimbiu iliyoongoza kongamo hilo ni **"Sekta ya Maendeleo ya Jamii: Msingi Imara wa Uwezeshaji wa Wananchi."**

***29. Mheshimiwa Spika,*** Kongamano lilihusisha watu mbalimbali wakiwemo viongozi wastaafu wa serikali wataalam wa maendeleo ya jamii kutoka katika taasisi za Serikali na binafsi pamoja na wadau wa maendeleo. Katika kongamano hilo ulifanyika Mkutano Mkuu wa wataalam wa Maendeleo ya Jamii na maadhimisho ya miaka 60 ya Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na jumla ya Wataalam 700 walishiriki. Vilevile, kupitia kongamano hilo mafunzo mbalimbali yalitolewa kuhusu umuhimu na mchango wa maendeleo ya jamii katika kuwezesha wananchi kushiriki kwenye shughuli za maendeleo.

***30. Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu pia ina jukumu la kuzalisha wataalamu wanaotekeleza afua za maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii. Katika kuhakikisha kuwa wataalam wanaozalishwa na Taasisi na Vyuo wanakuwa bora na mahiri na wenye weledi wa

kutosha, Wizara imefanya mapitio ya Mitaala inayotumika kutoa mafunzo ya taaluma kwa ngazi ya Astashahada hadi Stashahada. Mitaala hiyo imeandaliwa ikilenga kuwapa Wahitimu maarifa na ujuzi unaoakisi mahitaji ya soko la Ajira, Mahitaji ya Sekta na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Hadi kufikia Aprili 2024, mitaala hii iliyoboreshwa inatumika katika jumla ya Vyuo 67 (12 vya Serikali na 55 binafsi) vinavyotoa Mafunzo ya Programu ya Maendeleo ya Jamii nchini.

***31. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais, kwa kutupatia fedha za kuboresha miundombinu ya vyuo hivyo hali iliyotuwezesha kuongeza idadi ya udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi **5,255** (Me 2,089 na Ke 3,166) mwaka 2022/23, hadi wanafunzi **5,499** (Me 1,966 na Ke 3,533) kwa mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la wanafunzi **244** (**4.6%).** Aidha, mwaka 2022/23, wanafunzi 4,978 (Me 1,875 na Ke 3,103) walihitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ikilinganishwa na wanafunzi 4,710 waliohitimu mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la **5%**.

***32. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia vyuo vyake inatekeleza programu ya uanagenzi kwa wanafunzi waliohitimu mafunzo katika Vyuo vyetu. Wahitimu hawa huunganishwa na Makampuni, Mashirika na Taasisi mbalimbali kwa lengo la kuwapa ujuzi na stadi mbalimbali zitakazowawezsha kukabiliana na changamoto za soko la ajira. Maeneo ya waliopatiwa ujuzi ni pamoja na ujenzi wa miradi ya maji, *Material Testing*, *Road Construction na Building Construction.* Maeneo mengine ni utoaji wa elimu ya lishe, uandishi wa maandiko ya miradi na ujasiriamali, utatuzi wa changamoto za wananchi, kutatua migogoro ya ardhi, kusimamia mafunzo kwa vikundi vya kifedha, kutoa elimu ya kodi na ukusanyaji wa kodi za Serikali ngazi ya Kata na Halmashauri, kusaidia wananchi kujaza fomu za maombi ya vitambulisho vya Taifa na kushiriki vikao mbalimbali vya maamuzi kwa kushirikisha wananchi. Katika mwaka wa fedha 2023/24 jumla ya wanafunzi **2,200** walijiunga na program hiyo ambapo, kati yao wanafunzi **1,104** (**50.2%)** walifanikiwa kuhitimu. Aidha, wanafunzi **1,096** (**49.8%)** wanaendelea na mafunzo hayo. Kutokana na umuhimu wa program hii, Wizara inaendelea

kuhimiza wanafunzi/wahitimu wa Vyuo Jamii kujiunga na progamu hii ili kupanua fursa ya kuajirika, kujiajiri na kuajiri wengine.

***33. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kupitia programu za ubunifu inatoa fursa kwa wanafunzi na jamii inayozunguka Vyuo kufanya kazi za ubunifu unaosaidia kutatua changamoto zilizopo na kuzalisha ajira kwa wabunifu na wahitimu. Programu hii inatolewa na vyuo 9 vyenye vituo vya ubunifu na maarifa katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Buhare, Monduli, Mlale, Rungemba, Uyole, Ruaha, Mabughai na Misungwi.

***34. Mheshimiwa Spika*** katika mwaka wa fedha 2023/24 bunifu mbalimbali zinazolenga kutatua changamoto za kijamii ziliibuliwa ikiwa ni pamoja na;

i. Utengenezaji wa Oil kwa kutumia Malighafi zisizo za Viwandani pamoja na Sabuni kwa kutumia Jivu na malighafi zisizo za viwandani (Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare). Wazo hili liko katika hatua ya uatamizi (Incubation)
ii. Utengenezaji wa *Switches* mbalimbali za Umeme na *lift* ya baiskeli ya Walemavu katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba. Wazo hili liko katika hatua ya Sampuli kifani (Prototype);
iii. *App* ya dirisha la taarifa kwa Vijana katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli. Wazo hili liko katika hatua ya uatamizi (incubation);
iv. Bidhaa lishe kwa ajili ya kutatua changamoto ya utapiamlo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha. Wazo hili tayari ni bidhaa (Minimum Viable Product);
v. *App* kwa ajili ya wagonjwa kupata taarifa zao katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole. Wazo hili liko katika hatua ya wazo (Ideation);
vi. Teknolojia ya kupata taarifa za masomo bila kuwa na simu janja (Elitek) katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Mabughai. Wazo hili liko katika hatua ya uatamizi (incubation); na

vii. Teknolojia ya kugundua madini ardhini na kutumia pumba za mchele kutengeneza Simenti katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi Wazo hili liko katika hatua ya uatamizi (Incubation).

Mawazo haya ya ubunifu wa mifumo yaliyo katika hatua za uatamizi yanalenga kufikia hatua ya bidhaa kwa matumizi.

***35. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza programu ya ushirikishwaji jamii zinazozunguka Taasisi na Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka. Katika mwaka 2023/24, jumla ya wananchi na wanafunzi **6,740** walipata mafunzo mbalimbali yakiwemo: elimu juu ya maadili mema katika shule za Msingi zilipo katika Kata ya Ruaha na Igumbiro Mkoani Iringa; elimu juu ya ukatili wa kijinsia katika Kata tano (5) za Ruaha, Mshindo, Kitanzini, Makolongoni na Mlandege na katika vijiji vya Kinko, Ndabwa, na Migambo katika Wilaya ya Lushoto, Mkoani Tanga, elimu ya uibuaji na uanzishaji wa Miradi ya kujiingizia kipato kwa vijana katika vijiji vya Magagula, Masangu na Lusonga Mkoani Ruvuma.

***Nichukue nafasi hii kupongeza jitihada zinazofanywa na vyuo vya Maendeleo ya Jamii nchini kwa kutoa wataalamu katika fani hii. Pia, natoa rai kwa Wadau wa Maendeleo kutoa ajira kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii hususan ngazi za msingi ambapo kuna upungufu mkubwa ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa afua za kutatua changamoto zinazoikabili jamii yetu. Aidha, Wizara inatoa wito kwa wahitimu kujiajiri kwa kutumia fursa za Mikopo bila riba, kujinunulia vifaa na mitaji.***

## ENEO LA 2: KUTAMBUA NA KURATIBU WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZA MAKUNDI MAALUM

***36. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutambua, kuratibu na kusimamia mipango mbalimbali ya kuwezesha na kuendeleza Makundi Maalum katika mambo mbalimbali zikiwemo shughuli za kiuchumi. Makundi yanayolengwa ni wafanyabiashara ndogondogo halali wote mfano wakiwemo Machinga, Mama/Baba Lishe, Waendesha Bodaboda na Bajaji, wasusi, wanaofanya biashara za kushona nguo na wengine mbalimbali.

Makundi haya yanakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kutofikia fursa za kiuchumi kama kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha, kupata maeneo wezeshi ya kufanyia biashara zao pamoja na kuwepo kwa ofisi zao rasmi kuwawezesha kukutana na kuratibu masuala yao wenyewe.

***37. Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaondolea changamoto hizo, Serikali imekamilisha Mpango wa kutoa mikopo kwa kundi hili kupitia taasisi za kifedha ambapo tarehe 06 Mei, 2024 Wizara imeingia mkataba wa makubaliano na benki ya NMB. Benki hiyo itatoa mikopo kwa wafanyabiashara hawa kwa mujibu wa mwongozo ulioandaliwa na pande zote mbili. Kupitia makubaliano haya, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaipatia benki ya NMB kiasi cha shilingi bilioni 18.5 kwa ajili ya kutoa mikopo yenye riba nafuu ya (7%).

***38. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha mikopo hii inaratibiwa vizuri na kuwanufaisha walengwa Wizara, imeshirikiana na OR – TAMISEMI, Wizara ya Viwanda na Biashara, Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC), Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Shirikisho la Umoja wa Machinga (SHIUMA) Tanzania na wadau wengine kukamilisha maboresho ya mfumo wa utambuzi, usajili na utoaji wa vitambulisho ujulikanao kama *Wafanyabiashara Ndogondogo Management Information System* (WBN-MIS).

***39. Mheshimiwa* Spika,** mfumo huo kwa sasa umeunganishwa na Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mfumo wa Kieletroniki wa Malipo ya Serikali (GePG). Mpango wa baadaye ni kuunganisha na mifumo mingine ikiwemo Anwani za Makazi, Taasisi za Fedha, Bima ya Afya na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuwawezesha wafanyabiashara hao kunufaika na huduma mbalimbali.

***40. Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha zoezi la utambuzi na usajili kutekelezwa kwa urahisi nchi nzima, Wizara imekamilisha mafunzo kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii, maafisa biashara na maafisa TEHAMA wapatao 660 kutoka ngazi za Mikoa, Halmashauri,

Miji, Manispaa na Majiji yote. Aidha, tayari zoezi la utambuzi na usajili limeanza Machi, 2024 na linaendelea katika Halmashauri zote nchini na hadi kufikia Aprili 2024, wafanyabiashara ndogondogo 11,003 (Me 4,079 na Ke 6,924) wamesajiliwa kwenye mfumo huo wakisubiriwa kukamilisha hatua ya malipo ya shilingi elfu ishirini (20,000) na baada ya hapo kila mmoja atapatiwa kitambulisho kitakachomuwezesha kutambuliwa wakati wa kwenda kuomba mkopo.

***41. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI inafuatilia maendeleo ya ujenzi wa Ofisi za Wafanyabiashara ndogondogo katika ngazi ya Mikoa yote. Hadi sasa Mikoa 9 imekamilisha ujenzi wa ofisi hizo na Mikoa 17 ujenzi upo katika hatua mbalimbali kama inavyooneshwa kwenye ***Jedwali Na.3***. Ofisi hizo zitasaidia uratibu wa shughuli za wafanyabiashara hao nchini pamoja na kurahisisha mawasiliano kati yao, Wizara za Kisekta na wadau wengine wa maendeleo. Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inaendelea kuhimiza mikoa ambayo bado kukamilisha, wafanye hivyo kabla au ifikapo tarehe 30 Juni 2024.

**Jedwali Na. 3: Hali ya ujenzi wa Ofisi za Wafanyabiashara ndogondogo hadi kufikia mwezi Aprili, 2024.**

| NA. | MKOA | HALI YA UJENZI |
|---|---|---|
| 1. | Arusha, Mbeya, Katavi, Manyara, Songwe, Pwani, Lindi, Rukwa na Tanga. | Ujenzi wa ofisi umekamilika. |
| 2. | Morogoro, Dar es Salaam na Geita. | Ofisi zimepauliwa na kazi za umaliziaji zinaendelea. |
| 3. | Mtwara, Njombe, Kagera, Tabora, Dodoma, Shinyanga, Singida Kigoma, Mara na Kilimanjaro. | Ofisi zipo hatua ya lenta na ujenzi unaendelea. |
| 4. | Ruvuma, Simiyu na Iringa. | Ujenzi wa boma unaendelea. |
| 5. | Mwanza. | Hatua za awali za kuanza ujenzi. |

***42. Mheshimiwa Spika,*** eneo lingine ambalo Wizara imeliwekea mkazo ni la kutoa elimu kwa viongozi wao makundi haya maalum ili kuhakikisha wanakuwa na weledi ambapo, Wizara imefanya mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa ngazi ya Taifa na Mikoa kuhusu masuala ya utii wa sheria bila shuruti, uzalendo na umuhimu wa kuzingatia misingi ya utawala bora kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na mshikamano wakati wa kutatua changamoto zao. Mafunzo hayo yalifanyika mwezi Desemba 2023.

***43. Mheshimiwa Spika,*** eneo lingine muhimu la kuwezesha kundi hili kiuchumi ni kuwapatia maeneo rasmi ya kufanyia biashara ili kuwaondolea usumbufu na bughudha kwa kuweka mazingira wezeshi ya kupata wateja. Wizara kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI imeendelea kuboresha mazingira ya kufanyia ambapo, taarifa kutoka OR – TAMISEMI inaonesha kuwa, hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya masoko 367 yamejengwa na kuboreshwa katika maeneo mbalimbali nchini. Uwepo wa masoko hayo yamewezesha jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 136,041 kuendesha biashara zao katika mazingira rafiki. Kati ya masoko hayo, 16 yamejengwa na kuboreshwa kwa fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais, Shilingi Bilioni 5. Masoko hayo 16 (***Jedwali Na.4***) yamejengwa katika Mkoa ya Dar es Salaam (masoko 9) na soko moja moja katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Dodoma, Arusha, Mwanza, Morogoro na Tanga.

***Jedwali Na. 4:* Orodha ya Masoko ya Machinga yaliyojengwa kwa fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais.**

| Na | MKOA | HALMASHAURI | AINA YA MRADI KWA AJILI YA WAJASIRIAMALI |
|---|---|---|---|
| 1. | DSM | DSM CC | Ujenzi wa soko la Kigogo Fresh (Mashedi mawili makubwa na machinjio ya kuku). |
| | | Ubungo MC | Soko la wajasiriamali simu 2000. |
| | | | Mabibo Gamit (mabanda matatu). |
| | | | Soko la wajasiriamali Mbezi Luis (Banda Moja). |

| Na | MKOA | HALMASHAURI | AINA YA MRADI KWA AJILI YA WAJASIRIAMALI |
|---|---|---|---|
| | | | Soko la wajasiriamali Mbezi Njia ya Goba (Mabanda Mawili). |
| | | Temeke MC | Ujenzi wa Mabanda manne katika soko la Buza. |
| | | | Ujenzi wa Mabanda matatu katika soko la TAZARA. |
| | | | Ujenzi wa Karakana ya miundombinu ya soko la Mbande, mabanda matatu katika soko la TAZARA. |
| | | Kinondoni MC | Ujenzi wa Soko la Bunju B. |
| 2. | Mbeya | Mbeya CC | Ujenzi wa Soko- la Old Airport. |
| 3. | Songwe | Tunduma | Ujenzi wa Soko Tunduma. |
| 4. | Dodoma | Dodoma CC | Ujenzi wa soko la wazi la Machinga Complex. |
| 5. | Arusha | Arusha CC | Ujenzi wa soko – Engutoto. |
| 6. | Mwanza | Mwanza CC | Ujenzi wa soko la Mchafukoge. |
| 7. | Morogoro | Morogoro MC | Ujenzi wa soko la Fire. |
| 8. | Tanga | Tanga CC | Ujenzi wa jengo la soko la Kange. |

***Chanzo: OR -TAMISEMI***

***44. Mheshimiwa Spika***, katika kujenga uzoefu na kuongeza fursa za kibiashara, Wizara kwa kushirikiana na sekta nyingine hutoa nafasi za ushiriki katika maonesho ya biashara ya ndani na nje kwa wafanyabiashara ili kuweza kuonesha bidhaa zao, kuuza, kujifunza kwa wenzao na hatimae pia kujipatia uzoevu. Katika kipindi cha mwaka 2023, Wizara ilihamasisha wafanyabiashara ndogondogo kushiriki katika shughuli mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa zikiwemo Maonesho ya Kilimo ya Nanenane ambapo jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 968 walishiriki Maonesho hayo yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Mbeya.

***ENEO LA 3: HAKI NA MAENDELEO YA MTOTO***

***45. Mheshimiwa Spika***, Wizara inalo jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya mtoto pamoja na upatikanaji wa haki za msingi kwa mtoto kama zilivyoainishwa katika Mikataba ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2019.

***46. Mheshimiwa Spika***, haki za mtoto ni pamoja na kuishi, kulindwa dhidi ya vitendo vya ukatili, kuendelezwa kupitia vipaji na elimu, kushiriki katika masuala yanayomhusu kulingana na umri wake na kutobaguliwa kwa namna yoyote ile. Aidha, mtoto anahitaji malezi bora yenye kuzingatia haki na mahitaji yake ya msingi hasa katika kipindi cha umri wa miaka 0-8 ambapo ubongo hukua kwa 90%. Nguvu kubwa inahitajika hapa ili kuhakikisha mtoto anakua na kufikia utimilifu wake na hatimaye kuja kuwa nguvu kazi yenye tija kwa Taifa. Hata hivyo, baadhi ya watoto wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na malezi duni na vitendo vya ukatili kutoka kwa ndugu wa karibu, familia na jamii inayowazunguka.

***47. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta imeendelea kuboresha mifumo ya kisheria ili kuimarisha ulinzi na usalama wa mtoto kwa kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwemo **Sheria ya Mtoto**, Sura ya 13, **Sheria ya Ushahidi**, Sura ya 6 na **Sheria ya Makosa ya Mtandao**, Sura ya 443 kwa lengo la kumlinda mtoto nje na ndani ya Mtandao.

***48. Mheshimiwa Spika***, kupitia Bunge lako Tukufu, **Sheria ya Ushahidi**, Sura ya 6 imefanyiwa marekebisho katika kifungu cha 127(2) kupitia Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Sekta ya Sheria za mwaka 2023 (The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) ili kuhakikisha maslahi ya mtoto yanalindwa hasa pale anapotoa ushahidi wake mahakamani. Aidha, Wizara inaendelea **kurekebisha Kanuni za Vituo** vya Kulea Watoto Wadogo Mchana na Watoto Wachanga za mwaka 2012, **Kanuni za Makao** ya Watoto za mwaka 2012, **Kanuni za Uasili** Watoto za mwaka 2012 na **Kanuni za Malezi**

**ya Kambo** za mwaka 2012 ili kuhakikisha mazingira ya malezi ya mtoto wa kitanzania ni salama kwa makuzi stahiki.

***49. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa Mei Mosi, 2024 Mkoani Arusha, kuhusu waliojifungua watoto kabla ya siku zao kutimia (njiti) kwamba, kipindi cha uangalizi maalumu wa watoto hao hakitahesabiwa kama likizo ya uzazi; Wizara inashirikiana na Wizara nyingine za kisekta kwenye kuboresha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366. Lengo la marekebisho haya ni kuweka vifungu vya kumuongezea muda mama aliyejifungua mtoto njiti ili kuweza kupata muda wa kutosha wa kumhudumia mtoto vizuri tofauti na sheria ilivyo kwa sasa.

***50. Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya utafiti wa kujua kiwango cha ukatili dhidi ya Watoto kupitia mitandao (online child abuse) wa mwaka 2022, umebainisha asilimia 67 ya watoto wa umri wa miaka 12 hadi 17 wanatumia mitandao ambapo, kati yao 4% wamefanyiwa vitendo vya ukatili na uonevu bila ya ridhaa yao. Hii ni kwa kuwa Matumizi ya mitandao hayawezi kuepukwa kutokana na mapinduzi ya teknolojia ya habari na mawasiliano ambapo mitandao ni sehemu ya maisha hasa kwa kizazi kilichopo sasa.

***51. Mheshimiwa Spika***, katika kuwalinda watoto dhidi ya ukatili mitandaoni, Wizara ilizindua ***Kampeni ya Kitaifa ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto Mtandaoni*** tarehe 10 Februari, 2024 Jijini Dodoma ambapo wadau zaidi ya 460 walishiriki. Lengo la kampeni hiyo ni kuelimisha watoto, wazazi, walezi, walimu, viongozi wa dini, viongozi wa Taasisi zisizo za Serikali, Wizara za kisekta, na jamii kuhusu kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili mitandaoni sambamba na ukatili wa aina nyingine. Aidha, uzinduzi uliambatana na kuwajengea uelewa wahariri kutoka vyombo mbalimbali vya habari ili waweze kutoa kipaumbele katika utoaji wa taarifa kuhusu usalama wa watoto mtandaoni. Baada ya uzinduzi huo, Kampeni hii iliendelea kutekelezwa katika Mikoa yote kupitia majukwaa ya watoto, wazazi na walezi, viongozi wa dini na mikusanyiko mbalimbali katika Jamii. Aidha, Wizara imezindua Kamati ya Kitaifa ya Ushauri kuhusu Ulinzi wa Mtoto Mtandaoni kwa lengo la kuishauri Serikali kuhusu usalama wa mtoto mtandaoni.

***52. Mheshimiwa Spika,*** katika siku za hivi karibuni tumeshuhudia aina nyingine ya ukatili wa watoto kupitia ***Sanaa*** mbalimbali ambapo watoto wanashirikishwa kwenye matamasha ya usiku wakihusishwa katika michezo na shughuli za maonesho ya mitindo, sherehe za harusi na shughuli nyingine za starehe mazingira ambayo katika maeneo mengi yamekuwa yakichangia **mmomonyoko wa maadili** na pia ni kinyume na Sheria ya Mtoto kifungu cha 158(1)(b).

***53. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, waandaji wa vipindi, filamu na wanaoonesha filamu kwenye majukwaa mbalimbali baadhi yao wamekuwa hawazingatii kuandaa maudhui yanayoendana na mila na desturi zetu ili kumlinda mtoto na jamii kwa ujumla. Kupitia bunge lako tukufu, napenda kutoa taarifa kuwa, Wizara haitavumilia jamii kuletewa maudhui ambayo ni kinyume na sheria za usajili wa huduma inayotolea kwenye maeneo haya na mengine yanayohusu kuzalisha maudhui yanayopokelewa na jamii. **Hivyo, Wizara itakuwa mstari wa mbele kushirikiana na wizara za kisekta kuhakikisha sheria husika zinafanya kazi yake dhidi ya watu hao.**

***54. Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na suala zima la mmomonyoko wa maadili, Serikali imeunda Kamati Maalum inayojumuisha Wizara yangu pamoja na Wizara nyingine za Kisekta, na Taasisi za Serikali zilizo chini ya Wizara hizi ambapo, lengo la kamati hii, ni kubaini vyanzo vya mmomomyoko wa maadili kwa ujumla ukiwemo ule wa watoto, kutambua ukubwa wa tatizo na kuandaa mpango kazi wa kutekeleza ili kuzuia na kumaliza tatizo hili. Aidha, mbinu mbalimbali zitatumika katika kukabiliana na tatizo hili na kuishirikisha jamii kuhusu taarifa ya utekelezaji ili kupata elimu na kuchukua hatua kwa nafasi yao.

***55. Mheshimiwa Spika,*** suala la kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto ni jukumu la kila mmoja wetu, katika kutimiza azma hiyo, Wizara inashirikiana na vikundi mbalimbali vya kijamii kwa hiari vikiwemo SMAUJATA (Mashujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii), SAWATA (Sauti ya Watoto Tanzania), Malezi Bora Network, FAGDI (Foundation for Ambassodors Gender Development Initiatives) na vingine

kadhaa. Kupitia Kampeni ya Wizara kwa ushirikiano na SMAUJATA yenye lengo la kuelimisha watoto na jamii kuhusu kukabiliana na vitendo vya ukatili, hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya wananchi 10,525 wamejiunga na mtandao huu wa mashujaa katika mikoa yote na matokeo mojawapo ni jumla ya matukio 799 ya ukatili dhidi ya watoto yameibuliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka za kusimamia sheria kwa hatua zaidi.

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha *Haki ya Watoto ya Kushiriki* kwenye masuala yanayowahusu Wizara imeendelea kuratibu Uanzishwaji na uendeshaji wa **Mabaraza ya Watoto** katika ngazi ya Kijiji/Mtaa, Kata, Halmashauri, Mikoa na Taifa. Mabaraza ya Watoto ni jukwaa maalum kwa watoto kutoa maoni, kujadiliana na kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu uongozi, uadilifu, uzalendo na masuala mengine mtambuka ikiwa pamoja na elimu ya jinsia, mazingira na UKIMWI. Aidha, Mabaraza ya Watoto yamewezesha watoto kuwa na uwezo mkubwa wa kujitambua, kujieleza na kujiamini ambapo ni ishara nzuri kwa kizazi chenye tija katika Jamii kwa siku za usoni. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya Mabaraza ya Watoto 865 yameundwa nchini ikilinganishwa na Mabaraza ya watoto 592 yaliyokuwa yameundwa hadi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la 46%.

***57. Mheshimiwa Spika;*** katika kukabiliana na changamoto za Malezi na Makuzi duni ya watoto wenye umri kati ya miaka 0 – 8; Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia Programu mbalimbali zikiwemo; Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ya mwaka 2021/22 - 2025/26 inayojulikana kama MMMAM**.** Programu ina vipaumbele vya kuzingatia pamoja na afua mbalimbali zinazolenga kutoa elimu ya mafunzo ya malezi kwa maafisa wa Serikali wa kada mbalimbali, viongozi wa dini na walezi ambao kwa namna moja au nyingine wanahusika katika makuzi na malezi ya mtoto. Aidha, **programu hii pia inamlenga kijana balehe** kwa kumpatia elimu ya uelewa wa masuala ya makuzi na kujikinga na athari mbalimbali.

***58. Mheshimiwa Spika,*** kufikia Aprili 2024, Serikali kwa kushirikiana na Wadau imejenga uelewa kuhusu Programu hiyo kwa Maafisa 3,123 wa Serikali na Wadau wengine katika Mikoa yote 26 na Halmashauri 184 ikihusisha Wakuu wa Mikoa, Wajumbe wa Kamati za Usalama za Mikoa na Maafisa wa Sekretarieti za Mikoa. Aidha, mafunzo hayo yamefikia Wakurugenzi Watendaji, Wenyeviti wa Halmashauri, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Lishe, Maafisa Elimu na Waganga Wakuu katika Halmashauri zote nchini. Kupitia mikutano ya utambulisho wa Programu hii, washiriki waliweza kuainisha vipaumbele vya MMMAM **kwa ajili ya kuingizwa kwenye mipango na bajeti ya Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2024/25.**

***59. Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa nafasi kubwa waliyo nayo viongozi wa dini katika kusaidia na kuimarisha malezi na makuzi ya watoto wetu kupitia mafunzo ya dini; Wizara imeratibu na kusimamia mafunzo ya kujenga uelewa wa Programu ya MMMAM kwa Viongozi wote wa Dini wa ngazi ya Taifa kutoka muunganiko wa Taasisi za dini ambazo ni Wakatoliki (TEC), Jumuia ya Kikristo Tanzania (CCT), Wapentekoste (CPCT), Waadiventista Wasabato (SDA) na Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA). Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uelewa viongozi hawa kuhusu umuhimu wa kuwekeza kwenye MMMAM na hatimaye kuingiza maudhui ya MMMAM kwenye miongozo ya dini ili kuitumia katika mahubiri na mihadhara.

***60. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Viongozi wa dini imeandaa kitabu cha malezi ya watoto kwa muktadha wa dini ya kiislam na kikristo kinachoitwa ***"Wazazi wangu, Kesho yangu"***. Maudhui ya Kitabu hicho yanalenga kuimarisha malezi bora kwa watoto na familia kwa muktadha wa dini za kiislamu na kikristo. Na Maudhui ya kitabu hicho yataweza kutumika kuelimisha waumini wao kote nchini.

***61. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia ukuaji chanya wa watoto kupitia malezi ya familia pamoja na vituo vya kulelea Watoto wadogo na wachanga. Katika kufanikisha hili,

Wizara imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vituo vya kulelea Watoto wadogo na watoto wachanga ambavyo vinatoa huduma ya uchangamshi wa awali unaowasaidia watoto kukua kimwili, kiakili, kiafya, kihisia na kimaadili na hatimae kuwaandaa kujiunga na elimu ya awali. Aidha, vituo hivi ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha ulinzi wa watoto na usalama wao wakati wazazi na walezi wao wakijihusisha na shughuli za kiuchumi badala ya kuwepo mitaani. Vituo hivi vina jukumu pia la kusimamia afya na lishe bora kwa watoto, pamoja na kuimarisha malezi yenye mwitikio na nafasi ya kujifunza.

***62. Mheshimiwa Spika,*** kufikia Aprili 2024, jumla ya vituo 3,862 vya kulelea watoto wadogo mchana vimesajiliwa vyenye jumla ya watoto 397,935 (Me 175,517 na Ke 222,418) na vituo vya Kijamii 206 (vikiwemo 30 vya mfano) vyenye jumla ya watoto 11,675 (Me 4,833 na Ke 6,842), ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo kulikuwa na jumla ya vituo 3,033 na vya kijamii 200 vilivyokuwa na jumla ya watoto 184,606 (Me 86,832 na Ke 97,774). Hatua hii imefanya kuwa na ongezeko la vituo 829 sawa na 21.5% na ongezeko la watoto 225,003 sawa na 55%.

***63. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, **Tanzania ni miongoni mwa nchi za mwanzo Afrika** zilizoandaa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto mwaka 2021 baada tu ya mwongozo wa kimataifa kutoka mwaka 2018. Kutokana na utayari huo na mafanikio yaliyopatikana katika kuratibu utekelezaji wa programu hii, **Tanzania ilipewa Heshima ya kuandaa mkutano wa Kimataifa wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki** uliofanyika kuanzia tarehe 11 hadi 14 Machi, 2024 Jijini Dar Es Salaam.

***64. Mheshimiwa Spika,*** mkutano huu uliandaliwa na Wizara kwa kushirikiana na Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto Afrika yaani "*Africa Early Childhood Network*" na ulikuwa na Kaulimbiu "*Wekeza katika Malezi na Makuzi ya Watoto Wadogo;*

*Kujenga Rasilimali Watu Yenye Tija". Yaani "Investing in Early Childhood; Building Human Capital along the Life Course".*

***65. Mheshimiwa Spika,*** mkutano huu ulihudhuriwa na jumla ya washiriki 1,300 kutoka, Nchi za Afrika Mashariki, Bara la Afrika, Amerika, Ulaya na Asia ambapo, lengo lilikuwa ni kubadilishana uzoefu, maarifa na kuvutia uwekezaji katika afua za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto. Pamoja na kufanikiwa kutangaza Programu ya MMMAM, kupitia Mkutano huo, kama nchi kupitia ajenda hii ya maendeleo ya mtoto tumeweza kuitangaza nchi yetu katika sekta za utalii.

***66. Mheshimiwa Spika,*** afua nyingine tunayotekeleza kwa kushirikiana na wadau Katika Programu ya MMMAM ni ile ya Elimu ya Malezi Jumuishi yanayohusisha wazazi, walezi na vijana wa umri wa miaka 10 - 17. Programu hiyo inalenga kutoa elimu ya malezi kuhusu masuala ya msingi yanayohusu nafasi ya vijana balehe, wazazi na walezi katika makuzi yao kwenye familia kwa kushirikishana. Majaribio ya Programu hii yamefanyika katika mikoa ya Mbeya (Mbarali) na Songwe (Ileje, Mbozi na Tunduma) ambapo, Jumla ya Wazazi/Walezi 400 na Vijana Balehe 520 wameshiriki na tathmini yake inatarajiwa kukamilika June 2024 ambapo, itasaidia Wizara kufanya maamuzi juu ya hatua stahiki za kuchukua.

***67. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na inaratibu utekelezaji wa *Ajenda ya Taifa ya Kuwekeza kwenye Afya na Maendeleo kwa Vijana Balehe nchini yaani NAIA- AHW (2021/22 – 2024/25)*. Uratibu wa Ajenda hii unajumuisha Sekretarieti ya Taifa, Kamati Tendaji ya Taifa (Wakurugenzi); Kamati ya Uratibu wa Ufuatiliaji na Tathmini; Kamati Elekezi ya Taifa (Makatibu Wakuu), na Jukwaa la Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara za Kisekta. Lengo la autekelezaji huu ni kuongeza uwekezaji katika huduma mbalimbali kama Elimu (VVU/UKIMWI, kujikinga na Mimba za utotoni), vilevile kutoa elimu juu ya athari za utoro mashuleni pamoja na kuepuka masuala yanayopelekea mmomonyoko wa maadili ili kuwawezesha vijana kukua na kufikia ndoto zao.

***68. Mheshimiwa Spika,*** kufikia Aprili, 2024 jumla ya Vijana balehe 983,487 (wavulana 261,293, wasichana 722,194) walipatiwa huduma za upimaji wa VVU na kati ya hao waliopatikana na maambukizi walikuwa 6,154 sawa na 8.5% ya vijana balehe waliopima (wavulana walikuwa 772 sawa na 12.5% na Wasichana 5,382 sawa na 87.5%. **Waathirika wote waliunganishwa na huduma za matibabu (CTC).** Aidha, Jumla ya Vijana 8,380,871 (wavulana 5,394,334 na Wasichana 2,986,537) walipata elimu ya Afya ya Uzazi kwa lengo la kuwakinga na mimba za utotoni na athari nyingine zinazotokana na uzazi usio salama.

***69. Mheshimiwa Spika,*** suala la Lishe, ni moja ya afua katika mpango unaohusisha vijana Balehe ambapo, katika kuimarisha lishe kwa vijana hawa jumla ya shule za msingi na sekondari 921 zimehamasika na kuanzisha miradi ya kilimo cha bustani kwa lengo la kuzalisha vyakula vyenye lishe mashuleni. Aidha, wakufunzi 30 walipatiwa mafunzo ya elimu ya lishe; sambamba na kutekeleza kampeni za elimu lishe kwa jamii. Katika kuwapa vijana ujuzi na ufundi, jumla ya vijana 11,845, walipatiwa mafunzo ya uanagenzi katika fani mbalimbali ikiwemo TEHAMA ili kukuza ujuzi na jumla ya vijana 1,888 (wavulana 1,070 na wasichana 809,) wameunganishwa na ajira mbalimbali kupitia programu ya Mafunzo kwa Vitendo (internship). Vilevile, jumla ya vijana 1,411,254 (wavulana 698,076 na wasichana 713,178) walifaidika na mradi wa kusaidia kaya maskini kupitia TASAF (cash transfer).

***70. Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na mila na desturi zenye madhara kwa Watoto na jamii, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa mwaka 2020/21-2024/25 wenye lengo la kutokomeza vitendo vya ukeketaji kwa watoto wa kike na wanawake nchini.

***71. Mheshimiwa Spika,*** kufikia Aprili, 2024 Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imekuwa ikitoa elimu kwa njia mbalimbali ambapo watoto, viongozi wa kimila, viongozi wa dini, watu mashuhuri, mang'ariba na jamii kwa ujumla walifikiwa. Elimu

iliyotolewa imesaidia kuongeza uelewa wa jamii kuhusu kuacha vitendo vya ukeketaji ambapo, takwimu za Hali ya Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania za mwaka 2022/2023 zinaonesha kupungua kwa vitendo vya ukeketaji nchini kutoka asilimia 10 kwa mwaka 2015/2016 hadi asilimia 8 kwa mwaka 2022/2023.

***72. Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, katika baadhi ya mikoa kiwango cha ukeketaji bado ni kikubwa mfano, Arusha (43%), Manyara (43%), Mara (28%), Singida (20%), Tanga (19%), Dodoma (18%), Iringa (12%), Morogoro (10%), Kilimanjaro (9%), Njombe (7%), Pwani (5%) na Mbeya (3%). **Mikoa mingine, ukeketaji upo chini ya asilimia 1.** Wizara inaendelea na utekelezaji wa Mkakati huo ili kufikia lengo la kupunguza vitendo vya ukeketaji hadi asilimia 5 ifikapo mwaka 2025.

***73. Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa Tanzania inaendelea kufanya vizuri katika udhibiti wa ukeketaji, tarehe 9 - 11 Oktoba, 2023, **Serikali ilipata Heshima ya kuwa mwenyeji wa mkutano wa Kimataifa** wa Kutokomeza Ukeketaji kwa nchi za wanachama wa Umoja wa Africa uliokuwa na kaulimbiu "**Mabadiliko katika Kizazi**". Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kubadilishana uzoefu miongoni mwa Wadau katika kuimarisha mikakati iliyopo ya kutokomeza ukeketaji kwa watoto na wanawake miongoni mwa nchi wanachama. Aidha, Mkutano huo ulitoa fursa kwa Tanzania kuwasilisha ujumbe kwenye jumuiya ya kimataifa kuhusu juhudi na mchango wa nchi yetu katika kutokomeza vitendo vya ukeketaji nchini ikiwa pamoja na ukeketaji wa kuvuka mipaka ambao wahusika huvuka mipaka kwenda nchi jirani ili kutekeleza vitendo hivyo. Aidha, nchi ilipata mapato kupitia huduma zilizotolewa na fursa ya kutangaza uwekezaji na vivutio vya utalii vinavyopatikana hapa nchini. Mkutano ulifanyika kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo ambapo jumla ya washiriki zaidi ya 1,000 walihudhuria.

### *ENEO LA 4: HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII*

***74. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kutoa huduma za Ustawi wa Jamii hapa nchini zikiwemo: haki, matunzo na ulinzi kwa wazee; watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi; watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani; watoto walio katika mkinzano na sheria; huduma kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia na waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu; huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii. Majukumu haya yanatekelezwa na wataalam wa Ustawi wa Jamii kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mahsusi inayoongoza utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii.

***75. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Wizara imeendelea na utekelezaji wa kuratibu afua za ustawi ambazo ni pamoja na; huduma kwa makundi maalum; huduma kwa familia zisizo na uwezo; usajili na usimamizi wa makao ya watoto, nyumba salama, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga; makazi ya wazee na wasiojiweza; huduma za malezi ya kambo na kuasili; na utatuzi wa migogoro ya familia na ndoa; na huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

***76. Mheshimiwa Spika***, kuhusu huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utambuzi na utoaji wa huduma kwa kundi hili wakiwemo watoto waliotelekezwa, wanaoishi na kufanya kazi mitaani, wanaotoka katika kaya masikini, wanaolelewa na wazee wasio na uwezo, watoto wanaojilea wenyewe, watoto yatima, na wale wanaokinzana na sheria pamoja na watoto waliozaliwa nje ya ndoa na watoto walio katika familia zenye migogoro.

***77. Mheshimiwa Spika,*** utambuzi wa makundi haya ya watoto hufanywa na Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto ngazi ya Kijiji/Mtaa zilizoundwa kupitia Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) pamoja na mfumo jumuishi wa mashauri ya watoto *(National Intergrated Case Management System (NICMS)*.

***78. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024, jumla ya watoto 708,957 (Me 340,661, Ke 368,296) wanaoishi katika mazingira hatarishi wametambuliwa katika Halmashauri zote nchini na kupatiwa huduma kuendana na mahitaji yao ikiwemo watoto 275,058 (Me 127,667, Ke 147,391) wamesaidiwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau kupata vyeti vya kuzaliwa. Aidha, Kaya za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 457,450 (Me 141,507, Ke 315,943) zimesaidiwa kupata Bima za afya. Vilevile, watoto wengine wamesaidiwa kupata chakula, malazi, mavazi, elimu, matibabu, lishe, dawa za kufubaza VVU/UKIMWI, afya ya uzazi, ulinzi, msaada wa kisaikolojia na kijamii, marekebisho ya tabia, kuunganishwa na familia na mafunzo ya ufundi na stadi za maisha.

***79. Mheshimiwa Spika,*** katika suala la huduma za mahabusu kwa watoto, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za Ustawi katika mahabusu tano (5) za watoto za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Watoto hawa ni wale walio katika mkinzano na sheria. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya watoto 381 (Me 361 na Ke 20) waliopo katika mahabusu hizi walipatiwa huduma za msingi zikiwemo chakula, malazi, mavazi, matibabu, elimu, stadi za maisha na marekebisho ya tabia. Aidha, kati ya hao, jumla ya watoto 92 (Me 89 na Ke 3) waliohukumiwa kwa makosa mbalimbali na wanaendelea kuhudumiwa katika Shule ya Maadilisho ya Irambo Mkoani Mbeya. Shule hii inatoa pia marekebisho ya tabia na elimu ya msingi na stadi za maisha kwa watoto ili wanapokamilisha hukumu zao waweze kujitegemea na kuwa raia wema.

***80. Mheshimiwa Spika***, kuhusu huduma za Mahakama kwa watoto, Wizara imeendelea kuratibu huduma za Ustawi wa Jamii katika Mahakama za Watoto 133 nchini ambapo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, **mashauri 4,462** yalipokelewa yakijumuisha mashauri 1,034 ya matunzo (maintenance), 952 ya uangalizi wa mtoto (custody), 882 ya kuona watoto (access), 680 watoto waliokinzana na sheria, 13 ya kuasili, 7 ya vinasaba (DNA order), 22 ya uthibitisho wa baba (parentage), 872 ya Huduma za afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii (Mental Health and Pyscho-

social support - MHPS). Jumla ya mashauri 3,984 kati ya yote yaliyopokelewa yalisikilizwa na kufungwa na mashauri 478 yaliyobaki bado yanaendelea kusikilizwa.

***81. Mheshimiwa Spika***, huduma za **malezi ya kambo na kuasili** zimeendelea kutolewa kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kwa kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika ngazi ya familia kulingana na Sheria ya Mtoto, Sura ya 13. Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, vipeperushi na matangazo juu ya umuhimu wa malezi ya watoto ngazi ya familia kupitia huduma ya malezi ya kambo na kuasili. Kutokana na jitihada hizi, idadi ya watoto waliopata malezi mbadala imeongezeka ambapo kufikia Aprili 2024, jumla ya watoto 133 walipata malezi mbadala wakiwemo 74 malezi ya kambo, na 59 wameasiliwa, ikilinganishwa na idadi ya Watoto 75 (41 malezi ya Kambo na 34 walioasiliwa) mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la 43.6%.

***82. Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuharakisha maamuzi ya malezi mbadala, Wizara imefanikiwa kuwajengea uwezo watoa huduma 30 kutoka Halmashauri nane (8) za Mkoa wa Mwanza ikijumuisha Maafisa Ustawi wa Jamii, Mahakimu, Majaji, Maafisa wa Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto na Maafisa Afya ili kushughulikia maombi ya malezi ya kambo na kuasili kwa ufanisi na haraka pindi yanapowasilishwa katika Mamlaka zao.

***83. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwenye makao ya watoto ikiwemo usajili, malazi, chakula, malezi, matunzo, ulinzi, afya, elimu, msaada wa kisaikolojia na kijamii, mafunzo ya ufundi na stadi za maisha kwa watoto walio katika mazingira hatarishi nchini. Aidha, hadi kufikia Aprili 2024, leseni 35 za usajili wa Makao ya Watoto zimetolewa kwa watu binafsi na taasisi za dini na kufanya jumla ya makao yaliyosajiliwa kufikia 368 yenye Watoto 13,945 (Me 7,007 na Ke 6,938) ikilinganishwa na jumla ya Makao 333 mwezi Aprili 2023 ambapo jumla ya wahudumiwa ilikuwa watoto 12,077 (Me 6,050, Ke 6,027).

***84. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma kwa watoto waliopo katika Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo (Dodoma) na Kurasini (Dar es Salaam) ambapo jumla ya watoto 215 (Me 129, Ke 86) wamehudumiwa. Kwa sasa Wizara inaendelea kuboresha huduma katika Makao ya Taifa ya Watoto ya Kikombo kwa kuanzisha miradi ya ukumbi na huduma ya chakula, kilimo biashara na bustani za mbogamboga, ushonaji, pamoja mpango wa kuanzisha kituo cha kulelea watoto wadogo mchana kitakacho hudumia watoto wa kituoni na wa nje ya kituo.

***85. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta  na Wadau wa Maendeleo inaendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Mashauri ya Watoto (*National Intergrated Case Management*) ya Mwaka 2017, ambao **moja ya afua ni kuwaondoa watoto mitaani** kwa utaratibu wa kuwatambua na kuwapatia makazi ya muda kwenye Makao ya Watoto kwa ajili ya kupata huduma za msingi na hatimae kuwaandaa kuunganishwa na familia zao au kuwezeshwa kujitegemea katika jamii au utaratibu mwingine wa malezi mbadala ikiwemo kuasili na malezi ya kambo.

***86. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, Wizara kwa kushirikiana na OR TAMISEMI imepanua wigo wa utambuzi wa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani kwa kuyafikia maeneo mengi zaidi ambayo ni masoko, vituo vya mabasi, minada na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya shughuli za kiuchumi. Utambuzi huu, umewezesha kupata jumla ya watoto **8,372** (Me 4,218, Ke 4,154) kutoka katika Halmashauri za mikoa yote. Aidha, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023 jumla ya watoto waliotambuliwa walikuwa **5,728** (Me 4,583 na Ke 1,145), sawa na ongezeko la Watoto **2,644.** Hata hivyo, Serikali bado imeendelea kuwapatia watoto hawa huduma zikiwemo kuunganishwa na familia zao (**2,457)**, kuwawezesha kujitegemea katika jamii (**873)** na **5,042** wanaendelea kupatiwa huduma kwenye Makao ya Kulelea Watoto nchini kote.

***87. Mheshimiwa Spika***, takwimu hizi zinaonesha ukubwa wa tatizo la Watoto wa mtaani kuwa linaendelea kuongezeka. Sababu kubwa zinazochangia ongezeko hilo ni pamoja na hali duni ya maisha katika baadhi ya familia wanazotoka watoto hawa, msongo rika (peer pressure), malezi duni, pamoja na kuvunjika kwa ndoa. Sababu nyingine ni pamoja na vifo vya mzazi/wazazi, au mlezi/tegemezi mkuu katika familia na kukosekana mbadala wa kuwalea watoto. Hivyo, juhudi za pamoja zinahitajika katika kukabiliana na suala hili kuanzia ngazi ya familia, Mtaa au Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa kwa kushirikisha viongozi wa ngazi zote.

***88. Mheshimiwa Spika***, mkakati mwingine ambao Wizara kwa kushirikiana na OR TAMISEMI imeweka ni uanzishaji wa madawati ya watoto katika vituo vya mabasi 21 nchini kwa ajili ya kuwatambua na kuchukua hatua stahiki kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii ili kuwanusuru watoto hao dhidi ya athari wanazoweza kupata iwapo wataingia mitaani. Watoto waliookolewa na maafisa ustawi katika vituo vya mabasi ni 532 (Me 215 na Ke 317)

***89. Mheshimiwa Spika***, serikali kupitia wizara hii itaratibu wadau kuongeza kasi ya kuwaondoa watoto waishio na kufanya kazi mitaani sambamba na mkakati wa kuzia waiingie kuishi na kufanya kazi mitaani kwa kuelimisha jamii na viongozi wa mamlaka za serikali za mitaa kuhusu umuhimu wa kubaini watoto walio kwenye hatari ya kutoroka majumbani ili hatua stahiki zichukuliwe mapema badala ya kusubiri watoroke na kuanza kuwarejesha wakiwa tayari mitaani. Vilevile, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Wadau wa Elimu, Kamati za Ulinzi wa Mtoto na viongozi wa ngazi za Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji/Mtaa, tutaratibu ufuatiliaji endelevu wa mienendo ya mahudhurio ya watoto katika shule za msingi na sekondari ili kubaini wanafunzi watoro na kushirikisha wazazi na walezi kwenye kutambua changamoto zao ili kuzikabili na kuwawezesha watoto hao kudumu shuleni na kuepuka utoro wa majumbani.

**Nitumie fursa hii kuwaomba Wakuu wa Mikoa na Wilaya kupitia dhamana zao kuanza kufanya tathmini ya kaya zilizo katika mazingira hatarishi na kuziwekea mkakati wa kuwasaidia ili kuzuia**

**watoto kutorokea mitaani, kwa sababu tatizo hili linaanzia katika mamlaka zao.**

***90. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu huduma ya mawasiliano na Elimu kwa Watoto, Wizara inaendelea kuratibu huduma ya msaada wa simu bila malipo Namba 116 (Child Helpline) kwa ajili ya jamii kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya Watoto au kupata elimu juu ya masuala ya Watoto. Aidha, huduma nyingine ni ile ya huduma kwa mteja inayotolewa na Wizara kupitia kituo cha huduma kwa mteja kilichopo Dodoma. Mteja anapiga simu kwenye namba 0262160250, 0734986503 na pia anaweza kupiga na kutuma ujumbe na kubaki na ushahidi kwenye namba 0774112233, 0769608130 na 0766400168) kwa ajili ya kuwasilisha changamoto zao moja kwa moja wizarani na kusaidia kuwaunganisha na huduma za wataalam katika sekta mbalimbali. **Natoa wito** kwa mamlaka za mikoa na wilaya nao kubuni na kuanzisha vituo vya huduma za mawasiliano na wateja ili kupunguza msongamano ngazi ya wizara na kubaki na rufaa. Hii itaongeza ufanisi zaidi.

***91. Mheshimiwa Spika,*** kwa ushirikiano na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wizara inatoa elimu kwa watoto na jamii kwa ujumla, na kufikia Aprili 2024, wizara imefanikiwa kurekodi vipindi viwili (2) vya malezi chanya kwa watoto vinavyoitwa Malezi na Makuzi (MAMAKUZI) na maadili kwa vijana vinavyoitwa Kijana na Maadili (KIJADILI) vyenye mada 20 ambavyo vimelenga kuelimisha jamii na vimerushwa nchini kote katika vyombo vya habari vya kijamii 150 na inatarajiwa kufanyika tathmini ili kupata matokeo yaliyopatikana kutokana na elimu hii. Mara baada ya tathmini hiyo kukamilika awamu ya pili ya vipindi itaanza.

***92. Mheshimiwa Spika,*** kupitia Programu Jumuishi ya Malezi na Makuzi (PJT MMAM), elimu ya malezi na makuzi kwa wazazi, walezi na jamii imeendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari na mikutano ya hadhara katika ngazi zote kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Katika kufanikisha hili, Wizara imevitambua vyuo 63 vya mafunzo ya Malezi ya Watoto nchini pamoja na kutoa mafunzo kazini kwa walezi wa watoto wadogo na wachanga mchana.

Jumla ya walezi 12,547 (Me 3,623 Ke 8,924) wameshiriki katika mafunzo ya kuongeza ufanisi wa huduma za uchangamshi wa awali na ulinzi kwa watoto.

**93.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau inaratibu na kutoa huduma ya msaada wa akili na kisaikolojia kwa makundi mbalimbali yanayokabiliwa na changamoto mbalimbali za kimaisha katika jamii yetu kwa lengo la kuwasaidia kuwa na siha njema kiakili na kisaikolojia na kimaendeleo na majukumu yao bila changamoto. Katika kuhakikisha, huduma hii inatolewa kwa ufanisi kupitia maafisa Ustawi wa Jamii, Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisaikolojia kwenye jamii katika Halmashauri zote nchini. Hadi kufikia Aprili 2024, Jumla ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 284,308 (Me 183,124 na Ke 101,184), wazee wasiojiweza 245 (Ke 145 na Me 100) na waathirika wa matukio ya ukatili 2,682 (watoto 1,944 na watu wazima 738) wamepatiwa huduma hii. Aidha, katika kipindi hicho huduma hii pia imetolewa kwa wahanga wa vitendo vya ukatili 13,926 (ke 7,142 na watoto 6,784) pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili wa usafirishaji haramu wa binadamu 452 (Me 05, Ke 447).

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, kufikia Aprili 2024, Wizara imeratibu utoaji wa huduma kwa jamii ya waathirika wa maporomoko ya matope yaliyotokea katika Wilaya ya Hanang', Mkoani Manyara ambapo jumla ya waathirika 9,016 walipatiwa huduma ya afya ya akili na kisaikolojia ikiwa ni pamoja kuwatoa hofu na kuwapa utulivu; kufanya tathmini ya mahitaji ya waathirika kwa mtu mmoja mmoja; familia na jamii na kuwapa huduma stahiki kulingana na mahitaji. Aidha, pia uratibu ulifanyika kwenye kutoa huduma za kisekta kama vile afya na kutambua wazazi wa kuaminika (Fit Persons) kwa watoto waliofiwa na wazazi wao, kwa ajili ya kuwahakikishia usalama wao na kutoa malezi ya muda kwa watoto hao. Vilevile, waathirika wapatao 690, kutoka kaya 140 waliokuwepo katika kambi za muda na ambao walipoteza makazi yao, waliunganishwa na ndugu na jamaa zao ili kuweza kupata hifadhi ya makazi na huduma nyingine.

***95. Mheshimiwa Spika***, huduma ya akili na kisaikolojia imetolewa pia katika jamii ambazo zimeathirika kwa mambo mengine kama: Magonjwa, Ukatili, na Migogoro ya ndoa na familia. Katika maeneo haya, Wizara imeratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa familia za waathirika wa ugonjwa wa kipindupindu watu 79,513 (Me 38,142 na Ke 41,371) katika mikoa ya Simiyu, Dar es Salaam, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Morogoro, Manyara, Katavi, Kigoma, Rukwa na Dodoma. Aidha, Wizara pia kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na wadau imeendelea kutoa huduma kwa waathirika 8,920 wa mafuriko katika Wilaya za Rufiji, Kibiti, Nsimbo, Mbeya Jiji na Mlimba.

***96. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha huduma inatolewa kwa wakati, Wizara imetoa Elimu ya Mafunzo ya namna ya kutoa huduma ya afya ya Akili na Msaada wa kisaikolojia na Kijamii kwa wathirika wa majanga mbalimbali kwa wataalam 68 katika Mikoa mbalimbali, na utoaji wa elimu hii ni endelevu.

***97. Mheshimiwa Spika,*** huduma ya Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa na Familia ni moja ya Majukumu ya Wizara hii ya jamii. Ikumbukwe kuwa, utulivu wa Ndoa na Familia ni msingi mkubwa ustawi wa familia na jamii kwa ujumla, kwani huzuia athari nyingi zikiwemo ukatili, Watoto wa mtaani na kuvunjika kwa Ndoa. Katika kuhakikisha kuna ustawi na utulivu wa familia, Wizara kupitia maafisa Ustawi wa Jamii, imeendelea kuratibu huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia kupitia Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii lililopo Makao Makuu ya Wizara, Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Jumuiya, Ofisi za Ustawi wa Jamii, wasaidizi wa msaada wa kisheria na Kampeni mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 2024, mashauri yaliyoshughulikiwa yalikuwa 31,380 ikilinganishwa mashauri 28,773 yaliyoshughulikiwa mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la mashauri 2,607 sawa na asilimia 8.3.
**Natoa wito kwa viongozi wa dini zote kuendelea kutoa mafunzo kwa wanandoa wanaofunga ndoa na kwa vijana kupitia mikusanyiko ya vijana katika madhehebu yao, ili kuwaandaa kubeba majukumu ya ndoa na kujiandaa kwa majukumu hayo kabla ya kuingia katika ndoa.**

***98. Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha huduma za Msingi zinatolewa kwa Wazee na watu wasiojiweza, Wizara imeendelea kutoa huduma za chakula, malazi, mavazi, matibabu na msaada wa kisaikolojia na kijamii katika makazi 13 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali, pamoja na wazee wanaoishi katika jamii. Wazee hawa waasio na uwezo hutambuliwa kupitia Ofisi za Ustawi wa Jamii zilizopo kwenye Halmashauri zote nchini. Hadi kufikia Aprili 2024, wazee wasiojiweza 240 (Ke 95 na Me 145) walihudumiwa katika makazi ya wazee ya Kibirizi (26), Njoro (18), Kolandoto (18), Bukumbi (27), Ipuli (24), Fungafunga (21), Mwanzange (14), Misufini (18), Nunge (18), Nyabange (14), Kilima (19), Sukamahela (16), Magugu (7). Pia, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu huduma za msingi zinazotolewa kwa wazee kwenye makazi ya wazee ya Taasisi Binafsi 15 yenye jumla ya wazee 268 (me 150, ke 118) katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Kagera, Shinyanga, Arusha, Tanga, Dodoma na Lindi.

***99. Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto na upungufu katika utoaji wa huduma za ustawi wa jamii, Wizara imejipanga kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi kwa kuleta mapendekezo ya kutunga sheria ya usimamizi wa watoa huduma za ustawi wa jamii katika nyanja zote za sekta ya Umma na Binafsi kwa lengo la kuwatambua, kuwasajili na kudhibiti ubora wa huduma wanazozitoa. Aidha, katika kutekeleza maagizo ya Kamati ya Mheshimiwa Rais ya kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Maboresho ya Haki Jinai, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na Taasisi nyingine ipo katika hatua ya kukamilisha **uanzishwaji kisheria kwa Idara ya Ustawi wa Jamii kama Idara inayojitegemea**, ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

***100. Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Wizara ya Afya imeendelea kuimarisha utaratibu wa utoaji huduma za matibabu kwa wazee wasiojiweza na ambao wanaishi katika jamii kwa kufanya utambuzi na tathmini na kisha kuwapatia vitambulisho vya kupata huduma za Afya bure katika vituo vya Afya.

***101.*** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya wazee 574,321 (Me 214,739, Ke 359,582) ambapo kati yao wazee wasiojiweza 365,284 (Me 145,829, Ke 219,455) sawa na asilimia 63.6 ya wazee wote waliofanyiwa tathmini, wamepatiwa vitambulisho maalum kwa ajili ya msamaha wa matibabu. Vilevile, kampeni ya "MPISHE MZEE KWANZA" inaendelea kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali ya Taifa ili kutoa kipaumbele na kuhakikisha wazee wanapata huduma za afya kwa wakati. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 kulikua jumla ya madirisha 1,066 ya huduma kwa wazee nchini kote ikilinganishwa na madirisha 629 yaliokuwepo mwaka 2022/2023 ikiwa na ongezeko la madirisha 437 sawa na asilimia 69.48.

***102.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ipo katika hatua za Mwisho za kukamilisha mabadiliko ya sera ya wazee ambapo miongoni mwa maboresho yatakayozingatiwa ni pamoja na umuhimu wa jamii kujiandaa kabla ya uzee, huduma wa afya ya akili na msaada wa kisaikolojia kwa wazee, miundombinu na mazingira wezeshi kwa wazee na uwezeshwaji wa wazee kwenye mabadiliko ya Teknolojia kama TEHAMA.

***103.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu bado inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii 17,485 ambayo ni sawa na asilimia 94.6 ya Maafisa wanaotakiwa kuanzia ngazi ya Mkoa mpaka ngazi ya Kijiji/Mtaa kama inavyoonesha katika Jedwali Na.5

**Jedwali Na. 5**: Idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika Ngazi Mbalimbali

| **Na** | **Ngazi** | **Maafisa Wanaohitajika** | **Maafisa Waliopo** | | **Upungufu** | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi | % | Idadi | % |
| 1. | Mkoa | 26 | 36 | 138 | 0 | - |
| 2. | Hospitali za Rufaa na Mikoa | 157 | 42 | 26.8 | 115 | 73.2 |
| 3. | Halmashauri | 1,472 | 575 | 39.1 | 897 | 60.9 |

| Na | Ngazi | Maafisa Wanaohitajika | Maafisa Waliopo | | Upungufu | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi | % | Idadi | % |
| 4. | Hospitali za Wilaya | 552 | 163 | 29.5 | 389 | 70.5 |
| 5. | Kata/Vituo vya Afya | 3,956 | 190 | 4.8 | 3,766 | 95.2 |
| 6. | Mtaa/Kijiji/ Zahanati | 12,318 | 0 | 0 | 12,318 | 100 |
| **Jumla** | | **18,481** | **1,006** | **5.4** | **17,485** | **94.6** |

***Chanzo: WMJJWM, 2024***

***104.*** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutaarifu Bunge lako kwamba katika kuendelea kufanyia kazi upungufu wa maafisa ustawi wa jamii, Serikali imetoa kibali cha kuajiri Maafisa 350 watakao sambazwa kulingana na mahitaji na mchakato wa ajira umeshaanza. Nichukue fursa hii kumshuruku Mheshimiwa Rais kwa kutoa kibali cha ajira hizo. Vilevile, napenda kumshukuru Waziri-OR Utumishi Mheshimiwa **George Simbachawene** kwa ufuatiliaji wake hadi kufanikisha suala hili. **Nakiri kuwa, bado uhitaji ni mkubwa hivyo, serikali itaendelea kuongeza wataalamu hawa kadri uwezo wa ajira unavyoruhusu.**

***105.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeadhimisha Wiki ya Ustawi wa Jamii ambapo kilele chake kilikuwa tarehe 18 Desemba, 2023. Katika maadhimisho hayo yafuatayo yalifanyika:

i. Elimu kuhusu huduma za Ustawi wa Jamii kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, televisheni na mitandao ya kijamii imetolewa ambapo jumla ya vipindi 24 vya redio na vipindi vitano (5) vya Luninga vimerushwa;

ii. Huduma mbalimbali zilitolewa kwa watu 9,314 bila malipo katika mikoa ya Dodoma, Tanga, Geita, Kigoma, Arusha, Dar-es-Salaam na Songwe. Huduma hizo ni pamoja na afya ya akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii, huduma kwa manusura wa vitendo vya ukatili, huduma za usajili wa vyeti vya kuzaliwa na

vifo, huduma za afya, elimu ya upimaji wa vinasaba, huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi zilitolewa moja kwa moja.

iii. Jumla ya watu 2,027 walishiriki Mkutano wa mwaka wa kiutendaji wa Maafisa Ustawi wa Jamii uliofanyika Septemba 2023 mkoani Dodoma na Kilele cha maadhimisho ya Miaka 50 ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii kilichofanyika Dar-es-Salaam. Washiriki wa mikutano hiyo ni Maafisa Ustawi wa Jamii 1,025, wadau 189, wamiliki wa vituo vya kulelea wototo wachanga na wadogo vya mchana na kijamii 813.

*iv.* Uzinduzi wa Kamati ya kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto iliyopo chini ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. **Mary Chatanda**, Mwenyekiti wa UWT Taifa na washiriki 1,850 walihudhuria.

**ENEO LA 5: MAENDELEO YA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE**

***106.*** **Mheshimiwa *Spika,*** katika eneo la maendeleo ya Jinsia na Uwezeshaji wanawake, Wizara ina jukumu la kuhakikisha kuna usawa wa jinsia kwenye maendeleo katika jamii yetu kwa kuwezesha wanawake kiuchumi ili waweze kuchangia katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya familia na nchi kwa ujumla. Katika kufanikisha hili, Wizara, inatekeleza Programu ya Kitaifa ya Kizazi Chenye Usawa 2021/22 – 2025/26 (Generation Equality Forum Commitments - GEF) ambapo Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Kinara wa utekelezaji wa eneo la Haki na Usawa wa Kiuchumi.

***107.*** **Mheshimiwa *Spika,*** programu ya Kizazi Chenye Usawa (GEF) inahusu utekelezaji wa haki za wanawake za kiuchumi kwenye maeneo manne (4) yakiwemo uwekezaji wenye mrengo wa kijinsia katika huduma na kazi za matunzo kwenye sekta za umma na binafsi, kazi zenye staha, upatikanaji na umilikishaji wa rasilimali za uzalishaji kiuchumi kwa wanawake, mipango ya uchumi jumla, maboresho ya kibajeti na vichocheo vya kiuchumi kwa kaya maskini vinavyozingatia jinsia.

***108. Mheshimiwa Spika***, Serikali imeteua Waratibu wa Programu hii na kutoa mafunzo kwao ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi. Jumla ya Waratibu 234 kutoka Wizara na Taasisi za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote wamepatiwa mafunzo juu ya uratibu, usimamizi na utekelezaji wa programu hii. Aidha, Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara zote ambao ni waratibu wa program hii wamepatiwa mafunzo. Wakati wa Mafunzo hayo, msisitizo uliwekwa katika kujenga uelewa juu ya umuhimu wa kuandaa bajeti yenye mrengo wa kijinsia (Gender Responsive Budgeting) na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Haki na Usawa wa Kiuchumi ambalo ni eneo namba 2 la utekelezaji wa Mpango wa Kizazi Chenye Usawa (GEF). Vilevile, uelewa juu ya Programu hii, unatolewa kwa jamii kwa kutoa taarifa zinazotekelezwa katika maeneo kuhusu fursa zilizopo kwa wanawake na wasichana katika maeneo yao.

***109. Mheshimiwa spika,*** moja ya mkakati wa kumkomboa wanamke ambao unazingatiwa katika Programu ya Kizazi Chenye Usawa, ni kuhakikisha anapata muda wa kushiriki katika shughuli za kiuchumi ili kuchangia maendeleo ya familia na nchi kwa ujumla. Katika kufanikisha hili, Wizara imeweka mkazo katika utekelezaji wa afua ambazo **zinalenga kumpa muda zaidi mwanamke zikiwemo, matumizi ya nishati safi, uanzishaji wa Vituo vya Kulelea Watoto Wachanga na Wadogo na upatikanaji wa maji safi na salama.**

***110. Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha dhamira hii, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta imetoa elimu juu ya matumizi ya nishati safi na salama ili kuongeza idadi ya watumiaji wa nishati hiyo katika kupikia. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya wananchi 1,228,248 wanatumia nishati safi ya kupikia. Aidha, katika idadi hiyo, jumla ya wanawake 102,000 wasiokuwa na uwezo walipatiwa majiko ya gesi bure ikiwa ni jitihada za Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwezesha wanawake kutumia nishati safi ya kupikia akiwa kinara wa utekelezaji wa Programu ya kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia Barani Afrika.

***111.*** ***Mheshimiwa spika,*** nishati nyingine ambazo zinawekewa mkazo kutumika na wanawake ni umeme na nishati jadidifu ambapo, matumizi yake yatachangia kuwawezesha wanawake kuanzisha viwanda vidogo vidogo pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi ambazo wanawake wengi wamejiajiri. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya vijiji 11,837 sawa na asilimia 96.37 ya vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara vimeunganishwa na umeme. Aidha, kaya 5,193,148 sawa na asilimia 37 ya kaya zote 14,152,803 nchini zimeunganishwa na umeme.

***112.*** **Mheshimiwa *Spika,*** upatikanaji wa maji safi na salama, ni njia nyingine ya kutoa muda kwa mwanamke kwa kumuondolea adha ya kufuata maji kutoka umbali mrefu. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Wadau wengine imeendelea kuwekeza kwenye upatikanaji wa maji safi na salama, kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua na utunzaji wa vyanzo vya maji. Uhamasishaji umefanyika kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya kaya 861,944 za mijini na 541,482 za vijijini zinavuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Aidha, kupitia uhamasishaji huu jamii imeweza kutumia mbinu mbadala za upatikanaji wa maji na utunzaji wa miundombinu ya maji kwa manufaa yao na kumsaidia mwanamke na mtoto wa kike. Vilevile, upatikanaji wa maji kwa sasa umefikia asilimia 90.1 kwa mijini na asilimia 79.6 kwa vijijini hatua ambayo imewezesha kumpunguzia muda mwanamke ili aweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Pia, kumekuwa na ongezeko la wanawake viongozi kwenye Jumuiya za Watumia Maji ambapo asilimia 33 ya viongozi ni wanawake na sasa kuna mwanamke mmoja katika viongozi 3 wa juu.

***113.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuonesha dhamira ya Serikali katika kukuza usawa wa kijinsia, Wizara yangu imeratibu wadau wa kisekta na kukamilisha hatua za kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 iliyozinduliwa tarehe 8 Machi, 2024 siku ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Wilayani Chamwino, Mkoa wa Dodoma.

***114.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Sera hiyo imezingatia masuala mbalimbali kama mabadiliko ya Tabia Nchi, ushirikishwaji wa wanaume katika jitihada za kuleta usawa wa kijinsia, matumizi ya teknolojia katika uzalishaji na mawasiliano, na ukatili wa kijinsia na ukatili wa mtandaoni. Masuala haya yote yamewekewa matamko na mikakati ya utekelezaji. Kwa kuwa hii ndio Sera Mama ya masuala ya jinsia nchini, utekelezaji wake utachochea jamii na wadau kuendeleza mafanikio yaliyopo katika utatuzi wa changamoto za wanawake na wanaume ili kuwa na Taifa la kizazi chenye usawa.

***115.*** **Mheshimiwa *Spika,*** katika kutekeleza Sera hiyo na kuzingatia maelekezo ya Mhe. Waziri Mkuu aliyoyatoa katika vikao vya Bunge hili kuhusiana na kufanya mapitio ya Sheria zinazohusu ukatili wa kijinsia, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, itaendelea kuboresha sheria mbalimbali na kanuni zake ili kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia uliokithiri katika jamii nchini. **Ninapenda kutumia nafasi hii kushukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Bunge lako tukufu, Wizara za kisekta na wadau wote ambao wamechangia katika kufanikisha kukamilika kwa Sera hii.**

***116.*** **Mheshimiwa *spika,*** katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta na wadau wengine wa Maendeleo, imehamasisha upatikanaji wa masoko kidijitali (digital markets) kwa kutoa elimu ya fedha, ujasiriamali kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (*Tanzania Women Chambers of Commerce*) walitengeneza mtandao wa kidigitali ujulikanao kama *iSOKO App* kwa lengo la kuwezesha wafanyabiashara wanawake kupata masoko ya bidhaa na huduma zao kupitia simu za mkononi. Kupitia afua hiyo, jumla ya wafanyabiashara wanawake 11,500 **wakubwa na wa kati wamejisajili** na kutumia *App* hiyo. Aidha, kumekuwa na ongezeko la wanawake katika matumizi ya simu ambapo asilimia 71 ya wanawake na asilimia 80 ya wanaume wanatumia simu. Ongezeko

hili limeongeza chachu kwa wanawake kuimarika kiuchumi kwa kuweza kupata masoko ya mtandao (*Digital marketing*) ndani na nje ya nchi.

***117.*** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu ya fedha kwa makundi mbalimbali wakiwemo wanawake ambapo, jumla ya watu 11,336 walipatiwa elimu kupitia Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika tarehe 8 Machi 2024, na Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa iliyofanyika Arusha Machi 2024. Uhamasishaji huo umewezesha kuanzishwa na kusajiliwa kwa vikundi 6,994 na hivyo kufanya jumla ya vikundi 49,168 vilivyosajiliwa. Aidha, usajili wa vikundi hivi umeleta ufanisi wa utoaji wa huduma kwenye sekta ndogo ya fedha ikiwemo upatikanaji wa huduma za mikopo ya vikundi yenye masharti nafuu kwa wanawake.

***118.*** **Mheshimiwa *Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Benki ya NMB imezindua akaunti maalum inayoitwa ***Vikundi Account*** ambayo ilizinduliwa tarehe 3 Mei, 2024. Akaunti hii ni mahsusi kwa vikundi mbalimbali vinavyoanzishwa na itawezesha vikundi hivyo vikihusisha wanawake kutekeleza shughuli zao za kiuchumi. Akaunti hii itawezesha vikundi kufungua akaunti vyenyewe, kufanya miamala ya kibenki, kuhamisha fedha kwa wanakikundi bila makato yoyote, kuchangia michango na kukopeshana mikopo ya kikundi kupitia simu zao. Aidha, Akaunti inawezesha vikundi kupata taarifa za fedha bila kufika tawi la benki, na kwamba vikundi vikifikisha kiasi cha Shilingi 500,000 kwenye akaunti yao watapata riba ya 3% kwa mwaka. Akaunti hii ni fursa kwa vikundi kujiimarisha kiutendaji na kuongeza uwazi kwa wanachama wake. **Niwaombe Watanzania wenzangu tuchangamkie fursa hii kujiunga katika vikundi na kuhakikisha kikundi kinakuwa na akaunti kwa maendeleo ya wanachama wake.**

***119.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na uendeshaji wa biashara kwa wanawake wajasiriamali. Kuanzia Julai 2023 hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya wanawake 2,222,000 wamepatiwa

mafunzo ya ujasiriamali katika nyanja za elimu ya fedha, matumizi ya teknolojia, masoko, mnyororo wa thamani na uongozi bora. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024, mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 748** imetolewa kupitia Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambapo jumla ya walengwa 6,064,957 wamenufaika na mikopo hiyo; kati yao wanawake ni 3,288,186 sawa na asilimia 54 na wanaume 2,776,771, sawa na asilimia 46.

***120.*** **Mheshimiwa *Spika***, wanawake ni miongoni mwa wadau muhimu wanaochangia utekelezaji na uendelezaji wa Sekta ya Madini ambapo takribani **asilimia 26 ya wanawake wamejiajiri** kwenye sekta ya madini katika maeneo ya uchimbaji mdogo, uchenjuaji, uongezaji wa thamani na utoaji wa huduma. Katika kuhakikisha wanawake wanazidi kuwekeza katika sekta hii na kukuza ushiriki wao katika mnyororo mzima, Wizara kwa kushirikiana na Wizara mama ya Madini imewezesha vifaa kwa vikundi 10 vya wachimbaji wadogo.

***121. Mheshimiwa Spika***, kutokana na mikakati iliyowekwa na Serikali yetu kuhusu utekelezaji wa usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi, nchi yetu imepiga hatua kubwa ambayo, imesababisha, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, UN Women, na wadau wengine kupata heshima ya kuandaa kikao kazi cha viongozi wa juu wa Afrika (*African High Level Gender Financing meeting*) kilichofanyika tarehe 15 hadi 17 Novemba, 2023. Kikao hiki kilijumuisha wadau kutoka bara la Afrika na mataifa mengine. Lengo la kikao hicho ni kusisitiza umuhimu wa kutenga na kuwekeza rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa masuala ya kijinsia na uwezeshaji wa Wanawake.

***122.*** **Mheshimiwa *Spika,*** kupitia Mkutano huo na jitihada zinazoendelea kutekelezwa hapa nchini, **Tanzania ni miongoni mwa Mataifa ya mfano yenye ushahidi katika uzingatiaji na ujumuishaji na masuala ya jinsia katika mipango ya Kitaifa na bajeti za Kisekta na Taasisi** kutokana na uwepo wa Miongozo ya Bajeti ambayo hutolewa kila mwaka na Serikali. Mwongozo wa bajeti ya mwaka

2024/25 umeainisha kipengele kinachoelezea kila wizara na taasisi kujumuisha masuala ya Jinsia kwenye bajeti zao za mwaka 2024/25. Hivyo, ni matumaini yangu kuwa, Waheshimiwa Mawaziri na Wakuu wa Taasisi **mtakuwa mmezingatia kipengele hiki wakati wa uandaaji wa bajeti zetu za mwaka huu**. Suala la Jinsia ni mtambuka tukiungana kwa pamoja kama nchi tutaweza kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SGDs) kuhusu Jinsia kama yalivyoelekezwa.

***123.*** **Mheshimiwa *Spika*,** kupitia sheria iliyopitishwa ya kuwawezesha wanawake kupata zabuni mbalimbali, **asilimia 30** ya zabuni zote inatakiwa kupatiwa kwa makundi maalumu wakiwemo wanawake. Katika kutekeleza hili, Wizara kwa kushirikiana Wizara nyingine za kisekta pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeendelea kuhamasisha vikundi vya wanawake kutumia fursa hiyo kwa zabuni zinazotangazwa na Serikali. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya vikundi 33 vya wanawake wamepewa zabuni zenye thamani ya Shilingi 1,372,948,845.55 ili kuwawezesha wanawake kujiajiri, kuongeza kipato na kuinua uwezo wa shughuli za vikundi vyao. Tunashukuru na kupongeza Bunge lako tukufu kwa kupitisha Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma, 2023 ambayo imeimarisha ushiriki wa makundi maalum ikiwemo wanawake katika fursa za ununuzi wa umma.

***124.*** **Mheshimiwa Spika**, kwa kushirikiana na Sekta ya mifugo na uvuvi, jumla ya wavuvi wanawake 1,023 wamekopeshwa boti za kisasa za uvuvi na wanawake 446 wamekopeshwa vizimba vya kisasa vya kufugia Samaki bila riba. Aidha, Wanawake 24 wamepatiwa mafunzo yanayohusu utotoleshaji wa vifaranga vya kuku, na wanawake 38 wamewezeshwa kuwa wazalishaji wa vitotoleshi. Katika mlengo huo wa kuwawezesha wanawake, Wizara imefanikisha upatikanaji wa mashine 250 za ututoleshaji vifaranga vya kuku na vyerehani 425 vyenye thamani ya Shilingi Milioni 79 kutoka Serikali ya Watu wa China ambavyo vitasambazwa kwa wanawake nchini. Jitihada hizi zitawezesha wanawake kuongeza ari miongoni mwao na kuongeza fursa ya kujiajiri katika sekta ya uvuvi, mifugo na ushonaji.

***125.*** ***Mheshimiwa Spika***, uanzishaji wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ni fursa kwa wanawake kuweza kukutana na kujadili masuala mbalimbali wanayokabiliana nayo katika shughuli zao za kujikwamua kiuchumi ikiwemo kuweka mikakati ya ufumbuzi. Aidha, Majukwaa haya yameongeza kazi zenye staha kwa wanawake katika sekta rasmi na sekta isiyo rasmi kwa kufanikisha utambuzi na usajili wa vikundi vipatavyo 43,574 vya wanawake baada ya kukidhi vigezo vya kupata mikopo ya asilimia 10 inayoyotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri. Vikundi vilivyotambuliwa vina jumla ya wanachama 13,778,700 vinavyojishughulisha na ujasiliamali wa bidhaa na huduma mbalimbali. Katika kuhakikisha idadi ya majukwaa haya yanaongezeka, Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa Majukwaa haya. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya majukwaa 3,391 yameanzishwa yakijumuisha majukwaa ngazi ya Mkoa 26, Halmashauri 152 kati ya 184, Kata 1,354 kati ya 3,957 na Mitaa/Vijiji 1,859 kati ya Vijiji 12,348. Aidha, Wizara katika kuboresha utendaji kazi wa Majukwaa inakamilisha maandalizi ya Mwongozo wa Uundaji na Uratibu wa majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ili kuyafanya yawe na ufanisi zaidi.

***126.*** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na uanzishaji wa majukwaa haya, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa wanawake kwenye Maonyesho mbalimbali ya biashara. Maonesho haya huwapatia fursa wanawake kushiriki na kutangaza bidhaa zao ili kupata masoko ya ndani na nje ya nchi na kuchangia kuongeza wigo wa mtandao wa mawasiliano na mnyororo wa thamani wa bidhaa zao. Hadi kufikia Aprili, 2024, Wizara iliwezesha ushiriki wa wanawake 336 katika maonesho ya Sabasaba yaliyofanyika jijini Dar es Salaam na wanawake 1,880 katika maonesho ya Nanenane na Sherehe za Wakulima yaliyofanyika Kitaifa Jijini Mbeya.

***127.*** **Mheshimiwa *Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*Women Development Fund* - ***WDF***) ambao una lengo la kuwawezesha wanawake kwa kuwapatia mikopo ya fedha ili kujikwamua kiuchumi. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya Shilingi Milioni 77.5 zimerejeshwa kutokana na mikopo

iliyotolewa kwa wanawake ikiwa ni jumla ya Shilingi 664 zilizokopeshwa kwa wajasiriamali 104 kutoka kwenye vikundi 11 na wakopaji mmoja mmoja 14. Aidha, Wizara kuanzia Julai 2024 itarejesha mikopo hii kwa utaratibu utakaotangazwa.

***128.*** **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa wito kwa wanawake wote waliokopeshwa na watakao kopeshwa kuzingatia masharti ya mikopo kwa kufanya marejesho kwa mujibu wa mikataba. Aidha, ***ninatoa wito kwa Halmashauri zote zinazodaiwa fedha zinazotokana na mfuko huu kurejesha mikopo yao kwa makubaliano yaliowekwa ili kuuwezesha Mfuko huu kuwafikia wanawake wengi zaidi nchini.***

***129.*** **Mheshimiwa *Spika***, katika kuwawezesha wanawake katika nafasi za uongozi, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wadau wengine, imeendelea kutoa mafunzo ya uongozi kwa wanawake ili kuhamasisha na kuwajengea uwezo wa kujiamini na kuthubutu kushiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi na maamuzi, rejea Jedwali namba 6 linaloonesha hali ya nafasi za uongozi kwa wanawake kwenye baadhi ya nafasi.

**Jedwali Na.6. Wanawake na nafasi za Uongozi**

| Na | Nafasi ya Uongozi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| **1** | Mawaziri | 31 |
| **2** | Manaibu Waziri | 19 |
| **3** | Mabalozi | 25 |
| **4** | Wabunge | 37 |
| **5** | Madiwani | 34 |
| **6** | Makatibu Wakuu | 22 |
| **7** | Naibu Katibu wakuu | 28 |
| **8** | Wakuu wa Mikoa | 31 |
| **9** | Makatibu Tawala | 26 |
| **10** | Wakuu wa Wilaya | 33 |
| **11** | Wakurugenzi wa Halmashauri | 28 |

***130.*** **Mheshimiwa *Spika,*** kama inavyoonekana kwenye jedwali la takwimu hapo juu, ushiriki wa Wanawake katika nafasi za uongozi

na maamuzi hapa nchini umeendelea kuongezeka katika nafasi mbalimbali. Hii inachangiwa na dhamira ya dhati ya Kiongozi wetu Mkuu wa nchi ya kuhakikisha wanawake hawaachwi nyuma kushiriki katika nafasi za maamuzi***. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwaamini na kuwateua wanawake katika nafasi mbalimbali za Maamuzi na Uongozi.*** Hivyo, wanawake wenzangu tuendelee kuchapa kazi kwa weledi na uaminifu katika kila eneo tulilokabidhiwa huku tukiendelea kujiamini.

***131.*** **Mheshimiwa *spika,*** umiliki wa Ardhi kwa wanawake ni moja ya nguzo muhimu katika uwezeshaji wanawake kiuchumi, kwa sababu hati miliki za ardhi zinatoa utambuzi wa kisheria na usalama kwa wanawake na kuzitumia kama dhamana ya kupata mikopo hivyo kuongeza fursa kwa wanawake kijiwezesha Kiuchumi. Katika kulifanikisha hili, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wadau mbalimbali imeendelea kuhamasisha Wanawake kumiliki Ardhi, kupitia kampeni maalum ijulikanayo kama ***Stand for Her Land Campaign.***

***132. Mheshimiwa Spika,*** kupitia hamasa na Kampeni hii, mafunzo yalitolewa kwa jumla ya viongozi 3,063 wa Serikali za Mitaa (KE 1,234, ME 1,829) juu ya utaalam na umuhimu wa kusimamia, kulinda, na kutekeleza haki za ardhi za wanawake pamoja na kushughulikia masuala ya changamoto za umiliki wa ardhi zinazoathiri wanawake. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa wananchi 83,886 kuhusu sheria na kanuni zinazohusiana na ardhi, usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wa jamii, haki za ardhi kwa wanawake na nafasi ya wanawake katika umiliki wa ardhi.
Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **vyeti vya kimila** (*Certicate of Customary Right of Occupancy - CCROs*) vimetolewa kwa wanawake 45,528. Wizara itaendelea kuhamasisha jamii kutambua juu ya umuhimu wa Wanawake kumiliki ardhi ili kunufaika na fursa mbalimbali za uwezeshwaji Kiuchumi.

***133.*** **Mheshimiwa *Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta pamoja na wadau wengine, ina jukumu la

kuelimisha jamii kuachana na vitendo vya **ukatili wa kijinsia**. Katika kufanikisha hili, shughuli mbalimbali ikiwemo kampeni ya **"Zijue Fursa, Imarisha Uchumi, Kataa Ukatili, Kazi Iendelee" (ZIFIUKUKI)** huratibiwa na wizara. Tarehe 25 Novemba hadi 10 Desemba, 2023 Wizara kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali (WiLDAF) imeratibu Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia **katika mikoa yote nchini**, ambapo kilele cha kampeni hii ilifanyika Mkoa wa Mara tarehe 10 Disemba 2023. Lengo la Kampeni hii ni kuongeza jitihada za jamii kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia ambapo Kaulimbiu ya Mwaka huu ilikuwa **"Wekeza: Kuzuia Vitendo vya Ukatili"**.

***134.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ujumbe wa kampeni hii unawafikia wananchi wengi, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliratibu Msafara wa Kijinsia ambao ulipita katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Singida, Tabora, Kagera, Mara, Geita na Kigoma na jumla ya wananchi 9,393 wakiwemo wanafunzi 8,503, walimu 167, waendesha bodaboda 347, wafanyabiashara sokoni 146, na waumini wa madhehebu mbalimbali 230 walifikiwa katika nyumba zao za ibada. Msafara huo ulitoa huduma mbalimbali katika maeneo ambayo ulipita zikiwemo huduma za msaada wa kisheria, kisaikolojia, elimu ya masuala ya jinsia pamoja na uwezeshaji wanawake kiuchumi.

***135.*** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeratibu Matamasha ya Maendeleo mwezi Desemba 2023 na Machi 2024, katika mikoa ya Geita na Dodoma. Matamasha haya yalilenga kutoa elimu na uelewa juu ya fursa za kiuchumi, na athari za ukatili wa kijinsia. Kupitia Matamasha haya jumla ya wananchi 45,895 (Me 21,830 na Ke 24,065) kwa mikoa hii miwili walipata huduma mbalimbali zikiwemo huduma ya msaada wa kisheria, kisaikolojia, elimu ya masuala ya jinsia, na biashara na huduma za afya.

***136.*** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Mwongozo wa Uanzishwaji, Uendeshaji na Ufuatiliaji wa Madawati ya Jinsia Katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati (2021), Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji wa **madawati ya jinsia** katika Taasisi za Elimu ya Juu na

Maeneo ya umma. Sambamba na uanzishwaji wa madawati haya, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo pamoja na Waratibu wa Madawati haya ili kuwapa uelewa na uwezo wa kuyaratibu na hatimaye, kutokomeza ukatili katika maeneo yao. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya Madawati 612 yameanzishwa na kati ya hayo, 296 (48.4%) ni madawati ya jinsia.

***137. Mheshimiwa Spika,*** uanzishwaji wa madawati haya umekuwa nyenzo muhimu kwa wanafunzi, walimu, watoa huduma na jamii inayozunguka Taasisi hizo na vyuo kushiriki katika kupinga ukatili wa kijinsia. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya matukio 44 ya ukatili wa kijinsia yaliripotiwa katika maeneo haya ambapo matukio 39 yalipatiwa ufumbuzi na matukio 5 yalipewa rufaa kwenda kwenye Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo mbalimbali vya Jeshi la Polisi nchini**.** Matukio yaliyopatiwa ufumbuzi yanajumuisha matukio (3) ya shambulio la aibu, ujumbe wa picha (6), rushwa ya ngono (5), kutelekeza familia (7), kurubuni (1), shambulio la mwili (14), na matamshi/ ishara (8). **Wizara itaendelea kufuatilia na kuimarisha madawati haya ili kukabiliana na vitendo vya ukatili vyuoni.**

***138. Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia inatekeleza Mwongozo wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Dawati la Kutokomeza Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia katika Maeneo ya Umma (2023) kwa kutoa mafunzo kwa waratibu 47, wanaotoka katika masoko ya Halmashauri 46 za mikoa sita (6) ili kuwajengea uwezo wa kuanzisha madawati katika maeneo ya umma. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya waratibu 250 kutoka Halmashauri 46 za Mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam walipatiwa mafunzo ya uanzishwaji na uendeshaji wa Dawati la Jinsia katika maeneo ya umma. Aidha, baada ya mafunzo hayo, waratibu hawa walifanikiwa kuanzisha jumla ya madawati 115 katika maeneo ya masoko ya Mikoa hiyo. **Madawati haya yatasaidia kuondokana na Ukatili wa Kijinsia unaofanyika kwenye maeneo ya masoko ambapo wanawake ni wahanga wakubwa wa matukio haya.**

***139. Mheshimiwa Spika,*** uingizwaji wa masuala ya Jinsia ni kipaumbele ambacho Wizara imeendelea kusimamia ili kuwa na

Sera, Mipango, Programu, Mikakati, Miongozo na Bajeti za Wizara za Kisekta na Sekta binafsi zenye mlengo wa kijinsia. Katika kutekeleza hilo, Ofisi ya Rais Utumishi kwa kushirikiana na Wizara **imezindua Mwongozo wa Ujumuishaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma wa Julai 2023,** ambao unaimarisha utekelezaji wa masuala ya Jinsia katika utumishi wa Umma. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza nchini imewezesha kuandaliwa kwa mkakati wa uingizwaji wa masuala ya Jinsia wa Jeshi hilo unaozingatia kundi la wafungwa wanaohudumiwa.

***140. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Anayeishi kijijini ambayo huadhimishwa kila mwaka tarehe 15 Oktoba. Kwa Mwaka 2023, Wizara kwa kushirikiana na Mkoa wa Arusha pamoja na wadau wengine ilishiriki maadhimisho haya yaliyofanyikia Kata ya Levolosi (Wilaya ya Arusha, Mkoani Arusha). Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa ni "**Wezesha Wanawake wanaoishi kijijini: Kwa uhakika wa Chakula, Lishe na Uendelevu wa Familia".** Vilevile, maadhimisho hayo yaliambatana na Kongamano la wanawake wanaoishi kijijini lililobeba ujumbe wa umiliki wa ardhi, mirathi na Maadili kwa vijana. Mwanamke anaeishi kijijini amebeba taswira pana ya uchumi wa nchi yetu ambao kwa kiasi kikubwa unategemea Kilimo na shughuli nyingine kama ufugaji, uvuvi, uchimbaji ambazo hufanyika katika maeneo ya vijijini.

***141. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Wanawake 1,600 walifikiwa katika maadhimisho haya kwa Wilaya ya Arusha. Aidha, maadhimisho haya yalifanyika Mikoa yote hapa nchini ambapo kila Mkoa uliadhimisha siku hii kwa kushirikiana na Wadau waliopo katika Mkoa husika. ***Nichukue fursa hii, kuisihi jamii na wananchi wote kuthamini na kutambua mchango mkubwa unaofanywa na wanawake wanaoishi Vijijini katika kuzalisha chakula kinachotosheleza nchini.***

***142. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine iliadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani iliyofanyika tarehe 8 Machi 2024 katika mikoa yote nchini. Wizara ilishiriki maadhimisho haya katika wilaya ya Chamwino Mkoani

Dodoma. Lengo likiwa ni kujenga hamasa, mshikamano na uwezo wa wanawake kushiriki katika maendeleo ili kufikia usawa wa kijinsia. Katika maadhimisho hayo, wanawake zaidi ya 10,000 wa Mkoa wa Dodoma na mikoa jirani walishiriki na walipata huduma mbalimbali zikiwemo za kibenki na nyingine zilizolenga kuwawezesha kiuchumi. Katika Maadhimisho hayo katika Mkoa wa Dodoma, Mgeni rasmi alikuwa **Mhe; Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye nilimwakilisha. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa "**Wekeza kwa Wanawake: Kuharakisha Maendeleo ya Taifa na Ustawi wa Jamii".**

***143. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshiriki Mikutano ya Kimataifa na Kikanda kwa ajili ya kutekeleza masuala ya Jinsia na Uwezeshaji Wanawake ambayo nchi yetu imeridhia. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, Wizara ilishiriki Mkutano wa *Women Deliver* uliofanyika Nchini Rwanda Kigali Julai, 2023. Pia Tulishiriki katika Mkutano wa 13 wa Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya wanawake wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola (JYM) – *The 13th Commonwealth Women's Affairs Ministerial Meeting* (CWAMM) uliofanyika Agosti 2023, Jijini Nassau, Bahamas.

***144. Mheshimiwa Spika,*** *Wizara* imeshiriki katika Mkutano wa Mapitio kipindi cha kati cha utekelezaji wa Programu ya kizazi chenye Usawa (*GEF Mid-Point Review*) uliofanyika Jijini New York Marekani Septemba, 2023 ambapo nilimuwakilisha Mheshimiwa Rais, ambaye alialikwa kama Mgeni Mahsusi. Aidha kuanzia tarehe 11 mpaka 22 Machi 2024, Wizara tulishiriki Mkutano wa 68 wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake Duniani uliofanyika Jijini New York, Marekani, ambapo Mhe. Spika wewe binafsi ulishiriki Pamoja nasi kwa nafasi yako ya Rais wa Mabunge ya Dunia.

***145. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kutekeleza matakwa ya ushiriki wa nchi katika mikutano hii, ushiriki wetu umekuwa na manufaa mengi ikiwemo kujifunza kutoka kwa nchi wanachama masuala yanayohusu wanawake na uwezeshaji kijinsia na hatimaye kuongeza uzoefu wa nchi katika masuala haya.

***146.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha mtoto wa kike anapata elimu na kumuendeleza kielimu ili kuweza kujikomboa kiuchumi na kimaisha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na wadau wa maendeleo imeendelea kutekeleza mikakati ya kumuendeleza mtoto wa kike kupitia programu mbalimbali, zikiwemo ***integrated training for entrepreneurship promotion*** (INTEP), ambapo jumla ya wanufaika 2,101 (KE 1483, ME 618) walinufaika. Aidha, uhamasishaji wa wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali wakiwemo wasichana waliokatisha masomo ya Sekondari ulifanyika ambapo wasichana 3,022 waliandikishwa kuendelea Shule ya Sekondari kwa njia mbadala.

***147.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ufadhili wa masomo ya sayansi na hisabati kwa wasichana (STEM), wasichana 21,991 kati ya 46,455 walichaguliwa kusoma tahasusi za sayansi na hisabati. vilevile, kupitia Programu ya *Samia Scholarship* jumla wasichana 417 kati ya 1,025 wamepewa ufadhili kusoma masomo ya sayansi katika vyuo mbalimbali. Aidha, Uwekezaji mkubwa wa Serikali katika sekta ya Elimu hususan mikakati inayogusa kumuendeleza mtoto wa kike imewezesha uwepo wa **uwiano wa 1:1 katika uandikishaji wa watoto wa kike na kiume katika Elimu ya Msingi**. Hii ni hatua kubwa katika safari ya kumkomboa mtoto wa kike. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara ya Elimu kwa kushirikiana Wizara za Kisekta ilifanikisha maadhimisho ya kitaifa ya wanawake na wasichana katika sayansi yenye lengo la kuimarisha na kuhamasisha ushiriki wa wanawake na wasichana katika masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Jumla ya wanawake na wasichana 1,500 walishiriki maadhimisho hayo yaliyofanyika Februari, 2024.

***148.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa michezo na utamaduni katika kuchangamsha mwili, kuleta furaha, kuimarisha Afya, kutoa fursa za Ajira, na hali kadhalika kuitangaza nchi kimichezo na kitamaduni, Wizara kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Michezo na Utamaduni Pamoja Wizara nyingine za Kisekta na wadau wengine wa michezo imeendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake na wasichana katika michezo.

***149. Mheshimiwa Spika,*** kupitia jitihada za Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukuza ushiriki wa michezo kwa makundi mbalimbali nchini, yakiwemo ya wanawake na wasichana, hivi karibuni tumeshuhudia Timu ya Taifa ya Wanawake ya Mpira wa miguu "Twiga Stars" kufuzu kucheza mashindano ya WAFCON yanayotarajiwa kufanyika Juni, 2024 nchini *Morocco*. Vilevile, Timu ya Wavu ya KOROSHO Queens ya Mkoani Mtwara inayodhaminiwa na Bodi ya Korosho Tanzania walitwaa ubingwa wa Mashindano ya Wavu ya ukanda wa Afrika Mashariki yaliyofanyika nchini Rwanda mwezi Agosti, 2023. Wizara itaendelea kuhamasisha ushiriki wa Wanawake kwenye michezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa shule za michezo mahsusi kwa wasichana ili kuzalisha vipaji na ajira nchini.

***150. Mheshimiwa Spika***, wakati ninapohitimisha katika eneo hili la usawa wa kijinsia na Uwezeshaji wanawake kiuchumi, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, jitihada za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, ameiweka Nchi yetu katika nafasi nzuri Kimataifa katika utekelezaji wa usawa wa jinsia kwa vitendo katika nyanja zote. Hivyo, Bunge lako tukufu, watumishi wote, Wadau wa Maendeleo, jamii kwa ujumla, na kwa upekee **WANAWAKE WOTE** hatuna budi kumpongeza na kumuunga mkono katika jitihada hizi kwa kuendelea kujenga uelewa na fursa kwa mafanikio zaidi hapa nchini.

***ENEO LA 6: URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI.***

***151. Mheshimiwa Spika,*** usajili, uratibu na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unalenga kuweka mazingira wezeshi kwa mashirika hayo kuendelea kutoa michango yao katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla kupitia miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya Kilimo, Afya, Mazingira, Maji, Elimu, Jinsia na Utawala Bora. Aidha, Usajili na uratibu huu unafanywa kwa kuzingatia Sheria ya Mashiriki Yasio ya serikali, Sura ya 56. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara **imesajili** jumla ya Mashirika 1,028 na kufanya jumla ya mashirika yote yaliyosajiliwa kufikia 10,538. Kati ya Mashirika

yaliyosajiliwa katika kipindi hiki, Mashirika ya Kimataifa ni 43, Kitaifa ni 937, Kimkoa ni 29 na Kiwilaya Mashirika 19.

***152. Mheshimiwa Spika***, kuhusu ufuatiliaji, Wizara kwa kushirikiana na Wasajili Wasaidizi wa Mikoa na Halmashauri imeendelea kufanya ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kubaini kama wanatekeleza kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na pia matumizi sahihi ya fedha kwa kuzingatia malengo ya kusajiliwa. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili 2024, jumla ya Mashirika 1,124 yamefuatiliwa kati ya mashirika yote (10,538). Aidha, uchaguzi wa mashirika haya yanayofuatiliwa hufanyika kulingana na afua ambazo ni kipaumbele cha mwaka huo.

***153. Mheshimiwa Spika***, katika ufuatiliaji huo Mashirika mengi yalibainika kutekeleza kazi zao kwa kuzingatia sheria. Vilevile, miradi ya kisekta iliyotekelezwa imeinufaisha jamii mathalani ujenzi wa vyoo, kusaidia watu wenye ulemavu (kuimarisha utengamavu), kuwajengea uwezo walimu wa shule namna ya kuwahudumia watoto wenye ulemavu, kuwezesha makundi mbalimbali kiuchumi (kutoa elimu ya ufundi wa cherehani, kuwapatia wananchi mifugo kama ngo'mbe wa maziwa), kuchimba visima virefu vya maji; kuwezesha uundwaji wa mabaraza ya watoto na kuwezesha watoto kushiriki Baraza la Watoto Taifa. Vilevile, umefanyika uwezeshaji wa mtoto mmoja kushiriki kwenye Mkutano wa Dunia wa Watoto uliofanyika nchini Marekani.

***154. Mheshimiwa Spika***, aidha, Mashirika 775 kati ya 1,124 yalibainika kuwa na mapungufu yakiwemo, kutowasilisha kwa wakati ripoti za mwaka kuhusu kazi zao na kutokulipa ada za usajili za mwaka. Wizara kupitia Ofisi ya Msajili, ilitoa onyo kwao na kuwataka kuzingatia matakwa ya kisheria.

***155. Mheshimiwa Spika*****,** Katika suala la Uratibu, *Wizara* inaratibu shughuli mbalimbali zikiwemo za mikataba ya ufadhili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa kanuni namba 609 ya Mwaka 2018 inayoweka misingi ya uwazi na uwajibikaji wa fedha za

wafadhili. Katika mwaka 2023/24, Wizara imetoa vibali vya mikataba 316 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 377** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kisekta ikiwemo afya, elimu, mazingira, kilimo, maji, haki za binadamu na utawala bora. Nyingine ni uboreshaji wa miundo mbinu, uwezeshaji wa jamii na ulinzi wa jamii. Kabla ya kutoa vibali vya mikataba kusainiwa, ofisi ya usajili inalazimika kujiridhisha juu ya mfadhili anayetoa fedha na pia mpango wa matumizi ya fedha hizo kwa mashirika.

***156.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kufanya ufuatiliaji na uratibu kuwa rahisi pamoja na kuongeza uwazi wa kazi za mashirika yasiyo ya kiserikali, Wizara imeboresha **Mfumo wa Kielektroniki** wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuongeza sehemu ya **Ramani ya Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**. Ramani ya utambuzi imelenga kuwezesha wadau, Taasisi za Serikali na Jamii kwa ujumla kupata taarifa za Mashirika haya kwa urahisi mahali popote walipo.

***157.*** ***Mheshimiwa Spika***, mfumo huu ulizinduliwa na **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Wakati wa Mkutano wa Jukwaa la mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali lililofanyika jijini Dodoma tarehe 05 Oktoba, 2023. Hadi kufikia Aprili 2024 **jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 10,538 yameshatambuliwa kwenye ramani** na tayari yamewekewa taarifa kuanzia ngazi ya kata.

***158.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hali ya kuufahamisha umma na Wadau wa Maendeleo juu ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Kila Mwaka Wizara inaandaa taarifa ya mchango wa Mashirika hayo katika Maendeleo ya Taifa. Kwa mwaka 2022 Wizara ilikamilisha taarifa hii na tarehe 03 – 05 Oktoba 2023, Wakati wa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali taarifa hii ilisambazwa kwa wadau mbalimbali **yakiwemo Mashirika yenyewe**, Wadau wa Maendeleo na Taasisi binafsi.

***159.*** ***Mheshimiwa Spika***, aidha, taarifa hiyo imebainisha kuwa, katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2022, **jumla ya Mashirika**

**1,257 yaliyowasilisha taarifa zao yalipokea kiasi shilingi 2,249,244,846,280/=** kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,959,334,118,380/= zilitumika katika utekelezaji wa miradi kwenye afua za mazingira, afya, uwezeshaji jamii, ulinzi wa jamii, kilimo, elimu, utawala bora, maji, haki za binadamu na jinsia na kiasi cha shilingi 289,910,727,900/= zilitumika katika kulipa posho na mishahara, kodi za ujuzi, kodi za mishahara, michango katika Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

***160.*** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na manufaa ya ujumla kwa jamii katika Nyanja tofauti ambazo nimeelezea hapo juu, vilevile kazi na huduma za mashirika haya zimeweza kutoa ajira kwa jumla ya watu 9,974 ambapo, kati ya hao Watanzania ni 9,818 na Wageni 156. Manufaa Mengine ni kuchangia katika pato la Taifa kwa kulipa Kodi na michango mbalimbali kwa mujibu wa sheria.

***161.*** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na taarifa ya jumla ya mchango wa mashirika yasiyo ya Serikali ambayo hutolewa kila Mwaka, katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2023, Wizara kwa Kushirikiana na Mtandao wa TAWASANET chini ya Wizara ya Maji, imeandaa Taarifa ya Mwaka ya Mapitio ya Utekelezaji Katika Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira kwa kuangalia mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Sekta ya Maji. Taarifa hiyo ambayo iliwasilishwa kwa Wadau wa Maendeleo ya Sekta ya Maji wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Maji tarehe 16 - 22 Machi 2024, imeainisha mchango wa asasi za kiraia katika sekta hii kwa mwaka 2022 na 2023 ambapo, mchango umekuwa jumla shilingi 63,311,771,943, ambazo zilitumika katika kutekeleza wa miradi ya maji.

***162.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) inaratibu Majukwaa ya Mashirika Yasio Ya serikali kila Mwaka katika Ngazi zote (Wilaya, Mikoa, Taifa). Lengo la Majukwaa haya ni kuwezesha majadiliano kati ya mashirika, Serikali na wadau wa maendeleo kuhusu ukuaji na maendeleo ya sekta. Aidha, wakati wa Majukwaa hayo, shughuli mbalimbali za kijamii hufanyika kama sehemu ya

maadhimisho zikiwemo mfano; uchangiaji wa damu na upandaji wa miti. Katika kipindi cha mwaka 2023/24, majukwaa katika ngazi zote yalifanyika likiwemo lile la Ngazi ya Taifa lililofanyika tarehe 03 – 05 Oktoba 2023 ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa **Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***163.*** ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2,427 yalishiriki katika Jukwaa la Taifa na Kupitia jukwaa hilo; jumla ya chupa 165 za Damu zilitolewa na washiriki kama mchango kwa wahitaji, vilevile upandaji wa miti 300 katika shule ya sekondari ya Ilazo na kutoa mahitaji mbalimbali kwa Watoto 80 wanaoishi kwenye kituo cha watoto yatima cha Matumaini kilichopo Mihuji Dodoma.
***Mhe Spika Nichukue fursa hii, kuipongeza Mikoa na Halmashauri zote zilizojitokeza kuratibu majukwaa katika ngazi zao kwani majukwaa hayo yanaimarisha uratibu wa pamoja na ushirikiano na Mashirika hayo kuanzia ngazi za msingi hadi Taifa. Aidha, natoa rai kwa Mikoa kuendelea kuratibu mikutano hiyo muhimu kwa maendeleo ya sekta kwa mwaka 2024.***

***164.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaratibu uendeshaji wa ***bodi*** inayosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 kwa kufanya vikao kila robo. Lengo la vikao hivi ni kujadili, kushauri na kutoa maamuzi kuhusu uendeshaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Katika mwaka 2023/24 Vikao vya robo mbili za kwanza vilifanyika tarehe 25 Oktoba 2023 na tarehe 14 Machi, 2024 ambapo, kupitia vikao hivyo, wajumbe wa Bodi walitoa ushauri na kuelekeza Wizara na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kufanya uchaguzi wa wajumbe wa NaCoNGO ifikapo Juni, 2024. Aidha, vikao hivyo viliyafutia usajili Mashirika 15 kutokana na kushindwa kujiendesha.
***Naipongeza Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini. Aidha, natoa rai kwa Mikoa na Halmashauri kutoa ushirikiano katika kufanya Uchaguzi wa***

***wajumbe wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa maendeleo ya sekta.***

***165. Mheshimiwa Spika***, kwa vile shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hufanyika katika sehemu zote mbili za Muungano, kwa maana ya kwamba baadhi ya Mashirika yanayosajiliwa Bara hufanya kazi Zanzibar na pia yaliyosajiliwa Zanzibar hufanya kazi pia Bara. Wizara yangu inafanya kazi kwa karibu na kwa ushirikiano mkubwa na Wizara ya Maendeleo Zanzibar katika mambo mbalimbali ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii, lakini pia na Ofisi ya Rais- TAMISEMI Zanzibar katika suala la usimamizi wa usajili, uratibu na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia ofisi ya Msajili Zanzibar.

***166. Mheshimiwa Spika***, ushirikiano huu hufanyika kwa kubadilishana taarifa, uzoefu na utaalam baina ya watendaji wa Wizara hizi, na hasa katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Ushirikiano huu pia unalenga kuendeleza na kuimarisha Muungano wetu. Aidha, tarehe 17 Februari, 2024 Idara ya Msajili kutoka Wizarani kwangu na Ofisi ya Msajili Zanzibar zimefanya kikao cha mashirikiano ambapo pamoja na masuala mengine kiliazimia - kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwa ni pamoja na kuainisha Mashirika yatakayoshiriki katika utoaji wa elimu ya mpiga kura na usimamizi wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024 pamoja na kuanza maandalizi ya Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, 2024 linalotarajiwa kufanyika mwezi Septemba, 2024, Tanzania Bara.

**ENEO LA 7: URATIBU WA MPANGO KAZI WA TAIFA WA KUTOKOMEZA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO (MTAKUWWA).**

***167. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea na jukumu la kuratibu utekelezaji wa Mpango wa kupunguza/kuondoa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA-I) wa Mwaka 2017/18 – 2021/22). Mpango huu, ulilenga kuimarisha uchumi wa kaya pamoja na kuimarisha huduma za msaada wa waathirika wa vitendo vya ukatili.

***168.*** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuwa mapambano dhidi ya Ukatili ni Suala Mtambuka na endelevu, Mpango huu wa kwanza (MTAKUWWA-I) uliandaliwa kwa kushirikiana na Wizara nyingine za Kisekta, pamoja na wadau wa Maendeleo. Utekelezaji wa MTAKUWWA katika kupunguza au kumaliza ukatili ulizingatia takwimu za ukatili za ujumla zilizowasilishwa na *Tanzania Demographic Health and Malaria Indicator Survey ya mwaka 2022*, ambayo ilionesha kiasi cha ukatili wa kimwili kwa wanawake kuwa ni asilimia 40, na ukatili wa kingono kuwa ni asilimia 27, na ule unaotokana na ukeketaji kuwa ni asilimia 10.

***169.*** ***Mheshimiwa Spika***, wakati utekelezaji wa MTAKUWWA-I umeanza, hapakuwa na takwimu sahihi za ukatili dhidi ya watoto katika maeneo yote matatu. Aidha, napenda kutoa taarifa kwamba, sasa hivi Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kisekta tunafanya utafiti katika mikoa yote ya Tanzania bara na pia Zanzibar kupitia Wizara husika ili kubaini takwimu halisi za ukatili dhidi ya Watoto. Utafiti huu umefikia hatua nzuri na upo karibu kukamilika hivyo, itasadia kupata takwimu halisi za ukatili dhidi ya Watoto ambazo tutaziwasilisha kwa Umma na Bunge lako Tukufu.

***170.*** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia Takwimu za ukatili zlizowasilishwa katika taarifa ya TDHMIS ya mwaka 2022 kama kipimo cha utekelezaji wa MTAKUWWA-I, Tathmini iliyofanyika Oktoba 2022 imeonesha **kupungua** kwa ukatili wa kimwili kwa wanawake kutoka asilimia 40 mwaka 2015 hadi asilimia 27 mwaka 2022, na ukatili wa kingono umepungua kutoka asilimia 17 mwaka 2015 hadi asilimia 12 mwaka 2022. Aidha, vitendo vya ukeketaji vimepungua kutoka asilimia 10 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 8 mwaka 2022.

***171.*** ***Mheshimiwa Spika***, matokeo haya ya kupungua kwa ukatili, yanatokana na juhudi za ushirikiano zilizofanyika kati ya Wizara yangu na Wizara nyingine pamoja na vikundi vya kijamii vinavyopambana na ukatili na wadau wa maendeleo kupitia MTAKUWWA-I. Ili kuendeleza juhudi dhidi ya ukatili wa wanawake na watoto, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Kisekta, imeandaa

Mpango Kazi wa Taifa Awamu ya Pili wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA-II) kwa kipindi cha Mwaka 2024/25 – 2028/29) ambao umezinduliwa tarehe **15 Mei, 2024**.

***172.*** ***Mheshimiwa Spika***, mpango huu umeboreshwa kwa kuzingatia kuimarisha maeneo yenye upungufu ambayo yamebainika katika utekelezaji wa MTAKUWWA-I. Hivyo, MTAKUWWA-II **imepanua wigo wa washiriki** katika utekelezaji ikiwemo Jamii yenyewe kwa Ujumla. Aidha, umeweka malengo ya kupunguza ukatili wa kimwili kutoka asilimia 27 hadi kufikia asilimia 14, na ukatili wa kingono kutoka asilimia 12 hadi kufikia asilimia 6 na hali kadhalika kupunguza vitendo vya ukeketaji kutoka asilimia 8 hadi kufikia asilimia 2 itakapofika mwaka 2028/29.

***173.*** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha Malengo haya yanafikiwa na ikiwezekana kabla ya muda uliowekwa au kumaliza kabisa, Serikali kwa kushirikiana na wadau itatekeleza afua zinazolenga kumaliza changamoto zinazosabisha ukatili zikiwemo; kuimarisha uchumi wa kaya ikiwemo kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu na kuweka mazingira Rafiki ya kiuchumi, kutoa elimu kuhusiana na mila na desturi zenye madhara na kuimarisha mila zenye matokeo chanya, kuimarisha ulinzi wa mwanamke na mtoto katika maeneo ya umma na katika mitandao na pia kuongeza vituo vya kutolea huduma kwa wahanga wa ukatili kama vile nyumba salama na vituo vya mkono kwa mkono.

***174.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha Mpango huu, na hatimaye kumaliza suala la ukatili, ni muhimu kufanya kazi kwa ushirikiano na kwa kila mmoja kutambua wajibu wake. Hivyo, nitumie nafasi hii, kutoa Rai kwa makundi mbalimbali kushiriki utekelezaji wa mpango huu kama ilivyoainishwa kwa kila kundi. **Aidha, niwaombe Waheshimiwa Mawaziri kuubeba mpango huu na kuujumuisha katika Mipango na Bajeti ya Wizara zenu**. Vilevile, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kufuatilia utekelezaji wake katika majimbo yenu kupitia vikao vya halmashauri ambavyo nyie ni wajumbe au viongozi kuelekea mabaraza ya waheshimiwa madiwani.

## D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA.

***175. Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Arusha na Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Kijitonyama Dar es Salaam.

***176. Mheshimiwa Spika***, Taasisi hizi zina jukumu kubwa la kutoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii kwa ngazi za Cheti, Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Aidha, majukumu mengine ya Taasisi hizi ni pamoja na kufanya utafiti na kutoa huduma ya ushauri elekezi katika nyanja zinazo shabihiana na taaluma wanazotoa.

***177. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa mafunzo 2023/24, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeongeza idadi ya udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi **2,918 (Me 983 na Ke 1,935)** waliodahiliwa mwaka wa masomo 2022/23 hadi kufikia wanafunzi **3,019** (**Me 1,052** na **Ke 1,967**) katika mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la **3.5%.** Aidha, kwa mwaka 2023/24, jumla ya wanafunzi 1,651 (**Me 575** na **Ke 1,076**) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi **1,619** (**Me 498** na **Ke 1,121**) waliohitimu 2022/23 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.7.** Taasisi inaendelea kuboresha mafunzo na kutoa wahitimu wenye uwezo. Ili kufikia lengo hili, Taasisi katika mwaka wa masomo 2023/2024 imeanzisha jumla ya **mitaala mipya 12**.

**Jedwali Na.7** Taarifa za udahili na wahitimu kwa kipindi cha 2022/23 na 2023/24 katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru.

| **2022/23** | **Udahili** | | **Wahitimu** | |
|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | **Me** | **Ke** |
| | 983 | 1,935 | 498 | 1,121 |
| Jumla | **2,918** | | **1,619** | |
| | | | | |
| **2023/24** | 1,052 | 1,967 | 575 | 1,076 |
| Jumla | **3,019** | | **1,651** | |
| **Ongezeko** | **3.4%** | | **3.5%** | |

***178. Mheshimiwa Spika,*** katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, udahili wa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2023/24, umeongezeka kufikia 3,039 (Me 904 na Ke 2,135) ikilinganishwa na wanafunzi 2,966 (Me 1,102 na Ke 1,864) mwaka 2022/23 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 73 sawa na 2.5%. Aidha, Katika mwaka wa masomo 2023/24 jumla ya wanafunzi 2,829 (Me 1,016 na Ke 1,813) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 3,075 (Me 880 na Ke 2,195) waliohitimu mwaka 2022/23 ikiwa ni upungufu wa wanafunzi 246 sawa na 8% kama inavyooneshwa katika **jedwali Na.8** hapo chini.

**Jedwali Na.8**: Taasisi ya Ustawi wa Jamii, udahili na Wahitimu kwa Kipindi cha 2022/23 na 2023/24

| **2022/23** | **Udahili** | | **Wahitimu** | |
|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Me | Ke |
| | 1,102 | 1,864 | 880 | 2,195 |
| Jumla | **2,966** | | **3,075** | |
| | | | | |
| **2023/24** | 904 | 2,135 | 1,016 | 1,813 |
| Jumla | **3,039** | | **2,829** | |
| **Ongezeko (Upungufu)** | **2.5%** | | **(8 %)** | |

***179. Mheshimiwa Spika***, Aidha, katika hali ya kuimarisha mifumo ya utoaji wa mafunzo, Taasisi hizi zimeendelea kuboresha mitaala ya kufundishia pamoja na kuanzisha programu mpya zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira. Baadhi ya mitaala mipya iliyoandaliwa na kuboreshwa na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru inahusu **kazi za jamii**, **watoto na vijana** katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada ambazo ni; Taaluma ya Saikolojia; Ukuzaji Ujasiriamali, Utatuzi Mbadala wa Migogoro Mahali pa Kazi. Mitaala hii imeshawasilishwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa ajili ya kupata ithibati. Taasisi inatarajia kudahili wanafunzi katika programu hizi kwa mwaka wa masomo 2024/25.

***180. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi hizi pia hutoa mafunzo ya muda mrefu, kutoa mchango na kushiriki katika masuala mbalimbali ya

jamii. Katika eneo hili, Taasisi ya Tengeru ilitoa mafunzo ya elimu juu ya ukatili wa kijinsia kwa maafisa wa polisi na maafisa wa dawati la jinsia 954 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Pia, ilitoa mafunzo ya uongozi wa kimkakati kwa watendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Zanzibar. Mafunzo mengine yalihusu uongozi na utawala bora kwa viongozi wa Serikali za Mitaa na madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Aidha, kwa upande wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, mafunzo ya muda mfupi yaliyotolewa ni pamoja na; mafunzo ya msaada wa kisaikolojia kwa wanafunzi na Jamii, mafunzo kwa wanafunzi yaliyohusu ukatili wa kijinsia, mahusiano, mawasiliano na stadi za maisha.

***181. Mheshimiwa Spika**,* kama ilivyo katika vyuo vyote vya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, pia inatekeleza programu ya kuchochea na kuendeleza ubunifu (innovation) miongoni mwa wanafunzi kupitia Kituo cha Huduma Tandaa na Ubunifu wa Kidijitali (Jamii Outreach Digital Innovation Center – JODIC). Kituo hiki kinatumika kuratibu utekelezaji wa programu za ubunifu wa kidijitali, ushirikishwaji jamii na uanagenzi. Kupitia Programu hii, Taasisi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i) Kushiriki katika kuhamasisha na kuelimisha jamii ya wakazi wanaoishi ndani ya Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kuhama kwa hiari kwenda katika maeneo yaliyotengwa na Serikali (Msomera, Saunyi na Kitwai) pamoja na maeneo mengine watakayoamua wenyewe. Katika zoezi hili, jumla ya kaya **807** zilifikiwa na kaya zipatazo **306** zilijiandikisha tayari kwa kuhama kwa hiari;

ii) Kushiriki katika zoezi la kuwabainisha wahanga wa maporomoko ya matope yaliyosababishwa na mvua yaliyotokea Wilaya ya Hanang, Mkoani Manyara tarehe 03 -12 Desemba, 2023 ambapo jumla ya wahanga **1,291** katika Kaya **491** walibainishwa. Kati ya kaya hizo, wahanga **89** makazi yao yalikuwa yameharibiwa na mafuriko ambapo wahanga wote waliweza kupatiwa huduma ya ushauri kuhusu mpango wa makazi ya muda mfupi na muda

mrefu. Vilevile, wahanga walipatiwa huduma ya hali na mali pamoja na msaada kisaikolojia.

***182.*** ***Mheshimiwa Spika***, Kama zilivyo Wizara nyingine, Wizara yangu na Taasisi zake inao wajibu wa kushiriki katika masuala ya jamii na majanga mbalimbali kupitia wataalamu wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii. Wizara na Taasisi zake hizi mbili (2) pamoja na vyuo vingine vya kati ilishiriki kutoa huduma kwa wahanga wa majanga yaliyotokea katika maeneo mbalimbali. Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii walitoa huduma ya kuhamasisha na kuelimisha jamii ya wakazi wanaoishi ndani ya Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kuhama kwa hiari kwenda katika maeneo yaliyotengwa na Serikali (Msomera, Saunyi na Kitwai) pamoja na maeneo mengine watakayoamua wenyewe. Aidha, Wataalamu wa Ustawi wa Jamii walitoa huduma ya elimu, ushauri, msaada wa kisaikolojia, afya ya akili na namna bora ya kukabiliana na mazingira mapya.

***183.*** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, wataalamu hawa walishiriki katika zoezi la kuwabainisha wahanga wa mafuriko ya matope yaliyotokea Wilaya ya Hanang, Mkoani Manyara Pamoja na kuwashauri na kuwaunganisha na ndugu/jamaa zao ili kupata makazi ya muda mfupi na baadae makazi ya muda mrefu. Aidha, wahanga hawa walipatiwa pia huduma ya ushauri nasaha, saikolojia na afya ya akili. Huduma kama hizi, tulizitoa pia katika kama maeneo mengine ambayo yalitokea majanga mbalimbali ikiwemo Mikoa ya Pwani, Morogoro, Mbeya, Dodoma na Tanga. Wizara yangu itaendelea kushiriki na kutoa huduma pale majanga yatakapo tokea.

***184.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Jamii ina elimu juu ya majanga, ikiwa ni pamoja kujikinga na athari zake na kuchukua tahadhari, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru **inaandaa mtaala unaolenga kutoa taaluma juu ya mabadiliko ya tabianchi, madhara yake na jinsi ya kukabiliana nayo**. Aidha, elimu hiyo imejumuishwa na itaendelea kutolewa wakati wa utekelezaji wa

Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi wa mwaka 2022/23 - 2025/26 (Bottom Up).

***185.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha wana Taaluma wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii wanapata nafasi ya kubadilishana uzoefu pamoja na kufanya tathmini ya utendaji wa kazi zao, Taasisi zote mbili (2) kwa kushirikiana na Vyama vya Taaluma hizi, huandaa makongamano kila mwaka ambayo idadi kubwa ya wataalamu hushiriki. Kwa Mwaka wa 2023/2024 Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru iliandaa kongamano la mwaka ambalo liliambatana na maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwa Taasisi hiyo mwaka 1963. Kongamano hilo pamoja na maadhimisho hayo, yalihudhuriwa na Mhe. Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu ambae pia alikuwa Mgeni Maalum. Kupitia maadhimisho hayo, Taasisi ilifanya shughuli mbalimbali zikiwemo; uzinduzi wa kitabu cha maendeleo ya jamii (Community Development Handbook) kitakachotumika kama rejeo kwa wadau, wakufunzi, wahadhiri na wataalamu wa maendeleo ya jamii nchini; uzinduzi wa Mfuko wa Udhamini wa Masomo (Maendeleo Scholarship Fund) kwa wanafunzi ambao watapata changamoto ya kujilipia masomo baada ya kupata usajili na kuanza masomo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kufiwa na wazazi/wategemezi; na shughuli nyingine ni pamoja na upandaji wa miti 500 katika vyanzo vya maji na maeneo ya Taasisi.

***186.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii nayo, iliadhimisha kumbukumbu ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwake ambapo Mgeni Rasmi alikuwa **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Maadhimisho hayo yalitanguliwa na shughuli za utoaji wa huduma za ustawi wa jamii katika mikoa ya Dodoma, Tanga, Geita, Songwe, Kagera na Dar es Salaam ambapo jumla ya watu 3,066 walipatiwa huduma hizo. Maadhimisho hayo yalihitimishwa na kongamano lililohudhuriwa na washiriki zaidi ya mia nane (800) ambapo mada kuu iliyojadiliwa ilihusu "**Malezi na makuzi bora ya watoto na vijana ni tija kwa Taifa**".

***187. Mheshimiwa Spika,*** sambamba na makongamano na maadhimisho hayo, Taasisi pia ziliandaa na kuratibu mabonanza ya michezo, makala maalum (Documentary) ya miaka 60 ya Taasisi ya Tengeru na Ustawi wa Jamii ambapo viongozi wakuu wa Kitaifa walihojiwa. Makala hii imerushwa katika kituo cha luninga cha TBC na nakala 250 za toleo la miaka 60 ya Taasisi ya Tengeru zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

***188. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi kupitia Kituo cha Kitaifa cha Utafiti na Uhifadhi wa Machapisho ya Wanawake kiliandaa Kongamano la Kitaifa la Wanawake kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT). Kongamano hilo lilifanyika jijini Dodoma tarehe 07 Machi, 2024 na kufanikiwa kuwafikia wadau 300. Kauli mbiu ya kongamano kwa mwaka 2024 ilihusu **"Usawa wa kiuchumi: Kuwawezesha wanawake kuifikia jamii** yaani "*Economic Equality: Empowering Women, Enriching Societies*". Katika kongamano hilo kituo kilifanikiwa kukusanya tafiti 12 na mawazo bunifu manne (4) yaliyohusu masuala ya kuchochea na kukuza usawa wa kiuchumi kwa kuwawezesha wanawake kuimarika kiuchumi.

***189. Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la utafiti, ushauri elekezi na maandiko, Taasisi zote mbili (2) zimeendelea kutekeleza majukumu haya, kama ifuatavyo:

i) Kutoa ushauri elekezi juu ya kuandaa Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Mkuranga na Shirika la *Christian Social Services Commission* (CSSC) Tanzania;

ii) Kutoa ushauri elekezi juu ya kuboresha upatikanaji wa haki katika masuala yanayohusiana na familia kupitia njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika shirika la *Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organization* (KWIECO) mkoani Kilimanjaro; na

iii) Kuchapisha makala mbili (2) za kitaaluma pamoja na kutoa matokeo ya tafiti mbili (2) ambazo ni kuchunguza kanuni, maadili na mbinu zinazowalinda wanawake dhidi ya unyanyasaji nchini.

***190. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi, Serikali kupitia Wizara imepeleka fedha katika Taasisi na vyuo kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kufundishia na hosteli. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili 2024**,** Taasisi ya Maendeleo Tengeru imepokea kiasi cha Shilingi Bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa kumbi mbili pacha za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,008 pamoja na hosteli ya wasichana yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 568. Aidha, kiasi cha Shilingi Milioni 500 zilipokelewa katika Chuo cha Maendeleo Monduli kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hosteli ya wasichana ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 576 kwa wakati mmoja.

***191. Mheshimiwa Spika,*** kwa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, jumla ya shilingi 259,116,083.80 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Hosteli katika kampasi ya Dar es salaam. Aidha, Taasisi imepokea kiasi cha shilingi 28,116,083.80 kwa ya ujenzi wa ofisi ya Muangalizi wa hosteli (*warden)*, stoo, na chumba cha kufulia katika chuo cha Ustawi Kisangara.

***192. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kusimamia Taasisi hizi pamoja na vyuo vya kati ili kuhakikisha malengo na matarajio ya serikali yanafikiwa. ***Nichukue nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bodi za Taasisi hizi pamoja na wajumbe wote wa Bodi kwa kazi yao kubwa na nzuri ya kusimamia vyuo hivi.***

## E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

***193. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi, Wizara imeendelea kutekeleza **afua mbalimbali za miradi ya maendeleo ikiwemo;** utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa, kuimarisha afua za haki na ulinzi wa mtoto pamoja na miradi ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi na Vyuo vilivyo chini yake. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili 2024, Wizara imepokea fedha za ndani za maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni 4.88,** kwa ajili ya utekelezaji wa **Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii** (**Shilingi Bilioni 2),** utekelezaji wa shughuli za programu ya kizazi

chenye usawa **(Shilingi Bilioni 2.48)** na Mradi wa Huduma za Ustawi wa Jamii (**Shilingi Milioni 400)**.

***194. Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha za ndani zilizopokelewa **Shilingi Bilioni 2** zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru zimepokelewa **Shilingi Bilioni 1.5,** Chuo cha Maendeleo ya jamii Monduli zimepokelewa **Shilingi Milioni 500**.

***195. Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizotekelezwa kutokana na fedha hizo ni: Kuanza kazi za awali za ujenzi wa **Jengo la Utawala** katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na ujenzi huo unaendelea. Kwa upande wa chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli, fedha zilizopokelewa zimetumika kuendelea na **ujenzi wa hosteli** yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 576 kwa wakati mmoja na ujenzi huo bado unaendelea.

***196. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kusimamia utoaji wa huduma katika Mahabusu 5 za watoto zilizopo mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Aidha, katika kuboresha huduma katika eneo hili kati ya fedha za ndani zilizopokelewa kiasi cha **Shilingi Milioni 400** zimeelekezwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Mahabusu ya watoto Mwanza.

***197. Mheshimiwa spika,*** kati ya fedha za ndani zilizopokelewa, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.48** zimetolewa kwa ajili ya kuratibu na kufanya ufuatiliaji wa uanzishwaji na uendeshwaji wa Madawati ya Jinsia kwenye maeneo ya soko na Taasisi za Elimu ya Juu na ya Kati; kufanya mapitio ya Mwongozo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi; Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake; kutoa mafunzo kwa waratibu wa programu yenye Kizazi chenye Usawa katika ngazi za Mikoa na Halmashauri pamoja na mafunzo kwa Wakuu wa Idara ya Sera na Mipango; Uratibu wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na kuwezesha ushiriki wa nchi kwenye Mkutano wa mapitio ya kipindi cha kati cha Utekelezaji wa GEF uliofanyika Septemba 2023 jijini New York 2023.

***198. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha afua za kutoa elimu ya malezi chanya kwa watoto katika ngazi zote nchini na kuzuia aina zote za ukatili dhidi ya watoto ikiwemo ukeketaji na ukatili mitandaoni, Wizara imepokea fedha za nje kiasi cha **Shilingi Milioni 66** kwa ajili ya kufanya kampeni ya ulinzi na usalama wa mtoto mtandaoni.

**F. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/25.**

***199. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake itatekeleza vipaumbele sita (6) ili kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo: -

i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa Ngazi ya Msingi;

ii) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia na kutokomeza vitendo vya ukatili, uwezeshaji wanawake kiuchumi, upatikanaji wa haki, ulinzi na malezi chanya ya watoto;

iii) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za msingi za ustawi wa jamii;

iv) Kutambua, kuratibu na kuendeleza Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo;

v) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na

vi) Kuimarisha ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.

***200. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara kwa mwaka 2024/25 imekadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 67,905,259,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 47,487,079,000** ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo **Shilingi 21,650,426,000** ni

Fedha za Mishahara na **Shillingi 25,836,653,000** ni fedha za uendeshaji wa ofisi. Aidha, **Shilingi. 20,418,180,000** ni fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo **Shillingi 18,025,673,000** ni fedha za ndani na **Shillingi 2,392.507,000** ni fedha za nje. **Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na: -**

i) Katika eneo la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi (Generation Equality Forum - GEF), kiasi cha **shilingi Bilioni 3.2** zimetengwa.

ii) Katika eneo la kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.15** kimetengwa;

iii) Katika eneo la kutambua na kuratibu shughuli za kiuchumi za Makundi Maalum hususan wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo machinga, mama/baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji na ma makundi mengine yenye biashara ndogo halali zilizosajiliwa, kiasi cha **Shilingi Bilioni 10.5** kimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kuongeza mitaji na kuboresha shughuli zao za kiuchumi;

iv) Kwenye eneo la huduma za ustawi wa jamii na watoto, kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.2** kimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria; kufuatilia utoaji wa huduma katika Makao ya Watoto, Vituo vya Kulelea Watoto wadogo Mchana na Watoto Wachanga; Kukarabati Shule ya Maadilisho ya Upanga na Mtwara; na Kuendeleza ujenzi wa Mahabusu ya Watoto Mwanza;

v) Katika eneo la ustawi wa Wazee wasiojiweza, **Shilingi Bilioni 1.06** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma katika Makazi ya Wazee 13;

vi) Kwenye eneo la Taasisi na Vyuo, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii

Tengeru, na Vyuo vitatu (3) vya Maendeleo ya Jamii vya Uyole, Rungemba na Buhare;

vii) Eneo la Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali limetengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.5** kwa ajili ya kusajili na kufanya ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kuandaa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2024, kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/2023 - 2025/2026), na kuratibu vikao vya Bodi na Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

viii) Eneo la maendeleo ya jamii limetengewa kiasi cha **Shilingi Milioni 826.1** kwa ajili ya kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Kuamsha Ari ya Jamii kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi wa mwaka 2022/23 - 2025/26 (Bottom Up) katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara; na

ix) Katika eneo la ufuatiliaji na tathmini, kiasi cha **Shilingi Milioni 150** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Taasisi, Vyuo na Vituo vya Ustawi wa Jamii vilivyo chini ya Wizara.

## G. SHUKRANI

***201. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta mbalimbali zinazosaidia na kuchangia katika huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Aidha, Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi rafiki **zikiwemo;** Marekani, Japan, Ufalme wa Uingereza, Ufalme wa Sweden, Jamhuri ya Watu wa China, Ufalme wa Norway, Falme za Nchi za Kiarabu, Italia, Ujerumani, Ubelgiji, Ufaransa, Canada, Ufalme wa Denmark, Ireland, Jamhuri ya Uswisi, Bangladesh na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

***202. Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara ikiwa ni pamoja na: -**Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo** UNICEF, UNFPA, UN-Women, WHO, UNDP, ILO, IOM, WFP, FAO, UNESCO na UNHCR. Vilevile, ninashukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya za Umoja wa Nchi za Ulaya (EU). Pia nayashukuru **Mashirika ya Kimataifa** ambayo ni:-Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfuko wa *Abbott Fund*, *Global Fund* na *Hilton Condrad Foundation*. Aidha, nazishukuru **Taasisi za Kifedha** za hapa nchini zinazoshirikiana na Wizara ambapo ni pamoja na Benki za CRDB, NMB, Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Stanbic, Azania, NBC, Equity, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Akiba Commercial Bank (ACB) na Benki ya Mkombozi na Benki ya Biashara Tanzania.

***203. Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali** ya ndani ya nchi na **Mashirika ya Dini** kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na; *World Vision, PACT Tanzania, The Aga Khan Foundation, Foundation for Civil Society*, *HelpAge International, Compassion International*, *Responsible Organization Tanzania, Both Ends Believing* (BEB)*, Safe Society Platform Tanzania*, *Children in Crossfire*, *Care International Tanzania, Railway Children Tanzania*, WiLDAF, ICS, TAWLA, TAYOA, LSF, *SOS Children's Village Tanzania*, BRAC Maendeleo Tanzania, *Plan International - Tanzania*, Kivulini, Uongozi wa Mgodi wa Geita, FSDT, WFT, TANLAP,*Save the Children, Equality for Growth (EfG)*, Landesa, CAMFED, CSEMA; REPPSI, *Amani Girls Home*, Pelum Tanzania, LHRC, Haki Elimu, TWCC, TECDEN, EGPAF,FAGDI, na MEWATA.

***204. Mheshimiwa Spika,*** nitoe pia shukrani zangu kwa **Jumuiya za makundi mbalimbali** ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Wizara. Jumuiya hizo ni pamoja na: - Baraza la Wazee Tanzania, Chama cha Wazee Wanaume Tanzania, Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Tanzania (CHAMWAPITA), Machifu na Viongozi wa Kimila Tanzania, Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Chama Cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT), Jukwaa la ULINGO,

Jumuiya ya Wazazi CCM, Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TAWIA, Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) na Umoja wa Mama na Baba Lishe Tanzania. Pia naomba nizishukuru Klabu za Mpira wa Miguu Tanzania hususan Yanga, Simba, AZAM na vikundi/kampeni za Kijamii kama (Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), *Foundation for Ambassadors of Gender Development Initiatives* (FAGDI), Sauti ya Watoto Tanzania (SAWATA) NA MALEZI BORA NETWORK pamoja na vyombo vyote vya habari.

***205. Mheshimiwa Spika,*** nitoe shukrani zangu pia kwa viongozi na taasisi zetu za dini zikiwemo Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA).

***206. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yangu nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara. Naomba kumshukuru **Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe,** Katibu Mkuu na **Bw. Amon A. Mpanju,** Naibu Katibu Mkuu kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Makamishna, Wasajili, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wataalam wote wa Wizara kwa utendaji wao mahiri uliowezesha kukamilisha maandalizi ya Hotuba yangu kwa wakati.

***207. Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kuwashukuru Bodi na Menejimenti za Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Pia, nawashukuru Wakuu wa Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wao mzuri unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao.

***208. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kupitia OR – TAMISEMI nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala, Wakuu

wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote na Wataalam wote chini ya Ofisi zao na Wadau wote wa sekta mbalimbali wanao hudumia katika maeneo yao pamoja na wananchi mmoja mmoja na ***mitandao*** yote ya habari za kijamii ambao wamekuwa wakifuatilia na kutoa ushirikiano mkubwa kwenye utekelezaji wa majukumu ya wizara yangu hasa kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia.

***209.*** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, hususan **mume wangu mpendwa Wakili Msomi Methusela Gwajima** na watoto wetu pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu kwa uvumilivu wao wa kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, nawashukuru **wananchi wote wa Tanzania** kwa kuipatia ushirikiano Wizara ninayoisimamia wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu na pia kwa wao binafsi kuendelea kupambana kuhakikisha maendeleo na ustawi wa jamii kwa usawa wa jinsia huku wakitumia mawasiliano kupitia simu nilizozisema awali.

## H. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2024/25

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2024/25

***210.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara imekadiria kukusanya kiasi cha Shilingi 7,040,129,000 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Vyanzo hivyo ni pamoja na: Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii; Ada ya malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Usajili na Ada za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

### Matumizi ya Kawaida

***211.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 47,487,079,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 25,836,653,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 21,650,426,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

**Miradi ya Maendeleo**

***212. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 20,418,180,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,025,673,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi. 2,392,507,000.00** ni Fedha za Nje.

***213. Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) inaomba jumla ya **Shilingi 67,905,259,000.00** ili kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo na ustawi wa jamii.

***214. Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum *www.jamii.go.tz*

***215. Mheshimiwa Spika,*** **Naomba Kutoa Hoja.**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Dorothy Gwajima kwa kuwasilisha hiyo hoja na hoja imeungwa mkono, nakushukuru sana. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii aweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati, Mheshimiwa Fatma Toufiq, karibu. *(Makofi)*

**MHE. FATMA H. TOUFIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Naomba Taarifa hii ya kamati yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Aidha, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya

Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Uchambuzi wa Kamati; msingi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ni masharti ya Kanuni ya Bunge Kifungu cha 6(5)(b) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) kwa nyongeza ya 8 ya Kanuni za Bunge, vinaipa Kamati ya Kudumu jukumu la kufanya uchambuzi wa bajeti na makadirio ya Wizara hii. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inapaswa kabla ya kuchambua bajeti kukagua miradi ya maendeleo iliyopangiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwa na nafasi nzuri ya kuweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti inataka Taarifa ya utekelezaji na makadirio ya Wizara kuchambuliwa na kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lako Tukufu lijadili hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jami, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum pamoja na Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata wasaa wa kukagua mradi wa ukarabati wa makazi ya wazee Ipuli - Tabora na Bukumbi - Mwanza, Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhari na Misungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa makazi ya wazee Ipuli - Tabora na Bukumbi - Mwanza; Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka

wa fedha 2023/2024 makazi ya wazee Ipuli - Tabora na Bukumbi - Mwanza yalitengewa kiasi cha shilingi milioni 50 kwa kila kituo kwa ajili ya kufanya ukarabati wa makazi hayo. Hata hivyo, mpaka kamati inakagua miradi hii hakukuwa na fedha yoyote iliyotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo kamati imeshuhudia uchakavu wa majengo, ukosefu wa nyumba za watumishi, ukosefu wa magari ya kuhudumia vituo hivyo, ukosefu wa nishati safi na salama pamoja na ukosefu wa jenereta la kutoa huduma ya umeme pindi unapokatika. Kwa upande mwingine kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha miradi ya matunda katika Makazi ya Wazee Bukumbi. Hata hivyo, kamati inashauri kuendelea kuanzisha miradi mingine, kama ya ufugaji na mbogamboga, ili kuweza kuboresha lishe za wazee na pia, kuwawezesha wazee kujishughulisha na kazi ndogondogo za kuongeza kipato katika makazi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inaendelea kutoa rai kwa Serikali kuwa, fedha iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi itolewe kwa wakati ili kuboresha makazi ya wazee. Uboreshaji huo utawafanya wazee waweze kufurahia kuwepo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Buhare. Kamati ilielezwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 chuo kilitengewa kiasi cha shilingi milioni 500, kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 450. Jengo hili linajumuisha ukumbi wa mihadhara pamoja na ofisi saba za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati ilibaini kuwa, mradi huu ulitakiwa kukamilika Mwezi Desemba, 2023. Hata hivyo, mpaka kamati inatembelea, mradi ulikuwa haujakamilika licha ya kupelekewa fedha zote zilizotengwa. Kamati ilihoji sababu za mradi kutokukamilika kwa wakati na ilielezwa kuwa ni kutokana na changamoto ya upatikanaji wa maji, umeme, vifaa vya kupaulia na upatikanaji wa gari la kuinulia kechi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu licha kupatiwa fedha zote kwa wakati. Ni rai ya kamati kuwa, Serikali ihakikishe mradi huu unakamilika kwa wakati na kuwa, fedha hiyo inapopelekwa kutekeleza mradi itumike kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Misungwi. Kamati ilielezwa kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 chuo kilitengewa kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 352 ambapo ujenzi wa msingi na kumwaga jamvi umekamilika. Mradi ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 2.7 hadi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 mradi ulitengewa kiasi cha shilingi milioni 500, lakini mpaka kamati inatembelea mradi huu hakuna fedha iliyokuwa imepokelewa. Ni rai ya kamati kuwa, Serikali ihakikishe inatoa fedha kwa wakati, ili kukamilisha mradi huu ambao kwa kiasi kikubwa utasaidia kuboresha mazingira ya malazi kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naenda kwenye Matokeo ya Uchambuzi na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Matokeo ya Uchambuzi na Mkadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa kamati kuhusu hoja hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa kamati ulijielekeza katika mambo mahsusi manne yafuatayo:-

(a) Makusanyo ya Maduhuli.

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti ya Kawaida.

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 8.5. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 2.7 sawa na asilimia 32.12 ya makusanyo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika jedwali namba moja na chati namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchanganuo huo, kamati imebaini mambo yafuatayo:-

(a) Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kwa ujumla ni shilingi bilioni 2.7 sawa na asilimia 32.12 ya makusanyo yote ya Wizara hii yalikusanywa katika kipindi hicho.

(b) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 Wizara imekusanya asilimia 32.1 tu ya lengo, ingawa kwa kipindi hicho ilitarajiwa angalau iwe imefikia asilimia 65 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa kwa miaka miwili mfululizo Wizara hii imekuwa ikikusanya maduhuli chini ya matajario. Mathalani, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi kufikia Februari Wizara ilikuwa imekusanya kwa asilimia 32 tu. Halikadhalika katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, imekusanya asilimia 32.1 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, kamati ina maoni kuwa, makusanyo haya hafifu kwa miaka miwili mfululizo yanaweza kutafsiriwa kwamba, au malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi au jitihada za ukusanyaji zilikuwa hafifu au vyanzo vya maduhuli vilivyoainishwa havikuwa vya uhakika. Ni rai ya kamati kuwa, Serikali ipange bajeti yake kwa kuzingatia uhalisia wa vyanzo vya mapato, ili viweze kuakisi makusanyo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 43.6 kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 26.5 ni, kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 17 ni, kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 24.3 sawa na asilimia 55.67 ya fedha iliyoidhinishwa, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 2 na Grafu Na.1. Kutokana na uchambuzi huo kamati imebaini kuwa, mtiririko wa fedha, kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ya Wizara pamoja na taasisi zake ni wa kuridhisha kwani imepokea asilimia 55.67 ya fedha iliyoidhinishwa, ambayo kwa kiasi imeweza kuisaidia Wizara kufanya shughuli iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tathimini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 30.5, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 26.8 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3.7 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 4.4 sawa na asilimia 14.56. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.3 ni fedha za ndani na shilingi milioni 66 ni fedha za Nje. Mchanganuo wa fedha hizo umeainishwa katika jedwali Na.3 na Chati Na.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi uliofanywa na kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kama ifuatavyo:-

(a) Kwa jumla mapokezi ya fedha za nje yapo chini ya kiwango kilichopangwa kupokelewa ambapo ilipokelewa asilimia 1.7 tu ya makadirio, jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

(b) Mapokezi ya fedha za ndani siyo ya kuridhisha ambapo Wizara imepokea asilimia 16.35 tu ya makadirio, jambo ambalo limesababisha Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yaliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika uchambuzi wake kamati ilibaini kuwa, kulikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 18.5 kilichoidhinishwa, kwa ajili ya uratibu wa shughuli za wafanyabiashara ndogondogo ikiwemo kuwapatia mikopo itakayowawezesha kufanya shughuli zao kwa ustadi. Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2024 Wizara haikuwa imepokea kiasi hicho cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake, kamati imebaini kuwa, katika kipindi cha miaka miwili mfululizo hakuna fedha iliyotolewa, kwa ajili ya mikopo ya masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo. Jambo linalokwamisha juhudi za kuwawezesha Wafanyabiashara hao kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa mapokezi wa fedha za nje za kutekeleza miradi ya maendeleo uko chini ukilinganisha na fedha za ndani. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kwa wakati fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani kwa kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za nje ni wa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Mapendekezo ya Kamati. Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali, ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo ambayo hayakuzingatiwa kama ilivyotarajiwa na kamati. Maeneo hayo ni pamoja na uhaba wa watumishi wa ustawi na maendeleo ya jamii, hususani Kada ya Ustawi wa Jamii, uhaba wa nyumba za

watumishi na uchakavu wa miundombinu katika taasisi na vyuo vya maendeleo ya jamii. Kamati inaendelea kusisitiza tena masuala hayo yafanyiwe kazi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni saba ikilinganishwa na shilingi bilioni 8.5 katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Makadirio yamepungua kwa shilingi bilioni 1.45 sawa na asilimia 17.17 ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha. Mchanganuo wa lengo la kukusanya kwa Fungu 53 unaonekana katika Jedwali Na.4 na Chati Na. 3 hapo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo, kamati imebaini kuwa, makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yamepungua kwa asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imebaini kuwa, takwimu za miaka mitatu ya nyuma 2020/2021 – 2022/2023 Wizara imekusanya wastani wa asilimia 69 ya mapato ikilinganishwa na makadirio hivyo, Wizara imepunguza makadirio ya mapato kwa Mwaka 2024/2025, ili kuendana na uhalisia. Kamati inaipongeza Wizara kwa kufuata ushauri wa kamati kuwa, makadirio ya makusanyo yaendane na uhalisia wa vyanzo vya mapato. Hata hivyo, kwa kuwa, mapato ya Wizara yanategemea ada na malipo ya malazi katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi za Ustawi wa Jamii ni ushauri wa kamati kuwa, Wizara iendelee kuboresha na kuongeza miundombinu, ili iweze kudahili wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 47.48 ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 25.83 ni Matumizi Mengineyo na kiasi cha shilingi bilioni 21.65 ni fedha za mishahara. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 8.76

ikilinganishwa na bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Mchanganuo huo upo katika Jedwali Na. 5. na Grafu Na. 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka hadi kufikia asilimia 8.76 ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoisha. Kamati imebaini kwamba, moja ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya kamati kwamba, Serikali iongeze bajeti katika Wizara hii, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, Fedha za Matumizi Mengineyo *(OC)* zimeshuka kwa asilimia 2.8. Ni rai ya kamati kuwa, Serikali ione umhimu wa kuiongezea bajeti Wizara hii, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kutokana na ukweli kuwa, punguzo hilo litapunguza ufanisi kutokana na ukweli kwamba, bei ya bidhaa na huduma zimepanda sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara, imetengewa jumla ya shilingi bilioni 20.41, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 18 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2.39 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepungua kwa asilimia 49.66 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoishia, kama ilivyochanganuliwa katika Jedwali Na. 6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi wake kamati imebaini kuwa, Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepungua kwa takribani shilingi bilioni 10.14 sawa na asilimia 49.66 ukilinganisha na mwaka unaoisha. Punguzo hili limetokana na kupungua kwa fedha za uratibu wa wafanyabiashara ndogondogo kutoka shilingi bilioni 18.5 Mwaka wa Fedha 2023 hadi shilingi bilioni 10 kwa Mwaka wa Fedha 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inaona kuwa kupungua kwa fedha hizi kutaathiri nia njema ya Serikali ya kuwainua Wafanyabiashara ndogondogo. Aidha, bajeti ya nje imepungua kwa

asilimia 57. Kamati inatoa rai kwa Serikali kutotegemea fedha kutoka nje kwenye miradi ya maendeleo kwani fedha hizo hazina uhakika wa kupatikana na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati. Katika majadiliano yake na Wizara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo, kama ifuatavyo: -

(i) Kutokana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu kuwa, ni Wizara mtambuka hivyo, kusababisha uhitaji wa rasilimali fedha kuwa mkubwa. Kamati inasikitishwa kwa kupunguzwa kwa bajeti katika Wizara hii kutoka shilingi bilioni 74.22 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi shilingi bilioni 67.90 katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 sawa na punguzo la asilimia 9.3. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea bajeti Wizara hii, ili iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, iandae maandiko na kuyawasilisha kwa wadau, ili kusaidia kuongeza bajeti ya kuwawezesha kutekeleza afua mbalimbali.

(ii) Kamati imebaini kuwa takwimu za miaka mitatu kutoka 2020/2021 hadi 2022/2023 zinaonyesha kuwa Wizara imekusanya wastani wa asilimia 69 ya mapato ikilinganishwa na makadirio. Hali hii imetokana na kupungua kwa wanafunzi wanaodahiliwa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi za Ustawi wa Jamii. Kamati inaishauri Wizara iweke mikakati madhubuti ya kuvitangaza vyuo vyake, ili kusajili wanafunzi wengi zaidi sambamba na kuongeza miundombinu.

(iii) Aidha, Kamati imebaini kuwa moja ya changamoto kubwa katika Wizara hii ni uhaba wa watumishi na vitendea kazi. Upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii ni asilimia 56.7 na Maafisa Ustawi wa Jamii ni asilimia 95.3 katika ngazi

mbalimbali, hali hii inasababisha Wizara kushindwa kusimamia masuala mbalimbali ya kijamii. Kamati inaendelea kuishauri Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iandae mkakati wa kuajiri maafisa hao muhimu, ili waweze kutatua changamoto mbalimbali za jamii kama vile huduma za unasihi na ustawi wa jamii.

(iv) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge, kwa ajili ya miradi ya maendeleo kunasababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua na mingine kutokutekelezwa kabisa. Mathalani, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 fedha za maendeleo zimetolewa kwa asilimia 14.56 tu. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha nyingi za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa, ili kukidhi matarajio. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa, upatikanaji wa fedha za nje ni wa kusuasua.

(v) Ustawi wa wazee ni jambo lililopewa kipaumbele kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025 kwenye Ibara ya 91, ambayo imefafanua umuhimu wa kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee. Kukosekana kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa makazi ya wazee kunaathiri utekelezaji wa ilani ya chama kwa kiasi kikubwa na hivyo, kushindwa kuwapa wazee haki zao za msingi. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizotengwa, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa makazi ya wazee, ili kuchochea ustawi wa wazee nchini. Halikadhalika, ione umuhimu wa kutoa fedha, kwa ajli ya kuweka nishati safi na salama ya kupikia katika makazi ya wazee.

(vi) Kutokutolewa kwa fedha, kwa ajili ya mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo kwa

miaka miwili mfululizo kunaathiri juhudi za Serikali za kuwawezesha wafanyabiashara hao kujikwamua kiuchumi. Aidha, kamati inaona kuwa, kiasi cha riba ya asilimia saba ya mikopo kinachopendekezwa na Wizara ni kikubwa ukilinganisha na hali ya uchumi wa wafanyabiashara ndogondogo, hali itakayosababisha wafanyabiashara wengi kushindwa kukopa. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge, kwa ajili ya mikopo nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo kabla ya mwaka wa fedha kuisha, ili kuwawezesha kukuza mitaji yao na vilevile Serikali ifanye mapitio ya kiasi cha riba ya mikopo, ili kuwawezesha wafanyabiashara wengi zaidi kukopa.

(vii) Kupunguza fedha zenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) kutoka shilingi bilioni 18.5 hadi shilingi bilioni 10.5 hakuendani na uhalisia uliopo wa uhitaji wa mikopo kwa wafanyabiashara hao. Kamati inaishauri Serikali kuwa, iongeze bajeti, ili kuweza kuwanufaisha wafanyabiashara wengi zaidi.

(viii) Kasi ndogo ya usajili wa kidigitali kwa wafanyabiashara ndogondogo imetokana na wafanyabishara wengi kutokuwa na elimu juu ya uwepo wa usajili huo na manufaa yanayotokana na kujisajili. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mkakati wa kutoa elimu juu ya faida za kujisajili na manufaa yatokanayo na usajili huo.

(ix) Kutokuwepo kwa mikakati madhubuti ya uhamasishaji na kufuatilia ulipaji wa ada za mashirika yasiyo ya kiserikali kunaathiri kwa kiasi kikubwa Makusanyo ya Mapato ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya ufuatiliaji na uhamashishaji wa mashirika yasiyo ya Kiserikali kulipa ada, ili kuongeza mapato ya Serikali.

(x) Kukosekana kwa hatimiliki kwa maeneo yanayomilikiwa na vituo vya wazee na watoto, taasisi za ustawi wa jamii na

vyuo vya maendeleo ya jamii, kunasababisha maeneo hayo kuvamiwa na wananchi. Kamati inaendelea kushauri uandaliwe mkakati maalum unaotekelezeka wa kupima na kupata hati za maeneo yote ya vyuo na vituo ambavyo havijapimwa.

(xi) Wakati wa ziara Kamati ilibaini uwepo wa maeneo makubwa yanayomilikiwa na taasisi, vyuo na vituo vilivyopo chini ya Wizara hii ambayo kwa kiasi kikubwa hayajaendelezwa na hivyo kupekelea kukosa mapato kwa kutoyaendeleza. Kamati inashauri Serikali kuyaendeleza maeneo hayo kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji ikiwa pamoja na kutafuta wabia mbalimbali ili kujenga vitega uchumi kama vile *hostel*, sehemu za biashara ili kuongeza mapato na kupunguza tatizo la upungufu katika miundombinu lililopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao ambao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu za Kudumu za Bunge kama yalivyowasilishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Dkt. Dorothy Gwajima (Mbunge), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Mbunge, kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Watendaji wote wa Wizara pamoja na Taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa

Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Seif Shekalaghe na Naibu Katibu Mkuu Amon Anastaz Mpanju.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum -Fungu 53 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja**.** *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;
c) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;
d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na
e) Sehemu ya Tano ni hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6 (5)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inapaswa kabla ya kuchambua Bajeti, kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuishauri Serikali.
Kanuni ya 117 (4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lako tukufu liijadili hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Malaam pamoja na Taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,

Wanawake na Makundi Maalumu inagusa **Fungu 53.** Naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi tarehe 22 Machi 2024. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kufanya ziara za kujiridhisha na hali halisi ilivyo katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya fungu lililotajwa hapo juu. Uchambuzi wa Kamati ulikuwa kama ifuatavyo:-

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ilifanya Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024. Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilpata wasaa wa kukagua mradi wa Ukarabati wa Makazi ya Wazee Ipuli-Tabora na BukumbiMwanza, Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare na Misungwi.

### 2.1 Ukarabati wa Makazi ya Wazee Ipuli-Tabora na Bukumbi- Mwanza

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Makazi ya Wazee Ipuli- Tabora na Bukumbi- Mwanza yalitengewa kiasi cha **Shilingi 50,000,000** kwa kila Kituo kwa ajili ya kufanya ukarabati wa Makazi hayo. Hata hivyo mpaka kamati inakagua miradi hii hakukua na fedha yoyote iliyotolewa kwaajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo Kamati ilishuhudia uchakavu wa majengo, ukosefu wa Nyumba za Watumishi, ukosefu wa Magari ya kuhudumia vituo hivyo, ukosefu wa nishati safi na salama, ukosefu wa jenereta la kutoa huduma ya umeme pindi unapokatika.

Kwa Upande mwingine Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha miradi ya matunda katika Makazi ya Wazee Bukumbi, hata hivyo Kamati inashauri kuendelea kuanzisha miradi mingine kama ya ufugaji

na mbogamboga ili waweze kuboresha lishe za wazee, kuwawezesha wazee kujishughulisha na kazi ndogondogo na kuongeza kipato katika makazi hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kutoa rai kwa Serikali kuwa fedha inayotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi itolewe kwa wakati ili kuboresha Makazi ya Wazee. Uboreshaji huo utawafanya wazee waweze kufurahia uwepo wao katika maeneo hayo.

**2.2 Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Chuo kilitengewa kiasi cha Shilingi 500,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mihadhara wenye uwezo wa kuchukua Wanafunzi 450. Jengo hilo linajumuisha ukumbi wa mihadhara pamoja na ofisi 7 za watumishi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilibaini kuwa mradi huu ulitakiwa kukamilika Mwezi Disemba 2023 lakini mpaka Kamati inatembelea mradi ulikuwa bado haujakamilika licha ya kupelekewa fedha zote zilizotengwa. Kamati ilihoji sababau za mradi kutokamilika kwa wakati ambapo ilielezwa ni kutokana na changamoto ya upatikanaji wa maji, umeme, upatikanaji wa vifaa vya kupaulia na upatikanaji wa gari la kuinulia kenchi.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu licha ya kupatiwa fedha zote kwa wakati. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ihakikishe mradi huu unakamilika kwa wakati na kuwa fedha inayopelekwa kutekeleza miradi itumike kama ilivyokusudiwa.

**2.3 Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Chuo kilitengewa kiasi cha **Shilingi 300,000,000** kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Ujenzi wa Hosteli yenye uwezo la kulaza wanafunzi 352 ambapo ujenzi wa msingi na kumwaga jamvi umekamilika. Mradi ukadiririwa kutumia **Shilingi 2,277,3000,000** hadi kukamilika. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 mradi ulitengewa kiasi cha **Shilingi 500,000,000** lakini mpaka Kamati inatembelea mradi huo hakuna fedha iliyokuwa imetolewa.

Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ihakikishe inatoa fedha kwa wakati ili kukamilisha mradi huu ambao kwa kiasi kikubwa utasaidia kuboresha mazingira ya malazi kwa wanafunzi.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 3.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Hoja hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza kwa katika mambo mahsusi manne yafuatayo;-

(a) Makusanyo ya maduhuli;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya kawaida;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na
(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni.

### 3.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi. 8,500,000,000** kutoka vyanzo mbalimbali kama vile Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 6,204,497,000**, uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 40,000,000**; Ada ya Malazi kwa wanafunzi wa vyuo vya maendeleo ya jamii **Shilingi 600,000,000** usajili na ada za mwaka za NGOs **Shilingi 638,500,000,** Ada ya usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo **Shilingi 1,000,000,000,** Mauzo ya Nyaraka za Tenda **Shilingi 2,003,000** na uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **Shilingi 15,000,000**, Mauzo ya nyaraka za Tenda na Mapato mengineyo **Shilingi 2,003,000.**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari 2024, Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 2,729,931,363;** sawa na **asilimia 32.12** ya makusanyo yaliyokusudiwa. Makusanyo hayo yapo katika mchanganuo ufuatao**: -** ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 2,202,745,778** sawa na **asilimia 35.50,** Uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii

**Shilingi 48,500,000** sawa na **asilimia 121.25,** Ada ya malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, **Shilingi 166,031,239** sawa na **asilimia 27.67,** Usajili na ada za mwaka za NGOs **Shilingi 302,504,348** sawa na **asilimia 47.38,** Ada ya Usajili wa wafanyabiashara ndogondogo **Shilingi 1,800,000** sawa na **asilimia 0.18,** uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **Shilingi 7,500,000** sawa na **asilimia 50.00,** Mauzo ya Nyaraka za Tenda na mapato mengine **Shilingi 850,000** sawa na **asilimia 42.44**.

Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekena katika **Jedwali Na. 1**. na **Chati Na.1**

**Jedwali Na. 1: Makadirio na Makusanyo halisi katika Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| MAELEZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA] |
|---|---|---|---|
| Ada za vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 6,204,497,000 | 2,202,745,778 | 35.50 |
| Uuzaji wa Mitaala ya Maendeleo ya Jamii | 40,000,000 | 48,500,000 | 121.25 |
| Ada za Malazi ya Wanafunzi wa vyuo vya Maendeleo | 600,000,000 | 166,031,239 | 27.67 |
| Usajili na Ada za Mwaka za NGOs | 638,500,000 | 302,504,348 | 47.38 |
| Uuzaji wa Mitaala vya Vyuo vya Ustawi | 15,000,000 | 7,500,000 | 50.0 |
| Ada ya usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo | 1,000,000,000 | 1,800,00 | 0.18 |
| Mapato mengineyo/ Mauzo ya Nyaraka za Tenda | 2,003,000 | 850,000 | 42.44 |
| **JUMLA** | **8,500,000,000** | **2,729,931,363** | **32.12** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara 2023/24

**Chati Na. 1: Makadirio na Makusanyo halisi katika Mwaka wa Fedha 2022/2023**




**Chanzo:** Randama ya Wizara 2023/24

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(a) Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa jumla ya **Shilingi 2,729,931,363.00** sawa na **asilimia 32.12** ya makusanyo yote ya Wizara hii yalikusanywa katika kipindi hicho.

(b) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 Wizara hii imekusanya **asilimia 32.12** tu ya lengo; ingawa kwa kipindi hicho ilitarajiwa angalau iwe imefikia asilimia 65 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kwa miaka miwili mfululizo Wizara hii imekuwa ikikusanya maduhuli chini ya matajario, mathalani katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi kufikia Februari ilikuwa imekusanya kwa **asilimia 32** tu halikadhalika katika Mwaka wa fedha 2023/2024 imekusanya **asilimia 32.12** tu. kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, makusanyo haya hafifu kwa miaka miwili mfululizo, yanaweza kutafsiriwa kwamba au malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa

hayakuwa halisi; au jitihada za ukusanyaji zilikuwa hafifu, au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ipange bajeti yake kwa kuzingatia uhalisia wa vyanzo vya mapato ili viweze kuakisi makusanyo hayo.

**3.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 43,664,963,000** kwa matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 26,577,510,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na **Shilingi 17,087,453,000** kwaajili ya mishahara**.**


**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 24,310,052,212.97** sawa na **asilimia 55.67** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili Matumizi ya Kawaida, ambapo Shilingi **11,484,526,560.00** sawa na **asilimia 67.21** ni fedha kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 12,825,525,648.97** sawa na **asilimia 48.26** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC). Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2. Na Grafu Na.1**

**Jedwali Na. 2: Mapokezi ya Fedha ya Kawaida 2023/2024**

| **MAPOKEZI YA FEDHA MATUMIZI YA KAWAIDA 2023/2024** | | | |
|---|---|---|---|
| Matumizi | Fedha iliyotengwa 2023/2024 | Fedha zilizopokelewa | Asilimia ya mapokezi |
| Mishahara | 17,087,453,00 | 11,484,526,560.00 | 67.2 |
| Oc | 26,577,510,000 | 12,825,525,648.97 | 48.26 |
| Jumla | **43,664,963,000** | **24,310,052,212.97** | 55.67 |

**Chanzo:** Randama ya Wizara 2023/2024

**Grafu Na. 1: Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2024/2024**




**Chanzo:** Randama ya Wizara 2023/2024

**Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwaajili ya mishahara na matumizi mengineyo ya Wizara pamoja na Taasisi zake ni wa kuridhisha kwani imepokea **asilimia 55.67** ya fedha iliyoidhinishwa, ambayo kwa kiasi imeweza kuisaidia Wizara kufanya shughuli iliyokusudiwa.

**3.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ilitengewa jumla ya **Shilingi 30,558,230,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 26,800,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,758,230,000** ni fedha za nje.


Hadi kufikia Februari 2024 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 4,449,880,000** sawa na **asilimia 14.56** Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,383,800,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 66,080,000** ni fedha za Nje. Mchanganuo wa fedha hizo umeainishwa katika **Jedwali Na. 3** na **Chati Na. 2**

**Jedwali Na. 3: Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2023/2024**

| **MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2023/2024** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Namba na jina la mradi** | **Bajeti iliyotengwa 2023/2024** | | **Mapokezi ya fedha hadi kufikia Februari 2024** | |
| | Fedha za ndani | Fedha za nje | Fedha za ndani | Fedha za nje |
| **Na. 6290:** *Kuprogramu Mfumo wa Kompyuta na kuchakata Data* | 200,000,000 | 0 | 0 | 0 |
| **Na. 6330:** Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 3,100,000,000 | 0 | 2,000,000,000 0 | 0. |
| **Na. 6259:**Mpango wa Rasilimali kwa Program za Jinsia | 4,000,000,000 | 0 | 1,983,800,000 | 0 |
| **Na. 5414**: Uhai na Maendeleo ya Mtoto | 0 | 1,253,236,169 | 0 | 66,080,000 |
| **Na.5451:** Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii | 1,000,000,000 | 1,047,000,000 | 400,000,000 | 0 |
| **Na.6280:** Uratibu wa Makundi Maalumu | 18,500,000,000 | 0 | o | o |
| **Jumla Kuu** | **26,800,000,000** | **3,758,230,000** | **4,383,800,000** | **66,080,000** |

**Chanzo. Randama ya Wizara 2023/2024**

**Chati Na. 2: Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha 2023/2024**




**Chanzo. Randama ya Wizara 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo kama ifuatavyo:-

(a) Kwa jumla mapokezi ya fedha za nje yapo chini ya kiwango kilichopangwa kupokelewa ambapo ilipokelewa **asilimia 1.75** tu ya makadirio jambo lililoathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

(b) Mapokezi ya fedha za ndani si ya kuridhisha ambapo Wizara imepokea **asilimia 16.35** tu ya makadirio jambo ambalo limesababisha Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yaliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kulikuwa na kiasi cha **Shilingi 18,500,000,000** kilichoidhinishwa kwa ajili ya uratibu wa shughuli za Wafanyabiashara Ndogondogo ikiwemo kuwapatia mikopo itakayowawezesha kufanya shughuli zao kwa ustadi, hata hivyo hadi kufikia Februari 2024 Wizara haikuwa imepokea kiasi hicho cha fedha.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha miaka miwili mfululizo hakuna fedha iliyotolewa kwa ajili ya mikopo ya masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo

jambo linalokwamisha juhudi za kuwawezesha Wafanyabiashara hao kujikwamua kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa mapokezi wa fedha za nje za kutekeleza miradi ya maendeleo uko chini ukilinganisha na fedha za ndani. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kwa wakati fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani kwakuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha za nje ni wa kusuasua.

### 3.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri uliotolewa na Kamati. Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo ambayo hayakuzingatiwa kama ilivyotarajiwa na Kamati, maeneo hayo ni pamoja na Uhaba wa Watumishi wa Ustawi na Maendeleo ya Jamii hususani kada ya Ustawi wa Jamii, uhaba wa nyumba za watumishi na uchakavu wa miundombinu katika Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Kamati inaendelea kusisitiza tena masuala hayo kwenye taarifa hii.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 4.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 7,040,129,000** ikilinganishwa na **Shilingi 8,500,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kuna punguzo la **Shilingi 1,459,871,000** sawa na **asilimia 17.17** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha. Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo ni pamoja na**:** Ada za Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 4,641,029,000,** uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 40,000,000**; Ada ya Malazi kwa wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii **Shilingi 551,600,000** usajili na ada za mwaka za NGOs **Shilingi 640,000,000,** ada za usajili wa Wafanyabiashara

Ndogondogo **Shilingi 1,000,000,000,** uuzaji wa Mitaala ya Taasisi za Ustawi wa Jamii **Shilingi 7,500,000,** ada za mwaka za vituo vya kulelea watoto **160,000,000.** Mchanganuo wa lengo la kukusanya kwa Fungu 53 unaonekana katika **Jedwali Na.4** na **Chati Na. 3** hapa chini.

**Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli**

| **CHANZO** | **2023/2024 (Tsh.)** | **2024/2025 (Tsh.)** | **Nyongeza/ Pungufu (Tsh.)** | **Nyongeza/ Pungufu (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Ada za vyuo vy Maendeleo ya Jamii | 7,084,497,000 | 4,641,029,000 | -2,443,468,000 | -52.6 |
| Uuzaji wa Mitaala ya Maendeleo ya Jamii | 40,000,000 | 40,000,000 | 0 | 0 |
| Ada ya Malazi kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 720,000,000 | 551,600,000 | -168,400,000 | -30.5 |
| Usajili wa ada za mwaka za NGOs | 638,500,000 | 640,000,000 | 1,500,000 | 0.23 |
| Uuzaji wa Mitaala ya vyuo vya Ustawi | 15,000,000 | 7,500,000 | -750,000 | -50 |
| Ada za usajili w Wafanyabiashara ndogondogo | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **8,500,000,000** | **7,040,129,000** | **-1,459,871,000** | **-20.73** |

**Chanzo. Randama ya Wizara 2023/2024**

**Chati Na. 3: Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli**




**Chanzo. Randama ya Wizara 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa, makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepungua kwa **Shilingi 1,459,871,000** sawa na punguzo la **asilimia 20.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa takwimu za miaka mitatu ya nyuma 2020/2021-2022/2023 Wizara imekusanya wastani wa asilimia 69 ya mapato iikilinganishwa na makadirio hivyo Wizara imepunguza makadirio ya mapato kwa mwaka 2024/2025 ili kuendana na uhalisia. Kamati inaipongeza Wizara kwa kufuata ushauri wa Kamati kuwa Makadirio ya makusanyo yaendane na uhalisia wa vyanzo vya mapato. Hata hivyo kwa kuwa mapato ya wizara yanategemea ada na malipo ya malazi katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi za Ustawi wa Jamii ni ushauri wa Kamati kuwa Wizara iendelee kuboresha na kuongeza miundombinu ili iweze kudahili wanafunzi wengi zaidi.

### 4.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 47,487,079,000** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha


hizo, **Shlingi 25,836,653,000** ni matumizi mengineyo na kiasi cha **Shilingi 21,650,426,000** ni fedha za Mishahara. Kiasi hicho ni ongezeko la **Shilingi 3,826,116,000** sawa na **asilimia 8.76** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mchanganuo huo upo katika **Jedwali Na. 5.** na **Grafu Na. 2**

**Jedwali Na. 5: Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**

| **+ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 53 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **2023/2024 (tsh.)** | **2024/2025 (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (%.)** |
| Mishahara | 14,141,924,000 | 21,650,426,000 | 4,566,973,000 | 26.7 |
| OC | 18,169,057,000 | 25,836,653,000 | -740,857,000 | -2.8 |
| **Jumla** | **32,310,981,000** | **47,487,079,000** | **3,826,116,000** | **8.76** |

**Chanzo.** Randama ya Wizara2024/2025

**Grafu Na. 2: Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**




**Chanzo.** Randama ya Wizara2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 8.76** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ilikuwa **Shilingi 43,664,963,000** Kamati imebaini kwamba, moja ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali iongeze bajeti katika Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa fedha za Matumizi mengineyo (OC) imeshuka kwa **asilimia 2.8** ni rai ya Kamati kuwa Serikali ione umhimu wa kuiongezea bajeti Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kutokana na ukweli kuwa punguzo hilo litapunguza ufaninii kutokana na ukweli kwamba bei ya bidhaa na huduma zimepanda.

**4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwaajili ya Miradi ya Maendeleo.**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara, imetengewa jumla ya **Shilingi 20,418,180,000** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,025,673,000** ni fedha za ndani, na **Shilingi 2,392,507,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepungua kwa takribani **Shilingi 10,140,050,000** sawa na **asilimia 49.66** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha kama ilivyochanganuliwa katika **Jedwali Na. 6**.

**Jedwali Na. 6: Ulinganisho wa Bajeti ya Fedha za Maendeleo kwa**


**Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**

| **ULINGANISHO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Namba na jina la mradi** | **Makadirio kwa mwaka 2023/2024** | | **Makadirio kwa mwaka 2024/2025** | |
| | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Fedha za Ndani | Fedha za Nje |
| **Na. 6290:** Kuprogramu Mfumo wa | 200,000,000 | 200,000,000 | 150,000,000 | 0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kompyuta na kuchakata Data | | | | |
| **Na. 6330:** Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | 3,100,000,000 | 0.00 | 2,000,000,000 | 0 |
| **Na. 6279** Kuwezesha Wanawake kiuchumi na kupinga ukatili wa Kijinsia. | 4,000,000,000 | 1,257,993,831 | 3,200,000,000 | 0 |
| **Na. 5414** Utekelezaji wa Afua za kumlinda na kumuendeleza Mtoto. | 0 | 1,253,236,169 | 0 | 1,977,597,000 |
| **Na. 6280** Uwezeshaji Mfuko wa Wafanyabiashara NdogoNdogo | 18,500,000,000 | 0 | 10,500,000,000 | 0 |
| **Na. 5451** Uwezeshaji Huduma za Ustawi wa Jamii. | 1,000,000,000 | 1,047,000,000 | 1,000,000,000 | 414,910,000 |
| **Na. 6259** Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Shughuli za wizara | 200,000,000 | 200,000,000 | 1,175,673,000 | 0 |
| **Jumla Kuu** | **26,800,000,000** | **3,758,230,000** | **18,025,673,000** | **2,392,507,000** |

**Chanzo.** Randama ya Wizara 2023/2024

**Chati Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**




**Chanzo.** Randama ya Wizara 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo; -

(a) Bajeti ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepungua kwa takribani **Shilingi 10,140,050,000** sawa na **asilimia 49.66** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Punguzo hilo limetokana na kupungua kwa fedha za uratibu wa Wafanyabiashara Ndogondogo kutoka **Shilingi 18,500,000,000** mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi **Shilingi 10,500,000,000** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kamati inaona kuwa kupungua kwa fedha hizi kutaathiri nia njema ya Serikali ya kuwainua Wafanyabiashara Ndogondogo.

(b) Bajeti ya Fedha ya Nje imepungua kwa **asilimia 57,** ambapo kwa Mwaka 2023/2024 ilitengwa kiasi cha **Shilingi 3,758,230,000.**na katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imetengwa kiasi cha **Shilingi 2,392,507,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa rai kwa Serikali kutotegemea fedha kutoka Nje kwenye miradi ya maendeleo kwani fedha hizo hazina uhakika wa kupatikana na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, katika majadiliano yake na Wizara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na makundi Maalum kwa Mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati inatoa maoni, ushauri na Mapendekezo kama ifuatavyo: -

i) Kutokana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu kuwa ni Wizara Mtambuka hivyo kupelekea uhitaji wa rasilimali fedha kuwa mkubwa. Kamati inasikitishwa na kupuguzwa kwa Bajeti katika Wizara hii kutoka **Shilingi 74,223,193,000** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi **Shilingi 67,905,259,000** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 sawa na punguzo la **asilimia 9.3**. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea Bajeti Wizara hii ili iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha Wizara iandae maandiko na kuwasilisha kwa wadau ili kusaidia kuongeza Bajeti ya kuwawezesha kutekeleza Afua mbalimbali.

ii) Kamati imebaini kuwa takwimu za miaka mitatu kutoka 2020/2021 hadi 2022/2023 zinaonyesha kuwa Wizara imekusanya wastani wa **asilimia 69** ya mapato ikilinganishwa na makadirio. Hali hiyo imetokana na kupungua kwa wanafunzi wanaodahiliwa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Taasisi za Ustawi wa Jamii. Kamati inaishauri Wizara iweke mikakati madhubuti ya kuvitangaza Vyuo vyake ili kusajili wanafunzi wengi zaidi sambamba na kuongeza miundombinu.

iii) Kamati imebaini kuwa moja ya changamoto kubwa katika Wizara hii ni uhaba wa watumishi na vitendea kazi. Upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii ni **asilimia 56.7** na Maafisa Ustawi wa Jamii ni **asilimia 95.3** katika ngazi mbalimbali hali

inayopelekea Wizara kushindwa kusimamia masuala mbalimbali ya kijamii. Kamati inaendelea kushauri Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iandae mkakati wa kuajiri Maafisa hao muhimu ili waweze kutatua changamoto mbalimbali za jamii kama vile huduma za unasihi na ustawi wa jamii.

iv) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuna sababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua, na mingine kutokutekeleza kabisa. Mathalani katika Mwaka wa fedha 2023/2024 Fedha za maendeleo zimetolewa kwa **asilimia 14.56** tu. Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio. Aidha Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikanaji wa fedha za nje ni wa kusuasua;

v) Ustawi wa Wazee ni jambo lililopewa kipaumbele kwenye **Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 20202025** kwenye **Ibara ya 91** ambayo imefafanua umuhimu wa kuimarisha utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii kwa wazee, kukosekana kwa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Ukarabati wa Makazi ya Wazee kunaathiri utekelezaji wa ilani ya chama kwa kiasi kikubwa na hivyo kushindwa kuwapa Wazee Haki zao za Msingi. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizotengwa kwaajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Ukarabati wa Makazi ya Wazee ili kuchochea Ustawi wa Wazee nchini. Halikadhalika Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha kwaa ajli ya kuweka nishati safi na salama ya kupikia katika makazi ya wazee.

vi) Kutokutolewa kwa Fedha kwa ajili ya mikopo yenye mashari nafuu kwa Wafanyabiashara Ndogondogo kwa miaka miwili mfululizo kunaathiri juhudi za Serikali za kuwawezesha Wafanyabiashara hao kujikwamua kiuchumi. Aidha Kamati inaona kuwa kiasi cha riba cha asilimia saba (7%) ya mikopo

kinachopendekezwa na Wizara ni kikubwa ukilinganisha na hali ya uchumi wa wafanyabiashara ndogondogo hali itakayopelekea wafanyabiashara wengi kushindwa kukopa. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya mikopo nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo kabla ya Mwaka wa Fedha kuisha ili kuwawezesha kukuza mitaji yao na vilevile Serikali ifanye mapitio ya kiasi cha Riba ya Mikopo hiyo ili kuwawezesha wafanyabiashara wengi zaidi kukopa.

vii) Kupunguza kwa fedha za Uratibu wa Wafanyabiashara Ndogondogo kutoka **Shilingi 18.500.000.000** hadi Shilingi **Shilingi 10,500,000,000** hakuendani na uhalisia uliopo wa uhitaji wa mikopo kwa Wafanyabiashara hao. Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze Bajeti ili kuweza kuwanufaisha Wafanyabiashara wengi zaidi.

viii) Kasi ndogo ya usajili wa kidigitali kwa Wafanyabiashara Ndogondogo kumetokana na wafanyabishara wengi kutokuwa na elimu juu ya uwepo wa usajili huo na manufaa yanayotokana na kujisajili. Kamati inaishauri Serikali kuanda mkakati wa kutoa elimu juu ya faida za kujisajili na manufaa yatokanayo na usajili huo.

ix) Kutokuwepo kwa mikakati madhubuti ya uhamasishaji na kufuatilia ulipaji wa Ada za Mashirika yasiyo ya Kiserikali kunaathiri kwa kiasi kikubwa Makusanyo ya Mapato ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya ufuatiliaji na uhamashishaji wa mashirika yasisyo ya Kiserikali kulipa Ada ili kuongeza mapato ya Serikali.

x) Kukosekana kwa hatimiliki kwa Maeneo yanayomilikiwa na Vituo vya Wazee na Watoto, Taasisi za Ustawi wa Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kunapelekea maeneo hayo kuvamiwa na Wananchi. Kamati inaendelea kushauri uandaliwe mkakati maalum

unaotekelezeka wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ya Vyuo na Vituo ambavyo havijapimwa.

xi) Wakati wa ziara Kamati ilibaini uwepo wa maeneo makubwa yanayomilikiwa na Taasisi, Vyuo na Vituo vilivyopo chini ya wizara hii ambayo kwa kiasi kikubwa hayajaendelezwa na hivyo kupekelea kukosa mapato kwa kutoyaendeleza. Kamati inashauri Serikali kuyaendeleza maeneo hayo kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile Kilimo, Ufugaji ikiwa pamoja na kutafuta Wabia mbalimbali ili kujenga vitega uchumi kama vile Hostel, sehemu za biashara ili kuongeza mapato na kupunguza tatizo la upungufu wa miundombinu lililopo.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe.Tamima Haji Abass, Mb.
4. Mhe.Neema Gerald Mwandabila, Mb.
5. Mhe.Tecla Mohammed Ungele, Mb.
6. Mhe.Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe.Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
8. Mhe.Katani Ahmadi Katani, Mb.
9. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
10. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.
11. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
12. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.

13. Mhe. Alli Hassan Omar King, Mb.
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
15. Mhe. Sanya Juma Jafar, Mb.
16. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
17. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
18. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Doroth Onesphoro Gwajima (Mb) Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri Mhe. Mwanaidi Ali Khamis (Mb), Mb kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Seif Shekalaghe na Naibu Katibu Mkuu Amon Anastaz Mpanju.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**Fatma Hassan Toufiq, Mb**
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**
17 Mei, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza michango yetu naomba nitoe matangazo ya wageni ambao wapo tena kwa wakati huu. Kwanza tuna mgeni ambaye yuko kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika ambaye ni Mheshimiwa Mwantumu Mahiza wakati ule tulimtambulisha kama Mbunge na Waziri mstaafu lakini huyu ni Mwenyekiti wa Bodi ya Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Serikali, karibu sana Mheshimiwa Mwantumu Mahiza. *(Makofi)*

Pia tuna Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna Wageni wengine wa Mheshimiwa Dorothy Gwajima ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ni Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Maafisa na Wadau mbalimbali walio chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Wote kwa pamoja tunawakaribisha sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Maafisa Utumishi kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni majirani zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni ambao wamekuja kutembelea hapa Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni Wajumbe 21 wa Kamati ya Maendeleo ya Kata

ya Bupamwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 40 wa Chuo cha Biashara *(CBE)* Kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wageni wetu wote ambao mpo kwa muda huu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaanza sasa na uchangiaji wetu kama utaratibu wetu tutaanza na wale ambao hawajawahi kuchangia na ambao wamechangia mara moja ambapo tutaanza na Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo na Mheshimiwa Furaha Matondo watachangia kwa dakika 10 na tunaanza na Mheshimiwa Tamima Haji Abass.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu leo hii. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia uhai na nguvu mpaka siku ya leo naweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu kwa mara yangu ya kwanza kutoa mchango wangu wa maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea naanza kuunga mkono hoja. Kwa nafasi hii pia, nachukua fursa hii kuushukuru uongozi wa Chama changu Cha Mapinduzi unaoongozwa na Mwenyekiti wake mahiri mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi; na uongozi wote wa Chama Cha Mapinduzi na UWT Taifa hadi ngazi ya mkoa ambako wameniwezesha kuingia ndani ya Bunge hili mpaka hii leo naendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitakuwa na mchango mdogo kwa vile ni mara ya kwanza na siku zote huwa naambiwa; "Ghafla haina Hodari." Kwa hiyo kwangu mimi pamoja na kuwa hivyo lakini inakuwa kama ghafla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum imebeba sura ya mama na mwana, imebeba

sura ya Adamu na Hawa, Wizara hii ni mama kwa sisi sote. Namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiunda Wizara hii baada ya kuona umuhimu wake na kumchagua Mheshimiwa Dorothy Gwajima ambaye mara nyingi wanamwita *field marshal*. Nashukuru pia kwa kumchagua Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi. Pia nashukuru kwa kuchaguliwa Katibu Mkuu wa hii Wizara, Dkt. Seif.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli Wizara hii imekuwa ni kioo kwa Tanzania yetu hii. Tumekuwa tukisikia mambo mengi ambayo yanatokea huko mitaani yanayohusu ukatili, yanayohusu unyanyasaji na udhalilishaji kwa hiyo Wizara hii imebeba hayo yote na inayafanyia kazi kwa moyo wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya nchi yetu ambayo sisi sote tumeiona hata mataifa pia wameiona. Mheshimiwa Dkt. Samia anafanya kazi kubwa ya kuiletea maendeleo nchi yetu mpaka leo amekuwa akitambulika mpaka mataifa mbalimbali wameanza kumpa tuzo mbalimbali. Kama tulivyosikia juzi pia alivalishwa u-*doctor* kule Uturuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mchango wa hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii, kwanza naiomba Serikali iwaongezee pesa. Kwanza iwape pesa walizoomba na ikitokea nyongeza basi iwaongezee kwa sababu kazi kubwa wanaifanya na kazi hii sote tunaiona. Niseme kuna Mpango wa MTAKUWWA *number two* wameuzindua juzi. Ule mpango kama utatekelezwa utakuwa una manufaa makubwa kwa nchi yetu. MTAKUWWA huu unakwenda kufanya kazi ya kuelimisha jamii kutokomeza ukatili dhidi ya watoto, wanawake na makundi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Siku ya Familia Duniani iliyoadhimishwa pale Chinangali juzi tarehe 15, Wizara za Kisekta zilikuwa pale na zikatoa matamko yao. Wizara zilitoa matamko kwamba watashirikiana na Wizara hii kwa hali na mali kuweza

kufanikisha ule Mpango wa MTAKUWWA ambao utakwenda kutokomeza ukatili wa wanawake watoto na makundi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Niombe sana zile Wizara ambazo zilitoa matamko yake pale basi ziende zikatekeleze, kwa sababu kutekeleza ahadi walizozitoa ni ufanisi kwa Wizara hii. Kuna Wizara ya Katiba na Sheria ilitoa tamko pale na Wizara hii tunategemea sana yale mambo yenye ukakasi wao wanakwenda kuyawekea msimao ili yaweze kuwa rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wizara ya TAMISEMI. Wizara ya TAMISEMI hii tunaiona imeenea nchini kote imeanza tangu chini mpaka juu. Kwa hiyo wakitoa ushirikiano wao kwa Wizara hii basi naona mambo pia yatakwenda vizuri na ukatili itakuwa historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wizara ya Afya, Wizara ya Afya pia na yenyewe ilitoa tamko pale itashirikiana na Wizara hii, ambapo Wizara ya Afya na wenyewe watakapokwenda ikitokea watu wamepelekwa kule hospitali wakisimama imara watatoa matokeo au vipimo hawatavibadilisha vitakuwa vizuri ili mambo yaende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wizara ya Fedha na yenyewe ilitoa tamko pale kushirikiana na hii Wizara. Kwa maana Wizara ya Fedha ikitoa fedha basi haya mambo yatakwenda vizuri na huu mpango utatekelezeka. Pia, kuna Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na yenyewe pia ilitoa tamko pale. Kwa maana hiyo kama tutatazama zile Wizara kama zote zitatekeleza wajibu wake na zikitekeleza ahadi yake basi mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiona ukatili huko unafanyika na kila mmoja amekuwa akipiga kelele wanawake, watoto, makundi maluum na walemavu wote wanafanyiwa vitendo vilivyokuwa havina maana lakini mwisho wa siku wale watendaji au wale wahusika tunawakuta wanatembea huku barabarani hakuna

hatua yoyote inayochukuliwa au hatua zinazochukuliwa zinakuwa nyepesi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukimwona Mwenyekiti wetu mahiri jembe, Mama Mary Pius Chatanda amekuwa *champion* wa kupigania haki za wanawake na watoto ndani ya nchi yetu. Mama Mary amekuwa akionekana kila sehemu hata juzi tarehe 15 alikuwa na mkutano na akatoa matamko, maelekezo na mambo mengi tu ambayo yanahusu masuala ya kupiga vita ukatili. Kwa maana hiyo na sisi wananchi au na sisi viongozi tuko naye bega kwa bega, tuko bega kwa bega na Wizara hii ambayo tutakwenda kuyatekeleza kule katika maeneo yetu lakini mwisho wa siku Serikali au vyombo vya sheria vichukue hatua stahiki. Bila ya hivyo tutakuwa tunapiga makelele kila siku au watu watakuwa wanalalamika kila siku lakini hakuna kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale waliotekeleza vitendo vibaya kule nje wanakuwa wanapata nguvu kwa kuona hakuna sheria zinazowabana moja kwa moja au zinazowakaba sasa ndio wanaona bora wafanye hivi. Wengine nao wanakuambia wakisikia kuna mtu kakamatwa kapelekwa sehemu husika lakini katolewa basi anaona kumbe kitu hiki cha kawaida. Kwa hiyo niiombe sana Serikali iweze kulisimamia hilo, kila mmoja kwa nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tamima Haji Abass kwa mchango wako mzuri huo kwa mara ya kwanza katika Bunge letu. Nilimtaja Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, atajiandaa Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri dada yangu Mwanaidi, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi

kubwa ambayo wamekuwa wanaifanya kwenye Wizara hii, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akifanya kazi kubwa na nzuri lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kurejesha imani kwa vijana wa Kitanzania kwa kuweza kurejesha mkopo wa 10% kwa ajili ya wanawake vijana na watu wenye ulemavu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kurejesha mkopo huu kupitia Benki ya *NMB*, benki ambayo ina riba nafuu kwa mkopo wa asilimia saba, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais. Niombe kama Wizara muwape vijana elimu kama hizi pesa hazitoki kama hisani ila zinatoka kama mkopo, muweze kuwapatia elimu ili waweze kurejesha fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza tena Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenga milioni kumi kumi kwa kila mkoa kwa ajili ya kujenga masoko ya machinga. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuona kundi hili kubwa lenye uhitaji wa kupatiwa masoko lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutenga shilingi bilioni 18.5 kwa ajili ya machinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake hii, aje atuambie machinga hawa waliokusudiwa kunufaika na fedha hizi ni machinga wa aina gani? Kwa sababu tukiongelea kundi la machinga tunajua wapo machinga wa aina nyingi, je machinga waliokusudiwa hapa ni wapi? Wafanyakazi wa sokoni, wafanyakazi wa rendishaji nguo, wafanyakazi wa ma-*salon* tukizungumzia wafanyabiashara wamachinga ni kipengele kikubwa sana. Kwa hiyo aje atuambie machinga hawa ni machinga wa aina ipi waliokusudiwa kupata fedha hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara fedha hii itakapotoka isitoke kwa ubaguzi, waangalie namna nzuri ya kuweza kuitoa fedha hii lakini niwaombe vijana wote wa Tanzania kuweza kuchangamkia

fursa hii ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupatia sisi vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite na mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto bado vinaendelea kushamiri ndani ya jamii yetu. Vitendo hivi havipungui kama tunavyovisikia lakini vitendo hivi bali vinaongezeka. Niiombe sana Wizara ikae iangalie kama sheria inaukakasi basi iletwe tena Bungeni tuje tuipitie sheria upya ili kuona hatua gani za kisheria zinaweza kuchukuliwa ili kuweza kupunguza vitendo hivi vya udhalilishaji. Vitendo vya udhalilishaji vimekuwa vikishamiri siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu waokuwa wanafanya vitendo vya udhalilishaji wanapatiwa dhamana kitu ambacho huwa kinavunja mioyo ya wananchi wetu kwa sababu leo mtu anakamatwa kesho mtu anaonekana yupo nje anazurura. Wanakosa imani kupeleka kesi zao au kupeleka watoto wao kuonesha ni jinsi gani watoto wanadhalilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saizi imekithiri hasa watoto wa kiume wanalawitiwa kila siku, tutafute namna nzuri ya kuweza kuwalinda watoto wetu wa kiume, wenye watoto wa kiume tuna hofu kuliko wenye watoto wa kike. Watoto wa kiume saizi ndio wanadhalilishwa na kulawitiwa kila siku. Niombe sana Wizara ije na marekebisho ya kisheria kuweza kuhakikisha adhabu kali zinatolewa kwa wale ambao huwa wanahusika na kesi hizi. *(Makofi)*

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima hili la…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** …*NGOs* ambazo siyo za Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munira kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana kabisa na anachokizungumza Mheshimiwa Munira kwa jinsi ambavyo Taifa letu limefikia, kwa hatua ambayo Taifa letu limefikia kwa maana ya mmomonyoko wa maadili, ni wazi kuna umuhimu sana wa Serikali na kama Taifa kuamua kufanya mabadiliko ya sheria. Kwa sababu hawa watu wakitoka nje baada ya kufanya matukio kwenye rekodi tu anaonekana kama alibaka mtu mmoja akitoka nje anaenda kufanya matukio mara tatu mara nne. Sasa ni muhimu Serikali ikaona uwanja huu sasa ni fursa kutunga sheria ambayo inazuia dhamana kwenye makosa kama haya. *Otherwise,* Taifa linaenda kuzama na kizazi chetu kinazidi kiteketea, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munira unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hizi Taasisi Zisizo za Kiserikali *(NGO)s* je Serikali imejiridhisha na *NGOs* hizi ambazo ziko kwenye nchi yetu badala ya maandiko yao lakini na vitendo vyao vilivyopo hapa nchini? Ni kweli taasisi hizi hazifanyi mambo ambayo siyo sahihi yaliyopo kwenye nchi yetu kwa sababu ukiangalia kuna *NGOs* tunajua zinajihusisha kabisa na ndoa za jinsia moja. Je, Serikali imejiridhisha vipi kama hizi *NGOs* zetu zilizopo hapa nchini hazihusiki moja kwa moja kwenye vitendo hivi? Wanaweza kuwa kwenye maandishi yao wametuandikia vizuri wanafanya *ABC* lakini sasa kama Serikali je, mmeweza kujiridhisha kama *NGOs* hizi zilizopo nchini kwetu hazihusiani na vitendo hivi vya ukatili au vitendo hivi vya ndoa ya jinsia moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine…

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Agnes Marwa

**TAARIFA**

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naongezea kwa mchangiaji na sasa imepitiliza, kwenye shule zetu tunazowapeleka watoto wetu wanawapelekea vitabu vinavyoonesha na kufundisha mambo hayo waziwazi wakidai kwamba ni misaada ya *NGO's,* sasa naiomba Serikali waangalie hili suala, hivi vitabu huwa vinapita wapi? Je, Serikali inakuwa iko likizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munira taarifa hiyo.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, hawa maafisa wetu kwanza ni wachache lakini pili hawana vitendea kazi hususan magari. Maafisa hawa muda mwingi unawakuta ofisini, hawako *site* kwa ajili ya kufanya kazi. Tuwatafutie maeneo husika au vituo ambavyo kama mtu yeyote ana shida na maafisa hawa wanaweza kupatikana kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafisa hawa wa maendeleo ya jamii tunatakiwa tuwapatie magari ili waende *site,* waende kwenye vitongoji vyetu na Wilaya zetu wakaangalie changamoto zinazowakuta wananchi kule. Mpaka leo kuna walemavu kule wanafichwa majumbani hawajapatiwa elimu za majumbani, hawa maafisa wa maendeleo ya jamii waende kule wakawafichue watoto hawa ili waweze kupatiwa elimu nyumbani na wengine wapelekwe hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia mpaka vyombo vya habari vikienda ndiyo unakuta changamoto hizi za watoto walemavu au wenye mahitaji maalum ndiyo vinawainua kuwa kuna

changamoto (a), (b) na (c) ndiyo Wizara inaweza kuwafanyia kazi. Naiomba sana Wizara iangalie tena maafisa wetu wa maendeleo ya jamii kuweza kuwapatia magari waweze kufanya kazi zao. Watakapowaweka au watakapokuwa na kituo cha kufanyia kazi watu wengi watafika na kwenda kuonesha shida zao au kwenda kusikilizwa shida zao ambazo zinawapata ndani ya jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib. Nilimtaja Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo na Mheshimiwa Furaha Matondo wataongea kwa dakika kumi kumi.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, kabisa napenda kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na sasa niko katika Bunge lako Tukufu. Pili, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazoendelea kuzifanya katika Taifa letu kwa kuleta maendeleo kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kujielekeza kwenye mchango wangu. Napenda kuongelea jambo hili ambalo mchangiaji mwenzangu aliyetangulia katoka kuliongelea, suala la malezi na mmomonyoko wa maadili. Kwanza kabisa, nasikitika sana kwa kile kinachoendelea katika nchi yetu, watoto wetu wa kiume kwa sasa malezi yao yamekuwa ni taabu sana. Wakina mama au wazazi wengi wa kiume wanapata shida sana jinsi ya kulea watoto hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mtoto akishafikia darasa la saba unaanza kufikiria kumpeleka *boarding,* unapofikia kipindi hicho unaanza kuwaza, sasa nampeleka katika shule gani na shule hii mtoto wangu ataenda kupata elimu au anaenda kujifunza na vitu vingine? Maana yake shule za *boarding* ndiyo zinasemekana ni chanzo cha mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kwenye malezi yetu majumbani tunaishi na jamii mbalimbali na ndugu zetu, jamaa zetu na marafiki zetu lakini hao hao ndiyo wamekuwa chanzo kikubwa cha ushoga kwa watoto wetu kwa sababu anapokuja mgeni nyumbani, kwa mila zetu za kiafrika huwezi kumfukuza, tunakaa nao majumbani mwetu, anakaa siku kadhaa, labda wiki mbili au mwezi. Sasa hatujui watoto wetu wanafundishwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi kinacholeta haya matatizo kuchangia tatizo hili kuwa kubwa ni kutokana na sisi wazazi tumeshindwa kuwajibika kwa sababu, zamani malezi wakina mama au familia ilikuwa karibu sana na mtoto lakini labda kutokana na mazingira ya maisha magumu, kila mtu sasa anatoka nyumbani kwenda kutafuta riziki ili kusaidiana katika familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa imetokea jambo ambalo tumesahau watoto au tumesahau familia, tumebaki kukimbizana na pesa lakini huku mambo ya nyuma nyumbani hatuyajui. Kwa hiyo, napenda kuwakumbusha wazazi hilo pia liwe jukumu letu angalau hata kama tuko *busy* lakini turudi nyumbani tujaribu kuongea hata na watoto wetu, tujaribu kujua ni nini kilichojiri mchana kutwa tangu asubuhi mpaka jioni au kama ulikuwa umesafiri japo kwa ile wiki au wiki mbili mtoto ni nini amekutana nacho, je amekutana na unyanyasaji wa kijinsia? Lakini tunapokuwa tumenyamaza na kuendelea kufanya shughuli zetu ndiyo mmomonyoko huu wa maadili unapokuwa tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kuna baadhi ya mitandao ndiyo inachochea zaidi matatizo haya, kwa sababu tumekuwa tukiona *video* mbalimbali kwenye *WhatsApp,* ma-*group* mbalimbali na *Instagram* zikiwa kama zinajaribu kuuinua zaidi ule ushoga, kwa sababu unakuta kuna shoga mule anajinadi kwamba yeye, kwanza anavyoongea au anvyojaribu kutetea hoja yake anaonesha amefanikiwa kwenye hiyo sehemu labda anafanya biashara lakini akijionesha kwamba yeye yuko kwenye maudhui gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali isipokuwa makini na kukemea vitendo hivi kwa kufuata sheria na kutoa adhabu kali kabisa tatizo hili litaendelea kutusumbua na kuwaharibu watoto wetu na familia zetu. Kwa kifupi napenda nijielekeze kwenye mambo machache ambayo nimejaribu kufanya tafiti kuona chanzo hasa cha haya mambo ya ushoga yametokea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa ni kumomonyoka kwa maadili. Tumejisahau kufuata mila na desturi zetu. Zamani wazazi wetu tuliishi na ndugu na jamaa siku zote lakini mambo haya hayakuwepo kwa sababu wazazi tulikuwa karibu lakini pia mila zetu hazikusahaulika, leo tumeanza kufuata mila za kigeni zaidi na kwa sababu hasa ya hii mitandao ya kijamii, tunajaribu kuiga vitu ambavyo hatukuwa navyo tangu zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kama nilivyosema hapo awali, wazazi tumesahau wajibu wetu. Malezi, bado watoto wetu wanahitaji malezi ya karibu ya mzazi kwa sababu wanasema, uchungu wa mwana aujuae mzazi. Sasa sisi tukiwaachia Dada kule nyumbani kuwalea watoto kwa hiyo mtoto ana-*copy* vitu vyote, Dada kama ana tabia mbaya ina maana na mtoto atachukua vitu vyote vibaya, kama Dada ana tabia nzuri ndiyo hapo kidogo itakuwa utapata mtoto ambaye kidogo ana maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaangalia jambo jingine ni uelewa mdogo kuhusu athari zinazoweza kuletwa na tabia hii hasa umaskini, matumizi yasiyofaa ya teknolojia, mitandao (utandawazi), udhibiti mdogo wa vituo vya kutolea huduma za jamii kama mashuleni na baadhi ya taasisi, utekelezaji usiokuwa na msisitizo wa sheria inayokataza masuala haya ya ushoga na uzembe wa kutowabaini wanaofanya vitendo hivi, kwa sababu tukiwabaini hawa watu watachukuliwa hatua kali na tutapunguza hili tatizo kwa asilimia kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia ni nini hasa au ni nini ambacho kimepelekea jambo hili kuwa na kasi kubwa ya kuenea, lakini jambo kubwa kabisa ni mitandao, mitandao hii imeweza

kuchangia kwa asilimia zaidi ya 50, mambo yanayoendelea humo kwenye *instagram* na kwenye ma-*group* ya *Whatsapp* ni mambo mengi mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali na Wizara mjaribu kuelimisha jamii kwa ujumla hasa shuleni kuanzia elimu ya msingi, watoto waelimishwe na wafundishwe tamaduni zetu halisi, tuende na zile tamaduni tulizozaliwa nazo au tulizokua nazo angalau tutaokoa kizazi chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo. Nilimtaja Mheshimiwa Furaha Matondo baadae Mheshimiwa Neema Mwandabila na Mheshimiwa Mwatumu Dau Haji wajiandae.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara nyeti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema na kunipatia ridhaa na kibali cha kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu, namshukuru Mheshimiwa Waziri Dada yetu Dorothy Gwajima na wasaidizi wake wote, Naibu Waziri Mheshimiwa Mwanaidi, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu na kipenzi chetu Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya mambo makubwa sana sote tunayaona. Mama yetu kipenzi ndiye ameanzisha Wizara hii ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii, ameona kuna haja sasa ya kuanzisha hii Wizara ili kwenda

kupambana na vijana, wamama, machinga na makundi maalum, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa Wizara yetu ina bajeti ndogo sana. Mwaka uliokwisha tulikuwa tuna bajeti ya shilingi bilioni 74.2, mwaka huu tumeshuka tunayo bajeti ya shilingi bilioni 67.9. Hii inaonesha wazi ni jinsi gani Wizara hii ilivyo na umuhimu mkubwa na wa kipekee lakini bado haijachukuliwa kwa umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hii Wizara iweze kuchukuliwa kwa umuhimu wake mkubwa kwa sababu ni Wizara nyeti inakwenda ku-*deal* na maisha ya watu na maisha ya kundi kubwa zaidi ya asilimia 50 ya machinga wa Tanzania wako katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo za Wizara hii bajeti iliyopita ilitoa asilimia 14.5 pekee. Hii inaonesha wazi Wizara hii bado haijatiliwa maanani. Namuomba Kaka yangu na rafiki yangu Waziri wa fedha Mheshimiwa Mwigulu aone kuna haja ya kutoa fedha katika Wizara hii nyeti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii iweze kwenda kufanya kazi zake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyopita tulitengewa shilingi milioni 50 kwa wazee wetu na wazazi wetu wanaoishi Ipuli - Tabora lakini kwa masikitiko makubwa fedha zile hazikutoka. Tulitengewa shilingi milioni 50 kwa wazee wetu na wazazi wetu wanaoishi Bukumbi Wilaya ya Misungwi Mkoa wa Mwanza lakini zile fedha hazikutoka. Hii inaonesha wazi tukitoka hapa kwenda kuangalia makazi ya wazee wetu wanayoishi tunaona huruma, wazee wetu wanaishi kwenye makazi ambayo hayastahili. Tumetenga bajeti, bajeti haitoki, wazee wanahangaika, wametulea na wametukuza mpaka wametufikisha hapa, Mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan kaona haja ya kuwashika wazee wetu lakini fedha hazikutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu Tukufu kuona haja sasa fedha ziweze kutoka zikawaguse wazee wetu, vijana na

machinga ili waweze kuonekana wana umuhimu sana katika Taifa letu hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za machinga. Bajeti iliyopita tulitenga shilingi bilioni 18.5 lakini kwa masikitiko makubwa fedha hizo hazikutoka. Safari hii tumetenga shilingi bilioni 10.5 naomba sana fedha hizi ziweze kutoka ziweze kwenda kuwagusa machinga waweze kwenda kukopa ili nia njema na mapenzi mema ya Mama yaweze kuonekana kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la mchinga ni kubwa kama tulivyosomewa na Waziri, linakwenda kugusa mama lishe, wasusi, waendesha bodaboda na wale wote wanaofanya biashara ndogondogo ni kundi kubwa la machinga. Naomba waende sasa wakakopeshwe fedha hizi. Hii shilingi bilioni 10.5 ambayo iko kwenye bajeti yetu iweze kutoka na kuwafikia vijana wetu, mama zetu na watoto wetu waweze kwenda kuguswa na hili kundi ili waweze kufanya biashara maana kundi hili la machinga ni kubwa zaidi ya asilimia 50 liweze kwenda kuguswa na biashara zao ziweze kwenda vizuri. Nitaendelea kuomba palepale Wizara ya Fedha iweze kuliona hili kwa umuhimu Wizara yetu iweze kupatiwa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati tuliona asilimia saba ya riba ni kubwa, naiomba sana Serikali yangu kwa kuliona hili iweze kwenda kukaa na kuona watachakata vipi ili asilimia saba iweze kushuka angalau kidogo ili mama zetu na vijana wetu wanapofanya biashara wafanye biashara wakiwa na amani ya kurejesha mkopo na wenyewe kuweza kupata faida badala ya kufanya biashara wakijua wanakwenda kukimbizwa na kwenda kunyang'anywa mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba riba hii iweze kushuka ili kuwafanya vijana wetu wa machinga ambalo ndilo kundi ambalo tunalitegemea liweze kufanya biashara zao wakiwa wametulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kumpongeza Mama yetu na kipenzi chetu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli

ameendelea kulibeba kundi hili nyeti, kundi la machinga. Nasema hivyo kwa sababu mama ameona haja sasa ya kuanzisha kila Mkoa waweze kupata ofisi, hilo ni jambo nyeti na jambo zuri sana la kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama anayekaa na kutafakaroi watoto watafanya nini, mwanamke anayejua kwamba watoto wangu hawa ndiyo tegemezi kwangu na ninatakiwa kuwasaidia kwa hali na mali. Kwa hiyo, kila Mkoa kuna ofisi ya machinga na kama haijamalizika inakwenda kumalizika na inakwenda kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali yangu iweze kuona kuna haja ya kukaa na kuangalia muundo wa machinga kwa ujumla, kwa sababu sasa hivi ukiangalia ukienda Mkoani wana katiba ya machinga, ukienda Wilayani kuna katiba ya mmachinga, ukienda kwenye Kata kuna Katiba ya Mmachinga, naomba muundo wa machinga uundwe Serikalini uwe na Katiba moja itakayosimama, litakalokuwa limeongelewa huku iwe ni kitu kimoja hili linakwenda kuwafanya kuwa na matatizo na kupata shida kufanya kazi malalamiko na migogoro isiyoisha kwa sababu kila sehemu wana katiba yao. Ukitoka hapa wana katiba yao ukirudi huku kuna katiba yao. Naomba muundo sasa uundewe kwenye Taifa ili ...

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anayechangia muda huu anachangia vizuri sana, natamani kumuongezea nyama hapo kwenye mchango wake, Serikali ilikuwa inawajali sana machinga kwa kuwapa vitambulisho ambapo walikuwa wanakata kwa shilingi elfu 20; kwa sasa hivi wamekuwa wanapata shida sana namna wanavyochajiwa kodi. Hivyo natamani sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili. Hawa machinga wakipata vitambulisho vile walivyokuwa wanalipia shilingi elfu 20 na hawabugudhiwi tena na kodi zingine nadhani ingefaa sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha Matondo unapokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Suma Fyandomo?

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa na ndiko huko nilikokuwa naelekea, nakushukuru sana rafiki yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa, kuna ndugu zetu wenye ulemavu, tunapokwenda kwenye suala la mikopo natamani sana wasiambiwe wawe kikundi, kwa sababu wale wanakuwa ni wachache, naomba wakathaminiwe kutokana na hali zao waweze kupatiwa mikopo na waweze kufanya biashara wakiwa wametulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema ndugu wetu wenye ulemavu wajikusanye hamuwezi kuwapata kila sehemu, kwa hiyo ikitokea kwenye Kata au Kijiji kuna mlemavu mmoja naomba apate haki yake ya kupata mkopo ili aweze kufanya biashara na aweze kufanya maisha yake akiwa vizuri kwa sababu Mama amewathamini na kuona wana haja sasa ya kufanya shughuli zao wakiwa wametulia na wakiwa katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Furaha Matondo. Ambao nitawataja kuanzia sasa wote watachangia kwa dakika tano tano. Tutaanza na Mheshimiwa Neema Mwandabila Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yetu mzuri Mheshimiwa Giga, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu kabisa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Ninasikitika dakika tano ni chache lakini nitazitumia hizi hizi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote nataka tu kusema kwamba, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima pamoja na Mheshimiwa

Naibu Waziri na Katibu Mkuu wetu kiukweli pamoja na kwamba wana fedha chache lakini wanafanya kazi kubwa na nzuri. Nadhani ipo haja sasa ya Serikali kuona umuhimu wa kuwaongezea fedha kwa ajili ya kufanya kazi hizo wanazozifanya. Tanzania ni kubwa, wanahitaji fedha ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nielekee kwenye zoezi la usajili wa machinga. Ninafahamu kabisa machinga ni kundi muhimu. Machinga na wafanyabiashara ndogondogo wengine wote ni makundi muhimu kwa Taifa letu. Kuwatambua mahali walipo na kazi zao kwa kweli ni jambo la msingi kwa ustawi wa Taifa letu. Kwa hiyo, kwa kasi hii ya usajili ambayo ipo inaonyesha kabisa Wizara hawajawa na mkakati maalum wa kuhakikisha usajili unaenda kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimuombe Mheshimiwa Waziri kupitia kikao hiki aangalie namna ya kutengeneza *taskforce* na kutafuta vitendea kazi vya kwenda kusajili machinga. Kitendo cha kusema usajili ni hiyari hawawatendei haki wamachinga. Usajili unatakiwa uwe ni kitu ambacho ni cha lazima kama usajili mwingine wowote unaofanyika ili tuweze kuwabaini na tujue ni namna gani tunawasaidia hawa ndugu zetu wamachinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nieleze kwa masikitiko nikiwa kama Mbunge wa Viti Maalum ninayetokea Mkoa wa Songwe. Hii taarifa inayoendelea mtandaoni ya kusema kwamba Wilaya ya Momba ndani ya mwezi mmoja imepata mimba 194 ni kitu ambacho kinasikitisha sana. Hapa ninaongea mwili wangu mzima unasisimka. Hili niliwahi kuongea hata mwaka jana kwamba iko kazi ya kufanya kwenye Wilaya ya Momba kuwanusuru watoto wetu. Siyo Momba tu na Mkoa wa Songwe kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu za mimba za utotoni, Mkoa wa Songwe una asilimia 45. Sasa kwa kasi hii ya 194 kwa mwezi ninashindwa kuelewa ni nini kinaenda kutokea katika mkoa wetu. Kwa hiyo, niweze kumpongeza Mkuu wa Mkoa wangu kwa namna ambavyo yeye na timu yake wanafanya kazi nzuri ya kuendelea kupambana na hiki kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nilitamani hizi mimba 194 ambazo zimeonekana za mwezi huu, watoto wanajulikana wako wapi, wazazi wao wanajulikana, Serikali za vijiji wote wanawajua hawa watoto walipo. Kwa hiyo, ninatamani kama *sample* ya Taifa ianzie Momba, kwenda kuwashughulikia hawa watu 194, ijulikane ni nani katoa mimba na yuko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto moja ameiongea Mheshimiwa Munira na Mheshimiwa Festo akawa amekazia; suala la dhamana kwa watu ambao wanatoa mimba watoto wetu pamoja na dhamana kwa watu wanaooa watoto wetu wadogo. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri alichukue kwa uzito wake, ikiwezekana wakae na timu ya Wizara za Katiba na Sheria na Mambo ya Ndani waangalie ni namna gani wanaenda kutusaidia sisi kama Taifa kunusuru kizazi chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mtu anabaka kesho unamuona mtaani. Ushirikiano hauwezi kuonekana kwa sababu wale watu wanaenda kupoteza ushahidi mtaani. Kikubwa zaidi kwa sisi watu ambao tunakaa mpakani, wale watu wanabaka huku, wanaenda kuishi Zambia. Kwa hiyo inakuwa siyo kitu ambacho ni rahisi kuweza kuki-*manage*. Mhalifu anapopatikana ni *better* ahifadhiwe mpaka pale kesi yake itakapokuwa imeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hilo ni ombi langu maalum kwa Serikali na ninajua Mheshimiwa Rais ni msikivu na hili la mimba hizo za Songwe akilisikia ataenda kufanya kitu kule Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kuhusu hawa wasichana wa kazi majumbani. Tunaongelea ukatili, tunawalenga wale ambao wako mtaani lakini kuna kundi ambalo linafanyiwa ukatili ambalo takwimu zake mpaka sasa hatuwezi kuzipata. Mheshimiwa Waziri anatakiwa pia alione hili la wafanyakazi wa majumbani kwa namna ya tofauti. Inakuwa ni kama watu wanaona wale watu hawana umuhimu huku wanawategemea, wanawaachia majukumu makubwa ya kifamilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo yanapokuja kutokea kwenye familia yao, watoto wao na wenyewe wanafanyiwa ukatili na ndivyo tunavyoendelea kuharibu kizazi chetu. Kwa sababu kile unachomtendea mtu ndicho utakachovuna na wewe. Kwa hiyo, hilo pia naomba Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, haya mambo ya ukatili hayaendi hivi hivi bila kuwa na tatizo kwenye afya ya akili. Dada yangu hapa, balozi wa afya ya akili, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, amekuwa akipiga kelele sana lakini ipo haja maalum ya kuwezesha hizi huduma za afya ya akili ziende kwenye wilaya zote. Ikiwezekana, mimi natamani kungekuwa na *screening* au kitu ambacho kinaweza ku-*scan* watu kujua hii *mental illness* iko kwa kiwango gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii changamoto ya afya ya akili inaendelea kuongezeka kulingana na *stress*. Misongo imekuwa ni mingi, mambo yamekuwa mengi na fedha hazipo. Kwa hiyo lazima watu watatafuta kufanya mambo ambayo katika hali ya kawaida binadamu ukiwa *mentally fit* huwezi kuyafanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani wajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona saa hizi. Hizi Wizara mmetupangia nyinyi, tuchague Wizara anayetaka kuchangia achangie. Sasa hivi hapa tunaambiwa tuchangie kwa dakika tano, haya twende kazi. *(Makofi, Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kuwa na hali ya uzima

na afya. Pia, nawashukuru na nyinyi viongozi wetu kwa kutuweka hapa katika hili Bunge Tukufu tukaweza kuchangia na mkachukua maneno yetu mkayapanga katika Wizara zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kwanza nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Gwajima pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi, nawashukuru sana kwa kazi kubwa mnazozifanya. Mnahangaika nyinyi nawaona, Mheshimiwa Mwanaidi huna nafasi ya kuja mkoani Kusini ukafanya kazi, kwa kuhangaika na hii kazi uliyopewa na Mheshimiwa Waziri, tunakuona Mheshimiwa Mwanaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Gwajima hapa Bungeni tunamtafuta saa nyingine hatumuoni. Yupo anahangaika kwa kazi yake hii aliyopewa. Hata hivyo, Mheshimiwa Dkt. Gwajima na Mheshimiwa Mwanaidi, hii kadhia iliyokuwepo katika hii Hotuba yenu mliyoisoma hapa. Hotuba nzuri sana, ina kina, ina maneno mazuri, imejaa kila kitu lakini bado haijakuwa na mustakabali mzima wa watoto wetu na wenye ulemavu kwa vitendo wanavyofanyiwa na watu wanaobaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitambulike vizuri Mheshimiwa Mwantumu Dau ninavyosema, nisije nikafika nje nikaitwa chapa funga ulale, sitaki. Ninazungumza hili, watu wanaobaka, sheria iletwe hapa Bungeni. Sheria iletwe tuipitishe sote humu Bungeni ili hawa watu wabakaji wahasiwe. Watu hawa wanaobaka watoto wetu, mtoto kavishwa nepi anakwenda kumfungua *pampers,* anakwenda kumfanyia kitendo kibaya. Watoto wetu wanaume wanalawitiwa, kweli hii ni haki? Mwenyezi Mungu yuko radhi na hili? *(Makofi, Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria iletwe, itungwe hapa. Watu wanaofanya vitendo hivi, siyo kwa wanaume waliokuwa wao jadidi, wale wanaume waliokuwa wanabaka, mimi nasema; wahasiwe tena kwa ile sindano, watiwe sindano, hawana nguvu, wamekwisha. Hili ndiyo litakuwa mustakabali mzima wa Taifa letu. Hili lipitishwe humu Bungeni, maana mtu akishambaka mtoto, kama wanavyozungumza wenzangu hapa. Wote wamezungumza,

wanazungumza suala la ubakaji, unyanyasaji wa watoto wetu, wanawake, watu wenye ulemavu, hakuna mmoja ambaye hajasema hili. *(Makofi, Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hili limenikaa humu ndani ya nafsi yangu kila nikikaa najiuliza, kwanini watoto wadogo wafanyiwe kama hivi? Kuna wanawake wanaranda huko mapaja nje, nguo zinawekwa mpaka hapa, kwanini hawaendi kuwabaka wale? Wanawaogopa? Wanakwenda kuwabaka watoto wadogo, siyo vizuri wanavyofanya hao wanaume ambao wenye vitendo hivi vibaya, vichafu na viovu. Mheshimiwa Dkt. Gwajima na Mheshimiwa Mwanaidi hili suala bado linaendelea huko kwenye Taifa letu na Tanzania nzima. Halina mjadala hili, mlilete tulipangie sheria. *(Makofi, Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la kuzungumzia…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa vile uchangiaji ni dakika tano, sitatoa ruhusa ya taarifa.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia. Kwa kumalizia kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais wangu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwaweka viongozi wake hapo ili mlitetee hili suala. Namshukuru sana ndugu yangu, anaifanya kazi kubwa, Mwenyezi Mungu amuondolee kila la dhiki, kila la shari, ampe heri na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna masuala ya mashoga, kuna masuala haya ya watoto wanaume kufanyiana wenyewe kwa wenyewe, hili suala lifanyiwe kazi na lijulikane limefanyiwa kazi. Haya mambo mengi ninayo lakini tumeshakatishwa dakika kidogo. *(Makofi, Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Waheshimiwa Wabunge wakati tunaendelea na uchangiaji wetu

kuna wageni wawili wamesahaulika wa Mheshimiwa *Professor* Joyce Ndalichako ambao ni walimu wawili na wapigakura wake kutoka Kasulu. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa *Professor* Joyce Ndalichako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu dakika tano ni chache, tuwaachie wachangiaji watoe, sitaruhusu taarifa. Nilimtaja Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Ng'wasi ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hi muhimu sana. Kuna shida kubwa sana ya watu wanaoombaomba mitaani. Tatizo hili ni kubwa sana na hasa wanapoongozana na watoto wadogo kuwapeleka kuomba kwenye baa na sehemu zingine tofauti. Tunaomba sana Wizara hii ichukue hatua kali na za makusudi kuwanusuru watoto hawa. Kwa sababu leo hii mzee anatembea na mtoto mdogo ambaye alitakiwa kuwa shuleni na sisi kama Taifa tunaangalia tunaona ni kitu cha kawaida, yule mtoto hatima yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamjengea nini yule mtoto, kesho yake iweje? Ninaomba Wizara hii itoe katazo na ikiwezekana itungwe sheria kabisa watoto kwenye kuomba omba kwenye majiji makubwa kama Mbeya, Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma hapa ndiyo wanaongoza zaidi. Tunaomba sana tukatae watoto wetu kutumika katika masuala ya ombaomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, yamezungumzwa hapa masuala ya ukatili wa kijinsia na yamekuwa ni wimbo wa Taifa. Sheria imetungwa, ukikutwa umelawiti au umebaka ni miaka 30. Mimi binafsi nadhani tulifikiri miaka 30 ni mingi lakini wakati mwingine mtu anaenda jela miaka 30 mpaka arudi watu wamemsahau. Hebu apewe miaka mitano, apigwe, atengenezewe kesi mbaya kama ambavyo Mheshimiwa aliyemaliza kuongea, labda akirudi kijijini watu wataogopa. Mambo ya kukaa muda mrefu, miaka 30, labda watu wanasahau. Mimi najaribu tufikiri upya ni adhabu gani zinafaa tena kwa ajili ya kukatisha haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la ustawi wa jamii ni suala muhimu sana kwa sababu ustawi wa jamii ndiyo maisha ya Watanzania lakini leo ajira hakuna. Wanaoajiriwa hawapo; wako wachache wamesoma wako mtaani lakini mwisho wa siku kwenye kata, vijiji na vitongoji hawa watu ni wa muhimu sana. Mheshimiwa Waziri tunaomba ajira ya maafisa ustawi wa jamii, maafisa maendeleo ya jamii ni muhimu sana katika halmashauri, vitongoji na vijiji vyetu na hili nitalizungumza nitakapokushikia shilingi usipate mshahara mpaka tuhakikishe umeajiri hawa watu kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maadili katika Taifa hili. Leo hii Mheshimiwa na sisi viongozi tunaongoza; hatukai na familia zetu tukawaonya, tukawatunza watoto wetu bali tunawaachia wadada wa kazi. Dada wa kazi anakuja kufanya kazi akiwa ni mdogo zaidi ya watoto wetu. Tunahakikisha dada wa kazi ndiyo kila kitu kuanzia elimu ya watoto wetu, maisha ya watoto wetu wakati sisi tuko *busy* na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tusimamie maadili ya watoto wetu sisi kama viongozi kwanza na baadaye Watanzania wote. Unaondoka nyumbani toka saa 12 asubuhi kuwahi foleni, unarudi saa nne usiku, hujui mtoto wako anacheza na nani, hujui mtoto wako anaongea na nani, hujui amekula nini, hujui chochote zaidi ya dada wa kazi. Dada wa kazi naye ana mambo yake, ana *boyfriend* wake, ana mambo yake, anaangalia *pornography pictures* wewe mama hufahamu. Mimi ninaomba kama Taifa tuhakikishe maadili ya watoto wetu tunayasimamia na tunayafanyia kazi kwa sababu mwisho wa siku tunatengeneza mama na baba wa kesho na viongozi wa kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mitandao ya kijamii. Mimi ninaamini tumezungumza jana katika Wizara iliyoondoka lakini wewe kama Waziri unalo neno la kusema. Leo hii kwenye mitandao ya kijamii ukatili wa kijinsia unafanyika sana na hata kwa wanasiasa unafanyika ukatili wa kijinsia. Mwisho wa siku, picha za ngono; watu wanajitangaza kwamba mimi ni shoga, ninapatikana mtaa fulani, mahali fulani na namba ya simu ipo. Mheshimiwa Waziri tunaomba

matamko makali kuhakikisha watu hawa wnakamatwa kwa sababu siyo utamaduni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, zipo *NGO* ambazo zina-*support* mambo ya ushoga. Mheshimiwa Waziri tunaomba uzisimamie na ufuatilie hizo *NGO* zilizosajiliwa na kama ni za kimataifa zifuatiliwe. Tunaona vitabu vya jinsia moja vinauzwa. Kuna mzungu mmoja alikamatwa pale Mwenge, waziwazi anagawa vitabu vya jinsia moja. Pia, kuna katuni kwenye baadhi ya mitandao, hata kwenye baadhi ya *television* katuni zingine ni za kuziangalia. Katuni mpaka ipitishwe mtoto aangalie, kuna katuni za usagaji, ziko mle. Lazima tusimamie maadili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndiyo tunatengeneza watoto wa kesho na viongozi wa kesho. Tusipokuwa makini wenzetu wanaweza kutupenyezea vitu visivyofaa kwenye maisha ya kila siku ya watoto wetu. Mheshimiwa Waziri tunaomba, wewe ndiye mama namba moja unayetengeneza wanawake wa baadaye na Taifa la baadaye; tunaomba sana usimamie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo bado ninasisitiza kwenye *NGO*. Tunafahamu kuna utaratibu wa wilaya kusajili na kupeleka ripoti za kwenye *NGO* lakini bado ubabaishaji uko mwingi. Wanatoa posho za kutosha, vikao vya semina vya kila siku na kutoa fedha nyingi lakini *behind the scene* kuna mazungumzo ambayo sisi kama Taifa hatuyafahamu. Ninaomba sana tuyasimamie hayo, ninaomba sana tuangalie haki za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ninafikiria suala la asilimia 10 za mikopo ya wanawake. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri uangalie watu sahihi wa kupata mikopo hii. Isiwe watu wale wale wanarudia, wa chama fulani au wa sehemu fulani. Tunaomba watu wote wapate mikopo kwa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitakutana na Mheshimiwa Waziri pamoja na anayeajiri kwenye kushika shilingi

mpaka watakapotoa tamko la kuajiriwa maafisa ustawi wa jamii wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Nilimtaja Mheshimiwa Ng'wasi Kamani; Mheshimiwa Abeid Ramadhani, Mheshimiwa Ali King na Mheshimiwa Mwita Waitara, wajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Kwa sababu ya muda nitaenda moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto ni mbegu, yaani kama ambavyo mkulima anakuwa na mahindi yake ndani anavuna mwaka huu anatunza kwa ajili ya mbegu za mwaka ujao, watoto ni mbegu. Ndiyo maana kuna mataifa sasa hivi yanalipa fedha nyingi sana kwa watu wake kuhakikisha kwamba wanapata na kutunza watoto wao kwa sababu wanatambua umuhimu wa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mataifa kama Taiwan, Japan, China na Ujerumani yanatumia bajeti kubwa sana kuhakikisha kwamba yanawekeza kwenye upatikanaji na ulezi wa watoto. Kuna mambo yanaendelea kwenye nchi yetu leo ambayo kimsingi yanatishia sana ubora wa mbegu tunazopanda leo kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii haiwezekani kupita kwenye mitandao ya kijamii bila kupata kesi kuanzia tatu mpaka tano za ubakaji na ulawiti wa watoto. Tunavyozungumza sasa hivi, nashukuru Mbunge wetu wa Songwe, Mheshimiwa Neema Mwandabila, amezungumza. Kuna takwimu imetolewa na Mkuu wetu wa Mkoa wa Songwe, kwamba watoto 194 walio chini ya umri wa miaka 18 wa shule za *primary* na sekondari, wamepata ujauzito ndani ya mwezi mmoja kwenye Wilaya ya Momba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwenye Wilaya ya Ileje, watoto 170 wamepata ujauzito ndani ya miezi mitatu tu, wote chini ya umri wa miaka 18. Takwimu za Serikali na Wizara zinaonyesha kwa mwaka 2022 watoto 1,586 wamelawitiwa kwenye nchi hii. Watoto 6,827 wamebakwa kwenye nchi hii. Hata tunavyozungumza sasa, japo takwimu za mwaka 2023 hazijapatikana lakini inaonekana kuna ongezeko la zaidi ya asilimia 20 ya idadi hii. Tunapanda mbegu gani kwenye Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Hospitali ya Wilaya imetoa takwimu; kati ya mwezi Oktoba 2023 mpaka mwezi Disemba 2023 imezalisha watoto 394 walio na umri wa chini ya miaka 18, ndani ya miezi mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi katika wilaya hiyo wamekiri kuwa wamewaingiza watoto wao kwenye mpango kwa kutumia *contraceptives* na hizi njia za uzazi wa mpango kwa sababu hawajui wafanye nini. tunakwenda wapi? Watoto wetu wa kike tunawapeleka wapi kama tunaanza mapema mambo kama haya? Vilevile wamekiri kwamba maduka yetu ya dawa yanashiriki kuuza vitu hivyo kwa watoto wetu walio na umri chini ya miaka 18. Wizara imesema nini juu ya haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunajua kwamba wengi wanaofanya matendo haya, kuanzia ubakaji, ulawiti na unyanyasaji wa kingono wa Watoto ni wanafamilia, Wizara imetoa takwimu hizo. Kwa maana hiyo mengi yanakuwa ni siri, kwa hiyo hata takwimu tunazozipata ni chini ya asilimia 50, hatupati takwimu za usahihi kwa sababu yanafanyika kwa usiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hatua za haraka zinahitajika kuchukuliwa, kwa sababu tunavyokwenda hivi kwa miaka 30 ijayo takwimu itakayokuwa *uniform* kati yetu sisi wote vijana wa kipindi hicho, itakuwa ni kwamba wote wamewahi kubakwa na kulawitiwa. Hatuwezi tukatengeneza Taifa la namna hiyo, lazima tuchukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri, ushauri wangu wa kwanza ni kwamba tufanye mabadiliko ya sheria za adhabu. Mimi ni mwanasheria, najua kuna wengi watakuja na *issue* ya haki, lakini mimi ni mwanasheria ninaelewa. Ni lazima tuingie vitani, tuko vitani; na kwenye vita sisi wananchi ni lazima tuamue tunapigane kwa namna gani vita hiyo kwa maslahi makubwa ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfalme Louis XVI kati ya *speech* zake ambazo ni *famous* sana aliwahi kusema, mimi ni nchi na nchi ni mimi. Katiba yetu maneno yake ya kwanza yanasema *we the people*, sisi Watanzania; kwa maana ya kwamba namna ambavyo tutaipeleka nchi yetu ni maamuzi yetu sisi Watanzania. Leo hii wote najua hatufurahishwi na mambo haya, tutunge sheria, tufute dhamana za watu wanaoshitakiwa na mambo haya. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tuongeze adhabu, lazima tufanyie mapitio ya adhabu tulizoweka kwa sababu *it's clear* kwamba hazifanyi kazi. kama tumeweka adhabu ya miaka 30 na bado watu wanafanya kama vile hakuna uangalizi, lazima tuangalie namna bora ya kwenda na hivi vitu. Lakini pia tuweke adhabu kali kwa wale wazazi ambao watabainika kuficha mambo haya. Kwa sababu kuna wazazi ambao wanaripoti na baadaye wanakuja tena kusema kwamba hicho kitu hakipo; maana yake kuna vikao vya nyuma vimefanyika *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuweke adhabu ili nao wawe wanapata adhabu kwa sababu ya kuficha matendo hayo. Si hivyo tu, lazima tuweke utaratibu wa hizi kesi kuchukua muda mfupi. Haiwezekani, kitendo kimefanyika, daktari amethibitisha kwamba kuna kitendo kimefanyika na aliyefanya anafahamika, sasa tunakaa miezi sita au mwaka na hii kesi ili iweje? Hii ni shida, tunaleta shida ya kisaikolojia kwa yule mtoto. Lazima tuweke muda mfupi wa kesi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; ninaomba tuweke *database* ya wazi ili wale wanaoonekana kufanya vitu hivi wawekwe kwa uwazi picha zao na taarifa zao, wanapopatikana iwe wazi. Kwa

sababu kwenye Mkoa wa Kilimanjaro kuna mtu ambaye alikuwa amekwishakamtwa kwa kesi ya kulawiti, wakati akiwa nje kwa dhamana, akalawiti watoto wengine 18. Haitakiwi, Serikali ipo, ichukue hatua. Lazima taarifa za hawa watu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** …ziwe wazi, tuwekeze kwenye familia, tubadilishe sheria za utumishi wa umma ili familia ziwekwe pamoja. Kama baba ameajiriwa Mwanza, mama aeajiriwa Rukwa warudishwe sehemu moja ili waweze kulea watoto wao. Tuondokane na janga hili… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngw'asi.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Niliwataja Mheshimiwa Abeid Ramadhani, Mheshimiwa Mheshimiwa Ali King, Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Mimi nampongeza Mheshimiwa Rais wetu, kwa kazi nzuri anayofanya lakini pia kuunda wizara hii. Kwa masikitiko makubwa kwanza siungi mkono hoja ya wizara hii, lakini pia ninatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakaonifuata wasiunge mkono hoja ya wizara hii kwa sababu imeshindwa kuchukua hatua ya kulinda Watanzania hasa watoto pamoja na kulinda maadili yanayoharibiwa kwa kisingizio cha ushoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatenga rasilimali hapa kama Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kutoa nafasi kwa Serikali kwenda kufanya kazi lakini jambo hili nasema limewashindikana. Ningeenda mbali zaidi, ningesema hawa waliopo kwenye hizo nafasi wangeona

aibu kwa jinsi ambavyo wanamdhalilisha Mheshimiwa Rais kwa kushindwa kuchukua hatua; wangepisha hizo nafasi ili watu wenye uwezo wapewe hizo nafasi wakazitendee haki Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye Biblia, Warumi 1:26 inasema "Hivyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu, hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili." Aya ya 27 au Mstari wa 27 unasema; "Wanaume nao vivyohivyo waliyaacha matumizi ya mke ya asili, wakawakiana tamaa. Wanaume wakayatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mistari ya Biblia iko mingi; lakini ukienda kwenye *Quran* pia kwenye *Surah Al Mu'minun*, Aya ya 5 – 7 inasema "Na ambao tupu zao wanazilinda isipokuwa kwa wake zao, au kwa wale ambao mikono yao ya kiume inawamiliki." Ukienda pia kwenye Sura ya 7, Aya ya 80 – 81 inasema "Nyinyi mnawaendea wanaume kwa kuwa ndiyo mnaowatamani badala ya wanawake, ama nyinyi ni watu wafujaji, wakatili?".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda hata kwenye Katiba ya Nchi, ninayo hapa vifungu vinavyoonesha jinsi ambavyo sheria ipo inayopinga mambo ya ushoga. Kifungu cha 154 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 na Marejeo ya Mwaka 2022, inasema; kwanza kifungu hiki kinazuia kufanya mapenzi kinyume na maumbile na adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30 jela au kifungo cha maisha. Ikifanyika kwa mtoto, adhabu ni kifungo cha maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda tena Kifungu cha 155 kinakataza kujaribu kufanya mapenzi kinyume na maumbile na adhabu yake ni kifungo si chini ya miaka 20 jela. Pia yapo matamshi ya viongozi wetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana wakati anahitimisha Bunge hapa, alisema kabisa kwamba nchi yetu inapinga ushoga na matendo yote yanayoenda kinyume na tamaduni na desturi pamoja na mila za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nyie kigugumizi cha kuchukua hatua dhidi ya huu uovu, huu ualifu, huu uchafu, kigugumizi hicho mnakitoa wapi? Katika haya niliyoyasema humu, dini, Mungu pamoja na Katiba yetu ya nchi inapinga, nyie kigugumizi mnakitoa wapi? Naomba mfanyie kazi Ripoti ya Mwakyembe. Kataeni wale wasanii, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani wale watu wanaojitangaza kuwa ni mashoga, umekabidhiwa mapolisi nchi nzima kwa nini hauchukui hatua? Una kigugumizi gani? Mnatumia rasilimali ya nchi hii lakini hamtutendei haki kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Afya uko wapi? Taarifa zinatolewa lakini hamchukui hatua. Ninaomba mamlaka zote zinazohusiana na jambo hili, mkae mjitafakari kama kweli mnastahili kuendelea kuwa kwenye hizo nafasi huku kizazi cha Watanzania kinaangamia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana…

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** … rejeeni kile kizazi, ambacho Mwenyezi Mungu aliwapindua na kuwaangamiza, aligeuza ile ardhi juu chini. Ninyi mnasubiri nini kuacha kuchukua hatua? na sisi…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhani…

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** … taasisi mbalimbali zinazounga mkono hoja jambo hili, watu wanaojitangaza waziwazi kuwa wanafanya mambo haya, wachukuliwe hatua. Vinginevyo hatutaelewana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Ali King, Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru sana kupata nafasi. Lakini pia kutokana na maelezo

waliyoeleza Waheshimiwa Wabunge wote, hakuna Mheshimiwa Mbunge hata mmoja aliyekaa, akasifia katika wizara hii., kila mmoja anakuja analalamika, na malalmiko haya yamenipelekea kusema msemo wa wazee unaosema "Usipoziba ufa, utajenda ukuta".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni wizara tumeipa jina tukataja mambo yake lakini tukasema mwisho makundi maalum. Lakini tukitazama huo umaalum wake, mie sioni. Hata kuzungumza tumepewa dakika tano hapa, kuna umaalum gani, ni kama kundi, ni sawasawa na wizara ambayo ina makundi ambayo yamekuwa *disadvantaged*. Hata kuzungumza, dakika zake kidogo. Tunataka tumalize mapema, haraka haraka, hawana kipaumbele, umaalum wao nini? Mie sioni kama kuna umaalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya wizara yetu hii, mwaka huu tunaomaliza ni shilingi 74,000,000,000 ambayo ni sawa na asilimia 0.16; ya mwaka huu pia ni shilingi 68,000,000,000, imeshuka, ambayo inakwenda chini ya asilimia 0.1 pengine mbili au tatu. Kwa maana hiyo bajeti yetu inashuka, ni sawasawa na mtu ambaye ameona kwamba anatumia rasilimali katika jambo ambalo halina maana. Akishaona kwamba jambo hili halina maana, anaanza kuteremsha utumiaji wa ile rasilimali. Ni sawasawa na mlevi, akijigundua analewa sana anaanza kupunguza ulevi; na sisi wizara hii tumeanza kupunguza bajeti. Lakini tutazame Kenya, wenzetu Kenya wanatenga 7% kwa ajili ya makundi maalum. Wametenga shilingi bilioni 38.2 za kikenya ambazo ni sawasawa na shilingi 757,000,000,000 za Tanzania kwa makundi maalum; sisi tunashindwa nini? hizo barabara tunazojenga atakuja kupanda nani? Hivyo vitu tunavyovitengeneza watakuja kutumia akina nani kama huku chini kwenye msingi tunaharibikiwa? Hii ni bajeti ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema labda tuondoe kwamba hawa ni upendeleo labda makundi maalum, tuweke *disadvantaged group*, hata kuwajadili hakuna maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda katika sehemu nyingine, wamachinga. Ni sawasawa, walitengewa shilingi bilioni 22.9

hawakupewa. Wakatengewa shilingi bilioni 18.5 hawakupewa, zikashuka, sasa shilingi bilioni 10.5. maana yake nini, kwamba hii wizara tunahisi tunatumia fedha sivyo kwa hiyo ndiyo tunapunguza. Sasa kama tunapunguza, kwa nini tunawaita hawa makundi maalum? Umaalum wao uko wapi? shilingi 22,000,000,000 hazikutolewa kwa sababu Serikali imesema kwamba hazikuombwa kwa wakati. Sasa, kwa nini tusiwaongeze kwa sababu walikosa huko nyuma? Huko nyuma zimetengwa fedha lakini hawakupewa. Kwa nini hatuwapi hawa wamachinga fedha zao hizi shilingi 22,000,000,000? Mimi hapa naweza nikakamata shilingi kwa sababu nilizisemea hizi fedha lakini Serikali ilidharau haikuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tuna makazi ya wazee, jamani twendeni pale Zanzibar Sebleni tukayatazame. Tunawaweka wazee katika nyumba za wagonjwa wa ukoma. Tumeizunguka hii Tanzania, katika mikoa mingi Kamati imekwenda lakini wazee wanawekwa katika nyumba za ukoma, wakoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeanza kufanya mabadiliko, kwamba tunaanza kujenga nyumba zile kwa ajili ya wazee, lakini tumeshusha bajeti, bajeti ya maendeleo ya wizara hii imetoka shilingi bilioni 30.5 imekwenda kwenye shilingi 20,000,000,000. Tunaenda kufanya nini? kuna vyuo vya maendeleo ya jamii, kuna vyuo vya ustawi wa jamii, watu ambao watatusaidia kupeleka meseji ili haya maovu yote tunayoyasema hapa yakapungua, lakini tumekwenda kukata bajeti kwa bilioni 10. Tunataka nini? Kwamba hii ni *disadvantaged ministry*? Ina maana kwamba tunaongoza tunahisi tunatumia kitu katika kitu ambacho hakina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nasema kitu kimoja. Haya yote wanayoyasema hawa watu yaweze kufanya kazi. Tunaandaa wataalamu huko wa ustawi wa jamii, wa maendeleo ya jamii, kwa nini tusielekeze nguvu zetu huko na tunapunguza nguvu, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mie naunga mkono hoja, kwa sababu leo ni Ijumaa. Shilingi sitaikamata kwa sababu naenda zangu kusali. Kwa hiyo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali King. Nilimtaja Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mheshimiwa Jesca, Mheshimiwa Profesa Ndakidemi ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Niliomba makusudi kuchangia kwenye wizara hii. Hii wizara ni kubwa kwelikweli, unazungumza mendeleo ya jamii ya Watanzania. Maana yake sisi wote humu ndani wizara zote na sekta tunazungumziwa katika wizara hii. Hii wizara haina tofauti na TAMISEMI, tunayemzungumzia hapa ni mtu wa kawaida kabisa, kichochoroni kule kwenye kitongoji. Tunazungumza ustawi wa Taifa hili miaka 100 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii wizara inachukuliwa kwa namna nyepesi nyepesi sana, kama haina uzito. Hata taarifa ambayo imesomwa na Mheshimiwa Waziri hapa, angalia, anakwambia watumishi wa ustawi wa jamii, maafisa upungufu kwa ujumla ni asilimia 94.6, wanakwambia fedha za ndani ambazo wameshatoa za maendeleo za kawaida ni asilimia 16.35, hizo za ndani ni asilimia moja wamepewa. Bajeti imepunguzwa kutoka shilingi 74,000,000,000 hadi shilingi bilioni 67.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kwenye mjadala Waheshimiwa Wabunge hapa kila mmoja anapiga makofi. Kwa hiyo ina maana ukiangalia kwa kweli; Mheshimiwa Rais nampongeza, ameanzisha wizara ambayo alijua ina umuhimu sana; sasa, ni lazima waongezewe fedha ili kazi iweze kufanyika. Leo unamwambia aende kule Ileje, aende Songwe, na aende kule Tarime Shule ya Sekondari Mriba ambayo ndani ya miaka hii watoto wa sekondari 45 wameshapata mimba na wameolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maana yake hiyo ni data za mkoa mmoja umepewa, hivi tufanye *statistics* na tuchukue data nchi nzima,

ni watoto wangapi shule ya msingi na sekondari ambao wamepewa mimba na wengine wameolewa? Sasa hawa Mheshimiwa Waziri anaendaje? Hana magari, hana watumishi. Kwenye vijiji upungufu ni asilimia 100, hata kwenye kata asilimia zaidi ya 90. Kwa hiyo la kwanza, kama ambavyo Mheshimiwa Rais alianzisha hii wizara, ipewe uzito na heshima yake, fedha iongezwe katika wizara hii badala ya kupunguzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mambo ya msingi sana, Mheshimiwa Waziri anafahamu. Katika suala la ukeketaji, Wilaya ya Tarime imo na Mkoa wa Mara umetajwa hapa. Alipokuwa anataja mikoa kwa asilimia alicheka. Mheshimiwa Waziri, tutajie namna ambavyo 2015 mikoa ilikuaje ukeketaji na umepungua kwa kiasi gani kwa sasa hivi. Utaje hapa kwa sababu jambo hili kwa Wilaya ya Tarime, linakuwa *mishandled*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna ukeketaji lakini, wale watu wa Tarime wameingiza kwenye mila na desuri miaka 800 iliyopita. Sasa, ni lazima uende ukae nao, uwape elimu kwenye shule za msingi na sekondari, uwashirikishe viongozi, uwaoneshe madhara hayo na watu wabadilike. Huwezi ukapeleka polisi wakawa *changed*, huwezi kupeleka Jeshi. Kimsingi kule Masanga wanakusanya watoto miezi miwili, wanawarudisha kulekule baada ya miezi miwili, wote wanakeketwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale watoto wawachukue na wawapeleke kwenye vyuo, wawape miundombinu, stadi za Maisha ili wabadilike na hivyo akirudi nyumbani ajitegemee kisha wawahusishe na wenzao ndivyo watakavyokuwa wametusaidia. Lakini mimi Mheshimiwa Mbunge ambaye ni chifu pale, hajawahi kunishirikisha. Mimi ni balozi wake mzuri sana. Kwanza mke wangu mimi msukuma, mimi nimeenda shule, hayo mambo naweza nikakataa mahali popote, tushirikishane mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, suala la ukeketaji, Mheshimiwa Waziri ametunga mpaka kitabu hapa, ameandika kitabu cha ukeketaji hapa kimetolewa Julai, 2022. Sasa muulize, amezungumza

hapa, kwa nini Mheshimiwa Waziri hakutaja suala la ushoga hapa? Kwanini haoneshi mkakati wa Serikali wa kupinga ushoga? Kwa nini hasemi hapa hadharani? Yaani Mheshimiwa Waziri aje hapa asome hotuba yake amalize, anajua watoto wanalawitiwa shuleni, wanajinyea hovyohovyo na kila Mtanzania anajua kuna shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *NGO* ambao wanafadhili watu, hata kama wazungu wamekuja hapa tuwaambie, hatutaki ushoga Watanzania, hatutaki tabia chafu hapa Tanzania. Waelewe, kama ni misaada wanaleta wakome, waache kabisa. Lazima twende katika mila na desturi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Nyerere Burito, alikuwa na wanawake 22, hiyo ni mila ya Wazanaki na Wakurya. Katika wanawake wale mama Mgaya Nyang'ombe, mama yake na Mwalimu Nyerere, alikuwa mke wa tano ndiye aliyemzaa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, amepata heshima ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa hawataki mila zetu, wanapinga ndoa za mitala. Kule kwetu kwa Wakurya ukiwa na wake wengi ni utajiri. Uwe na ardhi, ng'ombe, ndilo jeshi. Halafu wewe unapinga ndoa za mitala, unapinga mila zetu ya Nyumbantobu na Nyumbamboke lakini unataka tusagane, unataka tufanye ushoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko hapa Dkt. Mahisa, yaani Mheshimiwa Waziri hajui kwamba Mwakyembe na mwenzake wametangaza hadharani, wanatuonesha ndoa za wanaume kwa wanaume, wanatuonesha ndoa za wanawake kwa wanawake halafu yeye anakuja hapa, hasemi kama hili ni shida ya Taifa, hasemi kuwa ni changamoto. Leo nimesikiliza *clip* mama analia anasema sipewi ushirikiano, polisi wamemtenga, walimu wamemtenga halafu mwalimu ndiye anayemlawiti mtoto wa mtu. Mama ana mtoto wa kwanza wa kiume, anamtegemea, anauza maandazi anasomesha, mtoto analawitiwa shuleni halafu Mheshimiwa Waziri hawezi kusema. Hapana, hiyo haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesikiliza *clip*, mama analia anasema sipewi ushirikiano, Polisi wamemtenga, walimu wamemtenga, halafu mwalimu ndiye analawiti mtoto wa mtu. Mama ana mtoto wa kwanza wa kiume, anamtegemea, anauza maandazi anasomesha, mtoto analawitiwa shuleni halafu Mheshimiwa Waziri huwezi kusema? Hapana, hiyo haikubaliki. Kama kuna mpango wa kuua watanzania Mheshimiwa Waziri Gwajima jiangalie mama, mtani wangu ujiangalie aki ya Mungu nakuhakikishia kwamba watanzania wamechukia sana ushoga, sisi Wabunge wote hapa. hebu niangalie, Mwenyekiti niangalie, yaani leo *giant* wa Kikulya *chief* niolewe, mimi niolewe? Nifungishwe ndoa na mwanaume mwenzangu? Au na mtoto wangu? Napambana hapa napeleka ugali, namsomesha halafu nikute kuna mwalimu kamlawiti aki ya Mungu ama zake ama zangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri *this is very serious,* amesema Mheshimiwa Nollo hapa Mheshimiwa Ighondo, nataka nikwambie tusichekeane. Kama ni misaada kataeni, kama ni misaada kataeni hii ni vita kama ilivyokuwa vita ya kukomboa bara la Afrika. Hii ni vita ya pili ya ukombozi wa fikra, lazima tusimame na nataka nikwambie, nataka nikwambie Mheshimiwa Mwenyekiti hii ni vita sawa na vita nyingine ni ya Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, Watanzania wanawategemea hii ajenda ilitakiwa iahirishwe tujadili hapa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu waliomba dakika, tulichagua Wizara hizi tuchangie, sasa unapunguza muda ndiyo unasema kwamba labda siyo muhimu, tukae hapa watoto wanasoma wanaolewa wanaume kwa wanaume halafu harusi zipo, kule Dar es Salaam maeneo maeneo yanajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekezo kwa Waheshimiwa Wabunge, tusitaniane katika nchi hii, tumepata fursa, tumepata heshima, tumepata dhamana. Lazima tusimamie kama Mwalimu Nyerere angekubali ushoga leo tungekuwa hapa sisi? Tungeolewa wote? Kama Mzee Karume angekubali ushoga tungekuwepo hapa wote? Wazee wa zamani wanajua mila na desturi, tunataka turudi

kwenye taratibu zetu, turudi kwenye mjadala wa kitaifa tupige vita ushoga na ulawiti. Kama ni mwanaume aoe mwanamke kwa taratibu ya mila zetu. Kama ni mwanamke atafute mwanaume mchumba aolewe, anaekuja hapa Tanzania na fedha zake mkononi msikubali lamba lamba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kataeni ushoga, ahsante…

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mwongozo wa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, ahsante sana.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes, unasemaje?

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Agnes Hokororo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ndiyo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Agnes Hokororo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ndiyo ndiyo unasemaje? Unaomba nini kwanza?

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hee! Mwongozo unaomba huku watu wanaongea bado?

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa ameishamaliza…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa au ulikuwa unataka kumpa taarifa? Basi subiri kwanza tumalizie halafu tutaenda na mwongozo. Wacha tumalizie halafu tutatoa ruhusa ya mwongozo, haya nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Thea Thara, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mheshimiwa Riziki Lulida jiandae. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi niseme tu kwanza nimpongeze sana msemaji aliyemaliza sasa hivi. Hili suala la maadili kumong'onyoka limejipenyeza sana kwenye maeneo hayo anayoyazungumza Mheshimiwa Waitara, ushoga, ulawiti, ubakaji na usagaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku kama alivyosema pia Mheshimiwa Ng'wasi idadi ya hizi kesi unazozisikia kila siku kwenye maredio kuhusu kulawiti, kuhusu kubaka, kuhusu watu kuoana wa jinsia moja. Yanaendelea na kuendelea badala ya kupungua, hii inaonyesha kwamba hata katika adhabu zinazotolewa hizo adhabu bado ni ndogo mno, mimi leo nitakuja tu na mfano lakini kabla sijasahau niseme moja, ukatili kwa watu wenye u-*albino* umeanza upya na hii kwa sababu uchaguzi unakuja, uchaguzi unakuja Geita tayari wamemfuata mtoto *albino*, tayari ukeketaji unaendelea, haya mambo ya uchaguzi ndiyo yanaleta hayo mambo, hiyo natoa taarifa Serikali ilijue hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo naenda kutaja tu mifano ili mpate uchungu wenzangu, muone tunakwenda wapi na taifa hili? Sisi tunawaonea huruma hata nyinyi wanaume, nimefurahi leo wanaume wawili mmeongelea hili suala. Sisi tunasikitika kwa sababu gani? Watoto wa kiume wakiharibiwa hatutakuwa na wanaume wa kuendelea kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Japan wanabembeleza watoto wao wazae, kwa sababu lile taifa limebaki na wazee tu, sisi tuna uwezo wa kuzaa vizuri lakini tunaanza kuwachezea watoto wa kiume ni balaa halafu leo tunasema kuna laana ya mafuriko, sijui udongo unatembea ni laana kwa haya tunayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu nazungumzia mwaka huu tu peke yake, Bunju mtoto wa miaka nane analatiwa, mtoto wa kiume huyo amelawitiwa, mwezi wa tatu mtoto wa miaka sita alilawitiwa na mwalimu, mwezi wa tatu mwaka huu mke anapewa adhabu ya kulawitiwa kila akifanya kosa, yule mwanamke kila akifanya kosa adhabu yake ni kulawitiwa, mwalimu anamlawiti mtoto wa kike halafu anatumia vidole vyake kumchezea mtoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimanjaro mama wa miaka 59 anafanya tendo la ndoa na kijana wa miaka 16 mambo hayo muyaone yanavyoudhi. Mtoto wa kike abakwe na kulawitiwa kwa siku tisini huko Kahama haya nakuja mwezi wa tano mwanafunzi wa *form two* juzi tu amebakwa na mwalimu wake. Naenda Zanzibar *Madrasa* watoto kule wanalawitiwa na wenzetu walifanya vizuri wale walimu wakamwondoa yule mwalimu, maana yake watoto wanaenda *Madrasa* kumbe alikuwa anawalawiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Handeni wanaume wawili wambaka mama pamoja na mabinti zake wawili, binti yake mmoja akiwa mjamzito, yunayaangalia tu. Mtoto wa msanii juzi anabakwa na baba yake mzazi nawapa takwimu ili mpate uchungu wenzangu, tusimame, tukatae haya mambo, tusimame tuone kabisa hayafai. Nakuja lingine ufukweni sasa hivi watoto wanalawitiwa huko ufukweni, mnajidai kuwapeleka watoto sijui wakaogelee, wanalawitiwa kwenye maji mle ndiyo mchezo inayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye hili kundi la watoto walemavu, jamani niwaambieni hawa watoto walemavu ambao hawawezi kwenda popote ndiyo wanakuwa rahisi sana kubakwa na kulawitiwa, nitawaambia kuna mtoto mmoja alikuwa anasoma sekondari pale Jangwani alikuwa anatembea na *wheelchair*, kuna mtu wa maana tu alikuwa anakwenda kumbeba yule mtoto na *wheelchair* anamweka kwenye gari anaenda kumlawiti msichana. Nataka niwaambie kwa bahati mbaya sana akampa na maambukizo ya magonjwa na yule binti alifariki na mimi nilihudhuria huo msiba na aliyemfanyia hivyo ni mtu mwenye akili timamu tena mwenye nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo nataka niwaambie shuleni huko nataka niwaambie kumeharibika, shuleni mchezo wa kulawitiana sijui kusagana ni wa kawaida na mikoa inayoongoza nilishaitaja; Mkoa wa Morogoro na shule zake, Mkoa wa Dar es salaam na shule zake, Dodoma na shule zake. Ndiyo maana tunasema adhabu ya kumfunga mtu miaka 30 unamwacha gerezani bado anapata zile hisia na kule gerezani siyo ajabu atawabaka wale wafungwa wengine, adhabu hiyo imepitwa na wakati leteni Muswada Bungeni hapa, Mheshimiwa Gwajima unajitahidi lakini kwa nini ubebe wewe peke yako? Katiba na Sheria anafanya nini? Waziri wa Mambo ya Ndani yuko wapi? Waziri wa Utumishi uko wapi? Waziri wa TAMISEMI mko wapi? Tunataka mlete sheria hapa, hatutaki hayo mambo ya miaka 30 anaenda kula ugali wa bure kule, waje hapa tuwahasi ili na wao wakae tu. Naomba wanawake wote, wanawake simameni, wanawake simameni tupinge kabisa… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara…

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *toufique*. Mwenyekiti wangu *toufique*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara…

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, simama katika nafasi yako. Wanaume pia, wanaume…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika, unavunja Kanuni unahamasisha watu wasimame. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu nilimtaja, Mheshimiwa Profesa Ndakidemi na Mheshimiwa Riziki Lulida. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi lakini mambo haya yanasikitisha sana. Tungetamani tuone taarifa ya Mheshimiwa Waziri imesheheni uchungu huu ambao Waheshimiwa Wabunge tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Usawa wa Jinsia na ili tupambane jamani na haya mambo ya ulawiti sijui ukatili, lazima tuhakikishe jamii yetu inakwenda kwa usawa. Tunawaangalia watoto wetu wa kike, tunawaangalia wa kiume, tunawaangalia wanaume na tunawaangalia na wanawake. Tukienda kwa pamoja tutaweza kwenda sawa na hatimaye tunaweza tukafika mahali tukapambana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi nasimama hapa ninaomba rasmi kabisa kama tunapitisha hii Bajeti ya Maendeleo ya Jamii, kama leo tutakubali kuipitisha namuomba Waziri atakaposimama atujibu vizuri haya nitakayoyasema, vinginevyo nimuombe Mheshimiwa Rais kwa heshima na tahadhima atupe Wizara nyingine ya jinsia ya kiume kwenye nchi hii ama waongeze wanaume. Kwa sababu nina sababu nne za msingi kabisa kwamba namna tunavyokwenda hakuna usawa katika kuzingatia makundi yaliyopo kwenye nchi yetu. Wanaume wanaachwa, watoto wa kiume wanaachwa na hawa ndiyo wako kwenye sehemu ya *risk*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye vipaumbele vya Wizara. Kipaumbele namba moja na namba mbili Mheshimiwa Waziri anasoma kwenye taarifa yake kuratibu hatua za kukuza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi, wanaume hawamo. Kuratibu utekelezaji wa mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, wanaume hawamo, MTAKUWA hiyo ni 2024 bajeti inayoisha. Vipaumbele vyake vya 2024/2025 hivyo hivyo, katika eneo la kukuza usawa wa kijinsia uwezeshaji wanawake kiuchumi anawatengea bilioni 3.2 wanawake, wanaume hawamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la kiasi cha kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, wanaume hawamo na anawatengea bilioni 3.15. Katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara Fungu Na. 53 pamoja na mambo yote waliyoyatekeleza anasema ni kuratibu utekelezaji wenye ufanisi wa Mashirika yasiyo ya kiserikali na kuratibu utekelezaji wa mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya

wanawake na watoto, wanaume hawamo, vijana wetu hawamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ninaomba leo hapa tupewe Wizara ya Wanaume, hatuwezi kupambana na hivi vitendo kwa kwenda wanawake peke yetu au watoto peke yao bila kuwashirikisha baba zao au bila kuwashirikisha ambao pia huwa wanahusika katika matendo haya kwa namna moja au nyingine na wao ni wahanga kwa namna moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tatu utekelezaji wa mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Anasema kabisa tathimini iliyofanywa Oktoba, 2022 inaonyesha kupungua kwa ukatili wa kimwili kwa wanawake kutoka asilimia 40 mpaka 2015 hadi asilimia 27 mwaka 2022 kwa wanawake. Ukatili wa kingono umepungua kwa wanawake, wanaume hawapo, wanaume hawafanyiwi ukatili nchi hii? Vijana wa kiume hawafanyiwi ukatili nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unataka kuwawezesha wanawake kiuchumi sawa. Unapowaacha wanaume wakiwa masikini, wanaume wataishi vipi? Hawa vijana wetu leo tusipoweka mipango ya kuwawezesha watakapokuwa wanahitaji narudia tena kauli hii. Watakapokuwa wanahitaji leo kuoa, watakapokuwa wanahitaji waoe ili yale matamanio yao ya ngono yaishie kwa wake zao, wataoa kwa kutumia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mila na desturi zetu za kitanzania lazima ukatoe mahari na unaonekana mwanaume lazima utunze familia yako ukishirikiana na mke wako. Leo tumewajengea wanaume kutokuwa na *confidence* na ndiyo maana kundi hili linaondoka linakwenda kwa watoto. Kwa sababu watoto wao wanashindwa kujitetea, hawa wanawake wakubwa wengine wanajitetea, mabinti wengine wanajitetea sasa wanakwenda kwa watoto wanaoshindwa kujitetea. Nataka kuuliza Mheshimiwa Waziri wewe unasema Wizara yako ni ya usawa wa jinsia, inakuwaje mipango yako ina *base* kwa wanawake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakwenda kupitisha, leo tunakwenda kupitisha hapa, lakini kama kweli Bunge hili, Mbunge mmoja amesema labda tukatae lakini kweli kama Bunge hili linakwenda kupitisha bajeti hii. Tunamuomba Mheshimiwa Rais, atupe Wizara nyingine itakayo-*deal* na vijana wetu wa kiume, itakayokuwa na mipango ya kupunguza ukatili kwa wanaume, itakayokuwa na mipanga ya uwezeshaji kiuchumi wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunalalamika hata ndoa watoto leo hata namna ya kuoana sasa hivi ni shida. Mabinti wanalalamika hawaolewi, wanaume watawaoa kwa vipi? *Confidence* ya mwanaume ni fedha na uchumi. Sasa sisi tumeletwa duniani Mungu akaona siyo vyema mwanaume awe peke yake, akatuongeza na sisi wanawake sasa leo tunawatoa wanaume halafu tunataka tubaki peke yetu haiwezekani. Kwenye mpango haiwezekani sisi tunaka mabinti zetu waolewe na wanaume, tukiendelea kuwa-*demoralize* watoto wa kiume na wanaume binti zetu wataoana wenyewe kwa wenyewe, ndiyo zinakuja ndoa za jinsia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ukisimama hapa mimi naomba uniambie kwa nini mipango hii MTAKUWA, mpango wa nini, wa utekelezaji kwa wanawake sasa sijui kwa wanaume inakuaje? Lazima tuangalie huwezi kusema Wizara ya Jinsia, *Government works with paper, Government works with paper* leo utafuata Waziri mwenye nafasi atakwambia mbona kwenye mpango wako, kwenye Hotuba yako haujaweka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mwenzangu wanavyosema kama mnakwenda kuongeza bajeti ya Wizara hii mliyopunguza karudisheni, turudishieni vipengele vya wanaume. Tunataka mpango kazi wa kudhibiti ukatili kwa wanaume na kwa watoto wetu wa kiume, hawa ambao wamepata ushoga sijui wanakwenda kwenye masuala ya shoga tunataka mpango kazi utakaoeleza hawa watoto wanasaidiwaje wasiendelee kujihusisha na masuala ya ushoga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka mpango kazi wa kupunguza umasikini na kwa vijana wetu wa kiume. Huwezi kuwa Waziri mwenye dhamana ya jinsia zote mbili unakuja na mpango wa jinsia moja na haya mambo ya *feminism* ndiyo yanatuletea tabu yatazidisha ushoga, yatazidisha ulawiti, yatazidisha mambo ya jinsia moja. Lazima wote twende sawa, tunataka *confidence* ya watoto wetu wa kiume kiuchumi, anaweza kwenda kutoa posa…

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa…

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaweza kwenda kutoa mahari, anaoa ili tamaa zake za mwili amalize kwa mke wake na siyo kwa watoto wetu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu nimalizie.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla, taarifa yako kwa ufupi. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda kuweka sawa jambo moja maana yake nimeona mchangiaji analirudia kila wakati. Kwamba anaona kama vile wanawake wanapewa *privilege* sana kuliko wanaume na kwamba anahisi ni tatizo la kimuundo hapana. Nilipenda kumpa taarifa kwamba katika mikakati ya kuleta usawa kwenye jamii mara zote

wanaotunga Sera waangali kundi ambalo kwa muda mrefu limekuwa likikandamizwa na mifumo ya kijamii na kiuchumi *systematically*. Kwa hivyo kutoa kipaumbele kwa wanawake, kutoa kipaumbe kwa watoto wa kike ni jambo la msingi kwa sababu mifumo ya kijamii tayari inatoa kipaumbele kwa wanaume.

**MBUNGE FULANI:** Usipokee hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jesca, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa siipokei. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa usiipokee.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa yake. Kwa sababu kama hayo makundi ya kijamii yanaona yanawapaga wanaoshindwa, wanaonekana wanaonewa hivi sasa hivi watoto wetu wa kiume hawaonewi wanavyoingizwa kwenye ushoga? Mmetoa kipaumbele gani? Taarifa yake siipokei na ninashangaa kwa sababu pia inatoka kwa mwanaume sijui kwa nini? Halafu daktari. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema Mheshimiwa Waziri ukiona umesimama hapo tuambie mpango wa wanaume kuwawezesha na kupambana nao. Mimi nimekwenda Iringa ni kweli naomba unipe kamuda nikushuhudie, watoto walibakwa sehemu moja kwenye mtaa wa watoto kumi na saba. Nikaenda kufanya Mkutano na wanawake na wanaume, wanaume wakaniambia kabisa tukienda Dawati la Jinsia sisi wanaume hatusikilizwi tunawekwa tu ndani. Wanaosikilizwa ni wanawake, ndiyo maana sisi tumeamua kuwaacha wanawake wabaki na watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaona shughuli inayotukuta tukitelekezewa, lazima kuwe na *strong voice* kwenye nyumba. Zamani tulikuwa tunaambiwa kabisa wewe mama amekupiga na miko

amekupiga na fimbo na vijinga vya moto baadaye anakwambia subiri baba yako akirudi. Akiingia simba pale lazima ubadilike, tabia unyoke, leo wanawake hatuwezi kuwalea watoto peke yetu, ndiyo maana sasa wanakaa wanakwenda kuwa mashoga wanakuwa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka *strong voice,* tunataka uchumi urudi kwa watoto wa kiume, kwenye familia zetu mabinti zetu wanataka kuolewa, tunataka wanaume wawezeshwe kiuchumi. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga Makofi na Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Ushangiliaji huo Mheshimiwa Dorothy Gwajima unawakalisha watanzania walio wengi naamini hivyo. Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa mchana umeisha tuna tangazo dogo la wageni ambao hawakutambulishwa. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna Chama cha Wanawake Wajane kutoka Dar es Salaam, kuna Baraza la Watoto, kuna CHIUMA, kuna CHIMA sijui imeandikwaje hii tena. Kuna Chama cha Wazee wa Tanzania Wanaume wa Tanzania Baraza la Ushauri la Wazee Tanzania, wote wapo hao? Wadau wa Maendeleo wa Wizara na *NMB, Equity Banks, CRDB Bank Foundation* pamoja na UWT, wote kwa pamoja tunawakaribisha sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa mchana umekwisha lakini tutaendelea na uchangiaji jioni tutaanza na Mheshimiwa Riziki Lulida tutaendelea na Mheshimiwa Kunti Majala na wengine watafuatia. Baada ya kusema hayo nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili. *(Makofi)*

*(Saa 7.01 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu. Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Kunti Majala, ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia wa kwanza jioni hii. Nianze moja kwa moja kwa kumpongeza sana Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima na Naibu wake Mheshimiwa Mwanaidi Khamis, Katibu Mkuu rafiki yangu Seif Shekalaghe na Naibu Katibu Mkuu, Amon Mpanju, kwa kazi nzuri na ngumu wanazofanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kusema kitu kimoja. Nchi yetu ina ulinzi mkubwa sana wa Mungu. Hii inatokana na ukweli kwamba, nchi yetu inaombewa sana na Masheikh, Maaskofu, Mapadre, Manabii na Wachungaji. Kwa hiyo, nchi yetu ina ulinzi mkubwa wa Mungu ndiyo sababu, tunaona mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo machafu yanajitokeza sasa hivi ambayo hata Mungu kwenye Vitabu Vitakatifu aliyakataa, mambo ya Sodoma na Gomora. Mungu alikataa na watu waliofanya huu uchafu na kuwanajisi watoto Mungu aliwapa adhabu na

kuwaangamiza kabisa. Sasa kama Mungu alitoa adhabu kama hiyo na hapa nchini tunaona kuna vitu vya ajabu ajabu vya Sodoma na Gomora vinatendeka kwa watoto wetu, sisi tunakaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kuna kitu hakipo sawa na ninaanza kwa kusema, wanyama kama kuku, bata, ng'ombe mbuzi, hawana akili na hawafanyi huu uchafu. Sasa sisi Mungu ametupatia utashi na akili zetu, mwanaume mzima unakwenda unakuwa shoga, hapana. Mimi kama mzee kuyataja haya mambo ilikuwa ngumu, lakini ni lazima niseme kwamba, haijakaa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipochukua hatua hiki kitu kimeshaanza kusambaa kwa watoto wetu. Wabunge wenzangu, sisi tutakuja kulaumiwa na Mungu kwamba, nyie ndio tuliwapa nguvu ya kutunga Sheria na Sera, kuilinda hii nchi, mlifanya nini kuwalinda watoto na nchi yenu kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tusikubali hii laana kutoka kwa Mungu kwamba, tumehalalisha haya mambo, Serikali ituletee Sheria. Mmeaona kule Uganda ilivyopkuwa, ilienda Sheria pale, hawaangalii sijui ni nani anakupa nini, kuna wanasaiasa wengine wanasapoti haya mambo ambao siyo wa huku ndani. Tusikubali kabisa, Sheria iletwe na Serikali hapa, kama ni kunyonga, watu wanyongwe wanaofanya huu ujinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo labda niende kwenye sehemu ya pili ya mchango wangu, ambapo leo ninapenda sana ujikite kwenye masuala ya wazee. Wazee hapa nchini kwetu ni hazina kubwa sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipofanya Sensa ya 2022 wazee waliongezeka kutoka milioni 2.5 mpaka karibia wazee milioni 5. Idadi ya wazee hapa Tanzania ni kama 8.1% ya *population* yetu yote. Kwa hiyo, naushukuru sana Mkoa wangu wa Kilimanjaro kwa sababu, tunajua kutunza wazee na ndio Mkoa unaoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wazee hapa Tanzania, ukifuatiwa na Mkoa wa Lindi

na Mtwara. Kwa hiyo, naomba tujipongeze tu Wana-Kilimanjaro kwa sababu, tunawatendea wazee haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wetu wana thamani kubwa sana na ni utajiri mkubwa kwenye jamiii yetu. Tukubaliane, ukiona vichwa vile ambavyo vina mvi ni *library* kubwa, ni maktaba kubwa ambazo zimesheheni elimu, busara, uzoefu na uwepo wao hawa watu wa namna hii ni baraka kwa jamii yetu yote. Kwa hiyo, wazee wetu, wanawake na wanaume, ambao wameshazidi miaka 60 tukubaliane kwamba, wametoa mchango mkubwa sana kwenye ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wakati wakiwa na nguvu walikuwa wanalima mazao, wanafuga ng'ombe, wanavua, wanazalisha na wanalisha watu wakati ule. Kwa wale wafugaji na wao walikuwa wanasaidia na wavuvi hivyo hivyo. Wale waliopata bahati ya kuajiriwa, *engineers,* walimu na wote wale walitoa mchango wao. Sasa hivi wameshaishiwa nguvu wapo nyumbani, lakini wameshafanya kazi kubwa sana ikiwa ni pamoja na sisi kuzaliwa. Bila wazee tusingekuwa hapa, walishirikiana na Mungu tukazaliwa sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutokana na mchango mkubwa ambao wameshaufanya, hawa wazee wetu ni baraka kubwa sana kwetu sisi wote. Ni watu ambao tunatakiwa tuwaangalie kwa jicho la pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hawa watu kuwa ni baraka, lakini wana changamoto nyingi sana na kubwa. Chagamoto ya kwanza ni kwamba, wazee ambao hawakuwa kwenye ajira na wameshazeeka na wapo kule vijijini hawana pesa za kujikimu, hata kununua chakula inakuwa ni shida, hiyo ni changamoto ya kwanza. Kwa hiyo, wale ambao hawana *pension* kuna shida pale, hawajikimu sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ni kwamba, Serikali haijafanya haki kwenye Sera ya Wazee. Sera ya Wazee ni ya 2003,

imeshapitwa na wakati. Hakuna sera ambayo ipo ya kusaidia wazee au sheria ya wazee. Bado hatuna Sheria ya Wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya tatu ni ukatili dhidi ya wazee. Katika baadhi ya mikoa bado wanawasumbua na kuwaua bila sababu za msingi. Hiki ni kitu kibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine kubwa kuliko zote ni kwamba, wazee wengi hawajapata zile kadi za kupata huduma ambazo Serikali imeshatoa. Ni kama wazee 500,000 tu kati ya miloni 5 ndio wamepatiwa hizi kadi kwa hiyo, hapa utakuta wazee wanaugua, wanakufa, bila kupata huduma za tiba kwa sababu, hawana kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaushauri kwa Serikali. Ushauri wangu wa kwanza ni, ninaiomba Serikali yetu pendwa iboreshe Sera ya Wazee na itunge Sheria ya Wazee, ili tuweze kuwapatia wazee haki zao kisheria na kisera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee ambao hawana *pension scheme*. Chonde chonde naiomba Serikali, kule Zanzibar wameshabarikiwa, walikuwa wanalipwa shilingi 20,000 kwa mwezi, lakini sasa Rais wa Zanzibar ameongeza shilingi 50,000 na sasa wanapata shilingi 70,000. Ni nini jamani kinatushinda huku Tanzania Bara wazee wetu na wao wapate *pension* kama wenzao wa Zanzibar? Ikibidi basi, hili suala liwe la muungano, ili tuwe tunaamua kitu kimoja. Kwa hiyo, naomba walipwe *pension,* ili waweze kujikimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tatu. Naiomba Serikali yetu, zile kadi isiwe tu ni kwa makundi fulani, hapana, bali ziwe ni kwa wazee wote ambao hawajiwezi, hawana uwezo na ambao hawakuwa kwenye ajira, sisi tulikuwa kwenye ajira, tuna Bima za Afya. Wale wazee na wao wapatiwe bima za kujitibu, ili waweze kwenda hospitali na bima iwapatie dawa zote za magonjwa ya wazee kama kisukari, *pressure* na kupoteza kumbukumbu ziwepo kwenye huo mpango. Kwa kufanya hivyo, tutapata baraka kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, Serikali kwa kushirikiana na Viongozi wa Dini na Wanahabari wawahamasishe watu, ili waache ukatili dhidi ya wazee. Tuache kuuwa wazee, bado tunawahitaji sana, kama nilivyosema, ni watu ambao ni hazina kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tano ni kwa wale wanaokamatwa kwamba, wamedhalilisha wazee, wachukuliwe hatua kali. Tunaona tu mtu amefanya kosa, lakini hakuna kinachofanyika, wachukuliwe hatua kali. Naiomba Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo kwenye yale ameneo ambayo hali ni mbaya tujenge vituo vya kuwatunza hawa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hapa kwenye Ripoti ya Mheshimiwa Waziri ametuambia, Serikali inahudumia wazee 240 na wadau binafsi wanahudumia wazee 268. Naiomba Serikali, hivi vituo 13 havitoshi, twende kwenye kanda zote tuhakikishe tuna vituo vya kusaidia hawa wazee, ili wakiwa na changamoto wapate mtu wa kuwasaidia kwa sababu, na wao walitusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho. Nawaomba Wakuu wa Wilaya na Wkuu wa Mikoa wawe na *forum* na hawa wazee. Kwa mfano, siku ya Wazee Duniani ambayo ni tarehe Moja Mwezi wa Kumi unawaita wazee, unakunywa nao chai, unawapa moyo na wanakupa mawazo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunawapa moyo na watajisikia kwamba, ni sehemu nzuri katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ile kampeni ya mpishe mzee kwanza, ili apate tiba, iendelee. Mmeshafungua madirisha 1,068 yameongezeka, lakini bado tuongeze zaidi, ili wazee wetu waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee ni hazina, ni chemchem ya maisha ya familia na jamii. Kwa ujumla, naomba tuwaangalie na tuwahudumie wazee wetu tukifanya hivyo, tutapata baraka kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umeshawasha pale. Baada ya kusema hayo, nilikuwa na mengi ya kusema, lakini naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Ndakidemi. Nilimtaja Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Kunti Majala na Mheshimiwa Suma Fyandomo ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetujalia sisi wote kupata afya njema na kuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya, kuhangaika kupata fedha angalau ziweze kuisaidia hii nchi, ili iweze kwenda na inaendelea vizuri na tupo katika maeneo salama. Nchi ipo katika ulinzi mzuri, tumuombe Mwenyezi Mungu azidi kumlinda na sisi tuweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri, Mheshimiwa Mama Dorothy Gwajima, Mheshimiwa Mwanaidi, Katibu Mkuu, Ndg. Seif Shekalaghe na Naibu Katibu Mkuu kwa kufanya kazi katika mazingira magumu sana. Wizara hii ilitengewa pesa, lakini mpaka leo tunavyozungumza imepata fedha za nje 1.75% hata 2% hazikufika na fedha za ndani imepata 16.35%. Leo umeona kazi waliyoiona wanawake na hamasa iliyoletwa humu ndani, ina maana wanawake wamepata hisia, mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko mtaani waathirika wakubwa sana katika Wizara hii ni wanawake. Wanawake wanaathirika kwa sababu, wanaona kuwa hali ni mbaya, Mheshimiwa Dorothy Gwajima anatamani aende huku na huku, lakini hana uwezo kutokana na fungu analotengewa ni dogo sana. Naiomba Serikali sikivu, iiangalie Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jumuiya ya Madola, Wizara ambazo zinapewa kipaumbele ni Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na Wizara ya Wanawake, Watoto na Jinsia. Hii Wizara inakwenda katika jamii na huko kwenye jamiii ndiko tunakutana na mmomonyoko mkubwa ambao hata sasa hivi tumeelemewa, hatujui cha kufanya ni kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii naiomba Serikali na Bunge, Kamati ya Bajeti ikakae na Wizara ya Fedha iwatengee kiasi cha fedha ambacho ni halisi. Kiasi ambacho kinatakiwa kitengwe, ili iweze kufanya kazi vizuri na kuyaangalia haya mazingira magumu ambayo tunayo yaweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, ametuletea *NGO's* ndani ya Bunge. Katika kamati yetu tunakwenda na *NGO's*, ili kujua ni nini kinafanywa ndani yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine tutasema hatuna ushaidi na hatutakiwi kuzungumza, lakini uhalisia wa hali iliyoko huko mtaani ni mbaya sana. Mpaka sasa hivi tumezinduka, tunakuja kujua ni nini kinaendelea, asilimia kubwa ya vijana wetu wameshaharibika kabisa. Hakuna ndoa majumbani, ndoa zinavunjika kwa vile vijana wengi wameshaathirika toka wakiwa wadogo mpaka wanaenda vyuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kulawitiwa watoto wadogo huanzia *nursery school,* ambapo watoto wanaingizwa ndani ya mabasi kupelekwa shuleni. Wale wanaofanya kazi ya kuwachukua watoto na wao wanawafanyia vibaya. Katika mabasi yote ya shule awekwe mwanamke au binti yoyote ambaye atakwendanao mpaka shule kwa ajili ya kuwakinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto anasema anataka kwenda *toilet,* anapelekwa na mvulana, kule *toilet* anakwenda kumshughulikia. Shuleni vile vile unakuta watoto wakubwa wanakwenda kuharibu wadogo, ina maana nchi imeingia katika ushetani. Mwenyezi Mungu aliumba binadamu na akaumba majini, ili wamuabudu, sasa

inakuwaje watu badala ya kumuabudu mwenyezi Mungu wanamuabudu shetani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ninayazungumzia ambayo yameathirika zaidi, kwanza ni shule. Shule zetu kuanzia chekechea, *primary,* mpaka vyuo vikuu hali ni mbaya sana. Tuna taarifa kuwa 40% ya watoto wengi waliopata *sponsorship* kutoka kwa baadhi ya taasisi mbalimbali katika vyuo vikuu wameingia katika ushoga ndani ya vyuo. Vile vile, kwa upande wa wasanii, wengi tunawaona kusuka nywele, kuvaa pete, kupaka *lipstick,* tukajua ni usanii, kumbe wengi wamepata mazingira hayo magumu ya kupewa pesa na pia kuhamasika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, Mwenyezi Mungu ambariki sana. Amefanya kazi ya kutangaza uhalisia anaouona huko mtaani. Ilibidi aje hapa apongezwe kwa kazi aliyoifanya kwa dhamira yake katika kuiokoa nchi hii na kuokoa watoto wetu wasiingie katika ushoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa tunaziona, lakini hazina Ushahidi. Taarifa hizi zinasema ni lazima Afrika tu-*depopulate* (wapunguze watu Afrika) na ndio maana tunaona kuna mikakati mikubwa sana ya kuhakikisha Waafrika wanapungua, lakini ni kwa nini wanalazimisha ushoga? Ni kwa vile hawa vijana baada ya muda watakuwa hawana watoto na hawazai, tunakwenda wapi? Hii ni Sodoma *and* Gomora ambayo imeikumba Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni ukiacha Wizara ya Elimu na Taasisi zake huko chini kusimamia hii, tuangalie Jeshi la Polisi. Watu wengi mtoto wake anapobakwa au anapofanyiwa vitendo vya kikatili, wakifika katika *desk,* mtuhumiwa akimpa pesa yule askari aliyekuwa pale, atazungushwa mpaka atakimbia. Anawaambia kakaeni huko mtaani mkamalizane, yaishie mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunamuona yule mama alipomuona mwanaye amelawitiwa na yule mama amekufa. Ina maana alipata uchungu mpaka ameshindwa jinsi ya kujizuia na yeye

amekufa, lakini yule kijana anazurura tu Tanzania nzima. Na yeye akamatwe huko aliko, amemtesa yule mama mpaka amepoteza maisha yake, amemuacha mtoto kuwa yatima, kwa ajili yake, afanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, utanisamehe sana, ni upande wa utalii. Tanzania *is a sovereign state*. Tuna sheria zetu, katiba yetu na kila kitu. Hawa watalii wanapokuja kutoka katika ubalozi huko huko, kama ana shughuli zake za kishoga asituletee Tanzania, tusikubali kwa vile nchi itapata dola, lakini ile dola kwetu itakuwa ni athari kubwa kwa kweli, inasikitisha sana. Tuombe kwa Mwenyezi Mungu katika jumuiya zote za kidini zisimame na hili. Hali ni mbaya sana Tanzania. Kila ukiamka hali ni hiyo, mtoto amefanyiwa hivi, tena wengine watoto wa miaka mitatu wanafanyiwa vitendo vichafu, inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine mimi nasema tena, kwanza maadili yanakuja hata na mavazi *(culture and tradition)*. Unaona vijana wanasuka nywele, kwa nini? Unamuona kijana ametinda nyusi, kwa nini? Kijana anapaka mpaka *lipstick,* unamuuliza kijana wewe kwa nini unapaka *lipstick?* Unataka nini? Kijana anabadilisha mpaka nguo anavaa nguo za kike, nini maana yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasikitisha. Tuwe na sheria ya kuhakikisha kama tunataka kusimamia utamaduni wetu *(culture and tradition),* tuhakikishe haya mambo ya mmomonyoko haya yapotee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawalaumu sana akinamama. Baadhi ya akinamama anamuona kabisa mwanaye yupo katika mazingira ya namna ile anashindwa hata kumkemea. Kama zamani tulikuwa tunaweza, mama, jirani, wawakemee, tukae na tushirikiane kwa pamoja Watanzania na Wabunge wote, tusiamame na hili jambo. Jambo hili ni Janga la Kitaifa ambalo baada ya miaka michache nchi hii tutakuwa hatuna vijana na vizazi. Tutakuwa katika mazingira ambayo hata cha kusimulia hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Afrika ni Bara lenye *population* ndogo sana ukilinganisha na *Europe* na nchi nyingine. Kwa nini wasimame na *depopulation,* kwa ajili ya Afrika? Kwa nini wasianze huko kwao?

Mheshimiwa Mwenyekitiki, wametuletea mazingira haya ya kutaka kupunguza watu katika misingi mingi sana. Tunaona *vaccine*; wanakwenda shuleni wanaambiwa msichana anachomwa sindano shuleni huko lakini tumevumilia, hatukubali, siyo watu wote tunakubali mambo kama haya. Leo mtoto wa darasa la nne unamchoma sindano asizae, halafu itakuwa nini mwisho wake? Atapata *cancer*. *(Makofi)*

Mhesimiwa Mwenyekiti, tunapewa ma-*vaccine* ambayo vilevile hayakufanyiwa kazi; hayana *research* ya kutosha. Matokeo yake tunaona hizi *vaccine* tunazoletewa je, zina uhai kwetu? Sisi Tanzania tunakula vyakula vyenye uhai, tunaletewa vyakula ambavyo vimerutubishwa nje, kwa nini utuletee vitu kama hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biskuti za watoto zinazopelekwa shuleni kama misaada zina madawa humo ndani. *Chocolate* zina madawa humo ndani, tutaishije? Tuangalie watoto wetu, kama zamani tuliweza kula mihogo tukaweza kuishi, kwa nini ulazimishe umpe mtoto biskuti? Kwa nini umpe mtoto *chocolate*? Turudishe utamaduni wetu kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NGO*; mimi ninamshukuru na bahati nzuri ninawapongeza; tulikuwa na Mama Mwantumu Mahiza akazungumzia sana masuala ya *NGOs*. Tuna *NGOs* 10,900 na sasa hivi kutokana na *speed* tunayokwenda nayo ningetamani Kamati nyingine zipewe baadhi ya *NGOs* zikawasikilize. Maana yake Kamati yetu moja haitaweza kuwasikiliza hawa watu na muda tuliokuwa nao ni mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NGOs* nyingi zimejiingiza katika shughuli hizi. Kuna muda walikuwa wanasema tume-*target* mikoa mitano, nikataka kuzungumza wakati wa Bunge lililopita. Mkoa wa Kilimanjaro,

Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Kigoma; Tanga na Pwani yote imeingia katika mazingira haya. Je, kama anaweza kufika kule kwa nini asiripoti kwanza kwa Mkuu wa Mkoa ajue anafanya nini? Bajeti yake iko wapi? Ile bajeti itatusaidia sisi kufanya nao kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo, wanakwenda mpaka Liwale kule chini, sisi wenyewe tumekaa hapa hatujui wanakwenda kufanya nini. Mkuu wa Mkoa hajui wanafanya nini. Ina maana kila *NGO* inayotaka kuingia Tanzania sasa hivi ikaripoti, kama inakwenda Mkoa wa Lindi ikaripoti kwa Mkuu wa Mkoa na awafanyie semina wale watu, wajue anakwenda kufanya nini. siyo unawacha kama nchi isiyokuwa na wenyewe, wanafanya wanachotaka. Sisi ni nchi huru tuna utawala wetu, tuna utaratibu wetu. Waje watuheshimu kama na sisi tunavyokwenda kuwaheshimu kule kwao. Kama kwao wanakubali hivyo vitu, Afrika hatukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi ninajisikia vibaya nimwone mwanangu ni shoga, nitazimia hapo hapo. Kwanza hata sijiwezi mnavyoniona hapa sasa hivi. Ninaomba tusimame tuilete kabisa siku nyingine maana yake hii bajeti umeifanya ya siku moja, mimi kwangu ninaona kama *it is a peanut*. Watu tuna machungu ndani ya roho zetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani hii bajeti ikae siku mbili ili angalau mtupe muda dakika 10 mpaka 15, tuongee tumsaidie Mheshimiwa Rais, peke yake hana nguvu hiyo. Ndiyo maana pakawepo na Mhimili wa Bunge ili kumsaidia Mheshimiwa Rais, kumsaidia Makamu wa Rais, kumsaidia Waziri Mkuu na kumsaidia Naibu Waziri Mkuu ili hili tupambane nalo, tunaliweza. Misaada ya hovyo hovyo Tanzania hatuitaki, tunataka misaada ... *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, ahsante sana ninakushukuru.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na kuhakikisha kuwa tunaomba bajeti hii ikarekebishwe, hii Wizara ipate bajeti yake inayotakiwa. Ninakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninakushukuru Mheshimiwa Riziki Lulida. Nilimtaja Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa Suma Fyandomo, Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Mwita Getere wajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia muda na mimi niweze kutoa mchango wangu. Tunaweza tukawa tunazungumza na Serikali inaweza ikawa haituelewi. Mwaka jana nilichangia hoja hii, watu wakaangua vicheko sana lakini wakati wanajibu tuliambiwa Serikali iko kwenye mchakato kuhusiana na suala zima la ndoa za jinsia moja. Tukaambiwa watu hawa lazima wachukuliwe hatua ili Taifa letu libaki kwenye mikono salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waziri mwenye dhamana anakuja anatoa taarifa yake ya bajeti hapa, ambacho tulikuwa tunakitegemea Wabunge, cha kwanza ni kuambiwa ni wahalifu wangapi wanaojihusisha na suala zima la mapenzi ya jinsia moja ndani ya Taifa letu. Wangetuambia hata kwa idadi kama siyo kuwataja. Tumekaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi, sasa tunakokwenda tunatoka kwenye jinsia moja tunaanza kutengeneza ama kuagiza na Serikali mnaruhusu vinaingia nchini na kodi mnachukua. Leo madukani tuna jinsi za kike na tuna jinsi za kiume. Kunti nikaolewe kwa sababu gani? Si nikanunue pale nifanye maisha mengine yaendelee? Tunazaaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi maadili ya Mtanzania leo yamefikia hapa ndani ya Taifa hili? Serikali ipo. Wafanyabiashara wanaofanya biashara hizi mnawajua, Wizara ya Mambo ya Ndani ipo, Wizara ya Fedha ipo na mnakusanya na ushuru. Mnafanya makusudi haya kwa

ajili ya nani? Wewe umri wako unakwenda, unaisha unazeeka, tunamwachia nani leo Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kama wazazi wetu wasingeamua kutuzaa sisi, leo hili Taifa tungekuwepo humu ndani? Kwa nini sisi leo tunafanya haya, tunayaruhusu haya? Kwa nini tunaruhusu vitu hivi? Leo hata Wabunge humu ndani tukiulizana una watoto wangapi, utasikia wawili, mmoja lakini jiulize wewe mama yako na baba yako, kwenye familia yenu mmezaliwa wangapi? Eti utandawazi, utandawazi unaotokomeza na unaodidimiza Taifa lako, ndiyo huo uzaledo tunaouita? Uzalendo unaokiuka maadili ya nchi hii? Hiki kitu hakiwezekani na hatutakubali. Binafsi yangu mimi sitakubali, asilani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mtoto wa kike na mtoto wa kiume lakini leo maadili tunayowalea watoto wetu, sisi wote humu tulizaliwa, tumelelewa na tulisoma shule za *Saint Kayumba*; ulikuwa ukifanya kosa unaadhibiwa na mzazi yeyote. Leo hakuna mzazi mwingine anayemwadhibu mtoto wa mwenzie, tunafungiana vibwebwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo walimu wetu shuleni wakimchapa mtoto mzazi unaenda na kibwebwe unamwambia huyo mwalimu utanikoma; Serikali mpo, wazazi tupo. Wakati ule mtoto alikuwa mtoto akiwa kwenye kiuno chako, tumboni mwako, akitoka hadharani ni mtoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Leo mtoto ni wa kwako peke yako. Hatuwezi kulea Taifa la namna hiyo hata siku moja. Ni lazima tuamue kuchukua hatua, ni lazima tuamue kusimamia maadili ya Mtanzania ili tuweze kuliacha Taifa letu kwenye mikono salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninatamani kulisemea ni unyanyaswaji wa watoto. Kwenye hili mimi nitaomba wanisaidie, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Maendeleo. Mimi mama ndiyo nimefanya kosa, nimekutwa na hatia nimeenda gerezani kutumikia kifungo. Nimejifungua mtoto wangu mimi anatumikia kifungo kwa kosa gani?

Kwa nini tunafunga watu wawili? Katiba na Sheria mnatwambia nini? Mambo ya Ndani mnasemaje? Wewe unayesimamia hawa watoto mbona uko kimya? Mimi nifanye makosa, mtoto aende akawajibike na yeye anaenda kupata adhabu ambayo haimstahili. Mheshimiwa Waziri tunaomba ukija hapa hebu tuambie, suala la mama mjamzito kakutwa na hatia amejifungua, kwa nini mtoto yule na yeye afungwe wakati yeye hana kosa lolote alilolifanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la ubaguzi kwa watoto wetu wa kiume na amelisema sana Mheshimiwa Jesca. Mimi ninaomba tu nimwambie Mheshimiwa Waziri, hata kwenye mikopo ile ya 10% watu hawa watoto wa kiume bado tumewatenga, utasikia ni wanawake, vijana na watoto. Mtoto wa kike anaingia kundi la vijana anaingia kundi la wanawake lakini huyu mtoto wetu wa kiume je, yeye anaingia kundi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wameendelea kulalamika kulalamika kila siku kwamba sisi mikopo hii haiwezi kutunufaisha kwa sababu sisi hatuko kwenye kundi lolote. Kundi la vijana nimeshatoka, siko kwenye jinsia yoyote. Kwa hiyo, ninaomba pia Mheshimiwa Waziri na wewe ukija hapa mtusaidie pamoja na TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la wazee. Suala la wazee Mheshimiwa Waziri ametuambia na amewazungumzia kwenye kitabu chako cha hotuba, wazee walioko kwenye kambi ama kwenye vituo, wazee walioko mtaani huko nje hujawasemea. Asilimia kubwa ya watu wanaoteseka na wanaishi kwa shida ni wazee walioko kule mitaani lakini mmekuwa mkisema na kuandika kwenye vitabu na kwenye makabrasha kadha wa kadha kwamba mzee huyu apewe kipaumbele. Ikiwa ni hospitalini mzee apishwe, akiwa kwenye taasisi yoyote mzee apishwe, akiwa sijui kwenye nini, hicho kitu huko chini hakifanyiki hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke haya mambo tunayoyafanya leo tukumbuke na sisi ndiko tunakoelekea. Huyu mzee hakuomba kuwa mzee na sisi tunakwenda hukohuko. Vilevile, kuna wazee ambao pia ni watumishi wanapomaliza muda wao, hata zile

kadi tu mnawaambia kadi zao za Bima ya Afya zimeisha hawawezi kutibiwa. Tunachowataka ni nini? Lakini mzee huyo huyo ambaye kuna wazee ambao mmewaweka huko kwenye hizo kambi zenu, mzee huyu mmemchagulia magonjwa ya kutibiwa. Magonjwa mengine mmembagua, akienda mnamwambia aende akatafute fedha aje atibiwe, anazipata wapi na yeye ni mzee? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama hakuwa mtumishi lakini kila mzee nchi hii amelitumikia Taifa lake. Kwa hiyo, Serikali ifike wakati ione muda umefika wa kuweza kuona ni namna gani tunawalinda wazee wetu kwa maana ya kuwahudumia. Kuna ambao wana wazazi lakini lazima tufanye sensa ya wazee. Ni wazee wangapi ambao wana watu wanaoweza kuwahudumia? Ni wazee wangapi ambao hawana watu ambao hawana watu wanaoweza kuwahudumia? Ili angalau waingizwe, kama wenzetu Zanzibar na Mheshimiwa Profesa Ndakidemi amesema, waweze kupata posho ili wazee hawa wanapoondoka hapa duniani wawe wametuachia radhi kuliko wafe wakiwa hawajatuachia radhi. Pia, ndiyo maana hata hizi laana zote ni kwa sababu hiyo, wazee wetu wanasononeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunti Majala. Nilimtaja Mheshimiwa Suma Fyandomo. Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Mwita Getere wajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niwe mchangiaji kwenye Wizara hii. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ambayo inanifanya nitimize majukumu yangu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Gwajima pamoja na Naibu Waziri wake. Wanafanya kazi nzuri, sina mashaka nao kabisa. Nikimpongeza Meheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake ni pamoja na Wizara kwa ujumla, mnafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijamsikia wala nikisoma kwenye kishikwambi changu, akiongelea mambo ya ushoga yanayoendelea kwenye Taifa hili la Tanzania. Ushoga umepamba moto, ushoga wa mwanamke kwa mwanamke, mwanaume kwa mwanaume, eti wanafunga ndoa waweze kuishi pamoja katika Taifa hili la Tanzania. Ninasikitika. Wizara ilipaswa kuliandika hili jambo na kwamba wamefikia wapi kwenye utaratibu huu mambo yanavyoendelea kwenye Taifa hili la Tanzania, kwa maana ya kukemea na kuweka utaratibu wa namna watakavyokuwa wanawachukulia hatua hawa mashoga ambao wanakwenda kuoana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanaume anamtambulisha mwanaume mwenzie kwamba huyu ni mke wangu. Mwanaume ambaye ana ndevu, mwanaume ambaye ana misuli anaitwa mke. Ndani ya Taifa hili la Tanzania hiki kitu hakikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wazima wakifanya hivi, watoto wetu ambao ndiyo wakati wao wa kuoa ama kuolewa, wao wafanye nini? tunawafundisha nini Taifa hili la Tanzania? Haiwezekani kabisa kijana anakuja nyumbani anasema mama ama baba nimepata mchumba, anamleta kijana mwenzie wa kiume, eti na wewe mzazi unakubaliana kwamba ndiyo utaratibu, ndiyo sayansi na teknolojia, hapana. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri kama kwenye hili ulipitiwa kuliandika kwenye hotuba yako, wakati unakuja hapa kuwasilisha tunaomba utuambie umechukua mikakati gani, umepanga mikakati gani na Wizara yako mmeliwekaje suala la ushoga kwenye Taifa hili la Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yako wazi yanaoneka, kwenye mitandao humu yamejaa tele, mahali pengi yanaonekana haya mambo ni kama Wizara mmefumba macho. Ama tunataka tujue kwenye hili jambo la ushoga bila kukemea au kutoa andiko lolote, Mheshimiwa Waziri unataka kutuambia nini? Umelipitisha? Unalikubali? Una mpango gani na hatima yake ni nini? Mwisho wake au hatima ya hili jambo ni nini? Tunahitaji utuambie. Utuletee hapa, kwamba lina faida, hapana. Hata kama umefanya tathmini kwamba

litakuwa na faida kubwa kwa namna unavyoongoza wewe Wizara yako, haitakubalika na haiwezekani kwenye Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wazazi ambao tukisikia haya mambo utumbo unakatakata. Tumbo linauma pale ambapo mama akisikia hivi na baba akisikia hivi haya mambo kwa sababu siyo asili yetu wala siyo utamaduni wetu. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri, hili lichukulie kwa umakini sana na lichukulie kwa uzito sana. Unavyokuja hapa nisikie jambo. Usiposema lolote kuhusu ushoga nitakamata shilingi. Nitakamata shilingi, sitakubaliana na wewe kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mtanzania, ni mzalendo wa Taifa hili la Tanzania. Taifa hili la Tanzania linajengwa na Mtanzania mwenyewe. Haiwezekani kwamba tunyamaze kimya eti tusubiri Taifa lingine ndiyo lije litusemee mambo yanayokwenda ndivyo sivyo kwenye Taifa hili na sisi wazawa wenyewe wenye Taifa letu, tulio na uchungu nalo tumenyamaza kimya, tunaangalia mambo yanakwenda ndivyo sivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili, takwimu za polisi kwa mwaka 2021, kulipelekwa kesi za ubakaji 29,373. Kwa mwaka 2022, walipokea kesi 30,566 sawa na 4.1%. Tathmini hizi kwa mwaka 2023 mpaka sasa, sijajua limeongozeka ongezeko la namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya masuala ya ubakaji, sasa hivi kinachoendelea na kinachoonekana ni kwamba hawa wanaofanya uhalifu, wanaofanya ubakaji na ulawiti wamechukulia kama ni jambo la kawaida kwa sababu ya adhabu ndogo iliyopo. Sheria inatungwa na Wabunge, Wabunge wenyewe ndiyo sisi wenyewe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria ya Adhabu ya yeyote anayebaka ama analawiti, ile miaka 30 ambayo ndiyo iliyokuwa imewekwa, ninaona ni midogo kabisa lakini sioni kama kuna haja ya kuendelea na vifungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri sana na ninaomba tuletewe Muswada hapa Bungeni ili tuweze kujadili upya adhabu itakayotolewa kwa hawa wanaobaka watoto wetu na wanaowalawiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwalimu, walimu kabisa ambao tunawapelekea watoto wetu wawafundishe. Kuna mwalimu wa shule mojawapo, shule ziko nyingi na kwenye simu humu tunazo, kwenye mitandao zipo zimejaa tele ambazo walimu wanawabaka na kuwalawiti watoto. Sijajua inachukuliwa sheria ipi. Mwalimu mmoja alimlawiti mtoto wa darasa la sita alikamatwa akapelekwa polisi kwa vithibitisho kabisa. Amekaa kule polisi kwa siku nne baadaye anatolewa polisi, anarudishwa na anaenda shuleni kuendelea kufundisha. Wale watoto watamwonaje huyo mwalimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mwalimu ana mwalimu mkuu wake wa shule anamruhusu huyo mwalimu aingie darasani kufanya nini? Bado wilaya hiyo ina Afisa Elimu lakini kuna Afisa Elimu wa Mkoa wanasikia hizi taarifa. Wanachukua utaratibu upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana hili jambo la ubakaji, ulawiti, kuwalawiti Watoto, kuwabaka watoto, hawa watoto wa Taifa hili la Tanzania, ninaomba sana Wizara izingatie hili mlete muswada hapa ili tutunge sheria kwa upya hili jambo la kufungwa kwa miaka 30, sijui miaka mingapi wamelizoea tunaomba sana iletwe sheria hapa tuijadili ili tuweze kutoa maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watoto wa kiume, mimi kama mama na mama yoyote hapa ndani hata baba yoyote hapa ndani tunazaa watoto wa kike na wakiume Mwenyezi Mungu anatupatia watoto wa kike na wakiume, kusema kwamba bajeti inapangwa peke yake watoto wa kike peke yake haikubaliki. Watoto wa kike hawa tuliyonao tunao na watoto wa kiume na wenyewe wapangiwe bajeti zao. Ninaomba utege masikio hapa, Naibu Waziri muache Mheshimiwa Waziri asikilize. Mheshimiwa Waziri na Wizara yako ninakuomba sana waangalieni na watoto wa kiume, hao nao ni

watoto wetu ni watoto wa Taifa hili la Tanzania, wanatakiwa na wenyewe wawe na fungu lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, naona umeshawasha *mic*, ahsante sana na Mwenyezi Mungu atubariki na abariki Taifa hili la Tanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Suma Fyandomo, nilimtaja Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Mwita Getere, baadaye Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Jumanne Sagini ujiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara hii nyeti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuona siku ya leo ambayo ni siku yangu mahsusi, siku ya kuzaliwa kwangu kumbukizi, nawashukuru wazazi wangu, nawashukuru familia yangu na nawashukuru Wabunge wenzangu wote kwa salamu zenu lakini nawashukuru wana UWT kwa makundi mbalimbali na wananchi wote ambao wamenitumia salamu za kunipongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapo adhimisha siku yangu ya kuzaliwa ninakumbuka namna gani malezi ya zamani ya wazazi wetu, ambapo wazazi walitulea wakiwa hawana mashaka yoyote, hawana hofu, wametulea kwa amani, kwa upendo tofauti na hali ilivyo sasa. Wazazi wengi sasa hivi tunachangamoto ya presha, mawazo na uhakika wa mtoto usalama wake. Kwa hiyo, ninapochangia leo ninazidi kumuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe Watanzania wanawake kwa wanaume na hasa ndani ya familia zetu, vita hii dhidi ya ukatili wa wanawake, watoto na makundi mbalimbali wakiwemo watu wenye ulemavu, Mwenyezi Mungu utuwezeshe tuishinde vita hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri, nikupongeze Mheshimiwa Waziri Dkt. Gwajima, unapambana mno, umekuwa Waziri

maarufu pia mitandaoni namna unavyopambana pamoja na Naibu wako Mheshimiwa Mwanaidi na Watendaji wote lakini pengine mapambano hayo ndiyo yamewezesha pengine taarifa mbalimbali kusikika za matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Haipiti siku mbili ama siku tatu au hata wiki ujasikia tukio la mtoto kabakwa, mtoto kalawitiwa na visa mbalimbali, mauaji ya wanawake kutokana na matatizo mbalimbali ya kifamilia, siku zote zimekuwa siku za matukio mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama hapa pia hivi karibuni ilitolewa taarifa ya ripoti ya haki ya 2023. Sasa kwa vile Mheshimiwa Waziri hotuba yako ni nzuri ni ndefu lakini haina takwimu ambazo nitazisoma hapa naomba nitumie takwimu hizi hizi ambazo zinaonesha waathirika wa ukiukwaji wa haki za binadamu kwa mwaka 2023, watoto waliyoathiriwa ni asilimia 45, wanawake ni asilimia 30, wanaume asilimia 10, wazee asilimia 12 na watu wenye ulemavu asilimia tatu, haki zilizokiukwa zaidi ni haki ya kuishi na haki ya usawa mbele ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kutokana na ongezeko la matukio, tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi wakati anafungua mkutano mkuu wa uchaguzi wa UWT alituasa wanawake tujitokeze, tushiriki katika vita hii kwa sababu wanaoathirika ni watoto wetu na uchungu wa mwana aujuaye mzazi hasa mwanamke. Kipekee ninaona fahari kutekeleza agizo lile chini ya uongozi wa Mwenyekiti wetu wa UWT, Mama Mary Chatanda na Makamu wake mama Zainab Shomari, tumefanya ziara nchi nzima zaidi ya Mikoa 17 na Kata 854 na moja ya hadidu ya rejea ilikuwa ni kupinga ukatili wa kijinsia wa wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeisemea kwenye mikutano ya hadhara, tumetumia lugha ngumu, tumesema kwa hisia ili mradi watanzania wenzetu katika maeneo mbalimbali hasa wanawake tushuhurike na masuala ya maadili lakini tulinde kizazi chetu hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa mara ya kwanza UWT Taifa imeunda Kamati na wewe ni Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Waziri Dkt. Gwajima ya kupambana na ukatili wa kijinsia, wanawake na watoto na imeanza kazi vizuri pamoja na wajumbe wako wote nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi tumekuja na mpango wa kuanzisha dawati la kusaidia masuala ya kisheria, tunatambua kazi nzuri inayofanywa na Mama Samia *Legal Aids* na Wizara ya Katiba na Sheria na vyombo vyetu lakini tunaona tataizo bado. Nataka niombe mimi kwa tathmini yangu ya haraka haraka ongezeko la matukio haya ni kutokana na kwamba hatuna sheria mahsusi ya kupambana na ukatili wa kijinsia. Kwa hiyo ninawaomba Wabunge wenzangu wanawake tuweke rekodi katika Bunge hili la 12 kama Serikali itachelewa kuleta sheria hiyo, sisi kwa kuwa Kanuni za Bunge zinaruhusu tuje na Sheria ya Kupambana na Ukatili wa Kijinsia, makosa yale yanapoelekezwa kwenye sheria ya kanuni ya adhabu yameelezwa kwa kifupi, haiwezekani hukumu zinavyotolewa miaka 30, kifungo cha maisha lakini matukio yanaendelea kama vile yanapata kasi zaidi, kwa hiyo ninaamini ikija sheria ya kupambana na ukatili wa kijinsia yenyewe mahsusi, makosa haya yatapata fursa ya kuelezwa kwa kina na adhabu yake na hakuna mbadala, adhabu ambayo itakuwa pengine itapunguza matukio haya, ama ni kuhasiwa au kunyongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona nchi nyingine zinatoa hizo adhabu, tumekuwa wenye huruma zaidi wakati kizazi kinaangamia, bajeti inayopitishwa matrilioni ya shilingi hapa, TAMISEMI, Wizara mbalimbali, Uchukuzi, Ujenzi, mabarabra, huduma za jamii yote hayo pamoja na uwekezaji mzuri unaofanyika lakini kama tunacho kizazi legelege, watoto wetu wa kiume wanalawitiwa, watoto wa kike wanabakwa, kizazi chetu hiki hakitatumia fursa ya bajeti kubwa hizi. Kwa hiyo, mimi niombe ukatili wa kijinsia lazima ufike mwisho. Tumefanya mikutano lakini bado hali inaendelea, dawa hapa ni kuhasiwa siyo kwenda kutumia bajeti katika magereza yetu miaka 30, watu wale unawaona wanavyohukumiwa wanatembea wanajiamini

hawana hofu ya Mungu, hawana wasiwasi wala hawajisikii vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niendelee kushukuru Mahakama zetu lakini nawaomba kasi bado. Kipekee nimpongeze Hakimu Mkazi wa Handeni, Mama yangu Veronica yeye huyu nimeona kuna kesi moja aliyoisema Mheshimiwa Dkt. Thea, mama alibakwa na watoto wake wote pamoja wawili, mmoja akiwa na ujauzito wa miezi tisa na mmoja ana miaka 13 walibakwa na watu wawili kwa pamoja lakini ilitokea tarehe 18/03/2024 na hukumu imetoka tarehe 27/04/2024 ni ndani ya mwezi mmoja. Tunaomba Mahakama zetu, Muhimili wa Mahakama pamoja na kazi inayoendelea tunaomba kasi ya usikilizaji wa matukio haya inawezekana ikawa pengine ni fundisho au kupungua kwa matukio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho katika mchango wangu Mheshimiwa Waziri, hii ni Wizara yako ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, umesema vizuri katika aya 130 ukurasa wa 69 na 70, namana ambavyo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa akijitahidi kuwateua wanawake mbalimbali kwenye nafasi mbalimbali walau uwiano unaendelea kusogea, lakini Mheshimiwa Waziri ninaomba, tunao uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uwiano bado upo wa chini sana na Wizara ya Wanawake ndiyo hii, ninakuomba katika mikakati yako mwaka huu ya kazi iwe mojawapo ya ajenda yako kuhamasisha, kutoa mafunzo mbalimbali. Hali yetu kwenye Serkali za Mitaa ni ngumu, kwenye vijiji na vitongoji tupo asilimia mbili tu ya vijiji 12,319 wanawake ni 258 tu na wanaume ni 12,061. Kwenye mitaa kati ya mitaa 4,263 wanawake wenyeviti ni 537, wanaume ni 3,726 asilimia 12 tu. Kwenye vitongoji 64,384 wanawake ni 4,314 asilimia sita saba. Kwa nini nakuomba utilie mkazo, matukio haya yanatokea kwenye vijiji, vitongoji na mitaa, endapo kutakuwa na uwiano kwenye uongozi maana yake sote kwa pamoja tutashiriki hii vita, ukweli ambao utabaki ukweli wanawake ndiyo ambao wana machungu makubwa sana na ndiyo ambao wanaweza kushiriki vizuri katika mkakati huu wa kupambana na ukatili wa kijinsia, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri tupambane ili kusogeza huu usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya naiunga mkono bajeti ya Wizara hii nakuomba Mheshimiwa Waziri tuendelee kukutana *site* kazi bado mbichi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Mgalu. Nilimtaja Mheshimiwa Mwita Getere, Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Jumanne Sagini ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niwashukuru Wizara hii, Waziri wa Wizara, Naibu wake, Katibu Mkuu, Viongozi wote na Watendaji wote wa Wizara hii, kiukweli hii Wizara inachapa kazi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Wizara hii, tatizo kubwa tunaloliona ni bajeti ya hii Wizara, robo tatu ya bajeti hii mnayoiona hapa ni ada za wanafunzi wa vyuo vya ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba wale wote ambao tunaunga mkono hii bajeti iongezeke ili ipate nafasi ya kushughulikia janga, hili suala la ushoga ni janga, ni jambo mtambuka haliwezi kushughulikiwa na Wizara moja. Kwa hiyo, lazima tulifanye kwenye Wizara zote zinazohusika, ni jambo gumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda moja kwa moja, Mheshimiwa Rais ameshasema wazi tu wala siyo kwa uficho ni wazi kabisa amesema haya mambo hayataki na amezungumza wazi kwenye maeneo mbalimbali, ametamka kwa kinywa chake ni sisi Wabunge tuseme tuleteeni hapa sheria ya nini kifanyike kwa hawa watu ambao wanafanya ushoga! Ni sisi tu tuamue kwamba sheria iletwe hapa ambayo itaamua yeyote anayehusika na ushoga itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuja na mambo machache tu, huwa naangalia nashindwa kuelewa hivi maadili ya Tanzania ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yameenda wapi? Tulikuwa tunafanya uchunguzi mdogo tu. Zanzibar kwenye hili suala la ushoga ni zaidi ya asilimia mbili, Tanzania Bara kwenye hili suala la ushoga linaenda mpaka asilimia tano mpaka sita, wanafanyaje Zanzibar, wanapunguza, tunafanyaje sisi bara tunaongezeka. Ni lazima kutafuta

maadili kama ni suala la dini, maana yake imetajwa dini Zanzibar inafanya kazi zaidi kuliko Bara, sasa kama ni suala la dini tuamue shule za msingi za kwetu, kuanzia shule za msingi tuzipelekee basi watu wa maadili, tupeleke dini zianze hapo kama ilivyokuwa zamani, kuna watu wa dini walikuwa wanaenda kwenye maeneo hayo lakini turudishe maadili ya Kitaifa, lazima turudishe maadili ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo unaweza ukaenda Arusha, unasikia watu wapo mitaani zaidi ya 500 eti wanaitwa wadudu, unaenda Mwanza watu zaidi ya mia tano na kitu sijui kuna jina linaitwa pole pole huku halijafika linaitwa nyuki weusi, unaenda Dar es Salaam watu wamejaa karibu 1,000 watoto wa mitaani wanaitwa panyaroad hivi ni nchi gani hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya tuzungumze basi tunazungumzia ushoga je, hawa wanafanya kazi gani?

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa muongeaji kuhusu hawa wadudu anaowazungumzia siyo watu wabaya, siyo wahuni ni kama wana-*entertain* kwenye fani ya muziki. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anajua yeye mimi sijui hilo, ninachojua ni kwamba ukiona watu wanashughulika na uoga, Taifa linawaogopa hao watu maana yake siyo wema! Tumewaona Mkuu wa Mkoa anawaapisha, tuache hayo maneno tu, je *panya-road* wa Dar es Salaam, je wengine waliyopo mitaani, je Mikoa mingine ambayo ina-*entertain* watoto wamejaa mitaani? Watoto wale hawasomi wapo mitaani, wamekuwa wengi

wanaosha magari wengine wanafanya vitu vingine vibaya, unajua wanalala wapi? Tunajua wanakazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kama Taifa tusifanye msako wa kuwajua watoto wote waliyopo mitaani kwenye nchi hii, kwenye Mikoa yote, wanafanya kazi gani? Maadili ya Taifa yameshuka, mbona haya mambo huko nyuma tulikuwa hatusikii hivyo? Kwani wakiwa wanamziki hawaeleweki, hawatambuliki? Wanakuwa tena wa kubembeleza? muziki siyo fani? siyo biashara? Hatuwezi kutetea matatizo ya watu waliopo mitaani, tunataka tujue hawa wanaokaa mitaani wana maadili gani. Kwa hiyo tuleteeni hapa sheria tuiweke wazi kwa watu wanaofanya ushoga tujue kitu gani kinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kamati ya Ustawi imeita *NGOs* zote, tumebakiza sijui tano kati ya mia moja sijui na ngapi, tumeita karibu zote. Mheshimiwa Waziri anakemea, huyu Mheshimiwa Waziri msimuone hivi jamani anahangaika, anakemea wazi wazi, anakuja mule ndani anakemea waziwazi. Mimi kwa kweli mimi kama ni mtu wa kunyonga huyu nitamnyonga wa mwisho, anafanya kazi kweli kweli lakini hali ndiyo hivyo inatakiwa sisi wote Polisi, Wizara zote, Elimu, TAMISEMI zote tushughulikie haya mambo, vinginevyo tutamuhukumu mtu mmoja hapa atafanya kazi gani? Kwa hiyo, maadili ya taifa yameshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wetu walikuwa wanakaa na watoto wao wanaangaika nao, siku hizi kuna tatizo na wanawake nao siku hizi watu wazima nao mna matatizo! Mtoto akitaka kuolewa unamuuliza unaolewa na nani, huyo bodaboda anakusaidia nini, punguzeni na ninyi ukali! mnataka tena watu matajiri ndiyo waoe, mtu anauliza wewe huyu mtoto anakusaidia nini, huyu ana nini? Jamani haya mambo ya kuoana ni hiyari ya watu, mtu anaweza kuwa maskini akatajirika, siku hizi mnawaambia watoto wachague wa kuwaoa.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, punguzeni na ninyi maneno hayo ili nchi iende vizuri.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa. Nampa taarifa muongeaji.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijajua mwezangu anakereketwa na nini sielewi na yeye anatokea Dar es Salaam na anajua kuna matatizo yako nchi nzima. Haya mambo siyo ya kuchekeana, haya mambo Wabunge tusichekeane ni lazima tuamue jambo la kufanya, hatuwezi kuwa na nchi ya mashoga. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na nchi ya mashoga ni lazima tukatae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mwita Waitara.

**TAARIFA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** *Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe Taarifa Mheshimiwa Getere kwamba ukiona unachangia hoja mahsusi ya janga la Taifa la ushoga halafu Mbunge mwanaume anasimama kukupa taarifa mtilie shaka huyo. (Kicheko/Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere naomba uendelee.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huyu atatoa mwongozo baadae. Tunashangaa Mbunge anaetoka Dar es Salaam anatoa taarifa kuhusu mambo ya ushoga.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitokei Dar es Salaam, sitokei Dar es Salaam, nitake radhi sitokei Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita naomba uendelee.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya basi nakuomba radhi basi.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitake radhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita endelea.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nafikiri kwamba kutokana na hali ilivyo na muda unaenda, naomba tuleteeni sheria ambayo itatusaidia kutuondoa kwenye hili janga linaloikumba nchi yetu ambalo halijawahi kuwepo, tunaomba tuleteeni sheria tuitunge hapa Bungeni ituondolee hili janga, hii nchi ni neema, tulipewa nchi hii bila damu, tulipewa nchi hii na Mungu, hatukumwaga damu, leo tunakuja kumwaga damu za mashoga haiwezekani!*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Getere. Nilimtaja Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Wizara kwa kweli wanajitahidi sana kwa ku-*respond* mapema sana. Sisi Wabunge wananchi wana namba zetu, kwa hiyo unakuta linatokea tukio mtaani huko mtu anakutumia meseji anakuletea na Ushahidi, bwana mtoto kafanyiwa ukatili wa kijinsia, mtoto kalawitiwa, mtoto amebakwa lakini unasoma unamtumia Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, unamtumia muda huo huo na anakurudia, hata kama atachukua muda kidogo lakini anakurudia. Waheshimiwa Wabunge najua hilo mnafahamu kwa kweli Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri wake Dkt. Dorothy Gwajima wanapambana na Jeshi lao lile la SMAUJATA wanaitwa wanapambana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke msisitizo kwenye hili kwa sababu jamani jambo la maadili, jambo la kulinda misingi ya maadili kwenye nchi yetu ni jambo kubwa sana, jambo pana ni jambo letu wote, tunachojitahidi kukifanya ni kukusanya nguvu kuwapa wenzetu wa Wizara kwa sababu wao ndiyo wapo mbele kwenye hili gurudumu lakini ni jukumu letu sote kukemea mmomonyoko wa maadili, kueleza na kulinda kwa sababu sisi ni viongozi n ani kielelezo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawapongeza Waheshimiwa viongozi wana-*respond* haraka sana. Ukimtafuta anakurudia, unampa na namba na anapiga simu anakupa mrejesho na ukikutana naye anakwambia Mheshimiwa lile jambo nilishughulikia limefika hapa. Kwa kweli wanapambana sana niwape hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitachangia eneo moja sana. Kuna jambo moja hii Wizara inaitwa Wizara wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Mheshimiwa Waziri ili hawa wanawake waje kuwa wanawake walikuwa wasichana. Mheshimiwa Waziri, ninasema hivyo kwa sababu wasichana wetu *especially* wa vijijini ninakotoka mimi, huko Mungaa, Makiungu, Siuyu na Ikungi huko vijijini kabisa bado hali ya maisha ni duni. Kwa hiyo, kabla hawajafika

*level* yako uje uwachukue wawe wanawake; walikuwa wasichana na walikuwa wasichana wa shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasichana hawa mpaka tunavyozungumza kama nchi tumeshindwa kutatua tatizo la wasichana kukaa shuleni mwezi mzima kuhudhuria masomo kama watoto wengine wa kiume kwa kukosa taulo za kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hili kwa sababu linahusiana na makundi maalum hivyo na mimi ninawa-*term* wasichana wadogo wa shule kama kundi maalum. Hii ni kwa sababu kwa mazingira ya maisha yetu wengi tunavyojifahamu, familia zinashindwa kumudu. Kama mama mwenye familia ananunua kitenge kwa mwaka mara moja, binti yake hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hivi kwa uchungu, kwa sababu huko kwetu kijijini watoto wa kike wanajisitiri kwa magazeti. Naomba hili liwaume sana, kwa sababu hii Wizara bahati nzuri Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri wote wanawake, Mhimili wa pili wa nchi kwenye ukubwa una Kiongozi mwanamke, Mhimili wa kwanza kwa ukubwa kwenye nchi una Kiongozi mwanamke na sisi Waheshimiwa Wabunge wanawake tupo humu ndani. Hivi ni kweli tumeshindwa kutatua tatizo la taulo za kike kwa wanafunzi ambao tunajua idadi yao? Wanafunzi wa kike tunajua idadi yao kuanzia shule za msingi, sekondari za chini na sekondari za juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa kijijini kupata shilingi 2,000 kila mwezi kununua *pad* ni kitu hakiwezekani kwa sababu tunajua maisha wanayoishi, wanagawana kipato kidogo wanachopata. Mheshimiwa Waziri, ninakuomba sana mama yangu, mzigo huu kwenye mabega yako ni mzito na mimi ninajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasoma kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI mwezi Aprili, akaeleza kuhusu swali moja la Mheshimiwa Mbunge alilouliza kuhusu upatikanaji wa taulo za kike na ni kwa sababu zinakwenda TAMISEMI kwenye shule. Akasema Serikali imetenga shilingi bilioni 1.64, ambazo ni fedha za uendeshaji na fedha za halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaambie kitu kimoja. Hizi *pad* zinazoenda kununuliwa kule au hizi taulo za kike wanazotumia wale watoto siyo *reusable* (huo mpango siyo *sustainable*). Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Gwajima, ninakuomba kitu kimoja; kama kila kitu kimetushinda, ninaomba katika uongozi wako utakaokaa hapa hakikisha hili jambo tunalimaliza. Tanzania iwe katika *record,* uki-*google* nchi ambazo zimemaliza tatizo la taulo za kike kwa watoto wa shule, Nchi ya Tanzania iwe inasomeka pale juu. Mpango huu hapa ninakupa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia TAMISEMI, Wizara ambayo ina-*deal* na wanafunzi wanatenga fedha lakini wanaenda kununua zile taulo za kike ambazo mtoto anatumia mara moja anatupa. Kuna taulo za kike ambazo ni *reusable* unaweza kutumia zaidi ya mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano Halmashauri ya Morogoro pale wakati *DC* Msando, yupo pale. Walitumia shilingi milioni 150 kuweka kiwanda kidogo cha kutengeneza *pad* ambazo mtoto wa kike anaweza kutumia akipewa *Form One* ana uwezekano wa kumaliza na *box* lile moja au akaongeza moja mpaka *Form Four*. Hivi kweli kitu kidogo kama hiki tunashindwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wa kike mnalijua hili jambo. Tukienda vijijini huko kwenye majimbo tunabeba ma-*box* matano ya *pad* unaenda kuwapa. Umewasaidia kwa mwezi mmoja; *it doesn't make sense* kwa mtu ambaye ana mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unahitaji fedha ndogo kuweka viwanda. Viwanda tunavyozungumza ni cherehani, ufundi na ujuzi wa kuweza kushona. Hii inakuwa *sustainable* kwa sababu Serikali itaweka miundombinu ya kiwanda kidogo cha ushonaji na Wizara ya Viwanda itatusaidia halafu Serikali inaweza ku-*provide material* kwa ajili ya kutengeneza taulo za kike ambazo zinaweza kutumika tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Wizara ya Elimu kupitia *SEQUIP* na watu wa TAMISEMI wamejenga zile shule ambazo wameweka miundombinu ya maji na miundombinu ya watoto wa kike kujisitiri. Tunaenda vizuri kama nchi. Hebu naomba tafadhali tumalize hili jambo linatutia aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda hapo *MSD* wanaweka *condom* chooni. Hilo la bajeti ya kuweka *condom* kuwapa watu wakafanye starehe wameweza. Mheshimiwa Waziri ninyi mnafahamu kuwa jambo la mtoto wa kike au mwanamke kupata hedhi siyo dharura. Tangu ulimwengu umeumbwa wanawake wanapata hedhi ndiyo maana tunazaliana. Hivi sisi wote humu 393 tumeshindwa kutatua tatizo la watoto kukaa shuleni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma ripoti zifuatazo ndiyo maana ninaongea kwa uchungu sana. Nimesoma ripoti ya *The 2015 Report by World Bank Group; Preparing the Next Generation in Tanzania: Challenges and Opportunities in Education,* nimesoma ripoti ya *UNICEF* ya *Menstrual Health Hygiene and Sanitation among School Girls in Tanzania*, nimesoma Ripoti ya *UNESCO 2021: Sanitary Pad Still Out of Reach for School Girls in Tanzania, The World Bank Report: Keeping Tanzania School Girls in School na* nimesoma pia *Paper* ya *Open University of Tanzania: Institutional Repository* 2019. Bado kuna *dropout* ya watoto ambao kila mwezi kwa miezi 12 anakosa masomo, kwa sababu ya kitu kama hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu mimi nilifikiri kwamba imefika muda sasa viishe tumalizane navyo na mpango ni huo. Kama itafika muda itabidi tu-*discuss* hili, kwa sababu ukiangalia kweli Serikali inapambana wanatenga fedha, lakini nafikiri hawana *sustainable plan.* Kwa sababu hiki ninachokuambia, Serikali inaweza ikaweka miundombinu, halafu vile vikundi vya kina mama zile 4:4:2 za Halmashauri zikatumika ili wale akina mama wawe wanaweza kujinunulia *material* wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaweza kuwa biashara ili iwe *sustainable,* kwa sababu Serikali haiwezi kufanya kila kitu. Inaweza

kuwa mzazi kama ambavyo mtoto ananunua vile vifaa vya mwanzo wakati anaanza *Form One* na kwa sababu madaftari atanunua, sehemu moja wapo ya mahitaji ya msingi ya shule itakuwa ni hicho. Mzazi anaweza, kwa sababu anajua ananunua mara mbili labda kwa miaka minne ni kitu ambacho tunaweza kukifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba mama yangu a-*intervene* hili ili hao wanawake ambao leo ni wasichana tuje kuwapata baadaye waje kuingia Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Ninawaambia hivyo nimesema magazeti, lakini ninyi mnajua jinsi watoto wetu huko wanajisitiri. Wakati mwingine tunaweza kuja kupata matatizo ya uzazi, *PID* na *infection* kwa sababu wanatumia mpaka magome ya miti na kinyesi cha wanyama. Ninyi mnajua mambo ni mengi huko maisha ni magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba mama yangu hili alibebe kama mama, alibebe kama mwanamke na sisi tutamsaidia ikibidi kwa sababu tulishajaribu kuzungumza kipindi fulani kuhusiana na kuondoa kodi. Ni bora tukaifanya hivi ili iwe *sustainable*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaweza kuanza kama *pilot* akachagua Halmashauri kadhaa, kwa sababu pale fedha zipo. Ni vile tu labda ilikuwa hili jambo hawajaliona kama ni la msingi. Wawekewe utaratibu ili afanye baada ya muda tukirudi tutaongea. Mimi ninapenda tukiongea sana ifike hatua tunafanya, ili tukifanya tunarudi tunasema tulifanya mpaka hapa, tumekwama hapa na tunataka twende hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanataka majibu ya shida zao na kwa watoto wa kike ambao wapo shuleni hili ni jambo moja ambalo tunaweza tukalifanyia kazi, tukalifunga na likaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda umebaki kidogo, ninaomba nizungumze jambo moja. Mimi nimekaa magereza wakati fulani. Mheshimiwa Kunti hapa alizungumza kuhusu watoto kufungwa (mzazi wake akifungwa na mtoto anafungwa). Nafikiri alichokuwa ana maanisha, kwa sababu mimi nimekiona kwa macho; kwanza, mtoto

lazima aende na mama yake kwa sababu mama anaweza akaingia magereza akiwa mjamzito kwa hiyo anajifungulia kule. Kwa hiyo nimewaona pia waliojifungulia kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto anabaki kule kwa sababu inabidi mtoto anyonye na sisi wenyewe tunataka watoto wanyonye akili zikae sawa. Changamoto ya magereza kule ni lishe. Mfungwa aliyefungwa anatakiwa ale chakula cha jela au kama ni mahabusu anatakiwa ale chakula cha pale na maisha yetu mnayajua. Hata kama ni mahabusu ambaye anaruhusiwa kuchukua chakula cha nje; je, ni watu wangapi ambao wanaweza ku-*afford* kupelekewa chakula cha nje na ndugu zao? Kwa hiyo, unakuta lishe ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunasema watoto pia wanateseka. Pia mazingira ya kule kama mama analala kwenye kirago na mtoto wake yupo hapa, kwa sababu kule kila mtu cha kwake chake. Kwa hiyo, tuwaombe Wizara waje na mpango kwa sababu unakuta gereza zima kuna watoto wadogo wawili au watatu. Waje na mpango wa kujenga hata *slope* za vyumba viwili kwa ajili ya watoto. Kwanza, *psychologically* huyo mtoto unamharibu, kwa sababu mtoto amezaliwa *day one* mpaka miaka miwili ndio anaondolewa nje ya gereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fikiria miaka yote miwili mtoto anajua mwisho hapa. Anaona mwisho wa ukuta na hapa mwisho wa ukuta akirudi analalia kile kirago na mavumbi. Kiukweli ndiyo maana tunasema ni kama mtoto na yeye amefungwa, kwa sababu anachopitia mama yake na yeye anapitia. Sasa huyu mzazi alikosea lakini si mtoto. Kwa hiyo, tuwaombe sana mama yangu Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, kama ni maendeleo ya jamii basi wewe upo na jamii yako ndogo ya hawa watoto wako kule mama yangu, nenda ukawatembelee uwaone. Ninajua pia utakuwa umeenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kukuta ni mzigo mdogo tu ambao anaweza kuu-*afford* huko na ikamjengea picha nzuri, kwa sababu pia ni mama. Tunatengeneza hawa watoto tunataka wawe

na afya ya akili nzuri. Pia, lishe wanayokula watapata katika mazingira mzuri, kwa sababu anaweza ku-*afford* ni namba ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na kuanza kuchangia kwa kumpogeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi zake nzuri anazozifanya katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Mheshimiwa Rais huyu ni mwanamke wa mfano. Ameona umuhimu wa kuiweka Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kujitegemea wenyewe bila ya kuunganisha na Wizara nyingine. Pia, ninapenda kumpogeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Wizara hii ina malengo mazuri sana kwa wanawake kwa kuwajengea wanawake mazingira ya upatikanaji wa mitaji, kuimarisha uwezo wao kiuchumi, kukuza kipato na kuongeza ajira na kuchochea wanawake kuanzisha miradi katika Sekta Binafsi, kwa mfano uvuvi na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia nzuri na lengo jema kwa wanawake na wananchi, lakini bado wale walengwa hasa waliokusudiwa hawajafikiwa kabisa hasa kule kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara kutoa elimu ya kutosha zaidi na uelewa. Pia, iweke mfumo mzuri zaidi na utaratibu ili mkopo huo uweze kufikia walengwa wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kesi za ubakaji na udhalilishaji. Kumekuwa na matukio ya ubakaji na udhalilishaji kwa watoto na wanawake katika maeneo mengi nchini. Mwenendo wa kesi hizi unachukua muda mrefu katika kutoa hukumu na kupoteza haki, ushahidi na baadaye mtuhumiwa kuachiwa huru jambo ambalo linapelekea hali hii ya ubakaji na udhalilishaji kuendelea siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kwa kesi kama hizi zisichukue muda mrefu kutolewa hukumu angalau mwezi mmoja. Pia, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ishirikiane na Wizara ya Katiba na Sheria kwenye kufanya marekebisho ya sheria kwani kuchelewesha hukumu kwa kesi hizi kunapoteza haki ya walalamikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ongezeko la watoto wa mtaani, maarufu ombaomba. Watoto hawana wazazi, watoto hawana makazi ya kuishi pia hawana chakula, wamekaa kama ndege. Watoto hawa wanaishi kwenye miji mikubwa kwa mfano, Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na hata hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara kupanga mkakati mahususi kwa ajili ya watoto hawa na kuwapelekea katika vituo ambavyo Serikali imeviweka. Serikali itakapofanya hivi itapunguza au kumaliza kabisa wimbi la watoto hawa pamoja na wanawake wenye tabia ya kuzurura ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa kurejesha mikopo ya asilimia 10 ya Halmashauri. Ninaiomba Serikali iweke utaratibu mzuri kusimamia mikopo hii ili iweze kuwafikia walengwa wengi zaidi, kwani zamani walikuwa wanafaidika wachache kutokana na utaratibu mbaya uliokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuipongeza Serikali kwa kuanza kutoa mikopo hii kuanzia mwezi Julai, 2024 kwa kuwa wanawake wataepukana na mikopo ya kausha damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Dkt. Gwajima na Naibu wake Mheshimiwa Mwanaidi kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa kuiomba Serikali iwaongezee bajeti kwa sababu pesa waliyotengewa ni shilingi bilioni 26 na walizopewa ni shilingi bilioni nne tu, hivyo Wizara inakuwa na wakati mgumu wa kuendeleza kazi zake kiufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhalilishaji. Udhalilishaji umekuwa mwingi sana na unaonekana sana kwenye shule na vikundi maalum kama ngoma. Kwa hiyo naiomba Serikali itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wanaothubutu kufanya vitendo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda ni vijana wetu waliopewa fursa ya kazi yao halali ya barabarani lakini hawa ni hatari sana kwa kuendesha kizembe barabarani. Ninaiomba Serikali iwawekee vizuizi vya kupunguza *speed* kwa makusudi katika bodaboda zao ili waweze kuendesha kwa salama na kuepuka ajali barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa jitihada ya kusaidia jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana ukilinganisha na kazi zinazopaswa kufanyika. Pia, angalau basi Wizara ya Fedha ifikirie kuwapa kiasi chote kinachokuwa kimepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, shughuli za Wizara zimejikita katika miji mikubwa tu na siku ya wanawake duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip* subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na Waheshimiwa Mawaziri na *Chief Whip* nilimuona alisimama, tuna tangazo dogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa ajili ya kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema kwamba, yupo nje ya Mkoa wa Dodoma kwa shughuli za kikazi kuanzia tarehe 17 Mei, 2024. Kwa hivyo, wakati hayupo Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, atakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakaporejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninaomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 76, ambayo inatuongoza pia kufuata taratibu tunapokuwa ndani ya Bunge na taratibu zetu ndani ya Bunge pia wakati wa kuchangia ni lazima kupeana heshima na kila Mheshimiwa Mbunge kumstahi Mheshimiwa Mbunge mwenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kanuni ya 71 ambayo inaweka huo utaratibu kifungu (1) ambacho kina kipengele kadha wa kadha mpaka kipengele cha (k). Kipengele kile cha (j) kinatuasa

Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia tusitumie lugha ambazo zinaweza kuudhi na kudhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhuru wa majadiliano ambao pia unaongozwa na Katiba kwa heshima kubwa, ninaheshimu michango ya Waheshimiwa Wabunge wote. Ninaheshimu pia mchango ambao ulitolewa hata leo asubuhi na Mheshimiwa Getere, lakini ninaomba kwa mwongozo huu uone ni namna gani tunaweza kufanya dhidi ya maneno aliyoyatumia Mheshimiwa Waitara katika kusimamia kile ambacho kilikuwa ni uhuru wa mawazo wakati Mheshimiwa Taletale alipotoa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako huo, tuone jambo hili tunaweza kulifanyaje? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kutoa kuhusu huo utaratibu. Ni kweli Mheshimiwa Hamisi Taletale, alimpa Taarifa Mheshimiwa Getere, lakini maneno aliyozungumza mimi, kwa sababu siyo mtu wa mjini sijui alikuwa anazungumzia wadudu ni kitu gani sikumwelewa. Mheshimiwa Waitara, lugha aliyotumia siyo lugha nzuri kwa kuwambia Mheshimiwa Mbunge, mwenzake, kwa sababu maana yake hairidhishi na haifurahishi. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waitara, aifute hiyo kauli.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya Kiti na kwa heshima ya Mwongozo wa Mheshimiwa Waziri *Chief Whip*, ametoa. Ninaomba niondoe maneno yangu yale ambayo nimempa Mheshimiwa Mbunge. Kwa muktadha huo, nimuombe radhi na Mheshimiwa Taletale, naomba apokee radhi yangu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, kwa hiyo maneno yamefutwa. Mheshimiwa Hamisi Taletale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni waungwana. Nimemsamehe *brother* yangu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninawashukuru wote kwa kuwa wastaarabu na kutunza nidhamu ya Bunge. Kwa hiyo, sasa tunaendelea na upande wa Mawaziri.

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Jumanne Sagini; Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, wajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani mchana huu. Kwa kweli nitambue hisia za Waheshimiwa Wabunge, walivyokuwa wanazungumzia masuala ya mmomonyoko wa maadili na baadhi kutoridhishwa na Sheria zilizopo na wengine kuhisi pengine hakuna sheria kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kama sehemu ya mchango wangu. Katika Kikao cha Sita cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, kama utakumbuka Mheshimiwa Spika alitoa Mwongozo na maelekezo kwa Serikali kufanyia kazi kama alivyochangia Mheshimiwa Mbunge Kunti, kwamba, tufanye mapitio ya Sheria zilizopo. Akazitaja Wizara kadhaa ikiwemo Wizara yangu ya Katiba na Sheria, hususani Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Tume yetu ya Kurekebisha Sheria imefanya kazi kama ilivyoagizwa na Kiti chako, ambapo imefanya uchambuzi na kubaini kwamba, zipo Sheria mbalimbali zinazogusa makosa ya maadili ya jamii. Moja, inabainishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambayo inaazisha vyombo vya haki na sheria na kutambua haki mbalimbali ikiwemo za ulinzi, kuishi na kuchukuliwa kutotenda kosa hadi itakapothibitishwa na Mahakama zenye mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni za Adhabu Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania (Sheria ya Kanuni za Adhabu) inatambua makosa na adhabu, inatambua pia umri wa kufanya makosa, inatambua makosa

ya kimaadili yakiwemo; kubaka, kubaka kwa kikundi, kujaribu kubaka, kutorosha mtoto wa kike chini ya miaka 16, udhalilishaji kingono, uwakala wa ukahaba na unajisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ushahidi Sura ya Sita, inasimamia utaratibu wa kupata na kuwasilisha ushahidi Mahakamani. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20, inasimamia taratibu za uchunguzi na uendeshaji wa mashauri ya jinai. Sheria ya Mtoto Sura ya 13, inatoa haki za mtoto ili kuwapa ustawi na wajibu wa wazazi na jamii kuwalinda na kuwatunza. Inaweka pia utaratibu wa kuendesha kesi zinazohusu watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura ya 443 inatambua na kuratibu makosa yanayotendwa kupitia mifumo ya kiteknolojia ikiwemo; kusambaza picha za utupu, ngono, kuhamasisha ngono na kadhalika. Hizo ni sehemu ya Sheria ambazo Tume yetu ya marekebisho ya Sheria imezipitia na kuona zina haramisha baadhi ya makosa ambayo Waheshimwia Wabunge, wameyazungumza kwa uchungu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume yetu imeenda mbele zaidi ikabaini sababu za mmomonyoko huu wa maadili ya jamii. Tumebaini kwamba kuna sababu za kijamii ambazo ni pamoja na mila na desturi, matumizi ya dawa za kulevya, imani za kishirikina, malezi, talaka, kazi za sanaa, vibanda umiza vinavyoonesha picha za ngono, tabia za wazazi, malezi mabaya, ulevi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, zipo sababu za kiuchumi, umasikini uliokithiri, kukosekana kwa ajira kwamba ni baadhi ya sababu za kiuchumi zinazosababisha matendo haya ya mmomonyoko wa maadili. Zipo sababu za kiteknolojia ambayo ni matumizi mabaya ya mitandao, simu janja, runinga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubaini mapungufu haya, Tume imepita maeneo mbalimbali na kubaini kuwepo kwa malalamiko ya wanajamii mbalimbali. Kwa mfano; Timu yetu imepita katika mikoa 18 ambayo ni Dodoma, Singida, Mwanza, Mara, Dar es

Salaam, Katavi, Geita, Shinyanga, Pwani, Tanga, Iringa, Mbeya, Arusha, Manyara, Mtwara, Lindi, Tabora, Ruvuma na Kigoma. Wamewahoji makundi mbalimbali ya watu ambao wote wameeleza kwamba, matendo haya ambao Waheshimiwa Wabunge wengi wamelalamikia kwa kweli yapo na ipo haja ya kufanya marekebisho katika Sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume inaendelea na michakato hiyo na itakapokamilika Tume italeta marekebisho haya kupita taratibu zetu za kawaida ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kujadili na kuona adhabu gani inastahili kwa watu wanaofanya makosa makubwa ya mmomonyoko wa maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wameongea kama vile wanaonesha hisia kwamba hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi ya watu wanaofanya makosa ya mmomonyoko wa maadili. Naomba nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu baadhi ya takwimu za makosa haya na hatua ambazo vyombo vyetu vya uchunguzi, vyombo vya uendeshaji mashtaka pamoja na Mahakama zetu zimechukua hatua dhidi ya wahalifu waliothibitika Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari, 2023 mpaka Mei, 2024 (mwezi huu), jumla ya mashauri 8,346 ya ukatili wa kijinsia yalisikilizwa katika Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi. Kati ya mashauri hayo, mashauri 5,668 yalikwisha. Katika mashauri yaliyokwisha Mahakamani, mashauri 2,420 yalikwisha kwa watuhumiwa kutiwa hatiani na mashauri 1,005 yalikwisha kwa watuhumiwa kuachiwa chini ya Kifungu cha 225(5) kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kuachiliwa kwao ni pamoja na waathirika wengi wa matukio ya ukatili wa kijinsia kuwa wanafamilia. Hivyo, baada ya kutoa taarifa zao polisi wakiwa na jaziba na baada ya hasira kuisha hukaa na kuimaliza kesi hiyo katika ngazi za familia.  Kwa maneno mengine hawatoi ushirikiano

Mahakamani. Sasa kama mtu aliyeathirika hatoi ushirikiano Mahakamani, Mahakama haina cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ni kwamba waathiriwa au wanafamilia hasa wazazi kupokea fidia na kukataa kutoa ushirikiano pindi kesi hizo zinapoanza kusikilizwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalo linarudi kwetu, kwenye jamii zetu, katika maeneo yetu, kwamba tunakopita ipo haja sote kwa pamoja tuzungumze kwa kinywa kipana kama tulivyoongea hapa kwa hisia, kwenye jamii zetu pia tuseme kwa mambo mabaya ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeongea kwa hisia. Kama mzazi mwenyewe inafikia hatua wanashauriana wanakubali kuyamaliza; hilo haliwezi kuwa la Serikali tu ni la jamii nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu waathiriwa wenye umri kati ya miaka 15-17 kutokuwa tayari kutoa ushahidi pindi wanapofika mahakamani au kukataa kabisa kufika mahakamani. Wapo watoto na pengine kwa *influence* ya wanafamilia hawaendi mahakamani. Sasa mahakama itafanyaje kama mtu hajaenda? Wengine wanahama kabisa maeneo ambayo ambayo matukio yametokea wanahamia maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni baadhi ya sababu ambazo zinaweza zikapelekea Waheshimiwa Wabunge kuhisi kwamba hatua hazichukuliwi lakini tumeona ni mwenendo wa kijamii. Mahakama zetu pia zimebaini tatizo kama hili ambapo mtu mwanzoni anakwenda anaongea lakini inafika hatua huko mbele anageuka. Sasa, Mahakama imekuja na mkakati ambao nadhani kama utatekelezwa ipaswavyo utatusaidia sana kuwatia hatiani wote ambao wanathibitika kufanya makosa haya. Baada ya kubaini kwamba watoto, baada ya shauri kuandikishwa kesi inapotajwa, wanaporudi nyumbani wakija sio wale waliokuja na jazba siku ya kwanza wanatoa ushahidi usioweza kumfikisha mtoto mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahakama imekuja na mkakati wa kesi inaposajiliwa, siku ile ile ya kuisajili kesi inasoma maelezo yote ya

walalamikaji, yale maelezo ya awali yanachukuliwa ili huko mbele yasiweze kubadilishwa. Hizi ni juhudi za vyombo vya utoaji wa haki vinavyoonesha kwamba vinakerwa na tabia hii ndiyo maana vinaanza pia sehemu ya mahakama kuchukuwa hatua za kujirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi nishukuru kwa mchango nilioutoa na ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Jumanne Sagini. Nilimtaja Mheshimiwa Festo Dugange, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Hamad Masauni wajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naomba nitumie nafasi hii kuanza kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa aliliona hili jambo la ustawi wa jamii mapema na akaanzisha Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI tunaendelea kushirikiana kwa karibu sana na Wizara hii na inafanya kazi kubwa sana kuhakikisha jamii yetu inakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais TAMISEMI ni Wizara muhimu sana katika kupambana na ukatili wa kijinsia pia katika kupambana na ukatili dhidi ya watoto. Kazi kubwa ambayo Ofisi ya Rais TAMISEMI tumeendelea kuifanya, jambo la kwanza ni kuhakikisha kwamba tunaweka mikakati ya kuzuia, pili tunaweka mikakati ya kupambana na tatu tunaweka mikakati ya kutokomeza ukatili wa wanawake na ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika, nikianza na eneo la watoto wa shule. Sote tunafahamu kwamba watoto wetu wa shule wapo katika maeneo na mazingira hatarishi zaidi mara wanaposafiri kwenda shule, katika mazingira ya shule na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kimefanyika? Moja, Serikali imeendelea kusogeza huduma za miundombinu ya shule karibu na wananchi kwa kujenga shule za madarasa ya awali. Madarasa 418 yamejengwa ili watoto wetu wasitembee umbali mrefu kufuata huduma za elimu ya darasa la awali. Pia tumeendelea kujenga madarasa ya shule za sekondari za kata. Katika kipindi cha miaka hii mitatu zaidi ya shule 460 zimejengwa katika kata ambazo hazikuwa na shule za sekondari. Lengo la shule hizi ni kuhakikisha wanafunzi wetu hawalazimiki kutembea umbali mrefu ambao ni hatarishi na ambao unapelekea kufanyiwa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanya mafunzo ambayo yanatolewa kwa maafisa ustawi wa maendeleo ya jamii, maafisa ustawi wa jamii, waratibu wa elimu wa kata na wakuu wa shule kuhusu jinsi ya kukabiliana na vitendo vya ukatili kupitia miradi mbalimbali ikiwemo *SEQUIP*, Mradi wa *Boost* lakini pia katika eneo la shule salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili Serikali imesisitiza suala la kupambana na *gender-based violence* kwa kuhakikisha waalimu wetu wakuu wa shule, waratibu, matroni na patroni wanapewa uelewa wa mazingira hatarishi, wanapewa mbinu za kupambana na mazingira hayo na pia wanapewa uelewa wa kuwaokoa watoto au watu ambao ni waathirika ili waweze kupata huduma mwafaka kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kujenga madarasa ya wanafunzi wa awali kama nilivyosema, na mpaka sasa madarasa hayo yamekwishakujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa eneo la afya pia tumehakikisha tunawajengea uwezo wataalamu wa afya, kwa sababu tunafahamu waathirika wakifika kwenye vituo vya afya lazima kuwe na ushahidi wa kitaalamu ambao utawawezesha kutoa ushahidi ambao utatumika katika vyombo mbalimbali vya dola lakini pia katika mahakama zetu. Pia tumewapa mafunzo wataalamu wa afya kama

vile madaktari na wauguzi. Tumewezesha upatikanaji wa vifaa vya kupata sampuli ambazo zitawezesha kutambua kwamba watoto au watu wengine ambao wameathirika na ukatili wa kijinsia wanapata haki yao pale wanapofika kwenye vyombo vya dola na vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika eneo hilo, Ofisi ya Rais TAMISEMI na siku tatu zilizopita Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi wa Rais TAMISEMI alitoa maelekezo mahususi kwa wakuu wa mikoa, wilaya, makatibu tawala, wakurugenzi na watendaji wote wa mamlaka ya Serikali za Mitaa kuanzia ngazi vya vijiji, ngazi ya mitaa mpaka ngazi ya Wizara ili kuhakikisha kila mmoja kwa nafasi yake anatekeleza mkakati wa kitaifa wa kupambana na ukatili wa kijinsia; na kuhakikisha katika eneo lake kunakuwa hakuna vitendo vya ukatili katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kutekeleza Mpango Kazi huu wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto awamu ya kwanza *(MTAKUWA one)*. Pia tumeendelea kuhakikisha kuwa tunaunda Kamati maalumu; na zimeshaundwa Kamati maalumu 115 katika mikoa yetu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zinafuatilia kwa karibu viashiria lakini pia zinahakikisha zinakomesha ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine muhimu ambalo Ofisi ya Rais TAMISEMI tumeendelea kulifanyia kazi ni kuhakikisha tunatoa elimu na kuhamasisha jamii. Waheshimiwa Wabunge wamesema vizuri kwamba moja ya changamoto inayoleta ukatili dhidi ya wanawake na watoto na watu wengine kwa ujumla wake ni mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu. Kwa hiyo sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI moja ya eneo ambalo tunalipa mkazo ni kuhakikisha tunatoa elimu kwa ngazi ya jamii, kuanzia vijiji kwenda kwenye mitaa, kata, halmashauri hadi katika mikoa; na kuunda Kamati maalumu mahususi kwa ajili ya kufuatilia na kuchukuwa hatua dhidi ya ukatili wa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa elimu na hamasa ambazo zimesimamiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI ni kufanya midahalo 4,748 katika maeneo mbalimbali kote nchini. Midahalo hiyo ilikuwa mahususi kwa ajili ya kuonesha ukubwa wa tatizo pamoja na kutoa elimu na hamasa kwamba kila mmoja awe mlinzi wa mtoto na kila mmoja awajibike kutoa taarifa katika vyombo vyetu vya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari imeshafanyika mikutano 61,387 ya kujadili masuala mbalimbali ya ukatili dhidi ya wanawake na dhidi ya Watoto. Zoezi hili ni endelevu. Tutahakikisha kwamba tunaendelea kufanya mikutano hiyo, tunawezesha jamii zetu, watendaji na viongozi kutambua ukubwa wa tatizo hili na kuchukuwa hatua ili tuweze kuthibiti changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kuratibu na kuweka mabango ya matangazo ambayo yanaelekeza hali ya ukatili na hatua ambazo zinastahiki kuchukuliwa. Tumeshafanya na kuweka mabango 8,015 katika mamlaka ya serikali za mitaa ili kuhakikisha taarifa, elimu na hamasa vinawafikia wananchi ili kupambana na ajenda hiyo ya ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hamasa tunahitaji kuwa na sheria. Tunazo sheria zetu za kitaifa, lakini pia tumeendelea kuhakikisha kuwa tunawezesha vijiji vyetu, mitaa yetu, kata zetu na halmashauri kutunga sheria ndogo ambazo zitawezesha kupambana dhidi ya ukatili wa wanawake na watoto. Mpaka sasa halmashauri 93 zimeshatunga sheria kwenye eneo la halmashauri na vijiji na mitaa yao. Pia tumeshafikia vijiji 5,156 ambavyo tayari vina sheria ndogo dhidi ya ukatili wa kijinsia na ukatili watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutahakikisha kwenye halmashauri zetu zote 184 na vijiji vyetu na mitaa yetu tunaendelea kuwa na sheria ndogo ambazo zitawezesha halmashauri na mabaraza ya madiwani kuchukuwa hatua kwa haraka na kuwafikisha wahusika kwenye vyombo vya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelekeza halmashauri zetu kuanza kutenga bajeti maalumu kwa ajili ya kutekeleza afua za mapambano dhidi ya ukatili wa wanawake na watoto ili kuwezesha uendeshaji wa afua hizo kuwa rahisi zaidi badala ya kuwa na changamoto za kibajeti ambazo mara nyingine zinapelekea kazi hizo kutokufanyika kwa ufanisi unaotakiwa. Mimi naomba nitumie nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba sisi kama Serikali tunatambua kwa dhati kabisa kuwa changamoto ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni tatizo kubwa katika nchi yetu. Sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI ndiyo ambao tuna watendaji wote kuanzia ngazi ya mitaa, vijiji, kata, halmashauri na mikoa. Tumekubaliana kwa kauli moja na wakuu wa mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI tarehe 15 mwezi huu wakati wa maadhimisho ya siku ya familia alitoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa; na naomba ninukuu; alielekeza kwamba; "Ninawaagiza wakuu wa mikoa kote nchini na wakuu wa wilaya kuweka mikakati madhubuti kwenye maeneo yao ili kuhakikisha ukatili dhidi ya wanawake na watoto inakuwa historia kwenye maeneo yao". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni dhahiri kwamba Serikali imedhamiria na tutahakikisha tunasimamia suala hili na tunatokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na makundi mengine yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nashukuru sana kwa fursa hii na mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Dugange. Nilimtaja Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Eng. Hamad Yusuph Masauni ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi naomba uniruhusu nianze kwa kuunga mkono hoja iliyowekwa mezani. Pamoja na kuunga mkono huko niendelee kumpongeza sana

Waziri na dada yangu Mheshimiwa Mwanaidi Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyotangulia wenzangu kwa kweli naomba nieleze kwa dhati ya moyo wangu juu ya uzuri wa michango iliyotolewa Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla. Waheshimiwa Wabunge wameeleza kwa hisia za ndani sana mgogoro uliopo katika mmomonyoko wa maadili. Waheshimiwa Wabunge wameeleza kwa kutumia mifano mingi. Binafsi niungane na mifano hiyo; lakini pia kuendelea kuwapongeza kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya za kusimamia maadili. Ndani ya michango yao wamezungumza lugha za kulaumu kwa upande mmoja lakini pili wamezungumza lugha za kushauri; na sisi kwa upande wa Serikali nataka niwahikikishie kwamba tutazichukuwa zote na kwenda kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza Waheshimiwa Wabunge katika mjadala kwa eneo kubwa sana wamezungumza; lakini nataka nieleze katika maeneo makubwa mawili ambayo kwa sura ya ndani ni jambo moja. Iko concept kwa lugha ya Kiingereza wanasema *concept* ya ustawi wa jamii lakini pia ipo *concept* ya maendeleo ya jamii. *Concept* mbili hizi ukizisoma kwa pamoja zote zinalenga kusaidia kuiweka jamii na ustawi wa jamii yetu katika maeneo mazuri sana. Kwa mfano kwa upande wa ustawi wa jamii, hili kwa mujibu wa vitabu vilivyoandikwa na wabobezi katika eneo hili; wanasema ustawi wa jamii ni kuwa na jamii inayozingatia haki, usawa na maendeleo kwa makundi yote yaliyo katika mazingira hatarishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wako wamelizungumza sana eneo hili na nisingependa kurudia kwenye kila mmoja aliyesema. Pamoja na hilo limezungumzwa jambo la maendeleo ya jamii ambapo wabobezi katika eneo hili wanasema kwamba maendeleo ya jamii ni kuwawezesha wanajamii na kuunda jumuiya imara zilizounganishwa pamoja. Nataka niombe kwa ruhusa yako dakika moja niwapongeze sana, kwanza Kamati ya Bunge ambapo wana hoja wengine wamezungumza pamoja na mambo

mengine mengi juu ya mapungufu makubwa yaliyopo katika uwepo wa namba ndogo ya maafisa ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niipongeze Kamati kwa sababu imekwenda ndani zaidi na kutuambia nini ambacho wangependa Serikali ifanye. Binafsi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi tumelisikia jambo hilo; na nataka nikuahidi kwamba tunakwenda kulifanyia kazi kama ambavyo umeelezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yeye kwa kipekee kabisa nataka nitambue kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wengi mchango mzuri uliotolewa na dada yangu Mheshimiwa Mwakagenda. Amezungumza vizuri sana, sisi Serikali tumemwelewa na nataka nimwambie kwamba tunakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nataka niweke nukta kwa kulieleza Bunge lako juu ya mambo makubwa ambayo Serikali imefanya ndani ya kipindi cha miaka miwili. Wewe na Bunge lako nataka kuwapa taaarifa kwamba maafisa maendeleo ya jamii zaidi ya 2,140 wameajiriwa. Hili ni kundi la kwanza la watu wale nilioeleza kwamba wanakwenda kusimamia au kuiwezesha jamii iendelee kujiunga na kuwa pamoja kama jumuiya ya pamoja. Katika kueleza jambo hili pia kwa upande wa maafisa wetu wa ustawi wa jamii ambao kilio kikubwa cha Kamati kilijikita hapo; tumeajiri maafisa 403 kwanza katika mwaka uliopita wa fedha (2023/2024) ambao tunakwenda kuumaliza sasa. Pia mwakani baada ya kilio cha Kamati yako Serikali imekwishatoa kibali cha kuajiri maafisa ustawi wa jamii 472 ambao moja ya kazi kubwa ni kwenda kufanya mikakati ya kupambana na hili janga ambalo wengi wanalizungumza; na nikikumbuka mchango mzuri wa Mbunge wa Iringa Mjini ambaye alisema anataka *strong voice*. *Strong voice* inakwenda kupatikana kwa kuwa na watu wanaokwenda kusimamia mustakabali mzima wa maendeleo ya jamii yetu lakini pia Maafisa wanaokwenda kusaidia kusimamia ustawi mzima wa jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nataka nimalize kwa kuendelea kuiomba jamii yetu. Kwamba, malezi ya familia zetu ni jambo la pamoja, sijambo ambalo unaweza kuiachia Serikali peke yake au ukawaachia viongozi wa dini peke yao au ukawaachia watu walio nje kama ambavyo wengine wamezungumza. Naombeni sana wazee wenzangu, mama zangu, wababa wenzangu na wanafamilia wenzangu, tuendelee kusimamia misingi hii ili tuweze kuisaidia jamii yetu na kujenga taifa ambalo litakwenda kuikomboa jamii yetu siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo naomba kuendelea kuunga tena mkono hoja lakini pili kuendelea kuwapongeza tena Waheshimiwa Wabunge. Kwangu mimi ninasema nchi yetu itajengwa kwa sisi sote kuwa pamoja katika kujenga ustawi wa jamii. Nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Naibu Waziri. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis ajiandae.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa wasilisho zuri la bajeti. Pia niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri ambayo ina nia ya kujenga. Wameonesha uchungu waliokuwa nao katika maeneo makubwa mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni eneo la mapambano ya vita dhidi ya ushoga na lingine ni mapambano ya vita dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia na watoto. Nikiri kwamba vita hii ni vita pana sana na kubwa, na mapambano ya vita hii nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwanza nimefarijjika sana kumbe Waheshimiwa Wabunge wanakwenda sambamba na Serikali yao katika mapambano makali dhidi ya vita hii. Kwa hiyo nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inadhihirisha kwamba mihimili yote tukishikamana kwa pamoja, Bunge, Serikali na Mahakama vita hii tutakwenda kushinda. Natambua kwamba vita hii ni kubwa kama nilivyosema na ambao tunapambana nao ni watu ambao wana nguvu kubwa. Ushahidi wa hili nyie wenyewe Waheshimiwa Wabunge mnasikia kwenye vyombo vya habari; unaweza ukasikia kuna nchi fulani kubwa tu kiuchumi, kiongozi wao mkubwa unaambiwa ni shoga. Sasa, katika mazingira kama hayo ni lazima tukiri kuwa tunapambana na watu ambao wana nguvu kubwa na wanaotaka ku-*influence* tamaduni zao katika maeneo mengine, jambo ambalo hatuwezi kulikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupambana na vita hii tunahitaji mbinu. Vita hii inahitaji kupambanwa kisayansi; na mimi niwahakikishie Serikali yenu inapambana na vita hii kisayansi. Mimi leo nataka niwathibitishie kwa kugusa maeneo ambayo yanagusa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niwathibitishie hapa leo, kwa kuzungumzia maeneo ambayo yanagusa Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi. Mimi ninaweza nikagusia maeneo kama manne hivi; eneo la kwanza ambalo nataka nigusie, ni eneo linalohusu Jeshi la Polisi, ni kwa namna gani Jeshi la Polisi linashiriki katika kudhibiti na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria dhidi ya uhalifu huu ambao uhalifu huu ama halifu hizi, zimeidhinishwa kwenye sheria zetu tulizonazo sasa *whether* sheria hizo zinatosha au hazitoshi, huo ni mjadala mwingine. Lakini ukiangalia kwa mujibu wa sheria zilizopo, kubaka, kulawiti, shambulio la aibu, kuzini na maharimu, kumpa mimba mwanafunzi, yamo kwenye sheria ya kanuni ya adhabu Sura 16 ya mwaka 2002 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia makosa dhidi ya maadili, ushoga, iko kwenye sheria ya makosa dhidi ya maadili ya jamii. Kwa hiyo, kimsingi sheria hizi hizi tulizonazo tumeweza kufanya hatua kadhaa, kwa hiyo, nitazungumzia kwenye Jeshi la Polisi kwa mantiki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nitazungumzia jinsi ambavyo idara yetu ya uhamiaji na yenyewe imechukua hatua gani, ikiwemo kama kuna orodha ya watu ambao wameweza kuchukuliwa hatua za kisheria. Ikiwemo kuwaondoa nchini wale ambao wanatuletea habari hizi ambazo hazipo katika misingi ya mila, sheria na tamaduni zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitazungumzia kwenye eneo la Ofisi ya Msajili, kama kuna jumuiya ambazo zenyewe vilevile zinahusika. Kama kuna hatua ambayo Serikali imechukua au haipo. Baadaye nitazungumzia, nadhani maeneo hayo matatu, hilo eneo la Magereza nitaligusia baadaye kwa hiyo hoja ambayo Mheshimiwa Mbunge amezungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye Jeshi la Polisi, naomba nianze haraka haraka kwa kutoa takwimu za Mwaka 2023 kuanzia Januari mpaka Disemba. Kwa sababu 2024 hatujamaliza bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye takwimu inaonyesha kwamba jumla ya makosa yalikuwa ni 8,691. Kati ya makosa hayo, makosa 4,987 ama kesi 4,987 ziko Mahakamani; kesi 1,232 Serikali imeshinda, kesi 773 imeshindwa, kesi 1,041 zimeondolewa na kesi 658 upelelezi bado unaendelea. Nini tafsiri ya takwimu hizi? Tafsiri ya takwimu hizi inaonyesha kwanza idadi ya kesi ambazo zimeondolewa ni nyingi ni 1041, lakini kesi ambazo ziko Mahakamani vilevile ni nyingi, 4,987. Sasa ni dhahiri hapa aidha Mahakama inapata tabu ya kupata ushahidi wa kutosha wa kuzihukumu, lakini kesi zilizoondolewa, zimeondolewa kwa sababu pengine zimekosa ushahidi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwamba lazima tukae tujue kwamba jambo hili siyo la Serikali peke yake. Jamii na wananchi kwa ujumla tuna wajibu wa kushiriki kikamilifu kwenye vita hii, Kama ambavyo Bunge linapambana, kama ambavyo Serikali inapambana na kama ambavyo Mahakama inapambana na jamii ipambane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunachukua jitihada kubwa kupitia dawati la jinsia kutoa elimu kwa jamii ili kuepusha takwimu kama hizi zisijitokeze. Masuala ambayo ameyazungumza vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sheria na Katiba. Kuna changamoto wakati mwingine ya usuluhishi. Unakuta kesi hizi zimefanyika watu wanasuluhishana pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingine ya kuficha aibu, familia wanamalizana hawaendi kutoa ushahidi. Kuna changamoto nyingine watu wanapewa pesa, wanasamehe. Changamoto ziko nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya yote pamoja na mashahidi kutokufika Mahakamani yanachangia takwimu hizi. Nimeona nitoe takwimu hizi ili sisi kama Waheshimiwa Wabunge ambao tunawawakilisha wananchi tutakapotoka kila mmoja kwa nafasi yake, ashirikiane na vyombo vya Serikali kuweza kutoa elimu kwa jamii ili kwa pamoja tuweze kushiriki katika vita hii ya mapambano dhidi ya haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna mambo yamezungumzwa hapa, wako watu ambao wanadhani kwamba kuna changamoto labda za upelelezi kutokufanyika vizuri. Wako watu ambao wanadhani labda kuna changamoto za rushwa na wako watu ambao wamesema kuna changamoto za uzembe katika baadhi ya askari wetu katika kutekeleza majukumu yao, nataka niwahakikishie na juzi mlinisikiliza wakati nawasilisha bajeti, ni jinsi gani Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya katika kufanyia kazi changamoto hizi. Moja katika jambo ambalo tumefanya, yako mambo ambayo tumefanya katika bajeti, nitayakumbusha hapa kwa ufupi, yako mambo ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya hata kabla bajeti hii haijapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya ni kuunda Tume ya Haki Jinai, na katika Tume ya Haki Jinai, katika mambo ambayo yameshaanza kufanyiwa kazi, moja ni marekebisho ya sheria zinazosimamia maadili na nidhamu hususan, Sheria ya Tume ya Utumishi ya Jeshi la Magereza,

Polisi na Uhamiaji, ili kuangalia masuala ya nidhamu ya askari wetu. Jambo la pili ni kutunga kanuni, yote haya yapo katika hatua nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mmezungumza hapa masuala ya kibajeti, jana nilisema, mapinduzi ambayo ameyafanya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika bajeti, hayajawahi kutokea katika historia ya nchi hii. Tulikuta bajeti ya shilingi trilioni 937 kwenda trilioni 1.7 kwa muda wa miaka mitatu hii ni miujiza. Miongoni mwa fedha hii inaelekezwa katika kuimarisha eneo la upelelezi katika Jeshi la Polisi. Ndiyo maana katika hili eneo ambalo lilikuwa lina changamoto, pengine ya uwezo mdogo wa askari wetu kushughulika na masuala ya upelelezi yanayohusu masuala ya ukatili wa kijinsia; tumeweka mkakati mahususi wa kujenga uwezo wa askari wa upelelezi na bajeti kubwa ya kutosha kabisa. Kwa mfano, kwa mwaka uliopita takribani wapelelezi 2,453 wamepata mafunzo mahususi kwa ajili ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, bado tunaendelea kufanya kazi kwa pamoja na vyombo vingine vya kijinai; Ofisi ya *DPP* na zinginezo, kuweza kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa kesi hizi za uzalilishaji na kuwasaidia hao ambao ni wahanga ili upepelezi uweze kwenda kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua nina mambo mengi na muda ni mdogo, nitapunguza. Nizungumzie masuala ya mifumo na TEHAMA. Idara yetu ya Upelelezi ya Jeshi la Polisi inakwenda kuwezeshwa kwenye mifumo ya kisasa ya kurahisisha upelelezi, nilizungumza jana nadhani mlisikia, sina haja ya kulirudia hapa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo ambayo Serikali inafanya katika eneo la Jeshi la Polisi. Yako mengine sasa kama hoja ya adhabu, labda ni ndogo na hoja ya dhamana, ni masuala ya kisheria na Bunge hili ni lenye mamlaka ya kufanya hayo mabadiliko ya sheria lakini kama Serikali tumeyapokea, tunasema hoja za Waheshimiwa Wabunge ni hoja za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba hoja hizo ni hoja za msingi na kuna haja ya kukaa kwa pamoja ili kutafakari kama kuna haja ya kuangalia sheria zetu na *off course* haja ipo kwa jinsi Waheshimiwa Wabunge mlivyozungumza hapa, kwa hiyo, tunapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni eneo la Idara ya Uhamiaji. Nina orodha ya majina hapa ya watu 64 kutoka mataifa mbalimbali, ukitaka nitakupa, ambao tumewatimua nchini na kuwapiga marufuku kuingia hapa. Tuliwagundua kwamba wana *element* hizi na siyo Uhamiaji tu, hata Idara ya Ukimbizi, wako wakimbizi 41, tumewapiga *PI*; ni marufuku kuingia katika nchi hii. Kwa hiyo, kazi hii inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi na jumuiya zinazosajiliwa vilevile kuna ambazo zimefungiwa. Kwa hiyo, kuna hatua ambazo zinachukuliwa kila sehemu katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kupambana na vita hii. Kwa hiyo, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba vita hii ni vita yetu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana na ninawapongeza kwa kuonesha msimamo thabiti wa mapambano ya jambo hili, haya ni mambo ya msingi. Kama Taifa hatuwezi kukubali kuona jamii yetu inaendelea kuharibiwa na vizazi vinaharibiwa, tukafumba macho, hilo haliwezi kukubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yusuph Masauni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ahsante sana kwa mchango wako. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi Ally Hamis na baadaye Mtoa Hoja ajiandae. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuwepo katika Bunge hili ili kuchangia baadhi ya hoja ambazo

zimeelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika hotuba yake iliyosomwa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; kuwa Naibu Waziri na kumsaidia kazi katika majukumu ya kazi katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, sina budi kumshukuru Katibu Mkuu ambaye anaiongoza Wizara hii, Dkt. Seif Shekalaghe pamoja na jopo la wataalam wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, namshukuru tena Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dotto Biteko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wote ambao wanatuongoza katika Bunge hili Tukufu na kuendelea kuhakikisha Bunge linafahamika na wananchi wanaelewa nini kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi wa Jamii kwa kuhakikisha kwamba wanatuongoza vizuri na kutuelekeza yale yote ambayo yanahitajika katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii na ndiyo maana leo tumesimama hapa kuhakikisha tunapitisha bajeti hii kwa ufanisi na kupokea maoni mengi kwa kuwa wananchi wanaielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wangu Dkt. Dorothy Gwajima, hakika yeye ni mama, *field marshal*. Anahangaika kuhakikisha jamii inapata elimu ambayo inahitajika katika maendeleo ya jamii yetu,

Mheshimiwa Rais hajakosea kumchagua Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima na mimi nafuata nyayo zake kuhakikisha nchi yetu hii inatekeleza maadili ya Mtanzania ambayo yanatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naishukuru jumuiya yangu ya UWT, pamoja na Mwenyekiti wake, Makamu na Kamati yenyewe kwa kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kwamba, inaisaidia Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii. Tunawashukuru sana viongozi wetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nisisahau familia yangu na mume wangu kwa kunipa nafasi ya kuhakikisha kwamba yale majukumu ambayo Mheshimiwa Rais amenipa, basi nayafanya kwa wakati. Pia, wanangu Ziana Mohamed Ali pamoja na Ali Mohamed Ali, kwa kunivumilia ili niweze kuendelea na majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, natamka rasmi kwamba naunga mkono hoja hizi kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie hoja hii ya Mheshimiwa Waziri kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge katika maeneo ya malezi, makuzi, maendeleo ya awali ya mtoto, vitendo vya ukatili vya mtandaoni na ukeketaji kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa hoja zao kwa hisia, kuhakikisha kwamba nchi yetu hii wanaitakia amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika hoja za malezi na makuzi. Katika malezi na makuzi kuna haki za Watoto, katika haki na maendeleo ya mtoto Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya mtoto. Kuna Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 na Sheria ya Mtoto namba 21 ya Mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2019. Haki ya mtoto ni pamoja na kuishi, kulindwa dhidi ya vitendo vya ukatili na kuendelezwa katika masuala yanayoenda na umri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa elimu, tuna mabaraza ya watoto katika shule zetu, kuna majukwaa ya watoto katika shule zetu na tuna Mabunge ya watoto katika shule zetu. Haya yote ni kwa sababu ya kumweka mtoto aweze kujiamini, kujielewa na kujikwamua pale anapokutana na changamoto za ukatili. Wizara yetu inaendelea kutoa elimu, kuhakikisha watoto wote wanakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta inaendelea kuboresha mifumo ya sheria ili kuimarisha ulinzi na usalama wa mtoto kwa kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Mtoto Sura 13, Sheria ya Ushahidi Sura 6 na Sheria ya Makosa ya Mtandao Sura 143 kwa lengo la kumlinda mtoto nje na ndani ya mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, sisi hapa ni kama wazazi na mabalozi tuliotumwa na wananchi wetu ili kuja kuziunda sheria hizi na wananchi wetu wawe salama. Tuwe na utamaduni wa kukaa na watoto wetu, najua tuna mambo mengi sana, elimu inatolewa ili ituwezeshe kukua kiuchumi na ninashukuru wanawake wameamka kukua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ili kazi zako ziende na mtoto awe na maendeleo, tuna vituo vyetu vya watoto ambavyo tumeviweka vya kulelea watoto. Tunaomba mama ambaye anajishughulisha na shughuli ili aweze kujiendeleza katika maisha yake kama ana watoto basi awapeleke katika vituo vya watoto ili kuwanusuru na majanga haya ya ukatili ambayo yanawakuta watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, na yeye ni mama, tena Mama wa Taifa. Mheshimiwa Rais ana uchungu sana kila akisikia matatizo haya ya ukatili yanayowapata watoto wetu. Kila anapopanda kwenye majukwaa basi anahimiza maadili ya Mtanzania, mmomonyoko wa maadaili na anahimiza mambo yote ambayo yananusuru watoto wetu ili waondokane nayo na kuwa na watoto walio na tabia njema; kwa sababu sisi sote tumelelewa na

mambo haya yanakuja kutokana na wigo uliopo sasa hivi katika mitandao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitandao imezidi sana na mitandao ndiyo inayosababisha watoto wetu kuharibika. Kwa hiyo, Wizara yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Wizara ya Ulinzi na Wizara ya Katiba na Sheria, tutahakikisha tunaunda sheria ambayo itamzuia mtoto kuwa na mitandao ambayo haifai na hili linawezekana. Tukiamua tunaweza, hakuna lisilowezekana katika Serikali hii na tutalifanya ili kurekebisha zile sheria ambazo zinakandamiza na kufanya mtu kutokupata adhabu stahiki kutokana na mambo ambayo yanafanyika katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nawaomba sana mtuamini kuhakikisha kwamba hili tunalichukulia kwa dhati na kwa makini suala hili la mmomonyoko wa maadili; maana hakuna ambaye halimkeri katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nizungumzie suala la wazee. Katika suala la wazee ambao wapo katika nchi hii ya Tanzania, Wizara yetu inashughulika na kuwahudumia kwa kuzingatia misingi inayotolewa na Serikali. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anajali sana wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila sherehe ambayo inakuwepo Tanzania hii lazima utamuona anatembelea wazee mbalimbali kuwajulia hali kuhakikisha wapo salama. Serikali ina vituo 13 vya kuwalea wazee na wapo wazee 240, Wizara ipo katika hatua ya mwisho ya kurekebisha na kuhakikisha sera ya wazee inafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ambayo tunayajadili katika Sera ya Wazee ni mzee kujiandaa kabla ya kustaafu, huduma ya afya, misaada ya kisaikolojia, mazingira wezeshi na uwezeshaji wa wazee kwenye mabadiliko ya teknolojia. Hadi kufikia Aprili, 2024 wazee 574,321 wamehudumiwa katika Serikali hii na wanapata haki zote zinazostahiki ikiwa ni pamoja na malezi, makuzi, nyumba, malazi

pamoja na chakula. Fedha hizi zote anazitoa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha wazee wa Tanzania wanakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imekabidhiwa jukumu la kuwashughulikia wazee hawa. Tutaendelea kujitahidi kuhakikisha wazee wetu wapo salama kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ambayo wazee wetu ndiyo wanaitegemea sana kuhakikisha kwamba, wanapata afya bora inayowasaidia kuishi katika umri wao ya uzeeni, maana mtu ukistaafu sanasana unafikiria maradhi huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulipo kila mtu ni mzee mtarajiwa. Tutahakikisha tunaifanyia kazi Sera hii ya Wazee, ili iishe haraka, iletwe hapa Bungeni na kupitishwa, ili wazee wetu watarajiwa waweze kufaidika na wazee waliopo waweze kupata matunda ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais ambaye ni makini, Rais mzalendo, Rais mwenye huruma na imani. Mambo yote yeye anayajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kila akisikia changamoto za wananchi au za mtu yoyote katika Tanzania hii, anatoa kipaumbele kuhakikisha zinatatuka kwa haraka sana. Tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa juhudi anazochukua na sisi tupo nyuma yake, kama wasaidizi wake kuhakikisha kwamba, tunaendanae sambamba, ili kazi zote zinaenda kama zilivopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya *GO* ambayo Waheshimiwa Wabunge hapa mmeyaeleza sana. Wizara inaratibu uendeshaji wa bodi inayosimamia mashirika yasiyo ya Kiserikali. Sura ya 56 hufanya vikao kila robo ya mwaka na taarifa hizo zinakuwa zinaletwa kuhakikisha kwamba, masuala yote ya *NGO* yanafanyiwa kazi na kufuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imeandaa mfumo. Mfumo huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa Mkutano wa Majukwaa yasiyo ya Kiserikali uliofanyika Jijini Dodoma, tarehe 05 Octoba, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya mashirika 10,538 yasiyo ya Kiserikali yametambuliwa kwenye ramani na tayari yamewekewa taarifa kwa kuzingatia ngazi za kata 9,818 na wageni 156 wenye manufaa mengine kwa kuchangia katika pato la Taifa katika kodi na michango mbalimbali. Mashirika haya ya Serikali sasa hivi tunayafanyia kazi kwa umakini mkubwa sana. Hapo mwanzo tulijua kwamba, Mashirika ya Serikali yanachangia kufanya vitendo hivi vya ukatili na ulawiti kwa watoto wetu, lakini baada ya kujua hayo tukayafuta yote na tukaanza kuyasajili upya na ripoti zake kila baada ya robo mwaka tunazipata. Sasa hivi mashirika yaliyopo yapo safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Mheshimiwa Mbunge au mtu yoyote ambaye anaona kuna shirika linaenda kinyume na Serikali basi atuletee taarifa tutahakikisha tunalifunga na kulichukulia hatua za Kisheria, ili kuondokana na kadhia ile. Kwa sababu, nchi yetu ya Tanzania tunahitaji watu ambao ni wema kwa watoto wetu ambao ni viongozi wa kesho, maana bila watoto hawa baadaye kutakuwa hakuna viongozi wa kesho. Kwa hivyo, sisi ndiyo wasajili wa mashirika ya Serikali, tuko makini na mashirika haya kuhakikisha hakuna hata moja ambalo linahujumu watoto wetu na kutenda vitendo ambavyo havitakiwi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya watumishi. Ni kweli, Wizara yetu ina tatizo la upungufu wa watumishi, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ameeleza hapa. Baada ya kulalamika sana Mheshimiwa Rais, kama nilivyosema ni mtu msikivu na makini, ameliona hili akatoa taarifa katika Wizara inayoajiri wafanyakazi. Mwaka huu wa 2022/2023 tumeajiri maafisa 350 na wapo tayari wanafanya kazi, tumewapeleka sehemu zote ambazo zinahitajika. Najua bado ni kidogo, lakini vilevile

tuna maafisa wa maendeleo ya jamii ambao hawa ndiyo wanaotoa elimu katika sehemu zote kuanzia Kata hadi Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa usikivu na upendo wake ameagiza kwamba, tupewe nafasi 666 za maafisa maendeleo ya jamii katika Mwaka 2023/2024. Vilevile aliona atazame mbele zaidi katika kutenga bajeti yake ya fedha ya Mwaka 2024/2025 tumetengewa nafasi 945 kuhakikisha maafisa hawa wanatosheleza nchi nzima, ili kufanya kazi na kutoa elimu kwa wananchi, ili wananchi wetu wawe salama na wapate elimu ambayo inastahili katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile maafisa hawa tunapendelea kuwapeleka kule vijijini, chini, ambako taarifa zinachelewa kufika. Maafisa hawa watasaidia kutoa elimu, ili na wao wafaidike na yale mazao au mafao ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anataka kuhakikisha wananchi wake wote wanapata uelewa na wanafaidika na Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Awamu ya Sita, ambayo inaongozwa na Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna Maafisa Ustawi wa Jamii. Mwaka 2023/2024 tumetengewa nafasi 403, kwa ajili ya maafisa hawa na Mwaka 2024/2025 tunatarajia kutengewa nafasi 472 kwa maafisa hawa wa maendeleo ya jamii kuhakikisha kwamba, kazi hizi zinafanyika kwa ustadi. Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa msikivu kuhakikisha kwamba, anawasikiliza wananchi ni nini wanataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum tunaendelea kusikiliza maoni ya wananchi kuhakikisha kwamba, nchi yetu inakuwa salama na yenye amani. Kila akisikia, Mheshimiwa Rais, nchi yetu ipo katika hali ya usalama na amani basi na yeye anakuwa na amani, lakini kila akisikia changamoto za wananchi anakuwa hana amani, kutwa anakuwa anashughulika na Mawaziri wanaohusika kuhakikisha vitendo ambavyo haviitajiki vinaondoka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia michango hii kwa hamasa. Inaonekana kwamba, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum sasa inafanya kazi na ndiyo maana mmepaza sauti kuhakikisha kazi ile inaifikia jamii. Sisi tumepata hamasa ya kufanya kazi kwa nguvu zaidi kwa kuwa, mmetuelewa na mmetufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kushikamana na ninyi Waheshimiwa Wabunge maana ndiyo wasaidizi wetu. Mnapoona vitendo vyovyote vya ukatili katika mitaa au katika vijiji tuleteeni ripoti kuhakikisha tunaungana pamoja, ili kadhia hii iishe kabisa. Hatutakubali kumuona mtoto wa mtu yeyote anaharibika kwa sababu ya kuoneana muhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuondoe muhali, tutashinda. Serikali hii haina muhali, kila mtu anahitaji kufanyiwa kazi zake na kila mtu anastahili kuwa na haki. Tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufanikisha yale malengo yote ambayo anayahitaji katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndiyo Waheshimiwa Wabunge tulioletwa hapa, ndiyo tuliotunga Sheria. Tuleteeni maoni yenu tutunge Sheria, tulete Miswada hapa ipitishwe, ili kuhakikisha watu wote wanaondoka kabisa katika nchi hii. Waheshimiwa Wabunge nawapongeza sana, sisi kila mkituletea changamoto, basi ndiyo tunakuwa tuna ari ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiposikia changamoto zenu tunaona mambo yenu yapo sawa. Kwa hivyo, tunahitaji haya mambo, hii ndiyo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara ya malezi, Wizara ya kuondoa uovu wote katika nchi yetu hii ya Tanzania. Kwa hivyo, naungana na ninyi, nawashukuru sana, milango yetu iko wazi katika kuhakikisha tunaijenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyingine kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kiti chako, ili tuweze kuidumisha na kuiimarisha nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, kwa kutupa moyo na mwenyewe kujipa moyo, tunakushukuru sana. Kabla sijamuita mtoa hoja, naomba niwatangaze wageni ambao wapo jioni hii.

Wapo wageni ambao wamekuja kutembea katika Bunge letu, kwa ajili ya mafunzo:-

Tuna wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. karibuni sana wanafunzi kutoka *UDOM*. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Hawa ni Mwenyekiti na Katibu wa Chama cha Wajane Tanzania.

Pia, tuna Mwenyekiti na Katibu *Kafika House Tanzania***.** Haya karibuni sana.

Vilevile yupo Mwenyekiti na Katibu wa Sauti ya Watoto Tanzania (SAWATA). Karibuni sana Waheshimiwa wageni wetu.

Sasa namuita mtoa hoja wetu, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ili aweze kuhitimisha hoja yake.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami namshukuru Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunipa fursa hii

kusimama mahala hapa, mbele ya Bunge lako Tukufu, kuweza kuhitimisha hoja ambayo nimeitoa leo asubuhi. Pili, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara nyingine tena kwa kuendelea kuniamini niiongoze Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru kwa sababu, agenda hizi ambazo leo tunazijadili hapa yeye ndiye Jemedari ambaye aliona mbali, akaona na iwe hii Wizara. Wizara hii imebeba hatima ya Watanzania, Wizara hii itengwe kutoka kwenye idara ya pamoja na afya, ili iweze kufanya mambo haya ambayo awali yalikuwa hayazungumzwi kwa kina na mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zimuendee yeye aliyeianzisha hii kazi. Naomba nitoe shukrani kwa wasaidizi wangu katika Wizara hii ninayoiongoza, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Seif Shekalaghe pamoja na msaidizi wake, Wakili Amoni Mpanju. Katika yote natoa shukrani kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, Mbunge, ambaye ametoka kutoa mchango wake hivi sasa kwa msaada mkubwa anaonipa katika kuiongoza Wizara hii, siyo rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge Mwanaidi Ali Khamis hakika watu wa jimbo lako wamepata chombo cha uhakika. Mungu akujalie uendeleze kazi hii ya utumishi wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani nyingi kwa Kamati yangu ya Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge, pamoja na Makamu wake Mheshimiwa Lulida, kwa uongozi mzuri uliofanya tuweze kufanya haya tuliyoyatekeleza na kuyawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani nyingine ziende kwako kwa kuongoza mjadala huu siku ya leo, hakika mjadala huu umekuwa na tija, umetubariki sana. Sisi tumefurahi sana kuleta hotuba hii ambayo Waheshimiwa Wabunge wameisoma, wameichambua, wameitathmini, wameitolea maoni na mapendekezo. Kwetu sisi ni

faraja kubwa, kupika chakula ukakipeleka mbele watu wakaja wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi ni faraja kubwa kuona tumeanzisha muziki watu wakaja kucheza pamoja na sisi. Hii ndiyo kazi tuliyokuwa tunaisubiri miaka yote kwamba, Wizara hii ni mpya, Wizara hii ni pana. Kuna Mheshimiwa Mbunge amesema hapa, Wizara hii ni kubwa pengine kama Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mimi kila siku huwa nasema hivi chukua Bahari ya Pacific, ilete Atlantic, ilete *Mediterranean Ocean,* ilete *Black Sea* na nyingine ndiyo unatengeneza Wizara ya mambo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa niliyokuwa nawaza mimi ni hizi *agenda* tunazozibeba na kuziinua. Tunainua pamoja au tunainua sisi Wizara hii ya jamii peke yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimefurahi na kubarikiwa sana na Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, kile nilichokuwa nakitamani kwamba, wachambue sauti iwe nene, ikue, leo nimekiona. Ile kazi ambayo Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alinituma nikaanzie wapi, nakumbuka nilianzia kwenye *agenda* hii MTAKUWWA ambayo nitaisema mbele, ambayo imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Kwamba, hili ni pori, naanzia kushoto-kulia, lakini leo nashukuru kazi ya kuinyanyua jamii ielewe, maana ninyi ni wawakilishi wa jamii nina imani mmeyatoa kwenye jamii. Jamii imeelewa na imemiliki hii Wizara yao wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vile vipaumbele ambavyo wao walikuwa wanadhani tu kwamba, nikienda kwenye Baraza la Madiwani nimtume diwani wangu akaseme afya, akaseme maji, akaseme umeme, akaseme mifugo, akaseme kilimo, akaseme elimu, leo nchi nzima imepindua *agenda* inasema ustawi na maendeleo ya jamii ni *agenda* ya kipaumbele mimi hili limenibariki. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wangu nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri ambao ni wa kisekta ambao katika jukumu la uendeshaji wa hii Wizara tuko pamoja,

wamesimama, wamesema waliyoyasema. Sitarudia, nitaongezea pale ambapo wao hawakupita hivyo, niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea pongezi ahsanteni. Sisemi lawama, nasema changamoto siyo hasi ni chanya, ambazo hizo ni petroli ya kutupeleka sisi mbele kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili. Tunapokea kwa mikono miwili kabisa, ni haki na ni halali mliyoyasema, Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zimekuwa nzuri sana hivyo basi, naweza nisijibu kila hoja lakini najaribu kuangalia zile hoja ambazo zimechangiwa na wengi sana. Nilivyotoka hapa nilikwenda kuchapa mwenyewe kwa mkono wangu, Wabunge wangapi wakati tunakwenda *break* walikuwa 15 na hoja zao nikazichapa kwa mkono wangu kutaka kujua kwenye *variables* ipi imechangiwa sana, nikagundua kwamba Bunge hili *tone* ya leo wameongelea katika sura nzima mmomonyoko wa maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmomonyoko wa maadili mpaka *break* ulichangiwa na Wabunge 12 kati ya 15. Ina maana karibu wote walilia na mmomonyoko wa maadili. Kumekuwa na maneno yakitumika hapa kwa Kiswahili, ushoga, ushoga, ushoga. Sisi kama Serikali tunapenda kusema kwamba hii ni dalili mojawapo ya matendo ya mmomonyoko wa maadili kama yalivyo mengine yale mtu anakwenda kumchukua kuku anambaka mpaka anakufa. Tumeona na tumeshuhudia na yuko ndani kafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine juzi amekwenda kumchukua nyoka akajivalisha akauambia umma wa Watanzania yeye anafanya mapenzi na nyoka anapata ela, maana huo ni ushirikina. Mimi nilitoka nikavaana naye nikamtafuta nikamwambia nikuone, uje na unieleze huyo nyoka ulikompata maana na huo nao ni mmomonyoko wa maadili. *Mbengo TV* waliorusha lile tangazo walikuja wakaomba radhi wakatoa picha zote kule mtandaoni na huyo mwenye nyoka aliyevaa, alijificha baada ya kuona nitamtafuta kwa ushirikiano na Mambo ya Ndani amejitokeza anasema mama nakuja kukuona hivi

Jumatatu nakwenda kukutana naye. Huo nao ni mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmomonyoko wa maadili una sura pana, lazima tuuonglee wote kwa ujumla wake yakiwemo hayo yanayosemwa mapenzi ya jinsia moja ambayo Taifa hili lilishagundua miaka mingi iliyopita kwamba hili ni tatizo na wakatengeneza sheria. Sheria ambayo hapa juzi kulikuwa na swali humu Bungeni lililojibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ndoa za jinsia moja au mahusiano ya jinsia moja yapo Kifungu cha 154 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 ya Sheria ya Tanzania kwamba; "Vitendo vya mapenzi ya jinsia moja au mahusiano kinyume na maumbile iwe faragha au kwa makubaliano ni kosa la jinai." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Haya yote tunayoyasema yalishajadiliwa na Bunge hili yakapitishwa kuwa sheria na leo tumepata takwimu za kuonesha wangapi wamechukuliwa hatua, mpaka wengine wamepewa *PI* kimyakimya 64 wameondoka nchi hii na wanaendelea kuondolewa. Kuna kazi inafanyika kutokana na maelekezo ambayo mmekuwa mkitupa na hususan kwenye Bunge lililopita. Mheshimiwa Spika aliagiza tukafanye hatua na baadhi ya hatua mrejesho umetolewa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendelee kuliongelea hili suala la mapenzi ya jinsia moja kama sehemu ya mmomonyoko wa maadili kwa mbele kidogo. Kuna Wabunge wengine wameni-*challenge*, mbona Mheshimiwa Waziri hatujakusikia ukizungumza kwa maneno yako. Ningelikuwa nakumbuka kanuni vizuri ningekuomba utengue ili nioneshe hapa *video* ambao iko *YouTube* wakienda wao ina dakika 3.19 nikiwa Shinyanga tarehe 5 Disemba, 2022, nilikwenda kwenye shule moja kufuatia tukio lililotokea Geita. Mtu mmoja aliendа huko, mwanaume kavaa manyonyo anafundisha watoto mambo kama hayo, nilitoka nikakemea. Namkumbuka mpaka Mheshimiwa Diwani wa Kata ile anaitwa Mheshimiwa Senzuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya mkutano *online* na watu wa Geita yule mtu akatafutwa na Jeshi la Polisi na nilisema *through my*

*dead body* tabia ya kuwafundisha watoto vitu kama hivi kwa maneno kama hayo ambayo yameandikwa *YouTube* na nimeyatamka. Hivyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge mniamini na Bunge lako Tukufu kwamba mimi ninapambana ki-*field marshal* kweli kweli siyo kimchezo mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nakosa ni hii *tone*, hii *tone* ya leo, hii *tone* ndiyo niliyokuwa naitafuta na leo imefika hapa tumeisikia, mimi nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye makakati gani sasa Serikali kama Serikali tulionao. Hivi tarehe 15 Mei juzi kushinda jana tulikuwa pale Viwanja vya Chinangali tukiadhimisha Siku ya Familia Duniani ambapo siku hiyo kwa mara ya kwanza kwa ukubwa unaostahili nimeona Mawaziri wa Kisekta wakija kutoa matamko yao moja baada ya mwingine kuhusu masuala haya ya kupambana na mmomonyoko wa maadili, chini ya mpango kazi wa Taifa unaoitwa MTAKUWWA, Mpango kazi wa Taifa wa Kupambana Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto, wametoa matamko yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Mpango kazi ulianza mwaka 2016/2017 umekwenda mpaka Juni, 2022 umekwisha, tathmini ikafanyika, nimeelezea kwenye kitabu changu cha hotuba. Tumekuja na mpango kazi mpya ndani ya mpango kazi huo naomba niseme siyo mpango kazi wa Wizara siyo mpango kazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu ni mpango kazi wa Taifa lote. Maana yake mikakati iliyowekwa mule ina Kamati za kupambana na hili tatizo tunalolijadili kuanzia kwa *VEO,* kwenda kwa *MEO* wenye mitaa kwenda *WDC* hizi kamati ziko huko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kamati ziko kumi na nane elfu karibia kumi na tisa elfu. Tatizo tunaloliona hapa tukienda kwenye hizi ngazi za mikutano ya *VEO* mikutano ya *WDC,* mikutano ile ya kina *MEO* zile kamati zinakuwa zinaoneana muhali, aliyefanya jambo hili ni mtoto wa pale wanakwenda kupatana. Sasa wewe uliyenda kuwaambia tumkamate ndiyo unakosa ushahidi. Sasa tukasema tutafanyaje na hizi kamati? Kamati hizi lazima zifanye kazi yake, kivipi?

Huu mpango tuliouzindua tumekaa na wadau waliokuja pale wakiwepo hawa wanaotusaidia kwenye malezi na makuzi ya watoto ambao ni wageni, wakasema uleteni tukae kikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawaambia ninachotaka ni fedha, sitaki fedha Wizarani, zishuke chini tupeleke kwenye zile kamati ili hizi kamati zilizoko vijijini, mitaani na kwenye kata zipate mafunzo. Zifahamu jukumu lao na zitekeleze ili yule Mheshimiwa Diwani anayetoka pale kwenye ile kata anapokwenda sasa kwenye vikao vya Baraza la Madiwani kuelekea *Full Council* kama anavyobeba *agenda* ya afya, maji na elimu ababe *agenda* ya mmomonyoko wa maadili unaotusababishia haya mambo yote, mpaka hayo mapenzi ya jinsia moja, mpaka hayo ya kubaka kuku, ng'ombe na mbuzi na mambo kama hayo. Kwa hiyo, huu ndio mkakati ambao Mawaziri wameutolea tamko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mchengerwa (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI alisimama pale bila kuchelewa akasema; "Natoa agizo na mniletee barua leo ninaporudi Ofisini usiku huu nisaini." Kwa sababu kumbe mpango huu wa mwanzo uliwaacha Wakuu wa Mikoa na uliwaacha Wakuu wa Wilaya hawakuwa na jukumu la moja kwa moja, sasa ndiyo wenye viti. Pia, akasema; "Naagiza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya asiyelibeba hili siyo mwenzangu kwenye safari ya uongozi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mabadiliko ya kimkakati ambayo tunayafanya katika zama hizi ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameiunda hii Wizara ina miaka miwili na nusu sasa lakini moto wa *agenda* zake nadhani jamii imeona na imepokea. Sasa najaribu kuangalia mwaka wa tatu unaokuja tutakuwa wapi, kama *tone* ya Bunge ni hii maana yake *RCC* zitaimba wimbo tunaoimba sisi wote. *DCC* zitaimba wimbo tunaoimba sisi wote. Maana yake *Full Council* iimbe wimbo huu tunaouimba hapa, maana yake Kamati za Mabaraza ya Madiwani zikiwemo huduma na ustawi wa jamii huko kwenye wilaya zetu ziimbe huo wimbo. Maana yake

kwenye *WDC* hii *agenda* tuikute ile inaitwa *monitoring and evaluation of compliance to the specific agenda*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea hapa, pia kumezungumzwa hoja nzuri sana. Hii Wizara wanaume wako wapi? Mimi niliwahi kuuliza huko nyuma, wanaume ndio viongozi wa kuanzia kwenye taasisi za familia, tangu tupate uhuru wa nchi hii wanaume ndio wamekuwa wengi kwenye nafasi za uongozi maeneo mbalimbali kuliko wanawake. Nikasema wanaume mpo, wakaniambia tupo, nikasema mbona siwaoni hawakunielewa, wakacheka wakatengeneza *memes*, wakatengeneza *reels* nikafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi tena kusema kama wanaume ndio viongozi wa taasisi za familia, haya mambo yanapotokea ya mmomonyoko wa maadili maana yake uongozi, urais kwenye ile taasisi na kwenyewe kuna kuyumba. Maadili yanakuwa hayashikwi na hayafundishwi. Hivi vikao tunavyovifanya kwenye taasisi rasmi siyo mbaya tukavifanya kwenye familia zetu, sisi tupite sasa na maendeleo ya jamii kuangalia kama watu walikaa kikao walijadili, baba mwenye nyumba yuko hapo anaongoza familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema tupite kwenye kaya tuangalie nini kinaendelea. Hiyo ni mikakati ya kuamsha amsha jamii ijue wajibu wake, lakini kizuri ni kwamba katika Sera mpya ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ambayo tumefanikiwa kuitoa mwaka huu 2023 baada ya kulala miaka 20 nyuma tangu ipite, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akasema tengenezeni hiyo sera mlete, imemtambua mwanamme kama ni mnufaika rasmi na mshirika kwenye safari ya maendeleo ya jinsia. Ingekuwa siyo kanuni na muda ningeisoma iko humu ukurasa namba 22 hiyo sentensi kwenye sera mpya lakini tutaisambaza na tutakuwa na semina za Wabunge wataijua hiyo sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanaume dunia pia imewatambua kuna Programu inaitwa *He for She* ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan miezi michache iliyopita

alinituma mimi *South Africa* katika Mkutano wa *Afrika* ambapo wanaume *champions, male champions he for she* katika masuala ya kutokomeza ukatili wa kijinsia ambayo ni jinsia mbili wanawake na wanaume. Hiki kitu kwenye sera hii tumekitaja na tunaenda kuanza. Ombi langu, nikisema wanaume mpo tukutane kwenye mkutano hata kama ni *online* wakina baba ninawaomba. Juzi nilikuwa nina mkutano *online twitter* bahati mbaya mtandao ulikuwa hauko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda wanaume waingie kama sera ilivyosema lakini siyo tu sera imesema huu Mpango Kazi wa MTAKUWWA umewatambua wanaume mule. Kizuri zaidi wageni watakuwa wameondoka, tumesajili mpaka vyama vya wanaume wanaopigwa na wake zao majumbani na Rais tunaye. Ni Wizara hii alikuja kwangu analia nimepigwa ikawa hivi madawati ya jinsia, nikamwambia madawati ya jinsia ni kwa jinsia zote, kwa ni jinsia ni moja? Tanzania jinsia zinazotolewa na Wizara ya Afya kule *labour ward* ni 'Me' na 'Ke'. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Bwana Rais wa wanaume wanaopigwa na wake zao akachekwa sana. Sasa mimi huwa nashangaa mtu akijitoa kwenda mbele, wanaume tunanyanyaswa wanaume wenzake wanamwambia kwani mwanaume unatakiwa kulia wewe, wewe vipi bwana, wewe tulia hapa. Mwisho wa siku wanayajaza, wanafunga na tai, kifua kinajaa wanafanya matukio ya ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, niseme haya madawati ya jinsia ni kwa mwanamke na mwanamme. Mimi hapa nimepokea mashauri mengi ya wanaume kupitia simu yangu ya wazi kupitia *DM* za *Instagram* za *Jamii Forum,* kupitia *DM* za *Twitter*. Mimi niko kwenye *Tik-Tok*, niko kwenye *Instagram,* niko popote natambaa na vijana kwa sababu gani? Natafuta jamii iko wapi, inisikie na inielewe. Mume wangu Mheshimiwa *Advocate Gwajima* halali usiku akiamka anasema nini? Nasema tayari huku kumewaka naona *notification* ngoja nipambane nipambanie Taifa langu kwa dhamana aliyonipa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mnyonge mnyongeni, naomba mnipongeze, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo utaona tunavyotambaa na *agenda* ya wanaume. Nirudishe tu kwenye historia kidogo kwa nia njema, masuala ya kwa nini wanawake wameonekana wako mbele ni nyakati tu. Wakati Katiba ya Nchi yetu inatengenezwa, ilitengeneza pia na viti maalum vya wanawake kwa sababu tu wakati ule hali ilikuwa iko hivyo ilivyo na Katiba ndiyo sera kubwa na ndiyo sheria kubwa. Kwa hiyo tumekuwa tukitembea nayo hiyo lakini zama zinabadilika, hata hii Wizara imeundwa ni kwa sababu ya zama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu tumeanza kuweka mikakati ya wanaume kwenye sera, tumeanza kuweka mikakati ya kusajili vyama vya wanaume, tumeanza kuanzisha Progamu za *He for She*, MTAKUWWA inasoma wanaume, madawati ya jinsia yanapokea wanaume, ukienda kwenye mabaraza ya watoto tuna watoto wa kike na wakiume wako ndani wanajengewa uwezo wa kujiamini, kuthubutu na kuongea. Ukienda kwenye madawati ya ulinzi ya watoto shule za msingi na sekondari ni watoto wa kike na wakiume ndio wanaongelewa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi itoshe tu kusema kwamba bila wanaume hatuwezi kufanikiwa, tutakuwa tunajenga upande mmoja upande mwingine unabomoka. Kwa hiyo Mheshimiwa Msambatavangu ahsante sana umekuwa *champion* eneo hili, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Badala ya kuanza na kuomba Wizara ya Jinsia ya Wanaume mtuamini kwamba hata jana ilikuwa ni siku ya mtoto wa kiume duniani, sijui Wabunge wangapi walipongeza hilo ila mimi nilipongeza na mawazo yakanijia tuombe na siku ya kuadhimisha siku ya mtoto wa kiume. Ikipendezwa na ikapendeza ili tuwe na siku hiyo, yote hiyo ni katika harakati za kumtambua mtoto wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele ya kwanza inalia, nami nataka niseme kwa habari ya sheria. tulielekezwa na kiti hapa Bunge lililopita mkatengeneze na mrekebishe Sheria ya Ushahidi, hii sheria inawakandamiza watoto, mara hamwamini maneno yao sijui mpaka muhtasari uje, kazi ile imefanyika. Nafikiri ni Kifungu cha 127(2) mimi siyo wakili msomi lakini imerekebishwa, yale mambo ya kusema mtoto

mpaka awe sijui alifanyafanyaje ndiyo hukumu yake isikilizwe, yameondolewa. Mahakama imerekebisha hicho kifungu na sisi tunawapongeza kwa sababu inatusaidia sasa yule mtoto kusikilizwa kwa usawa kulingana na mazingira aliyoenda nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kidogo kuhusu masuala ya hawa ma-*house girls (Housemaid)* wasaidizi wa nyumbani niwaite wa kike na wakiume wanakuwa wanakatiliwa na kunyanyaswa hili nalo ni tatizo. Tunashirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na mwaka huu mtaona Umoja wa Mataifa kuna kitu wamekipitisha ambacho tulikitangaza. Katika ku-*address* hizi kazi za matunzo hizi za majumbani, nini kifanyike? Hilo litaanza kuadhimishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya ya wakina mama wajamzito gerezani na mtoto tumeyasikia hapa. Uone hii Wizara ilivyo na Bahari nyingine inaitwa *Blue Sea* ina mambo mengi. Tutaenda kulifanyia kazi, tuone mazingira gani mama akienda huko ili huyu mtoto asiwe na shida. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema tujenge *creches, creches* ni sehemu ndogo ambazo mtoto huenda wakatunzwa pale ambapo wazazi wao wanakuwa na shughuli zingine zikiwemo hata hizo za Mahakama. Ziko wapi hizi *creches* ambapo huyu mtoto ataishi kama yuko nyumbani ananyonyeshwa, mama yake anakwenda kwenye adhabu zake lakini mtoto awe salama na Maafisa Ustawi wa Jamii na ndiyo hawa wanaongezewa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *reusable pads;* ni hoja nzuri sana na nimpongeze Mheshimiwa Nusrat Hanje. Nilikuwa hapa nawasiliana na Katibu Mkuu wangu umesikia, zile mashine za kushona 350 tulizoandika *proposal* tukapewa na Serikali ya Watu wa China na tuna vyuo vya maendeleo ya jamii, hivi haya si ndiyo mawazo unaambiwaga mawazo upewe na wenzako ambao mnaongoza pamoja. Twende tukaweke kwenye chuo kimojawapo cha maendeleo ya jamii hawa wanaofanya uanagenzi waanze kushona pale, tutafute hela zitengenezwe hizi *reusable pads* tusambaze. Ndiyo

namna ya kupata mawazo ya Bunge na kuyatumia kiroho safi kwa sababu ya kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa na faida sana, nimefurahi sana, nimebarikiwa sana kwa sababu nilikuwa nawaza sasa nikipeleka tu wasipojadili jamani mimi nitakuwa nateseka peke yangu tu huko mitandaoni. Leo wamenitendea haki na wamewatendea haki Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wamemtendea haki Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyeunda hii Wizara maana asingeiunda leo tungekuwa tunaongelea tu *MSD,* tunaongelea tu dawa, tunaongelea tu mambo ya afya ya wagonjwa kwa sababu na yenyewe ni moto, lakini tunayaongelea haya kwa sababu yeye ameweka msingi wa nyumba kubwa inayokwenda kujengwa likawa ghorofa la kumeremeta na watu wakaja kujifunza hapa. Niseme mikutano mitatu ya kimataifa imekuja kuhusu ukeketaji tumefanya vizuri, *ECD* tumefanya vizuri, kuhusu mambo ya bajeti za kijinsia *(Gender Budgeting)*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hitimisha hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo haya ni mambo ambayo dunia inatujua Tanzania kwamba sisi tupo, yupo Mheshimiwa Dkt. Samia, yuko *Field Marshal* na liko Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo linatoa hoja makini na mikakati yetu ni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si rahisi kujibu kila kitu kwa sababu ya muda ila tutakuwa na semina na Waheshimiwa Wabunge wote ili waweze kuyaelea haya na watakapokwenda kule kwa Madiwani kwenye *full council* wasimame waseme hoja imesimama hivi, tuanzie huku na tupeleke taarifa kule ili *monitoring and evaluation* ikija sisi tufuate *performance score card* ambayo itatumbalisha Halmashauri kwa Halmashauri ni kwa namna gani tunazibeba hizi ajenda ambazo ni za kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo naomba kushukuru tena na tena, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya naomba kutoa hoja kwamba..

**MWENYEKITI:** Yuko sawa. Mheshimiwa hitimisha hoja yako upo sahihi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na kuhitimisha hoja Bunge lako sasa likubali litupe nafasi tukatekeleze haya mambo na kujumuisha yote waliyotuambia kwenye mipango, Kamati yangu makini kabisa itakapokuja kipindi kinachokuja ije ikiwa mambo yako safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, Katibu tuendelee.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 (1) naongeza muda ili tuweze kukamilisha kazi yetu.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*......................................Sh. 4,119,266,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki ndicho kinashika mshahara wa Mheshimiwa Waziri na hapa nina Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaye tutaanza naye.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama Mheshimiwa Waziri alivyojieleza pamoja na mikakati na mipango aliyonayo, pamoja na Mheshimiwa Waziri Ridhiwani ambaye yeye anahusika na kuajiri. Kwa sababu nafahamu Mheshimiwa Dkt Gwajima pamoja na kwamba hii ni Wizara yake lakini bado kuna shida kubwa sana ya Maafisa Ustawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza hapa na malalamiko haya, sote tunatambua zamani kwenye vijiji walikuwa na uwezo wa kufika nyumba kwa nyumba ili kueleza Mama mwenye mimba ale chakula gani, kula chakula bora, redio ya Taifa ilikuwa ikisema na vitu kama hivyo, kwa hiyo wafanyakazi hawa ni wa muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kufanyia siasa wafanyakazi kwa sababu ndiyo kwenye msingi kabisa wa kumsaidia Mheshimiwa Waziri aweze kufanikisha yale ambayo ameyapanga. Kwa hiyo, mimi naomba ufafanuzi, sina haja ya kushika shilingi lakini nataka ufafanuzi na *commitment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyopita Mheshimiwa Tendega alilieleza Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Simbachawene alijibu akasema, tunakwenda kuajiri Maafisa Ustawi 360 mwaka jana na mwaka huu tunarudia yale yale tunasema tumeajiri kwa *numbers*,

tunaomba ndugu zangu tumsaidie na tuisaidie hiyo Wizara ambayo mnasema tunataka ifanye kazi ile ambayo tumeikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *commitment* ya Serikali kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii ambao wataenda mpaka chini na kusimamia afya za Watanzania na ukatili wa kijinsia kule vijijini ambako kiukweli hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kupata maelezo ya Serikali, ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Ridhiwani.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu hili jambo analifuatilia sana, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeendelea kulifanyia kazi jambo hili, hata hiyo taarifa kwa mfano anayoisema ya mwaka uliopita wa fedha, Serikali iliahidi katika Bunge lako kwamba itaajiri watumishi 360 katika kada ya ustawi wa jamii, Mheshimiwa Rais kwa kutambua *extent* ya tatizo hili alitoa kibali cha kuajiri watumishi watakaokwenda kufanya kazi ya ustawi wa jamii 403, ikiwa ni ongezeko la watumishi 43 wa ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu mwaka huu wa fedha kibali kimeshatolewa cha kuenda kuajiri watumishi 472 ikiwa ni ongezeko kubwa zaidi ya lile ambalo lililotolewa mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba, Serikali ina nia ya kupambana na jambo hili. Nataka nikuhakikishie kwa sababu kuajiri kunategemeana na ikama ya mishahara na kibajeti, tutakapokuwa tumejenga uwezo hata kama unataka watu 1,000 tutaajiri hapa kwa sababu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kupambana na vita hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalihakikishia Bunge lako kwamba tupo tayari kulifanya hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, umepokea hayo maelezo vizuri.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kanuni inasema sikutaka kushika shilingi, nimepata ufafanuzi, tafadhali naomba lifanyiwe kazi.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nisipopata ufafanuzi wa kina basi nakusudia kushika shilingi ya mshahara wa Waziri kwa dhamira njema kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa mchango wangu nimezungumzia suala la ulezi kwa wazee wetu, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anahitimisha amejaribu kutueleza Waheshimiwa Wabunge kwamba, wazee wanaohudumiwa ni 5,000, lakini hawa hivyo hawa wazee wanaohudumiwa ni wale wazee ambao wako kwenye makambi ama vituo. Tunahitaji wazee wetu nchi nzima bila kujali yuko kwenye kituo ama hayuko kwenye kituo apate stahiki yake anayotakiwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya wazee hawako kwenye mfuko wa *TASAF* hawapewi, kuna wazee ambao hata jamii zetu tu huko wana uwezo wa kuwasaidia lakini wanashindwa kuwasaidia ni kwa sababu tu pia sheria nayo haimlazimishi mtu kwenda kumsaidia huyu mzee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ina wajibu wa kumhudumia mwananchi wake, nahitaji *commitment* ya Serikali ni lini na ni kwa namna gani inakwenda kuwasaidia wazee hawa kuwahudumia kwa kupatia chakula, malazi, matibabu pamoja na huduma nyingine zote ambazo zinastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata maelezo ya kina na ya kushiba nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja, maelezo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na ninamshukuru sana Mheshimiwa Kunti kwa hoja yake nzuri kabisa ya kuwatetea wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia naungana na majibu ya awali ya Mheshimiwa Naibu Waziri aliyoyatanguliza, wazee hawa kwa kweli tumekuwa tukiwawaza kwamba, hivi tutakuwa tunashughulika na hawa tu ambao wapo kwenye makambi? Hawa walioko kwenye makambi watakaa pale milele? Wengine si wanakuja na shida tu akishapata uwezo wa kuondoka, wanaondoka? Tunawaendelezaje? Hilo ni swali tunalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema kuna wengine wako kule kwenye jamii, wasingependa kuja kwenye makambi lakini hawajiwezi, tunawaendeaje? Tukaketi na shirika moja Tanzania ambalo linawahudumia wazee kwa miaka mingi linaitwa *HelpAge International* lakini kwa sasa ni *Local NGO* ya *HelpAge* Tanzania, tukaunda kikosi kazi na kikaandika andiko kwamba, hata huu usaidizi unaokuja kutoka kwenye mifuko mikubwa inayosaidia Serikali yetu ni lazima wai-*acknowledge* hii *intervention* ya kwamba kuna maisha baada ya utoto, baada ya ujana na tunaelekea uzeeni, hivi haya mafungu tunayoyaona wanatusaidia, kundi la wazee wanalipeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili andiko linakamilishwa na tunakwenda kuliwasilisha kwenye hii mifuko mikubwa kama *Globa Fund, USAID* na wengine, tujadili nao kuhusu kuwekeza kwanza magonjwa ya uzeeni ambayo ni *non communicable diseases* yanawaumiza sana wazee wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sera ambayo tunayoisema inaelekea kwenye Baraza la Mawaziri ni hoja ambayo imejadiliwa kwenye mabaraza ya wazee ambayo tumeyaunda na tuna baraza la kitaifa. Hii ikitoka, Sheria husika zitabadilika kwa mujibu wa sera, mikakati itabadilika na haya masuala ya pensheni yatakuwa huko ndani na hoja zote za wazee siyo kwenye makambi tu, mpaka wa kwenye jamii kwa ujumla wake. Vinginevyo, tutakuwa na jamii inayotuletea wazee wa kwenye makambi, sisi tusingependa tukae na wazee kwenye makambi tungependa wakae kwenye jamii, kwa hiyo, hoja yako ni *valid* naomba uachie mshahara wangu tuendelee, siku nyingine baada ya sera kutoka utuulize tunaendeleaje na hiyo mikakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti umeridhika na hayo maelezo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa …

**MWENYEKITI:** Umeridhika ama haujaridhika?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Menyekiti, sijaridhika. Hatuwezi kuwahudumia wazee wetu kwa kutumia *NGO's*

**MWENYEKITI:** Toa hoja kama haujaridhika.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja Wabunge waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono, tuendelee na Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi sikusudii kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri lakini naomba tu ufafanuzi na *commitment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Taifa letu umejengwa kwenye malezi ya mtoto wa mwenzako ni wako, *currently* hilo jambo

kwenye Taifa letu limekufa. Mtoto wa mwenzako ni wako Tanzania sasa hivi hilo jambo halipo, ndiyo maana mmomonyoko wa maadili umekuwa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipongeze hatua za Mheshimiwa Waziri anazozichua, amekuwa *active* sana kwenye kuchukua hatua kwenye matukio mbalimbali, zaidi Mheshimiwa Rais ambae amekuwa akijitokeza hadharani kukemea zaidi matukio mbalimbali ambayo ni maovu ikiwemo vitendo hivi vibaya vya ukatili lakini pia mambo ya ulawiti. Mheshimiwa Rais amekwishatoa muelekeo kwamba siyo utamaduni wa kiafrika na siyo utamaduni wa kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa kuwa jamii inalia, Kanisa linalia, Misikiti inalia na sisi Wabunge tunalia na kwa sababu hiyo hiyo ndani ya nchi hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya mabadiliko ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 2018 kwa kuongeza makosa yasiyokuwa na dhamana kutoka matano hadi kufikia kumi na moja, mojawapo ikiwepo makosa ya Ulawiti, ubakaji, ushoga na makosa mengine yanayohusiana na hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu iko hapa Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa sisi ndiyo Bunge tunaotegemewa na Watanzania, tumepaza sauti, tumepiga kelele na umma umesikia, hatuwezi kuishia hapo tu, ni upi mkakati wa Serikali au *commitment* ya Serikali kuleta sheria ama kwa hati ya dharura na sisi tuweke haya makosa kuwa makosa yasiyokuwa na dhamana ili tuioneshe njia jamii mwelekeo wa Bunge jinsi ambavyo linakataa haya matatizo, kwa sababu kuacha *loophole* hii ya mtu amebaka, kesho anatoka inatengeneza *syndicate* nje kwamba hili jambo ni jepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu amefanya vitendo vya kishoga au amelawiti, kesho anapewa dhamana anatoka, inatengeneza *syndicate* ya kwamba hili jambo ni jepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kama Bunge wajibu wetu ni kulibeba Taifa, kama tunalibeba Taifa, ni upi mkakati na *commitment*

ya Serikali kuleta mabadiliko ya sheria ili haya makosa yawe ni makosa ambayo hayana dhamana ili tulilinde Taifa, tulinde kizazi na tuweze kulisaidia Taifa letu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo, umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Jumanne Sagini.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, nilikurudisha nyuma. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa hoja hii aliyoitoa na namna anavyoizungumza kwa uzito wake, ni kwa kweli inamkera kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwenye maelezo wakati nachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri kwamba, Tume ya Kurekebisha Sheria chini ya Wizara ya Katiba na Sheria imeshaanza kufanya utafiti juu ya jambo hili, badala ya kuendelea kuwa tunachukua kidogo kidogo au kimoja kimoja tunaleta, ningeomba Mheshimiwa Mbunge avumilie na kwa sababu ni maelekezo yaliyotolewa na Kiti chini ya uongozi wa Mheshimiwa Spika, tutaharakisha mchakato huo ili tutakapoileta hapa iwe ni Sheria nzima *comprehensively* badala ya kuchukua kimoja halafu tunaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nafikiri umeridhika ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lemburis.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposoma taarifa ya Mheshimiwa Waziri alipoiwasilisha asubuhi, katika maeneo yote hata katika michango ya Wabunge walipokuwa wakichangia sikuona sehemu yoyote ambayo Mheshimiwa Waziri taarifa yake imeonesha jinsi ambavyo Serikali au Wizara yake inashughulikia masuala ya ushoga, usagaji na ulawiti, jinsi ambavyo Wizara yake ina mikakati gani, imeeleza *in a very shallow way*. Pia, katika maelezo yake ya kujibu hoja mbalimbali hajaonesha uzito wa michango ya Waheshimiwa Wabunge kuanzia asubuhi kwa jinsi ambavyo wamechangia kwa uzito wa hali ya juu kuhusu suala la ushoga na usagaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah, ulikuwepo wakati Waziri anahitimisha hoja yake?

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo na nilisikiliza lakini ninachozungumza hapa ni kwamba, hajaonesha uzito kama Serikali kwa jinsi ambavyo Wabunge walikuwa wanachangia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ulitaka alie au afanyeje? Enhe endelea, malizia *(Kicheko)*

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema Kimasai kwamba, tunacheka kwa mdomo wenye meno lakini hatumaanishi kile ambacho tunakisema na ndicho hapa ambacho tunataka kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema Taifa hili linatakiwa linusuliwe kwenye masuala ya Sodoma na Gomora, sasa kama tunataka kulipeleka Taifa hili kwenye Sodoma na Gomora, tunataka kupata *commitment* ya Serikali kweli ituoneshe kwamba dhahiri shahiri kwamba kweli imechukia tatizo hili kama ambavyo Wabunge wameonesha kuanzia asubuhi mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli sitapata kauli nzito ya Mheshimiwa Waziri akisikitika, akituonesha masikitiko yake ya kupinga na kukemea ushoga na usagaji, mimi sitaridhika. *(Kicheko/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah, umeeleweka. Mheshimiwa Waziri jaribu kurejea kwa masikitiko zaidi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Bunge lako Tukufu, yaani ninasikitikaaaa, moyo unaniuma, nalia silali na Watanzania ni mashahidi.*(Kicheko)*

*(Hapa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum aliongea kwa kuonesha msisitizo)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nimechukulia kwa uzito, nimeandika mpaka nimechapa na kuchambua hoja na kutoa mifano ya mapambano yangu katika kusema sitaki ushoga na mtoto awe shoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamtumia *clip* yangu ya Shinyanga nilienda shuleni, Kanuni tu zinanisumbua ningeweza kuiweka hapa mkasikia. Nilisema ni maarufuku *over my dead body*. Michango hii nikasema iliyotolewa leo kwangu ni barakaaaa kwa sababu ni *petrol* ya kwenda mbele na nikasema nilikosa hii *tone* ambayo leo nimeiona hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema kwa *tone* hii na kwa mkakati tuliouzindua wa tarehe 15 Mei, 2024 wa MTAKUWA kazi yetu ni kutafuta fedha, hatutaki zikae Wizarani tutembee sisi na magari ziara, tuzipeleke kwa *VEO* na *WEO* kwenye zile Kamati karibu 19000 nikasema wafanye kazi, kwa sababu nyumba na watu wanajulikana, watu wanaoneana muhali, tuwasaidie kwa kutoa taarifa. Kituo cha *call center* cha Wizara tumekitangaza na namba zake tano na namba zangu zipo, watuambie ili sisi tutumie mbinu zetu za kwenda kuwadaka na ushahidi bayana ili hivi vitu viende na hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge niachie shilingi, mimi nimeumia sana sana yaani nimeumia mno, naomba kuwasilisha.*(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah Lemburis.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme mpaka sasa sijamuona Waziri kama yuko *serious*, kwa sababu ni kama anaona utani tu, hayo maelezo yake anaona utani utani tu, naomba niishie hapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah nafikiri kila mmoja na uwezo wake wa kuelezea hisia zake. Kwa hiyo tukitaka ku-*judge* mtu kutokana na hisia zake mimi naweza nikaongea machozi yakanitoka huku ninacheka. Kwa hiyo kila mtu na maelezo yake na namna ambavyo ana hisia. Naomba tumwamini Mheshimiwa Waziri kwa hilo ambalo amezungumza kwa sababu amezungumza kwa undani wake. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee kuendelea kusikiliza hivyo.

Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kimsimgi ninashukuru kwanza ufafanuzi ambao umetolewa na Waheshimiwa Mawaziri kwa hatua mbalimbali ambazo wamekuwa wakizichukua *silently* au *openly* kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo nzuri ambazo Serikali imekuwa ikizichukua bado tunaona ombwe. Bado tunaona *gap* kubwa kati ya matukio yanayotokea siku hadi siku na usimamizi ama zile hatua ambazo zinachukuliwa katika kudhibiti haya matukio. Inawezekana labda usimamizi ni mbovu au *seriousness* katika usimamizi wa sheria au vyovyote vile kwa sababu sheria tumeziona zipo lakini bado tunaona tatizo lipo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka kutoa ushauri. Hoja yangu kimsingi ilikuwa inafanana na wenzangu waliotangulia. Bado tunakasirishwa kwa sababu *seriousness* bado ni ndogo. Ninapenda kushauri na naomba Serikali ilichukulie jambo hili *seriously.* Tuunde chombo mahususi ambacho kitashughulika na jambo hili peke yake kwa maana ya kupata taarifa sahihi ya matukio yanayotokea, kupata ushahidi wa matukio yanayofanyika lakini pia na kupeleka Mahakamani ama kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki chombo kiwe maalum yaani kiwe kina *full mandate* kwa sababu sasa hivi nimemsikia Waziri anasema alienda Shinyanga halafu akaenda Polisi. Polisi yupo kwenye mamlaka nyingine siyo ya kwake. Nimemsikia Naibu Waziri wa TAMISEMI akielezea upande wa TAMISEMI jinsi wanavyochukua hatua lakini hawana Polisi wala mamlaka ya kuchukua hatua. Kwa hiyo kuwe na chombo kimoja ambacho kikiona jambo kiwe na uwezo wa kuchukua hatua. Ninashauri tufanye hivyo na hiki chombo kiende kwenye maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona mitaani taarifa zipo, mashuleni taarifa zipo na kwenye kumbi za starehe tunaona mambo yanayofanyika huko. Watu wanajitangaza kufanya mambo ya aibu ikiwemo ushoga kwa sababu unakuta hakuna mtu anayeweza akachukua hatua. Ninashauri kuwe na chombo ambacho kitakuwa na *link,* kiwe na meno ya kufanya haya mambo yote kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la ushoga ni kubwa, tusipolichukulia hatua za makusudi hatuwezi kufika mahali. Tunafanya hivi siyo kwa nia ya kumdhalilisha mtu wala hatuna nia ya kusema tumchafue mtu heshima yake au kutaka kunyang'anya mamlaka za watu. Tuna nia njema kwa ajili ya kulinda kizazi hiki na tuna nia njema ya kulinda utamaduni wa Mtanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramadhani umeeleweka na muda wako umekwisha.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba jambo hili Serikali ilichukue na ilifanyie kazi na kuwe na *seriousness* kwenye hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na ndiyo maana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ameiunda Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa sababu ameona changamoto zinazowakuta watoto wetu na wanawake ambao wako katika jamii hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanzo ilikuwa katika Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii. Tulikuwa tumebanwa, sera zetu hazionekani na kazi zetu hazionekani lakini Mawaziri wa kisekta wote wameelezea sababu na juhudi ambazo wanazichukua katika matendo haya ya ukatili wa jinsia hasa kwa watoto wetu na masuala haya ya mmomonyoko wa maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara tutaendelea kuchukua maoni yenu na jitihada zenu zote ambazo mnatuletea kuhakikisha jambo hili linakwisha kwa amani. Pia, tutahakikisha kwamba tunamsaidia Mheshimiwa Rais wetu ili awe na amani na kuondokana na changamoto hizi za mmomonyoko wa maadili ili nchi yetu iwe na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, tumepokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge na tutayafanyia kazi kwa pamoja na sekta zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge kwa Kanuni ya 123(2) tunaingia kwenye *guillotine*.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*............................................ Sh. 4,119,266,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*........................ Sh. 923,232,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.......................... Sh. 1,278,714,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*........................................Sh. 703,386,028
Kifungu 1005 - *Government Communication Unit*.............Sh. 376,866,000
Kifungu1006- *Procurement Management Unit*....................Sh.622,872,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology*....................................................Sh. 563,869,000
Kifungu 1008 - *Legal Service Unit*......................................... Sh. 455,960,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit* .................. Sh.447,838,000
Kifungu2001-*Community Development Institutes*..........Sh.16,038,613,743
Kifungu 2002 - *Community Development*........................Sh. 1,477,294,257
Kifungu3001- *Gender Development*................................Sh.1,810,418,000
Kifungu 3002 - *Children Development*............................. Sh. 1,056,006,000
Kifungu 3003 - *Special Groups*..........................................Sh. 1,789,872,000
Kifungu 4001 - *Non-Government Organizations*..............Sh. 2,920,506,000
Kifungu 5001 - *Social Welfare Division*............................ Sh.12,902,365,972

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*...........................Sh. 1,175,673,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*....................Sh.150,000,000
Kifungu 2001-*Community Development Institutes*..........Sh. 2,000,000,000
Kifungu 2002 - *Community Development*............................................ Sh.0
Kifungu 3001 - *Gender Development*.............................. Sh.3,200,000,000
Kifungu 3002 - *Children Development*.............................. Sh.1,977,597,000
Kifungu 3003 - *Special Groups*......................................... Sh.10,500,000,000
Kifungu 5001- *Social Welfare Division* ............................... Sh.1,414,910,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Sasa namkaribisha mtoa hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono na sasa nitalihoji Bunge.

Wanaoafiki kwamba, Bunge lilikubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 waseme ndiyo.

Wote wameafiki. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa natangaza rasmi kwamba Bunge limekubali, limepokea na limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. kwa hivyo sasa iliyobaki ni kuwaombea tu kila la heri katika utekelezaji wa yale ambayo yote tumeyakubali leo kama Wabunge.

Kwa ujumla wake nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yao nzima lakini bila kusahau hekima na busara iliyotumika na mamlaka ya Rais kuitenganisha Wizara hii kubwa na muhimu sana katika Taifa letu. *(Makofi)*

Ningependa niweke sawa wale wote ambao walifikiri toka asubuhi kwamba Wizara hii imedogoshwa. Wizara hii haijadogoshwa, ni kubwa na ndiyo Mamlaka ya Rais ikaamua kuiweka peke yake kwa ukubwa wake na umuhimu wake. Uchangiaji kama mnavyoona

wengi tunatamani tuchangie na ningeweza kutoa fursa hata wiki nzima nafikiri Wabunge wote wangechangia lakini kutokana na wingi wa Wabunge ndiyo maana tukapeana dakika tano tano angalau kila Mbunge ambaye ameomba kwa siku ya leo aweze kupata. Ndiyo maana tukatoa muda huo lakini sio kwa udogo wa Wizara wala kuidogosha ama kuwa imekosa hadhi. Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii yetu. Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima tunakuamini na Serikali ya Awamu ya Sita yote. Nitoe wito kwa Watanzania wote, Serikali peke yake kama Serikali bila jamii kushiriki kikamilifu tutakuwa tunadanganyana kuanzia sisi Waheshimiwa Wabunge hapa kama wawakilishi wa wananchi pamoja na viongozi wote kuanzia vijiji mpaka Taifa. Suala hili ni janga la Taifa zima na siyo Wizara peke yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lazima tuwe wakweli hii kazi ni yetu sote na utamaduni wa nchi yetu ni wetu sote. Maporomoko ya maadili si mazuri kwa Taifa letu lote. Hakuna Waziri hata mmoja ama Serikali anayependa Taifa hili liporomoke kimaadili. Mimi mwenyewe hapa kwenye Bunge la Kumi na Moja nilisimama nikasema; tusipovalia njuga suala hili, hapa mbele leo tuna kiongozi mimi mwanamke ambaye nina mume mwenye jinsia ya kiume itafika wakati atakuwepo mtu ambaye ana jinsia hiyo ya kike lakini aidha atakuwa na mume ambaye ni jinsia ya kike mwenzake ama atakuwa na mume ambaye ni mke.

Kwa hiyo tuone uzito wa hilo jambo. Kila mtu ana uwezo wa kueleza kwa hisia zake, wakati Wajumbe mnachangia nilikuwa nakatika maini na chango na kila kitu lakini nilikuwa natoa fursa ili Wizara na Serikali na wananchi waelewe. Kwa hiyo baada ya kusema hayo nawaombea kila la heri naamini Mwenyezi Mungu atatulinda na Taifa letu liondokane na mabalaa yote. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo naahirisha Shughuli za Bunge hadi Jumatatu saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.10 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 20 Mei, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*